

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 21 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. JOHN W. HECHE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI
RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MADINI:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 113

Ahadi ya Ujenzi wa Barabara za Lami-Arumeru

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga barabara ya Sangis Toangam Kwenda Aken, Kimundo hadi Ubungo Kwa Kiwango cha lami. Vilevile Rais Dkt. John Magufuli wakati wa kampeni aliahidi ujenzi wa barabara ya kilometa 5 kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hizo zilizotolewa kwa wananchi wa Arumeru Mashariki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali kupitia *TARURA* imepanga kujenga kilometa mbili za barabara ya Sangis – Duruti – Nambala kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 1.0 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, *TARURA* imeanza ujenzi wa barabara kwa

kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 64 kwa fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 33 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizozitoa wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Hivyo, azma ya Serikali ni kuhakikisha ahadi zote za Mheshimiwa Rais zinatekelezwa kikamilifu.

Na. 114

Sheria na Viwango vya Riba Vinavyotumiwa na Makampuni ya Simu

MHE. MAULID S. MTULIA aliuliza: -

Makampuni ya Simu pia hutoa huduma ya kusafirisha fedha na kukopesha kwa wateja wao wenye sifa.

(a) Je, ni sheria ipi inayotumika kusimamia utoaji wa huduma hizi za fedha kwa Kampuni za Simu?

(b) Je, viwango vya riba vinavyotumika vimepangwa na mamlaka husika?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake zinazofahamika kama Kanuni za Utoaji Leseni na Idhini za Kutoa Huduma za Mifumo ya Malipo za mwaka 2015; na Kanuni za Huduma za Fedha za Kielektroniki za mwaka 2015 zinaipa mamlaka Benki Kuu ya Tanzania kusimamia Mifumo yote ya Malipo nchini. Makampuni ya simu yanayotoa huduma za kifedha yanapewa leseni kwa kupitia Sheria na Kanuni hizi.

Mheshimiwa Spika, viwango vya riba vinavyotumika kwa mikopo midogo midogo inayotolewa na Kampuni hizi hutokana na nguvu ya soko kama zilivyo kwa taasisi nyingine za fedha zinazotoa mikopo bila kuchukua amana ambapo mfumo wa soko huria unatumika kuamua kiwango cha riba kinachotozwa. Hivyo, viwango husika havipangwi na mamlaka yoyote bali ni soko ndiyo hupanga.

Na. 115

Tanzania Kuwa na Uchumi wa Kati

MHE. OTHMAN OMAR HAJI aliuliza:-

Serikali inaamini kwamba mtangamano wa kisiasa ni nguzo muhimu katika kujenga nchi yoyote kwa maendeleo makubwa na ya uhakika na kwa sababu sifa hii ya mtangamano wa kisiasa haipatikani hapa nchini.

Je, Serikali haioni kuwa inawadanganya wananchi wake kwa kuwaeleza kwamba inayo nia ya kuifanya Tanzania kuwa na uchumi wa kati?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kuwa mtangamano wa kisiasa ni moja ya nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya maendeleo iliyojiwekea kupitia sera na mipango yake mbalimbali. Katika kuthibitisha hili Serikali imeendelea kusimamia misingi imara ya utawala wa kidemokrasia nchini kupitia uwepo wa mtangamano wa kisiasa katika masuala mbalimbali ya maendeleo inayotekeleza kwa kuvishirikisha vyama vyote vya siasa katika kujenga uchumi wa viwanda utakaopelekea kufikia uchumi wa kipato cha kati kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imeainisha malengo yanayotakiwa kutekelezwa ili kufikia uchumi wa kipato cha kati ambapo kama Taifa tunatakiwa kutekeleza na kusimamia misingi mikuu mitatu ambayo ni fikra za kimaendeleo zinazoambatana na hali halisi ya kijamii, uwajibikaji na kuthamini mila na desturi ili kutoa fursa zaidi kwa umma; Ustadi wa kazi na ari ya ushindani; na uongozi na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Tanzania Toleo la 12 iliyotolewa na Benki ya Dunia mwezi Julai, 2019 (*Tanzania Economic Update July 2019, 12th Edition*) inaonesha kuwa Tanzania itavuka kiwango cha kipato cha uchumi wa nchi maskini na kuingia kwenye uchumi wa kipato cha kati kabla ya mwaka 2025. Hivyo, ni dhahiri kuwa lengo la Tanzania kuwa na uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 litafikiwa kama lilivyopangwa.

Na. 116

Migogoro Kati ya Hifadhi na Wafugaji Nchini

MHE. RHODA E. KUNCHELA aliuliza:-

Kumekuwepo na migogoro ya muda mrefu kati ya hifadhi na wafugaji nchini hali inayosababisha jamii ya wafugaji kupata madhara mbalimbali ikiwemo vifo, uonevu, mifugo kutaifishwa na kutozwa faini zinazokiuka sheria za nchi:-

(a) Je, Serikali inawatambua wafugaji waliopata madhara hayo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya Askari Wanyamapori wanaofanya uonevu huu unaokiuka sheria mbalimbali kwa wafugaji?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuwatambua wafugaji ambao wamepata madhara, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa nyakati tofauti, wafugaji ambao wamekuwa wakiingiza mifugo yao ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Utaratibu unaotumika kuwakamata wafugaji hao mara zote unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, askari wa wanyamapori wamekuwa wakifanya kazi zao kwa kufuata sheria za nchi katika ulinzi wa rasilimali za Taifa. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa msisitizo kwa watumishi hao kufuata sheria na taratibu kuwakamata wale wote wanaoingiza mifugo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, katika ukamataji wa wahalifu hao, taratibu za kisheria zinafuatwa. Hata hivyo, kwa nyakati tofauti kumekuwa na matukio ya wafugaji kuvamia vituo vya askari na kuwashambulia kwa silaha za jadi kwa lengo la kuchukua mifugo yao, suala ambalo ni kinyume na sheria za nchi. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa Ruaha mnamo tarehe 09/10/2018 Askari Wanyamapori mmoja aliuwawa na wananchi waliovamia kituo kiitwacho Nyota kwa lengo la kukomboa mifugo yao iliyokuwa imekamatwa baada ya kuingizwa katika hifadhi hiyo kinyume na utaratibu. Aidha, katika hifadhi hiyo hiyo, tarehe 03/07/2016 askari mwingine wa Wanyamapori aliuwawa na wananchi waliovamia kituo cha Ikoga kwa lengo la kukomboa mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa Askari wa Wanyamapori wanaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu, Wizara imekuwa ikiwachukulia hatua stahiki za kinidhamu kulingana na sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi. Aidha, katika kuendelea kutafuta suluhisho la uingizaji wa mifugo ndani ya hifadhi, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yanayozunguka hifadhi kadiri bajeti itakavyokuwa inaruhusu.

Inapotokea wananchi kuvamia wahifadhi Jeshi la Polisi hulazimika kutumia nguvu kujilinda na kuwakamata wahalifu. Nitoe wito kwa wananchi kufuata na kutii sheria bila shuluti.

Na. 117

Kuongeza Ushuru wa Mazao ya Misitu-Liwale

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Kumekuwa na uvunaji mkubwa wa mazao ya misitu ya asili Wilayani Liwale ikiwemo ya vijiji na ile ya Serikali Kuu ambapo huvuna mbao na magogo lakini ushuru wa halmashauri ni shilingi 400 kwa ubao na shilingi 1,000 kwa gogo kiasi ambacho ni kidogo kulingana na uharibifu unaofanywa.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza viwango hivi ili kuwezesha halmashauri kuwa na mapato makubwa ili kuendana na bei ya mazao sokoni?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 255 la mwaka 2017 mfanyabiashara wa mazao ya misitu anapaswa kulipa mrahaba wa Serikali Kuu (*royalty*) na asilimia tano ya mrabaha, ambayo ni *cess* kwa ajili ya Halmashauri husika. Aidha, vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kupitia Sheria Ndogo za Vijiji wanatoza tozo zifuatazo:-

(i) Ushuru wa kijiji ambayo haya ni makubaliano ya mvunaji na kijiji husika wakati wa maombi ya uvunaji na makubaliano hayo ni shilingi 400 kwa kila ubao; na shilingi 2,000 kwa kila gogo; na

(ii) Shilingi 400,000 za maendeleo ya kijiji na makubaliano hayo yanakuwepo kwenye muhtasari wa vijiji ambayo ndiyo inayojadiliwa na Kamati ya Uvunaji ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haioni kama kuna haja ya kuongeza viwango vya tozo kwa sababu tayari Serikali za Vijiji zimeshaweka tozo zaidi kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu katika vijiji vya Wilaya ya Liwale. Kuongeza viwango hivyo kutamuathiri mlaji wa mwisho.

Lengo la Serikali ni kuwezesha rasilimali za nchi yakiwemo mazao yatokanayo na misitu kunufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na halmashauri yake kuhakikisha kuwa fedha zinazokusanywa zinatumika vizuri katika kuwaletea wananchi maendeleo na kuhifadhi misitu.

Na. 118

Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Nyakanazi – Kabingo

MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Nyakanazi hadi Kabingo yenye urefu wa kilometa 50 ulianza tangu mwaka 2014, lakini hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 60 tu.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha barabara ya Nyakanazi – Kabingo inakamilika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Kabingo hadi Kidahwe?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa mtaji wa kutosha wa mkandarasi, ujenzi wa barabara ya Nyakanazi – Kabingo (kilometa 50) kwa kiwango cha lami haukukamilika kwa wakati. Baada ya Serikali kutambua kuwa mradi hautekelezwi kama ilivyokuwa imepangwa, ilichukua hatua mbalimbali za kiusimamizi ambapo sasa utekelezaji umefikia asilimia 76 na umepangwa kukamilika mwishoni mwa Septemba, 2020.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kidahwe–Kasulu (kilometa 63) itakayoungana na barabara ya Kabingo – Kasulu - Manyovu umefikia asilimia 93 na utakamilika Juni, 2020. Barabara ya Kasulu - Kabingo yenye urefu wa kilometa 192.35 ni sehemu ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (kilometa 260) ambayo itajengwa kwa kiwango cha lami kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*).

Hivyo, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, kipande cha barabara kutoka Kabingo - Kidahwe (sehemu ya Kasulu hadi Kabingo) kitajengwa kupitia mkopo wa *AfDB* unaojenga barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kabingo –Kasulu - Manyovu chini ya *AfDB* imegawanywa katika sehemu nne za Kasulu Junction – Manyovu ikijumuisha Kasulu Town Links (kilometa 68.25); Kanyani Junction – Mvugwe (kilometa 70.5); Mvugwe – *Nduta Junction* (kilometa 59.35) na *Nduta Junction* – Kabingo (kilometa 62.5). Mikataba ya ujenzi kwa wakandarasi wanne watakojenga sehemu hizo nne ilisainiwa tarehe 20 Februari, 2020 na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza tarehe 20 Mei, 2020.

Na. 119

Ujenzi wa Barabara ya Ziba Hadi Chankola na Ziba Hadi Puge

MHE. SEIF K. S. GULAMALI aliuliza:-

Barabara ya Ziba - Choma – Chankola na Ziba kwenda Nkinga – Simbo – Ndala - Puge ni ahadi ya Mheshimiwa Rais hasa ikizingatiwa barabara hii inapita katika Hospitali ya Rufaa Nkinga na Hospitali ya Ndala na hutegemewa na wakazi wote wa Mkoa wa Tabora na mikoa jirani.

Je, ni lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu ili barabara hii ianze kujengwa?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ziba – Choma – Chankola yenye urefu wa kilometa 27 na Ziba – Nkinga – Simbo - Puge yenye urefu wa kilometa 83 ni barabara za mkoa zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Nzega – Tabora (kilometa 114.7) kuunganisha Mkoa wa Tabora na Shinyanga na Singida umekamilika, ujenzi wa barabara ya Tabora – Itigi – Manyoni (kilometa 259.7) sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya (kilometa 89.3) na Nyahua – Tabora (kilometa 85) umekamilika na sehemu iliyobaki ya Chaya – Nyahua (kilometa 85.4) ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tabora – Usesula (kilometa 30) umekamilika. Kwa sehemu ya Usesula – Sikonge – Ipole – Inyonga – Mpanda

(kilometa 343) mikataba ya ujenzi imesainiwa na wakandarasi watatu (3) wanaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Mkoa wa Tabora na mikoa ya Katavi na Rukwa. Vilevile, ujenzi wa barabara ya Tabora – Urambo (kilometa 94) na Kaliua – Kazilambwa (kilometa 58.9) umekamilika na ujenzi sehemu ya Urambo – Kaliua (kilometa 28) unaendelea ili kuunganisha Mkoa wa Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kuunganisha makao makuu ya mikoa na nchi jirani kwa barabara za lami. Baada ya miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kuunganisha makao makuu ya mikoa kukamilika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za mikoa zikiwemo barabara za Ziba – Choma – Chankola na Ziba – Puge utafuata kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Na. 120

ICD Zilizopo Mkoa wa Dar es Salaam

MHE. LUCY T. MAYENGA aliuliza:-

Serikali imeweka utaratibu maalum wa kuhifadhi makontena ya wafanyabiashara tofauti na ule uliokuwepo hapo awali.

Je, hadi sasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam kuna *ICD* ngapi?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ya Bandari Kavu yametambuliwa kwa mujibu wa Kanuni za Bandari Kavu zilizotungwa chini ya Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania (*The*

Tanzania Shipping Agencies (Dry Port) Regulations, 2018). Kanuni hizi pia zinaweka utaratibu wa jumla wa namna maeneo haya yatakavyofanya kazi na kupata makasha kwa ajili ya kuyahifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zinabainisha njia mbili ambazo bandari kavu zinaweza kupata makasha kutoka bandarini; njia ya kwanza ni kuwa na makubaliano na bandari na hivyo kufanya kazi kama sehemu ya bandari (*Port extension mode*), njia ya pili ni kupata makasha moja kwa moja kutoka kwa wafanyabiashara wa nje wanaotuma shehena kuja nchini (*shipper's nomination*).

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kanuni zinampa uwezo Waziri mwenye dhamana kusimamisha kwa muda matumizi ya njia ya pili (*shippers nomination*) kwa kipindi cha miezi sita (6) pale ambapo maslahi ya umma yanakuwa hayajalindwa vizuri. Utaratibu huu umekuwepo tangu awali na haujabadilishwa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna jumla ya vituo 14 vyenye leseni ya kutoa huduma za bandari kavu kwa ajili ya kuhifadhi makasha yanayoingia nchini (*imports*). Aidha, kuna vituo 19 vyenye leseni ya bandari kavu kwa ajili ya kupakia shehena (*stuffing*) katika makasha na leseni 6 zimetolewa kwa ajili ya bandari kavu zinazohifadhi makasha tupu (*empty containers*).

Na. 121

Sera ya Nyumba na Makazi

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Sera ya Nyumba na Makazi nchini?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Phillip Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mtaalamu Elekezi Chuo Kikuu Ardhi ilianza kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 kwa lengo la kuihuisha ili iendane na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya sasa na miaka ijayo. Aidha, lengo la pili la kufanya mapitio hayo lilikuwa ni kutenganisha masuala ya nyumba na makazi ambayo yapo katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ili kuwa na Sera ya Taifa ya Nyumba inayojitegemea.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Rasimu ya Sera ya Nyumba imeandaliwa kwa kushirikiana na Mtaalamu Elekezi na mpaka kufikia Februari, 2020 ukusanyaji wa maoni ya wadau umefanyika katika mikoja ya Mtwara, Ruvuma, Lindi, Mbeya, Songwe, Iringa, Rukwa, Mwanza, Kagera, Geita, Dodoma, Singida, Moshi, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. Ni mategemeo yetu ukusanyaji maoni ya wadau na uboreshaji wa rasimu ya sera utakamilika ifikapo Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua ya kukusanya maoni kukamilika, maoni ya wadau yatajumuishwa katika Rasimu za Sera hiyo na hivyo kuendelea na hatua inayofuata ya uidhinishaji wa sera.

Na. 122

Hitaji la Soko la Shayiri kwa Wakulima wa Karatu

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Wakulima wa shayiri katika Wilaya ya Karatu wamekosa soko la uhakika la zao hilo kutokana na wanunuzi wakubwa ambao ni Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kutonunua mazao hayo.

Je, Serikali inawasaidiaje wakulima hao?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kampuni za Bia nchini *Tanzania Breweries Ltd. (TBL)* na *Serengeti Breweries Ltd. (SBL)* huingia mikataba na wakulima kuzalisha shayiri kila mwaka. Katika msimu wa 2018/2019 kampuni ya *TBL* iliingia mkataba na wakulima kuzalishiwa tani 230 za shayiri kwa matumizi ya kiwanda hicho. Aidha, kutokana na uzalishaji mkubwa wa wakulima kampuni ilichukua shayiri kutoka kwa wakulima kwa awamu ambapo shehena ya mwisho ilichukuliwa kwa Sh.800 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya soko la shayiri kwa wakulima wa Wilaya ya Karatu yametokana na wakulima kuzalisha shayiri nyingi nje ya mkataba wa kuzalisha ambapo kwa msimu wa 2018/2019 ulikuwa tani 230. Kufuatia changamoto hiyo, Serikali iliwakutanisha kampuni ya *TBL* na wakulima ambapo ununuzi wa shayiri iliyozalishwa nje ya mkataba ulifanyika kwa bei ya chini ya ile ya mkataba. Aidha, kampuni hiyo imelazimika kuihifadhi shayiri hiyo kwa muda mrefu kwa kuwa mahitaji ya kampuni ni tani 230 tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha zao la shayiri nchini, Serikali inaendelea na mpango wa kupunguza kodi kwa kimea kinachozalishwa na kusindikwa nchini. Uamuzi huo unatarajia kuongeza uzalishaji wa shayiri na viwanda vinavyosindika shayiri hapa nchini. Pia, Serikali inaendelea na kuwasiliana na Kampuni ya Kutengeneza Bia ya *TBL* ambayo pia ni wamiliki wa kinu cha kusindika shayiri Mkoani Kilimajaro; kufufua kinu hicho au kumpa mwekezaji atakayeweza kukiendesha kinu hicho ili kiweze kusindika kimea kinachozalishwa nchini. Aidha, hatua ya ufufuaji wa kinu hicho utawezesha kuongeza uzalishaji wa shayiri nchini na hivyo kuwanufaisha wakulima na kupunguza uagizaji wa shayiri kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda wakulima wa shayiri na ngano nchini, Serikali inaanda mpango wa kupunguza uagizaji wa ngano na shayiri kwa kutumia mfumo wa *quota system*. Mfumo huo utawahitaji waagizaji wa ngano na shayiri nchini kununua kiasi cha shahiri na ngano kinachozalishwa ndani ya nchi kwa kila tani wanayoagiza kutoka nje ya nchi kwa lengo la kuongeza uzalishaji kwa wakulima wa ndani.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Mwongozo! Huo mmoja tu. Tuokoe muda kwa sababu Wizara ina siku moja. Nani mwingine jitaje jina mwenyewe. Hao wawili tu! Tuanze.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo wako nikitumia Kanuni ya 69(1) kwamba Bunge liahirishe mjadala ulioko mbele yetu, tuweze kujadili hali ya maambukizi ya ugonjwa wa *corona* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia Taarifa ya Serikali iliyowasilishwa jana. Tumeona kuna ongezeko kubwa sana la wagonjwa waliopata virusi hivi vya *corona* na ukiangalia taarifa zilizotolewa kati ya tarehe 16 mpaka tarehe 20 tuna ongezeko la watu 160 kitu ambacho kinatufanya Watanzania kuona kwamba jambo hili sasa limekuwa ni kubwa na maambukizi ni makubwa na yanaendelea kuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni vizuri na busara kama Bunge, Serikali ije hapa Bungeni tujadili, ituambie ina mikakati gani ya kupunguza maambukizi. lakini namna gani tunadhibiti maambukizi kwenye majiji makubwa ambayo tayari imeshaonekana kwamba kuna maambukizi makubwa zaidi ikilinganishwa na Miji mingine. Serikali pia ije ituambie ni kwa namna gani Wataalam wetu wa afya ambao wako mstari wa mbele kutoa huduma kwa waathirika hawa wanaweza kukingwa, wanatengenezewa mazingira mazuri, wanapewa na motisha kwa sababu wanafanya kazi kwenye hali ambayo kwa kweli ni ku-*risk* maisha. Vile vile Serikali...

SPIKA: Malizia dakika tatu.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Serikali ije na mkakati hapa Bungeni ituambie na kutupa taarifa pia ya masuala mazima ya kiuchumi, ya kibajeti, namna gani sasa inaenda kukabiliana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kutoa hoja ili tujadili jambo hili.

SPIKA: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kutokana na janga lililoko duniani na Tanzania tayari tunaendelea kuathirika na virusi vya *corona*. Pia niendeleo kukupongeza kwa hatua ambazo umechukua, leo hii tunapita kwenye *sanitize machine* na tunapuliziwa nguo. Tumeona umechukua hatua mbalimbali ukumbi una watu wachache na kutokea ukumbi wa Msekwa, sehemu zote mbili tumekuwa tunachangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Bunge na kuweza kupitisha bajeti ili wananchi wakatekelezewe miradi mbalimbali na matumizi mbalimbali lazima shughuli za Bunge ziendeleo. Kwa msingi huo naomba mwongozo wako ni namna gani ambapo sasa Bunge litaimarisha *safety gears*. Kwa mfano vitakasa, mashine za vitakasa, hizi za *manual* zibadilishwe zije za *automatic* na aina nyingine ambayo tumeona.

Mheshimiwa Spika, kama kuna mji ambao tayari umekwishaingiliwa kwamba wametambulika kuna mgonjwa mmoja, basi Serikali imekuwa ikichukua hatua kwa kuweka *quarantine* wote katika ule mji na kuweza kuwapima. Sasa kwa misingi hiyo kwa sababu tayari kuna Mbunge mmoja Kiti chako kilimtangaza jana, kwa hiyo ningeoomba mwongozo wako, kwamba kwa hiari kama Kanuni zinavyosema lakini kama ikiwa ni azimio la Bunge, basi Wabunge na *Staff* wote tunaoingia katika maeneo haya tupimwe ili wale ambao watakuwa wameonekana kwamba tayari wapo *positive*

wawekwe sehemu maalum ya *quarantine* wapate tiba, baadaye tuweze kuendelea nao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema wote tupimwe, ni umuhimu kwa *staff* na Wabunge wote kupimwa. Ingekuwa ni uwezo tunganasema Wabunge wote wakae hoteli fulani, ni hotelini Bungeni, hotelini Bungeni, lakini hilo haliwezekani. Basi tuwe na utaratibu wa kupimwa ambapo Kiti chako kitaona ni busara ili kuhakikisha kwamba watu wote tunaingia katika maeneo haya watu wa usalama, wafanyakazi wote kwamba tuko katika watu ambao hawana maambukizi ya hivi virusi vya *corona*.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa hatua ambayo wameendelea kuichukua. Basi na ikipendeza na Viongozi wa Dini, kama alivyo Askofu wa Ngara alivyoitikia, basi na Viongozi wa Dini nao waitikie wito huo, nyumba za ibada zisimame kwa muda...

SPIKA: Ahsante sana malizia.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge liazimie Wabunge na *Staff* wote wanaoingia hapa ndani tuweze kupima.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa kwa kuwa wote wawili *almost* mmeongelea jambo lile lile, niwashukuruni sana Waheshimiwa wote wawili kwa kuja na mawazo mbalimbali, mema tu kwa ajili ya hili janga ambalo linaendelea duniani na sisi tukiwa ni sehemu ya dunia basi linatugusa pia katika nchi yetu. Niwahakikishie hakuna *effort* ambayo tutaibakiza katika kuhakikisha mnakuwa salama kama Wabunge, katika mazingira haya. (*Makofi*)

Kwa hiyo kila aina ya ushauri kama ambavyo huwa nasema mara kwa mara sisi tunaupokea, Tume ya Bunge imekuwa ikikutana mara kwa mara kwa ajili ya kuzingatia ushauri wa aina mbalimbali. Hata ninyi mnaona kila wakati mkija mnakuta kuna mabadiliko katika hatua ambazo tunazichukua na tukumbuke sio kila mtu anaishi hapa masaa

24, hatuwezi ku-*control* maisha ya Wabunge wote na wafanyakazi wote wanapoodoka kwenda majumbani kwao. Ni aina gani ya watu wanaokutana nao, ni wageni gani wanawapokea, wanatoka wapi na kadhalika. Wengine hata tunaposema tuwe Dodoma hapa, wengi tu wala hawapo na huko walipo wanajua wenyewe na wanachanganyika. Yaani bado inaelekea kuna baadhi ya watu hata miongoni mwa viongozi, hili jambo halijatugusa hivi kuelewa vizuri hiki kitu tunachoambiwa.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, la kwanza ni hilo, kwanza wewe mwenyewe mmoja mmoja ujali maisha yako na ujali na maisha ya watu wengine na ya familia. Tuchukue hatua, tufuate maelekezo yote tunayopewa na Serikali na maelekezo yote ambayo tunayapata na wataalam wa Afya. Hilo ndio kubwa kuliko yote.

Ni kweli na sisi tumeanza kuguswa kwa namna moja au nyingine, sisi ni sehemu ya jamii, tunategemea jamii iguswe sisi tusiguswe! Itakuwa ni kitu cha ajabu sana tukiguswa kwa namna moja ama nyingine. Tuendeleo kujipa moyo, kama Kiongozi wenu ningependa kuwatia moyo kwamba tusonge mbele, tufanye hii kazi ambayo tumepewa na wananchi. Ng'ombe tumeshamla bado mkia tu, maana hii ndio kazi yetu ya mwisho kabla hatujatawanyika. Niwahakikishie *if it comes to the worst*, bado kazi hii tutaimaliza hata kama ni kwa muda mfupi namna gani, tutafanya *innovation* tutamaliza. (Makofi)

Mawazo ya kwamba kazi hii italala, hayo hapana, Ndugai akiwa hayupo atakuwepo mwingine na kazi hii itaisha. Si lazima iwe kwa muda ambao tumejipangia mpaka tarehe 30 Juni, vyovyote itakavyokuwa lakini sisi hawa hawa tutashauriana kazi hii itaisha. (Makofi)

Kwa hiyo tunapokea kila aina ya ushauri, niwaombe tu wenzetu Serikalini, tulikubaliana kwamba itafutwe siku lije lielezwe Bunge, mambo yanayohusiana na hili jambo. Yakiwemo yale ambayo Waheshimiwa mmeyazungumza na kwa maana hiyo tusaidiane kuona namna gani tunaenda kwa pamoja. Katika maeneo mengine tulipaswa labda

tuunde Kamati Maalum ya ufuatiliaji ambayo Serikali inakuja kujibu, inakuja kutoa maelezo kwa maana ya *oversight*, maana yake ile *role* ya *oversight* ya Bunge bado iko pale pale lakini tumeona haina sababu, viongozi wako *busys* sana na jambo hili kuanzia Mheshimiwa Rais mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Afya, Mawaziri wote, Wakuu wa Mikoa, *everybody* anahangaika na jambo hili. Kwa hiyo tumeona tuwaache wakikimbia na jambo hili lakini *at some point* wafike hapa watueleze na haitakuwa mara moja, labda baada ya hapo watatueleza tena, watatueleza tena na kadhalika. Nina hakika kwa hilo *Chief Whip* na wenzake Serikalini wanajipanga.

Kwa upande wetu niseme tu, kwa Mbunge yeyote anayejisikia vibaya, katika dalili mojawapo ya zile, au kadhaa katika zile ambazo zinatajwa mara kwa mara. Usisite kutuarifu, usisite kabisa na ikiwezekana fanya *self isolation*, anza kufuata utaratibu ule na ripoti katika mahali pa huduma ya afya kwa haraka, ukianza labda na Kituo chetu cha Afya au mahali pengine popote ili uanze kupata huduma. Usisite, masuala ya kuhusu utaratibu hayo niachieni mimi, hayana wasiwasi kabisa, msiwe na wasiwasi yaani mtu asijilazimishe kuja hapa huku akiwa hajisikii vizuri kwa sababu tu anaona kwamba sasa itakuwaje kuhusu utaratibu, masuala ya utaratibu tunazingatia.

Mwisho, kama mnavyofahamu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Rwakatare amefariki, taarifa zote mmekwishapewa, tunaendelea na mawasiliano na familia kama ilivyo taratibu, kama ilivyo ada. Katika mazingira ya sasa kwa kawaida huwa Mbunge akifariki kipindi ambacho tupo Bungeni, huwa tunaacha Kikao kimoja na hilo tulilifanya jana, lakini pia huwa tunafanya mpango wa kumleta mwenzetu katika mazingira ya Bunge. Huwa tunawaaga na baada ya hapo wanapelekwa katika mahali pa nyumba yao ya milele. Hata hivyo, mazingira ya sasa hayaruhusu kufanya zoezi hilo, kwa hiyo hatutaweza kumleta mwenzetu hapa kwa sababu ya hali halisi mnayoiona. Maelezo mengine tutayapata kesho, baada ya kuwa tumemaliza mazungumzo kati ya Ofisi ya Bunge na familia ya marehemu. Wakati huo

Serikali nayo wakijiandaa katika kutusaidia pale ambapo tunaweza tukaomba msaada wowote unaohitajika.

Kwa hiyo kwa jinsi hiyo basi naomba kwa muda huu mnikubalie kwamba tuendelee na *programme* iliyopo. Niwahakikishie tena tunajali sana maisha yenu, tunajali kweli kweli. Hakuna hatua tutaacha kuchukua, tutakayobakiza kuichukua katika kuwakinga na janga hili au katika kuwalinda. Tunawaomba na ninyi mbebe wajibu wa kuelimisha wapiga kura, familia na ninyi wenyewe mjuzuie katika maisha ya mazoea mliyokuwa nayo.

Mwisho kabisa, nimshukuru *Chief Whip* wa Upinzani, kwamba hata kabla hajaja tukaongea kama alivyosema majuzi. Hotuba ya leo mtaiona hata ninyi wenyewe kwa kweli ina mabadiliko makubwa sana. Sasa inakuja kibajeti bajeti, kiuchambuzi kama inavyotakiwa. Mheshimiwa Heche hongera sana. Haya ndio mambo hatukukatazi! Heche katupiga kweli kweli mle lakini wala, lakini jinsi alivyoteremka ndio ile kibajeti bajeti sio mtu anaandika kama ilivyokuwa kule nyuma. Nafikiri *it's a good change*, hilo nawa-commend kabisa, tuendelee hivyo hivyo, mtaona tunakwenda vizuri. Ahsante sana.

SPIKA: Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Madini

SPIKA: Sasa moja kwa moja naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dotto Biteko ili awasilishe Hotuba yake katika muda wa nusu saa.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Nishati na Madini ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Madini, Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kwa mara nyingine kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini. Napenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya inayoendelea hapa nchini. Pamoja na mafanikio hayo naomba pia nimshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa hatua madhubuti alizozichukua yeye binafsi katika kulinda rasilimali madini na kuhakikisha kuwa zinawanufaisha Watanzania hasa wanyonge kwa kulinda maslahi ya Taifa na Watanzania. Sisi ni mashahidi kwa mafanikio mbalimbali yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Serikali imejenga ubia wa Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* na kuanzisha Kampuni ya *Twiga Minerals Corporation Limited*. Uwekezaji huu unaipa Serikali umiliki wa hisa asilimia 16 na Kampuni ya *Barrick Gold Corporation* umiliki wa asimilia 84.

Mheshimiwa Spika, aidha nashawishika kusema maono yake Mheshimiwa Rais ni baraka kwa Watanzania, kwa dhamira yake ya kuanzisha masoko 28 na vituo 28 vya ununuzi wa madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2019 hadi Februari, 2020

kupitia masoko haya wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini ya thamani ya shilingi trilion 1.09 na wameiingizia Serikali mapato kwa kupitia mrabaha na ada ya ukaguzi ya shilingi bilioni 78.1.

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile katika eneo hilo imeweza kuanzisha Eneo Tengefu la Mererani kwa kujenga ukuta na hivyo kusababisha kuongezeka kwa mapato kutoka milioni 166 hadi bilioni 2.15 baada ya ukuta huo kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa azma ya kutetea haki za wanyonge, Mheshimiwa Rais alifuta Kodi ya Ongezeko la Thamani na Kodi ya Zuo kwa wachimbaji wadogo. Hii ilikuwa huruma ya kipekee kwa ajili ya kuwafanya wachimbaji waweze kunufaika na uchimbaji wao. Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuunga mkono juhudi za Serikali katika kulipa kodi na kujisimamia wenyewe na kuepuka ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi makini na miongozo mbalimbali ambayo amekuwa akitupatia katika kutekeleza majukumu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge na hotuba yake nzuri aliyoitoa wakati akiwasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutoa shukurani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu na wewe mwenyewe binafsi, Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini chini ya Uongozi wa Mwenyekiti makini, Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula

na Makamu wake Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano walionipatia wakati wa kutekeleza katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuwashuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini; Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Madini, Profesa Simoni Samweli Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini; pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kufanikisha majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, naomba kuunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki na wananchi wa Jimbo la Newala kwa kifo cha Mheshimiwa Radhid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wao na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kilichotokea tarehe 15 Januari, 2020. Vile vile naomba kutoa pole nyingi kwa familia ya Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Getrude Rwakatale ambaye alifariki hivi karibuni. Naomba Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahususi ya hotuba hii ambayo ni ukuaji wa mapato katika Sekta ya Madini, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka 2019 na 2020, kazi zilizotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020 na Mpango wa Bajeti na Makadirio na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuaji wa mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa; katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2019 kasi ya ukuaji wa Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 12.6. Ukuaji huu umeifanya Sekta ya Madini kushika nafasi ya pili ikitanguliwa na Sekta ya Ujenzi ambao ukuaji wake ulikuwa kwa asilimia 14.8. Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 476.38, kati ya fedha hizo

shilingi bilioni 470.89 zilipangwa kukusanywa katika hazina ambapo hadi kufikia Machi, 2020 shilingi bilioni 358.87 zimekusanywa na kuwasilisha Hazina. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 102 ya lengo la shilingi bilioni 353.17 katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Wizara ya Madini ilitengewa kutumia jumla ya shilingi bilioni 49.47. Bajeti hii inajumuisha shilingi bilioni 42.43 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.04 ya fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 25.95 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo yaani *OC* na shilingi bilioni 16.47 nikwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa Machi, 2020 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni shilingi bilioni 31.44; kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12.09 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 19.35 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara na Taasisi zake. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 470.89 katika mwaka wa fedha 2019/2020, hadi kufikia Machi 2020 jumla ya shilingi bilioni 358.86 zimeshakusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti utoroshwaji wa madini, Wizara imefanya ukaguzi na kuweka mikakati ya kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na mamlaka nyingine za Serikali ambazo zimewezesha kukamatwa kwa madini yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 3.21 na shilingi bilioni 1.56 ili kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetoa elimu ya Sheria ya Madini sura Na. 123 kupitia maonyesho mbalimbali. Aidha, Wizara iliainisha na kugawa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuratibu utoaji wa leseni 11 zenye hekta 54 ya wachimbaji wadogo na vikundi 10 vya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini, Wizara imehamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya metali, madini ya viwandani, madini ya ujenzi pamoja na vito. Aidha, katika kipindi rejewa Wizara ilitoa leseni mbili ya uyeyushaji madini (*smelter*) na leseni tatu za usafishaji madini (*refinery*).

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama migodini, Wizara imefanya kaguzi za usalama wa afya mahali pa kazi na utunzaji wa mazingira katika kipindi rejewa. Migodi mitano ya kati, migodi 19 na migodi midogo 100 ilikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamasisha uwekezaji wa Wizara katika Mkutano wa Kimataifa wa uwekezaji katika Sekta ya Madini mwaka 2020 mkutano mkubwa ulifanyika Dar es Salaam tarehe 22 hadi tarehe 23 Februari ambapo ujumbe wa mkutano huu ulikuwa ni uwekezaji na ushirikiano endelevu katika Sekta ya Madini. Mkutano huu ulihudhuriwa na nchi mbalimbali ambazo zilikuwa zimealikwa pamoja na kutolewa kwa cheti cha uasilia wa madini ya *TIN* ambayo hutolewa na *ICGRL*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa leseni Tume ya Madini katika kipindi cha Julai, 2019 hadi mwaka 2020 ilitoa jumla ya leseni 5,935 za madini. Kati ya leseni zilizotolewa, asilimia 47.2 ni za wachimbaji wadogo. Kuhusu kazi za ugani, utafiti wa Jiosayansi na uboreshaji wa ramani za Jiolojia za upatikanaji wa madini, *DST* ilikamilisha kazi za ugani wa Kijiolojia na Jiokemia katika *QDS* 293. Matokeo ya awali ya utafiti huo yalionyesha uwepo wa madini ya *Kinywe (graphite)* yenye ubora mkubwa na viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti wa Jiolojia ulifanyika katika ramani *QDS* 4 ambazo ni *QDS* 38, 39, 52 pamoja na 53 ulifanyika. Utafiti huo huo kulibainika uwepo wa vivutio vipya vya Utalii vya *Embulbul Depression, Moving Sand* pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za maabara, napenda kurialifu Bunge lako Tukufu kuwa maabara ya *GST* sasa imepata ithibati ya uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya tanuru na kupewa *ISO 17025* ya kukidhi vigezo vya Kimataifa kupitia ukaguzi uliofanywa na Taasisi ya *SADC*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini *STAMICO* limekusanya maduhuli ya shilingi bilioni 4.13 sawa na asilimia 112.61. Lengo la makusanyo yalikuwa ni shilingi bilioni 3.66 katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi, 2020. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 mgodi wa Kiwira ulizalisha tani 9,908.43 za makaa ya mawe ambapo kati ya hizo tani 4,419.1 ziliuzwa kwa shilingi milioni 271.64 na kuipatia Serikali kiasi cha shilingi milioni 30.83. Aidha, kampuni ya *STAMIGOLD* imezalisha na kuuza wakia 9,107.45 za madini ya dhahabu na Wakia 1,170.21 za madini ya fedha, vyote vikiwa na thamani ya shilingi bilioni 31.54. Mgodi umelipa jumla ya shilingi bilioni 2.3 kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika shirika limeanza ujenzi wa mradi wa kusafisha dhahabu Jijini Mwanza kwa ubia wa kampuni ya *Mwanza Precious Metals Refinery*. Mradi huo utakuwa na uwezo wa kusafisha wastani wa kilo 480 kwa siku na kufikia kiwango cha *purity* ya asilimia 99.9. Mradi huo unatarajiwa kugharimu dola za Kimarekani milioni 58.204 na utakamilika Desemba, 2020.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza shughuli za uchorongaji shirika limefanikiwa kupata kandarasi nne cha uchorongaji. Kati ya hizo, Kandarasi tatu zenye thamani ya shilingi bilioni 1.99 zimekamilika. Kutokana na mafanikio yalipatikana katika kipindi hicho, shirika linatarajia kuchangia katika Mfuko wa Serikali shilingi bilioni 1.1 ifikapo Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uwazi, uwajibikaji katika rasilimali madini mafuta na gesi asilia (*TEITI*). Mwezi Desemba, 2019 *TEITI* iliweka wazi kwa Umma *report* ya ulinganishi wa malipo ya kampuni za madini ya mafuta asilia na mapato ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. *Report* hiyo inaonesha

kuwa Serikali ilipokea shilingi bilioni 441.83 kutoka katika kumpuni 22 za madini, mafuta na gesi asilia zilizoingia katika zoezi la uliganishi wa hesabu zake. Aidha, *TEITI* inatarajia kukamilisha *report* ya uliganishi wa makampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa mapato yake katika mwaka wa fedha 2017/2018 kabla ya Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 548 waliodahiliwa katika fani za mafuta na gesi asilia na mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 70 kutoka katika migodi na Taasisi mbalimbali. Baada ya Wizara kubaini uwepo wa changamoto za kitaalam katika chuo hicho, Wizara iliona kuna uhitaji wa chuo hicho kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kifanyiwe ulezi wa vyuo kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hati ya makubaliano kati ya Wizara na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya kukilea chuo, kimekamilika na kusainiwa na tayari kazi ya utekelezaji imeanza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jimolojia Tanzania kimedahili wanafunzi 36 kwa ngazi ya cheti (*NTA Level 4*) katika fani ya teknolojia ya Madini, Usonara. Aidha, wanafunzi 39 waliodahiliwa na kujiungana mafunzo ya muda mfupi katika fani ya utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji madini ya vito ambao kati ya hao wanafunzi 11 wamehitimu mafunzo na wengine wanaendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umezingatia dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020, mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021, Mwongozo wa Kutayarisha Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2020/2021 pamoja na maagizo yaliyotolewa na viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali

vikiwemo; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji madini na kusimamia uwekezaji na uwezeshaji wachimbaji wadogo katika sekta; kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini nchini; kuweka mikakati ya kuimarisha Soko la Tanzanite na madini mengine ye vito na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani ya madini na kuimarisha shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa; kwanza, Tume ya Madini katika mwaka wa fedha 2020/2021 inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo; usimamizi wa Sekta ya Madini na kuongeza mapato katika ukusanyaji wa maduhuli na ukaguzi wa migodi na kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi yetu ya Jiolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo: kwanza, kuboresha kanzidata ya miamba na madini ya Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo, kuboresha huduma za maabara, kukabiliana na majanga ya asilia ya Jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kujikinga na majanga haya.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini *STAMICO* kwa mwaka wa fedha 2020/2021 linatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo: kuimarisha shughuli za uchimbaji na uzalishaji madini; kuanza kutekeleza miradi mipya na kuimarisha shughuli za uchorongaji na kuendelea kuratibu na kuendelea shughuli za wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhamasishaji Madini; Uhamasishaji na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini Mafuta na Gesi (*TEITI*). Katika mwaka wa fedha 2020/2021 *TEITI* inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo; kukamilisha na kutoa kutoa kwa Umme *report* ya ulinganisho wa malipo ya kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali kwa kipindi cha mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini, katika mwaka wa fedha 2021 kinapanga kutekeleza yafuatayo: kwanza, kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia; kuendelea kuboresha miundombinu ya chuo na kuwajengea uwezo watumishi wa kada zote na kuendelea kufanya tafiti kwa kutoa ushauri elekezi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jimolojia Tanzania (TDC) katika mwaka wa fedha 2020/2021 kitatoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani za uongezaji thamani madini na kutoa huduma za usanifu madini ya vito na miamba, huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara.

Mheshimiwa Spika, kipekee nachukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuliongoza Taifa letu na kuwaletea Watanzania maendeleo. Kwa kweli maendeleo yanaonekana kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo wafuatao: Benki ya Dunia, Serikali ya Jamhuri ya watu wa China, Jamhuri ya watu wa Korea ya Kusini, Misri na Australia. Aidha, nazishukuru pia Taasisi, Mamlaka mbalimbali na wadau wa Sekta ya Madini ambao wameisaidia Wizara katika masuala mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nashukuru Uongozi *Institute* na *REPOA* kwa kutujengea uwezo katika masuala ya uongozi na uandaaji wa sera katika Wizara yetu ya Madini. Shukurani zangu za pekee na za dhati nizitoe tena kwa wananchi wema wa Jimbo la Bukombe kwa kuniadini na kunichagua na kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kipekee kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Bernadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wetu kwa kuendelea kunivumilia wakati nikiwa katika shughuli hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 naomba sasa Bunge lako Tukufu sasa liridhie na kupitisha makadirio ya jumla ya shilingi 62,781,586,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Bajeti ya maendeleo ni shilingi 8,500,000,000/- ambazo zote ni fedha za ndani; na

(ii) Bajeti ya matumizi ya kawaida ni shilingi 54,281,586,000/= ambapo shilingi 21,045,927,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 33,235,659,000/= ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Kwa kuwa hili ni Bunge la mwisho na tunaelekea kwenye uchaguzi, naomba niwaombe kila kheri Waheshimiwa wote na ikimpendeza kila mmoja kwa namna yake Mungu akambariki Jimboni kwake, wananchi waliomtuma hapa, wamtume tena aweze kurudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (MB.),
WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2020/
2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Madini, Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa 2019/2020 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi

ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/2021.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kwa mara nyingine kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

3. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini. Napenda kutoa pongezi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi wake makini na thabiti. Mafanikio hayo yanajidhihirisha katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ya maendeleo ikiwamo Mradi wa Ufuaji Umeme wa Bonde la Mto Rufiji (Julius Nyerere Hydro power project), ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway), ununuzi wa ndege mpya kufufua Shirika la Ndege Tanzania na miradi mingine kadhaa.

4. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ya Kitaifa, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais, kwa hatua madhubuti alizochukua yeye binafsi katika kuzilinda rasilimali madini na kuhakikisha kuwa zinawanufaisha wananchi hasa wanyonge na kulinda maslahi ya Taifa. Watanzania watakuwa ni mashahidi wa mafanikio hayo kama ifuatavyo:

(i) Uanzishwaji wa Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited

5. Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais, Serikali ya Tanzania imeingia ubia na Kampuni ya Barrick Gold Corporation na kuanzisha Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited. Uwekezaji huu unaipa Serikali umiliki wa hisa asilimia 16 na Kampuni ya Barrick Gold Corporation umiliki wa hisa asimilia 84. Katika makubaliano hayo imekubaliwa

pia kwamba kutakuwa na mgawanyo wa manufaa ya kiuchumi ya 50:50 hii ikiwa na maana ya kwamba faida na mapato mengine nje ya uendeshaji kuondolewa itatakiwa kuwekezwa nchini kiasi kisichopungua asilimia 50. Hatua hii itasaidia kulinda maslahi mapana ya nchi na kuongeza uhibitaji katika shughuli za uzalishaji madini. Kipekee kabisa nikiri, uthubutu wa namna hii uliwahi kufanyika wakati wa Uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Serikali ilipokuwa na ubia na Kampuni ya Williamson Diamond Limited (WDL). Hakika uongozi wake ni Tunu kwa Taifa.

(ii) Uanzishaji na Usimamizi wa Masoko nchini

6. Mheshimiwa Spika, nashawishika kusema maono ya Mheshimiwa Rais ni baraka kwa Watanzania, kwa dhamira yake tumeweza kuanzisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za uchimbaji madini nchini. Nikiri kuwa, Masoko haya yamesaidia kutatua changamoto za muda mrefu ambazo zilikuwa zikiikabili Sekta ya Madini hususan wachimbaji wadogo kukosa masoko ya uhakika na bei stahiki ambapo katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020 kupitia masoko wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 1,088,693,000,153.19 na wameingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa shilingi 78,008,413,233.13. Masoko haya yameleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa Sekta hii kwa kipindi cha Januari hadi Septemba iliongezeka kutoka asilimia 0.9 mwaka 2018 hadi asilimia 12.6 mwaka 2019 kwa kipindi kama hicho. Masoko hayo yameleta manufaa mengine kwa wananchi ikiwemo kuzalisha fursa za ajira na kuongezeka kwa kipato cha wachimbaji wadogo tofauti na hapo awali. Namuomba Mungu azidi kumjalila maono zaidi na zaidi ili Watanzania wazidi kuneemeka.

(iii) Uanzishwaji wa Eneo Tengefu la Mirerani

7. Mheshimiwa Spika, katika namna isiyokuwa rahisi kuaminika katika macho ya wengi, pale neno la Mungu

lilipomjia Mheshimiwa Rais hakutaka kukimbia wito kama " *Yona mwana wa Amitai, kwenda Ninawi*", amekamilisha ujenzi wa Ukuta kuzunguka machimbo ya madini eneo la Mirerani na kuweka vifaa vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha kuwa madini ya Tanzanite ambayo ni rasilimali ipatikanayo Tanzania pekee inalindwa. Kufuatia uwekezaji huo, sote tumeshuhudia kuongezeka mara dufu kwa mapato yatokanayo na madini ya Tanzaite katika eneo hilo hususan kutoka kwa wachimbaji wadogo kutoka shilingi 166,094,043 kabla ya kujenga ukuta hadi shilingi 2,150,000,000 baada ya kujengwa kwa ukuta. Kipekee namuomba Mungu azidi kusema nae.

(iv) Uendelezaji wa Uchimbaji Mdogo Nchini

8. Mheshimiwa Spika, kwa azma ileile ya kutetea haki za wanyonge, Mheshimiwa Rais alifuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Zuiwa kwa wachimbaji wadogo hii ikiwa ni huruma yake kwa wachimbaji wadogo na mkakati wake wa kuhamasisha uendelezaji wa uchimbaji mdogo nchini. Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuunga mkono juhudi za Uongozi Shupavu wa Awamu ya Tano kwa kuhakikisha wanatumia fursa hiyo ili kujinufaisha na rasilimali madini ambazo nchi yetu imejaliwa.

9. Mheshimiwa Spika, nikiri kuwa, sio siri kuwa Mheshimiwa Rais ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa kuwa chini ya uongozi wake maendeleo ya Taifa letu yanaonekana kila mahali. Nawiwa kusema hakika mioyo ya watanzania inamwomba afya njema ili aendelee kuliongoza Taifa hili kuelekea *Nchi ya Ahadi ya Maziwa na Asali*. Hakika historia imeandikwa na itaendelea kukumbukwa na kizazi hiki na kijacho.

10. Mheshimiwa Spika, kwa dhati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa usimamizi makini na miongozo mbalimbali ambayo amekuwa akitupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Vilevile, nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Bunge lako Tukufu. Pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini nchini.

11. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limefanya katika kipindi cha uongozi wako. Aidha, ninakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza Bunge letu kwa hekima na busara kubwa katika kipindi chote cha Bunge la 11. Ni dhahiri kuwa, Bunge hili limefanya kazi ya kutukuka ya kuisimamia na kuishauri Serikali pamoja na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Chini ya uongozi wako mahiri, Bunge limeweza kupitisha Sheria mbalimbali ikiwemo Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123 ambayo yamesaidia katika kuimarisha na kukuza Sekta ya Madini na kuiwezesha kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Marekebisho haya yamewafanya Watanzania waweze kunufaika na rasilimali madini ambazo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa.

12. Mheshimiwa Spika, naishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula (Mb.), Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri (Mb.) Makamu Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na ushauri mzuri walionipatia katika kipindi chote cha mwaka 2019/2020. Aidha, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2019/2020; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021. Ushauri, maoni na maelekezo ya Kamati

vimesaidia katika kuboresha Mpango na Bajeti inayowasilishwa leo. Nikiri kuwa, mafanikio makubwa ya Sekta ya Madini yamechangiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na michango na miongozo inayotolewa na Kamati hii.



Picha Na. 1: Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakibadilishana mawazo na Viongozi wa Wizara ya Madini

13. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wabunge wote kwa ujumla wao kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutupatia ushauri kwa nyakati tofauti katika kipindi chote cha Bunge la 11. Hakika wamefanya kazi nzuri ya kuwawakilisha wananchi na kuisimamia Serikali kwa kuhakikisha maslahi mapana ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla yamezingatiwa.

14. Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini kwa kifo cha Mheshimiwa Ajali Rashid Akibar aliyekuwa Mbunge wao na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kilichotokea tarehe 15 Januari, 2020. Aidha, ninatoa pole za dhati kwa wananchi

waliopoteza ndugu na mali zao kutokana na ajali, maradhi na maafa yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Ninaomba Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

15. Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Madini, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Naibu Waziri na Profesa Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu, Mhandisi David Mulabwa, Kamishna wa Madini na viongozi wengine wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kufanikisha majukumu yangu.

16. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kuniunga mkono na kunipa ushirikiano katika kuteteleza shughuli za maendeleo jimboni kwa ufanisi. Nawashukuru sana.



Picha Na. 2: Wananchi wa Bukombe wakimsikiliza Mbunge wao Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko katika moja ya ziara zake

17. Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa; Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka 2019/2020; Kazi zilizotekelezwa na Wizara na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020; na Mpango na Bajeti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

B. UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA MADINI KATIKA PATO LA TAIFA

18. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa, katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2019 kasi ya ukuaji wa Sekta ya Madini ulifikia asilimia 12.6. Ukuaji huu uliifanya Sekta ya Madini kushika nafasi ya pili ikitanguliwa na Sekta ya Ujenzi iliyokua kwa asilimia 14.8. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini mbalimbali yakiwamo dhahabu, makaa ya mawe, tanzanite na almasi.

19. Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa (GDP) umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la kasi ya ukuaji wa sekta ikilinganishwa na sekta nyingine za kiuchumi. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2019 mchango wa Sekta katika Pato la Taifa ulifikia asilimia 4.7.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/2020

I. Mapato

20. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 476,380,613,492. Kati ya fedha hizo, shilingi 470,897,011,000 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina ambapo hadi kufikia Machi, 2020 shilingi 358,870,785,797 zimekusanywa na kuwasilishwa Hazina. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 102 ya lengo la shilingi 353,172,758,250 katika kipindi husika. Aidha, Taasisi zilizo chini ya Wizara zilipangiwa kukusanya shilingi 5,483,602,492.00 kwa matumizi ya Taasisi hizo. Hadi kufikia Machi, 2020 Taasisi zilikusanya jumla ya shilingi 4,624,906,145.34 ambazo ni sawa na asilimia 112 ya lengo la shilingi 4,142,379,369 katika kipindi husika.

II. Matumizi

21. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2019/2020, Wizara ya Madini ilitengewa jumla ya shilingi

49,466,898,200.00. Bajeti hii inajumuisha shilingi 42,427,088,000.00 sawa na asilimia 85.77 ya bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 7,039,810,200.00 sawa na asilimia 14.23 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

22. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 25,953,263,000.00 zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi 16,473,825,000.00 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Kwa upande wa Fedha za Maendeleo kiasi chote cha shilingi 7,039,810,200.00 ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini (SMMRP) na Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI).

23. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2020 Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa ni shilingi 31,440,490,478. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,085,773,578 sawa na asilimia 38.44 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi 19,354,716,900 sawa na asilimia 61.56 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake.

24. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Wizara iliendelea na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kutumia kiasi cha shilingi 6,197,175,564.39 ambazo zilizopokelewa mwaka wa fedha wa nyuma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Mirerani, usimikaji wa Mfumo wa Ulinzi na Kamera za Usalama pamoja na miundombinu ya umeme kuzunguka ukuta wa eneo Tengefu la Mirerani.

III. Vipaumbele vya Wizara

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Madini ilikuwa na vipaumbele vifuatavyo: kuhimiza utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini; kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini; kudhibiti utoroshaji wa madini; kuwaendeleza wachimbaji wadogo

na wa kati wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini; na kuendeleza rasilimaliwatu katika Wizara pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

IV. Utekelezaji wa Vipaumbele

(a) Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini

26. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara ya Madini ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi 470,897,011,000 katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Hadi kufikia Machi, 2020 jumla ya shilingi 358,870,785,797 zimekusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali ambazo ni sawa na asilimia 102 ya lengo la shilingi 353,172,758,250 katika kipindi husika.

27. Mheshimiwa Spika, pamoja na uanzishwaji na usimamizi mzuri wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini, pia juhudi za Wizara kuendelea kudhibiti utoroshwaji wa madini nchini; kufanya ulinganishi na usimamizi wa bei elekezi za madini ya dhahabu na vito kulingana na mwenendo wa bei ya dunia; na matumizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (GePG) ambao umerahisisha ulipaji wa tozo mbalimbali; vimechangia kwa kiasi kikubwa kufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli.

(b) Uanzishwaji na Uimarishwaji wa Masoko ya Madini

28. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2020 jumla ya Masoko ya Madini 28; na vituo vya ununuzi wa madini 28 vimeanzishwa na kuwezesha kutatua changamoto kubwa zilizokuwa zinaikabili Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu, zikiwemo wachimbaji wadogo kukosa sehemu za kuuza madini yao na uwepo wa utoroshaji na biashara haramu ya

madini. Changamoto hizo zimekuwa zinasababisha Serikali kukosa malipo stahiki ya tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za madini; kukosekana kwa bei stahiki za madini kwa wachimbaji wadogo; na kukosekana kwa takwimu za uzalishaji na mauzo ya madini kutoka kwa wachimbaji wadogo.



Picha Na. 3: Soko Kuu la Dhahabu Chato (kulia) na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (kushoto) wakifurahia Madini ya Dhahabu baada ya kutembelea Soko la Dhahabu Geita katika moja ya ziara zao kukagua shughuli za madini.

29. Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwa masoko hayo mwezi Machi, 2019 hadi Februari, 2020 kiasi cha tani 10.33 za madini ya dhahabu; karati 13,685.74 za madini ya almasi; tani 20.10 za madini ya bati; tani 550.87 za madini ghafi ya vito; na karati 90,532.41 za madini mengine ya vito kiluzwa kupitia masoko hayo ambapo katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020 kupitia masoko wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani ya shilingi 1,088,693,000,153.19 na wameiingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi shilingi 78,008,413,233.13.

(c) Kudhibiti utoroshwaji wa madini

30. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti dhidi ya utoroshwaji wa madini, Wizara imeendelea na mkakati wa kukabiliana na biashara haramu ya madini ambapo Wizara kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Bandari Tanzania imeweza kufanya kaguzi kwa

kutumia kikosi kazi katika viwanja vya ndege, Bandari na mipaka ya nchi.

31. Mheshimiwa Spika, katika kaguzi hizo, madini yenyethamani ya Dola za Marekani 3,210,976.35 na shilingi 1,556,209,334.61 yalikamatwa katika maeneo ya Tunduru, Kyerwa, Mwanza, Mirerani, Holili, Babati, Hai, Dodoma, Nzega na Kahama. Kaguzi hizo zitaongeza tija na kukuza mchango wa sekta katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Nitoe wito kwa wafanyabiashara na wadau wa Sekta ya Madini kwa ujumla kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazosimamia Sekta ya Madini.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kuzuia na kudhibiti utoroshaji wa madini ili kuondokana kabisa na tatizo hili hapa nchini na hivyo kuwa na taswira chanya kuhusu biashara ya madini. Mikakati hiyo ni pamoja na: kuimarisha usimamizi kwenye maeneo yote ya uzalishaji katika migodi mikubwa na ya kati kwa kuanzisha ofisi za Maafisa Migodi Wakazi yaani *Mines Resident Officers* (MROs); kuweka wasimamizi katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipakani ili kudhibiti utoroshaji wa madini; kuendelea kuhamasisha wauzaji na wanunuzi kutumia Masoko ya Madini ambayo hutoa bei elekezi; na kuendelea kutoa elimu ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo zinazohusu Sekta ya Madini.

33. Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti biashara haramu na utoroshwaji wa madini ya *Tin*, *Tantalum* na *Tungsten* (3Ts), tarehe 27 Januari, 2020 Tanzania ilipatiwa ithibati ya kutoa cheti cha uasilia kwa madini hayo. Upatikanaji wa ithibati hiyo ulifuatia Wizara kukamilisha taratibu za utoaji wa cheti cha uasilia wa madini hayo kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Ukanda wa Maziwa Makuu (International Conference on the Great Lakes Region-ICGLR). Uzinduzi wa cheti hicho ulifanyika tarehe 23 Februari, 2020 na ulifanywa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF MINERALS
THE MINING COMMISSION
ICGLR REGIONAL CERTIFICATE

This is to certify that Shipment No. _____ comprised of designated minerals
 If est certifié que la cargaison N° _____ comprendrait les minéraux désignés

mined in _____ Region in the United Republic of Tanzania has been
 extrait, commercialisés et traités conformément aux exigences de la CARGL

mined, traded and handled in accordance with the ICGLR requirements.

Exporter's Name and Address: _____
 Buyer's Name and Address: _____
 Date of Shipment: _____
 Date of Expiry of Certificate: _____
 Transmitting Through: _____

Designated Mineral (s)	Contained Metal(s)	Net Weight (kg)	Purity (%)	Value (USD)
Minéraux désignés	Contenus en métal	Poids net (kg)	Pureté (%)	Valeur (USD)
Total				

Name of Authorized Officer: _____
 Position: _____
 Signature and Official Stamp: _____
 Date: _____

Stamp of importing authority
 To be returned to:
**The Executive Secretary,
 The Mining Commission,
 P.O. Box 2292, Dodoma,
 TANZANIA**

Picha Na 4: Muonekano wa cheti cha ICGLR

(d) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa Kati wa madini

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kutoa elimu juu ya Sheria ya Madini Sura ya 123 na Marekebisho yake ya Mwaka 2017 kwa wachimbaji wadogo na wa kati pamoja na wadau wengine wa Sekta ya Madini. Katika kutekeleza hili, Wizara imetoa elimu hiyo kwa wachimbaji zaidi ya 1,500 kupitia Maonesho ya Pili ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika tarehe 19 hadi 30 Septemba, 2019 katika Mkoa wa Geita na kwenye mkutano wa madini uliofanyika Dar es Salaam, tarehe 22 Februari, 2020. Aidha, kuanzishwa kwa masoko ya madini kumewawezesha wachimbaji wadogo kuongeza kipato chao kwa kuuza madini yao kwa bei elekezi.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara iliainisha na kugawa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuratibu utoaji wa leseni 11 zenye jumla ya hekta 54 za uchimbaji mdogo kwa vikundi kumi (10) vya wachimbaji wadogo Wilayani Nzega. Aidha, leseni 22 zilitolewa kwa vikundi 22 vya wachimbaji wadogo katika eneo la Bululu Wilaya ya Nyang’hwale zenye jumla ya hekta 71.94 na leseni 15 zenye jumla ya hekta 131.47 zilitolewa kwa Ushirika wa Wachimbaji wa Dhahabu Irasanero, Buhemba Mkoa wa

Mara kutoka kwenye eneo la utafiti mkubwa linalomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Vilevile, leseni 23 zenye jumla ya hekta 189.73 zilitolewa tarehe 28 Juni, 2019 na kukabidhiwa rasmi tarehe 5 Julai, 2019 kwa vikundi vya wachimbaji wadogo wa dhahabu wa Mwakitolyo Mkoa wa Shinyanga. Lengo la kutenga maeneo haya ni kuhakikisha kuwa wachimbaji wadogo wanapata maeneo ya kufanyia shughuli zao kwa uhakika na kujipatia kipato kwa mujibu wa Sheria.



Picha Na.5: Mheshiwa Doto Mashaka Biteko, Waziri wa Madini akitoa Leseni ya Uchimbaji Madini kwa mmoja wa Wawakilishi wa Vikundi vya Wachimbaji Wadogo.

36. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na STAMICO na wadau wengine imekuwa ikiwaelimisha wachimbaji wadogo namna bora ya utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili kuwaongezea tija. Mpaka sasa jumla ya wachimbaji 900 wamepata mafunzo hayo sambamba na kuwasambazia kitabu cha Mwongozo wa Wachimbaji wadogo kilichoandaliwa na Wizara kwa ajili yao. Pia, Serikali inaendelea kuziimarisha Taasisi hizi ili ziweze kuwasaidia zaidi wachimbaji na kuwaongezea uwezo wa kufanya shughuli zao za uchimbaji kwa ufanisi.

(e) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini ya metali, viwandani, ujenzi na vito. Aidha, katika kipindi rejewa Wizara ilitoa leseni mbili (2) za uyeyushaji madini (Smelters) na leseni tatu (3) za usafishaji madini (Refinery).

(f) Kuimarisha Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini Katika Migodi

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya kaguzi za Usalama, Afya Mahali pa Kazi na Utunzaji wa Mazingira katika migodi mikubwa, ya kati na midogo. Katika kipindi rejewa, jumla ya migodi mikubwa mitano (5) ya *Pangea Minerals Ltd* (Buzwagi), *Bulyanhulu Gold Mine Ltd*, *North Mara Gold Mine Ltd*, *Geita Gold Mine Ltd* pamoja na mgodi wa *Williamson Diamonds Ltd* ilikaguliwa.

39. Mheshimiwa Spika, jumla ya migodi 11 ya uchimbaji wa kati ilikaguliwa. Ukaguzi huu ulifanyika katika migodi ya: *Nsoromero Minerals Co-operative Society Ltd*; *Mara Mine Development Ltd*; *Nyamongo (T) Ltd*; *Nyamongo Gold Mine Ltd*; *P.Z. Gold Mining Co. Ltd*; *MMG Gold Ltd*; *CATA Mining Co. Ltd*; *Perfalbion Minerals Ltd*; na *ZEM(T) Co. Ltd* iliyopo mkoani Mara. Pia, ukaguzi ulifanyika katika mgodi wa *Sunshine Ltd* uliopo katika Mkoa wa Songwe.

40. Mheshimiwa Spika, pia, kaguzi hizo zilifanyika katika maeneo ya wachimbaji wadogo ikiwemo: Mgodi wa *Sekenke One Mining Society*, eneo la *Mwakitolyo*, Maeneo yanayozunguka *Ziwa Manyara*, Migodi ya *Bati- Kyerwa*, Mgodi wa *Busolwa*, Mgodi wa *Dhahabu wa Nsangano* na eneo la uchimbaji wa *Tanzanite*.

41. Mheshimiwa Spika, Kaguzi hizo zilibaini uwepo wa maboresho ya mapungufu yaliyobainishwa katika kaguzi zilizotangulia. Hata hivyo, kaguzi zilibaini uendeshaji wa shughuli za madini usiozingatia Sheria na Kanuni hususan katika utunzaji wa mazingira ikiwemo: kutokuwa na Mpango wa Ufungaji Mgodi; kutokuwa na utaratibu wa utupaji mawe taka; na mabwawa ya kuhifadhi topesumu yaliyoidhinishwa. Migodi husika ilielekezwa kufanya marekebisho katika mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kaguzi hizo na ufuatiliaji unaendelea kuhakikisha kasoro hizo zinarekebishwa.

42. Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutunza mazingira, Wizara ilifanya Kongamano la usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira katika Sekta ya Madini. Kongamano hilo lilifanyika jijini Dodoma kuanzia tarehe 16 hadi 17 Desemba, 2019 na lilijumuisha taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC, GST, Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Maji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi. Kongamano hili lilihusisha pia makampuni ya madini ya wachimbaji wakubwa na wa kati, na washauri waelekezi wa masuala ya mazingira. Madhumuni ya kongamano hilo yalikuwa ni kujadili kwa pamoja changamoto za utunzaji wa mazingira katika Sekta ya Madini na namna ya kukabiliana nazo; Kuwaleta pamoja wadau wa Sekta ya Madini kwa maana ya Serikali na sekta binafsi; na kupeana uzoefu kuhusu utunzaji endelevu wa mazingira na ufungaji migodi.

(g) Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini

43. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye Sekta ya Madini Ndani na Nje ya Nchi, kupitia ushiriki katika mikutano ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa Kwanza wa Uchumi na Biashara uliofanyika China tarehe 26 Juni hadi 01 Julai, 2019; Mkutano wa 16 wa Kimberly Process Certification Scheme (KPCS) uliofanyika New Delhi, India tarehe 18 hadi 22 Novemba, 2019; Mkutano wa Sita wa Nchi za Afrika zinazozalisha Madini ya Almasi (ADPA) uliofanyika nchini Namibia tarehe 8 hadi 9 Julai, 2019 na Kikao cha Kamati cha Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR) kilichofanyika Burundi tarehe 1 hadi 4 Oktoba, 2019.

44. Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya ziara ya mafunzo nchini Brazil yaliyohusu uchimbaji wa madini ya *Rare Earth Element* (REE) Februari, 2020 na kushiriki katika maonesho yaliyofanyika Afrika Kusini (Mining Indaba 2020 Conference) kuanzia tarehe 02 hadi 06 Februari, 2020 na maonesho yaliyofanyika Canada (PDAC 2020) tarehe 01 hadi 04 Machi, 2020. Wizara pamoja na Taasisi zake ilishiriki katika maonesho ya 39 ya Nchi Wanachama wa SADC yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 17 hadi 18 Agosti, 2019.



Picha Na. 6: Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini akiwasilisha mada katika maonesho ya Indaba (Mining Indaba 2020 Conference) yaliyofanyika Afrika Kusini kuanzia tarehe 02 hadi 06 Februari, 2020.

45. Mheshimiwa Spika, pamoja na mikutano hiyo kutoa fursa za kubadilishana uzoefu katika masuala ya madini, pia imesaidia kukuza ushirikiano baina ya nchi wanachama na kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, Wizara imeendelea na mazungumzo ya Makubaliano ya Awali ya Ushirikiano (MoU) na nchi za Namibia, Zimbabwe, India na Qatar katika kubadilishana uzoefu kwenye maeneo ya utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani madini na biashara ya madini.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara iliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2020 uliofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 22 hadi 23 Februari, 2020. Ujumbe wa mkutano huo ulikuwa ni **"Uwekezaji na Ushirikiano Endelevu katika Sekta ya Madini"**. Mkutano huo uliambatana na siku tatu (3) za maonesho ya Sayansi na Teknolojia katika Sekta ya Madini ambapo Wachimbaji Wakubwa, wa Kati na Wadogo walishiriki katika kuonesha vifaa vya uchimbaji madini na bidhaa zitokanazo na madini. Aidha, katika mkutano huo kulikuwa na mawasilisho ya mada mbalimbali ikiwemo jiojio ya Tanzania, uwekezaji barani Afrika, uongezaji thamani madini, masoko ya madini na Mabadiliko ya Sheria ya Madini nchini ikilinganishwa na Sheria katika nchi zingine.

47. Mheshimiwa Spika katika ufungaji wa mkutano huo mgeni rasmi **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua Cheti cha Uasilia kwa madini ya *Tin, Tungsten na Tantalum* (3Ts) kufuatia Tanzania kukamilisha vigezo vya kupata idhibati ya kutoa cheti hicho. Mkutano huo ulihudhuriwa na nchi 11 Wanachama wa ICGLR pamoja na wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini.



Picha Na. 7: Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifunga Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini 2020

48. Mheshimiwa Spika, mbali ya mkutano huo wa kimataifa, Wizara pia ilishiriki katika maonesho ya teknolojia ya madini yaliyofanyika Geita tarehe 19 hadi 30 Septemba, 2019. Mikutano yote hii ni sehemu ya jitihada za Wizara kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini hapa nchini.

49. Mheshimiwa Spika, ziara, mikutano na makongamano hayo yaliyofanyika ndani na nje ya nchi yameleta matokeo chanya ikiwemo kupewa leseni za uchimbaji wa madini ya kinywe (Graphite) kwa kampuni tatu (3) ambazo ni za ubia kati ya watazania na wageni (China); STAMICO imepata wawekezaji wawili katika mradi wa kusafisha dhahabu wa Mwanza na mradi wa kuchimba dhahabu wa Buhemba; STAMICO imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Shirika la Madini la Indonesia PT TIMAH tarehe 17 Desemba, 2019 ya

kuendeleza leseni za Madini na tayari wawakilishi wa Shirika hilo wameshatembelea maeneo ya leseni hizo; na mwezi Julai, 2019 GST ilisaini MoU na Taasisi ya Jiolojia ya China (China Geological Survey) kwa ajili ya kufanya tafiti za jiosayansi katika mikoa ya Shinyanga na Mbeya.

(h) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini

50. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuhakikisha wamiliki wa leseni za uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini pamoja na wakandarasi wanawasilisha na kutekeleza mipango ya ushirikishwaji wa watanzania katika mnyororo wa uchumi wa madini (Local Content). Mpango huo ni pamoja na kuwataka wawekezaji hao kuweka kipaumbele katika matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini, kuajiri watanzania na kuondoa tofauti kubwa ya mishahara kwa kazi zinazofanana na kufanywa na wageni na Watanzania.

51. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Wizara ilipitia na kuidhinisha Mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika utoaji wa huduma mbalimbali katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini kutoka kampuni 20 kati ya kampuni 76 zilizowasilisha ili zipatiwe leseni za madini. Sababu zilizosababisha kampuni 56 kukosa sifa za kuidhinishiwa mipango iliyowasilishwa ni pamoja na kutowasilisha kiapo cha uadilifu (Integrity Pledge); uhawilishaji wa teknolojia; kushindwa kuwasilisha bajeti ya utafiti na maendeleo; na kutokuwasilisha mpango wa mafunzo. **Napenda kuchukua nafasi hii kuyahimiza makampuni yote yanayoomba leseni za madini kuzingatia Sheria na Kanuni za utoaji leseni ikiwa ni pamoja na kuwasilisha Mpango wa Ushirikishwaji Watanzania unaokidhi vigezo vinavyohitajika.**

(i) Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi

52. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza weledi na ufanisi wa utendaji kazi, Wizara imewezesha watumishi 43 kuhudhuria

mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Kati ya hao watumishi 22 wa kada mbalimbali walihudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika ngazi za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Stashahada ya Uzamili, Shahada na Stashahada. Aidha, Wizara imewezesha watumishi 21 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utunzaji Kumbukumbu, Takwimu Mtandao (e-statistics), TEHAMA, Mfumo wa Manunuzi, Usafirishaji, Utendaji wa Makatibu Mahsusni na Jimolojia.

53. Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilitoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kwa watumishi wa wizara kama ifuatavyo: watumishi 35 walipatiwa mafunzo ya uandishi na uchambuzi wa Sera; Menejimenti ya Wizara na Maafisa Bajeti wa kila Idara na Kitengo walipatiwa mafunzo ya uandaaji na utengenezaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi wa Taasisi; na watumishi 99 walipata mafunzo ya ndani ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) Agosti, 2019.

V. Utekelezaji Katika Maeneo Mengine

(a) Ukaguzi wa Kimkakati

54. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kudhibiti utoroshaji wa madini nchini kwa kufanya kaguzi maalum na za kimkakati. Kaguzi hizo zimesaidia kubaini wanaotorosha na kufanya biashara haramu ya madini. Katika kipindi rejewa, Wizara ilifanya kaguzi katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Mwanza, Mara, Arusha, Mbeya na Songwe, ambapo watuhumiwa 95 walikamatwa kati yao 52 tayari wamefikishwa Mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili. Aidha, watuhumiwa 43 waliachiwa baada ya kukosekana ushahidi wa kuwapeleka mahakamani. Kaguzi hizo zilifanywa kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali zikiwemo Kamati za Ulinzi na Usalama katika maeneo husika na Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

Picha Na. 8: Baadhi ya Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watumishi wa Wizara ya Madini Wakishiriki katika Semina ya Udhhibiti wa Rasilimali Madini

55. Mheshimiwa Spika, kaguzi hizo zimepunguza utoroshwaji wa madini na biashara haramu na hivyo kuongeza utii wa Sheria ya Madini bila shuruti. Hali hiyo ilifanya mauzo ya madini katika masoko na vituo vya ununuzi kuongezeka. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Novemba 2019, mauzo ya madini ya dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo kuongezeka kutoka gramu 1,188,397.95 hadi gramu 5,546,658.20. Kwa kipindi hicho makusanyo yaliongezeka kutoka shilingi 7,124,934,647.07 hadi 37,022,685,977.00 sawa na ongezeko la asilimia 420. Aidha, kabla ya kaguzi hizo, idadi ya leseni za biashara zilikuwa 696 ikilinganishwa na leseni 1,004 baada ya kaguzi, ikiwa ni ongezeko la leseni 308. Madini yaliyokamatwa yakiuzwa nje ya mfumo rasmi ikiwemo dhahabu, almasi, tanzanite na vito mbalimbali. Madini hayo ambayo yalikuwa na thamani ya jumla ya shilingi 349,618,546.09 yamehifadhiwa Benki Kuu ya Tanzania wakati taratibu za kisheria zikiendelea.

(b) Ujenzi wa Vituo vya Umahiri, Vituo vya Mfano na Jengo la Taaluma

56. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ujenzi wa Vituo vinne (4) vya Umahiri ambavyo ni Bariadi, Bukoba, Musoma

na Handeni na vimeanza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Ujenzi wa vituo hivyo umegharimu jumla ya Shilingi 5,033,286,450.88. Pia, Wizara ilikamilisha ujenzi wa Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini ambalo limegharimu shilingi 2,721,110,846.74. Ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Umahiri vya Mpanda, Chunya na Songea upo katika hatua za mwisho hadi sasa jumla ya shilingi 1,661,012,747.06 zimetumika.



Picha Na. 9: Baadhi ya Vituo vya Umahiri kati ya Vituo Saba Vilivyojengwa katika Mikoa Mbalimbali Nchini

57. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Katente – Bukombe na Lwamgasa – Geita umekamilika na vipo katika hatua za majaribio. Aidha, Ujenzi wa kituo kingine cha mfano cha Itumbi – Chunya upo katika hatua za ukamilishwaji. Ujenzi wa vituo vyote vitatu(3) umegharimu jumla ya shilingi 4,347,098,128.63.

58. Mheshimiwa Spika, vituo hivyo vya mfano ni mahsusni kwa ajili ya kutoa mafunzo mbalimbali kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo. Mafunzo hayo yatahusu uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini. Aidha, vituo hivi vitatumika kufanyia maonesho ya madini na vifaavinavyotumika katika

shughuli za uchimbajimadini. Pia wachimbaji wadogo watafundishwa kuhusu uandaaji wa takwimu nataarifa mbalimbali ambazo pamoja na mambomengine zitakazowasaidia kupata mikopokutoka kwenye taasisi za fedha. Vilevile, Wachimbaji Wadogo watapatiwa mafunzo kuhusu tathmini ya mashapo; uongezaji thamani madini; upatikanaji wa taarifa za masoko na utunzaji wa mazingira.

(c) Mnada wa Almasi Shinyanga

59. Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya majadiliano na Kampuni ya Petra Diamond Ltd ili iweze kutenga asilimia 5 ya madini yanayozalishwa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuuzwa katika soko la ndani. Kampuni ya Petra Diamond Ltd iliridhia jambo hilo. Kwa mara ya kwanza mnada wa almasi ulifanyika nchini tarehe 18 hadi 20 Februari, 2020 katika kituo kidogo cha mauzo ya almasi Mwadui. Lengo la mnada huu ni kuhamasisha biashara ya madini ya almasi nchini.

Picha Na. 10: Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Naibu Waziri wa Madini akishuhudia zoezi la uthaminishaji Madini ya Almasi katika Mnada wa Almasi Mwadui - Shinyanga

60. Mheshimiwa Spika, katika mnada huo jumla ya wafanyabiashara wadogo (mineral brokers) 27 walishiriki na kuwasilisha zabuni 122 kwa vifurushi 44 vilivyokuwa sokoni. Kutokana na mnada huo, Serikali ilikusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 39,460,800.29 zilizotokana na mauzo ya

shilingi 155,971,542.63 ya almasi kwa vifurushi 11. Fedha hizo zinatokana na malipo ya mrabaha, ushuru wa huduma na ada ya ukaguzi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wadogo wananufaika na biashara hii ya madini ya almasi na kuimarisha soko la madini Shinyanga.

(d) Uimarishaji wa Taasisi

61. Mheshimiwa Spika, Ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Sekta ya Madini, Serikali ilitoa jumla ya shilingi 10,702,227,000.00 kwa ajili ya ununuzi wa magari 36, XRF, mizani, kompyuta mpakato na *printer* vitakavyosaidia kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa maduhuli na ununuzi wa vifaa vya masoko. Aidha, Chuo cha Madini (MRI) kilijengewa jengo la taaluma. Ujenzi wa jengo hilo uligharimu shilingi 2,721,110,846.74.

(e) Uanzishwaji wa Kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited

62. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha majadiliano na kusaini mkataba (Framework Agreement) na kampuni ya Barrick Gold Corporation tarehe 24 Januari, 2020. Mkataba huo, pamoja na mambo mengine umewezesha kuanzishwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Minerals Corporation Limited* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Serikali (hisa 16%) na Kampuni ya Barrick (hisa 84%). Vilevile, kufuatia kuanzishwa kwa kampuni hiyo Serikali imeshateua wajumbe wa Bodi ikiwa ni hatua ya awali ya kuanza utendaji kazi.



Picha Na. 11 Mhe. Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Tukio la Utiaji Saini wa Mkabata Kati ya Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Barrick wa kuanzishwa kwa Kampuni ya Ubia ya Twiga Minerals Corporation Limited Januari 24, 2020

63. Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa kampuni ya Twiga Minerals Corporation Limited kutaiwezesha Serikali kuwa mbia mwenza katika miradi ya uchimbaji mkubwa wa madini ili kulinda maslahi mapana ya nchi. Ushirika huu unahusisha migodi yote iliyo chini ya Kampuni ya Barrick ambayo ni North Mara Gold Mine Ltd, Bulyanhulu Gold Mine Ltd na Pangea Minerals Ltd (Buzwagi). Hatua hii itaongeza udhibiti zaidi katika shughuli za uzalishaji zinazofanywa na migodi iliyokuwa ikimilikiwa na kampuni ya Barrick Gold Corporation hivyo kuongeza wigo wa mapato kwa Serikali na kufungua milango ya ajira kwa watanzania.

(f) Uzalishaji wa Ajira Katika Sekta ya Madini

64. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini imekuwa ikitoa ajira kwa watanzania katika shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020 inakadiriwa kuwa zaidi ya ajira 1,000,505 zilizalishwa ambapo ajira 190,809 ni ajira za moja kwa moja na 809,696 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

(g) Masuala Mtambuka

65. Mheshimiwa Spika, katika kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kudhibiti Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) Wizara imeendelea kutoa huduma saidizi kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwa kutoa fedha taslimu kwa ajili ya huduma ya lishe bora, madawa na vifaa kinga. Aidha, Wizara imekuwa ikiandaa bonanza mbalimbali za michezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha afya za watumishi na ushirikiano mahali pa kazi. Vilevile, wajumbe 20 wa menejimenti ya Wizara pamoja na kamati ya Uadilifu walipatiwa mafunzo Machi, 2020 kuhusu masuala ya rushwa na athari zake.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kupambana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID – 19) kwa kuhakikisha watumishi na wadau wa Sekta ya Madini wanafuata na kuzingatia ushauri wa kitaalam unaotolewa na Serikali.

(h) Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Baruti

67. Mheshimiwa Spika, Matumizi ya baruti ni muhimu sana katika shughuli za uchimbaji madini na ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Hata hivyo, matumizi ya baruti yasiyozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu yanaweza kusababisha athari kubwa za kiusalama, kiafya na uharibifu wa mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Wizara iliendelea kusimamia na kudhibiti matumizi ya baruti kwa kuhakikisha kuwa watumiaji wa baruti wanaingiza, wanasafirisha, wanatunza na kutumia baruti kwa kufuata Sheria ya Baruti Sura ya 45 na Kanuni zake. Wizara imefanya kaguzi katika maghala 26 ya kuhifadhi baruti katika maeneo ya Lugoba- Pwani, Kilosa -Morogoro, Geita, Ihumwa- Dodoma, Mirerani-Manyara, Rufiji - Pwani na Nzega-Tabora. Ukaguzi huo ulihusu taratibu za ununuzi, usafirishaji, matumizi, utunzaji wa kumbukumbu za baruti na utunzaji wa mazingira kuzunguka maghala ya baruti.

68. Mheshimiwa Spika, katika kipindi rejewa, jumla ya vibali 170 vya kuingiza baruti nchini vilitolewa na leseni 28 za maghala ya kuhifadhia baruti katika maeneo ya Dodoma, Rufiji, Geita, Nzega, Musoma, Mirerani na Mbozi zilitolewa na kibali cha kujenga maghala Buhalahala – Geita kilitolewa. Aidha, jumla ya tani 22,233 za baruti zimetumika migodini na vipande 2,745,018 vya fataki vililingizwa nchini kwa shughuli za ulipuaji kwenye maeneo ya uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

69. Mheshimiwa Spika, ukaguzi ulifanyika pia katika kiwanda cha kutengeneza baruti cha kampuni ya *Nitro Explosive Ltd* kilichopo Kilwa-Lindi. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kujiridhisha na utekelezaji wa Sheria ya Baruti Sura ya 45 na Kanuni zake kwa kampuni hiyo kwa lengo la kutoa kibali cha kutengeneza Baruti. Aidha, ukaguzi wa matumizi ya baruti ulifanyika katika eneo la Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere Hydropower ulioko Bonde la Mto Rufiji kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya baruti.

70. Mheshimiwa Spika, pamoja na wamiliki wengi wa maghala ya baruti kutekeleza wajibu wao, kaguzi zilibaini uwepo wa baadhi ya wamiliki wa maghala kutotunza ipasavyo mazingira kuzunguka maghala yao. Aidha, katika mradi wa ujenzi wa reli ya kati ya kisasa kwa kiwango cha Kimataifa – *Standard Gauge Railway* (SGR) kulikuwa na changamoto ya kutokadiria vizuri matumizi ya baruti kwenda kwenye maeneo ya kazi hivyo kusababisha baruti nyingi kurudi ghalani. Kufuatia changamoto zilizobainika, Wizara iliwataka wadau husika kurekebisha mapungufu hayo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya taratibu za ununuzi, usafirishaji, matumizi, utunzaji wa kumbukumbu za baruti na utunzaji wa mazingira kuzunguka maghala ya baruti. Hivyo, napenda kuwasahi wadau wa baruti kufanya shughuli zao kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia baruti.

(i) Uelimishaji Umma kuhusu Sekta ya Madini Nchini

71. Mheshimiwa Spika, Wizara ilianzisha kampeni ya kuelimisha Umma iliyopewa jina la ‘Madini Yatatutoa’.

Kampeni hiyo ililenga kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sekta ya Madini, kutambua fursa zilizopo na kuzitumia. Aidha, kampeni hiyo ilielezea mafanikio yaliyopatikana kwenye Sekta ya Madini kufuatia Marekebisho ya Sheria ya Madini Sura ya 123. Kampeni iliendeshwa kupitia vipindi mbalimbali vya Redio, Runinga na pia kusambazwa katika Tovuti ya Wizara na mitandao mbalimbali ya kijamii.



Picha Na. 12: Mh. Stanslaus Nyongo Naibu Waziri wa Madini (Kushoto) na Katibu Mkuu wa Madini Prof. Simon Msanjila (kulia) kwa nyakati tofauti wakishiriki katika Kipindi cha Jambo Tanzania (TBC1) ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kuelimisha Umma ya 'Madini Yatatutoa'

72. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Habari - MAELEZO, iliandaa Kipindi Maalum kuonesha Mafanikio ya Uanzishwaji wa Soko la Madini la Chunya na mchango wake katika kukuza uchumi wa eneo hilo. Taarifa kuhusu kipindi hicho zilisambazwa katika mitandao ya kijamii, Magazeti na Vyombo vingine vya habari.

73. Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliratibu ushiriki wa Viongozi Wakuu na Waandamizi wa Wizara katika Vipindi Maalum vya Redio na Runinga. Lengo la vipindi hivyo lilikuwa ni kuelimisha na kutoa ufafanuzi kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya madini. Masuala hayo ni pamoja na: Sheria ya Madini Sura ya 123, wajibu wa wamiliki wa leseni za uchimbaji madini kwa jamii zinazoizunguka migodi (CSR), ushiriki wa nchi na wananchi katika mnyororo wa uchumi wa madini (Local Content). Aidha, elimu kuhusu

aina mbalimbali za leseni za madini, matumizi na faida ya Masoko na Vituo vya kuuzia na kununua madini (Buying Centres) na uwekezaji katika Sekta ya Madini ilitolewa.

(j) Uundwaji wa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Masoko ya Madini

74. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikisha kuundwa kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Masoko ya Madini wa kufuatilia mwenendo wa mauzo. Mafunzo ya matumizi ya mfumo huo yamefanyika kwa wafanyakazi wa masoko ya madini yaliyopo katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Geita, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Lindi, Njombe, Mtwara, Manyara, Songwe, Ruvuma, Kagera na Shinyanga. Mfumo huu ulianza kutumika Januari, 2020. Aidha, mafunzo hayo yanaendelea katika mikoa mingine iliyobaki. Miongoni mwa taarifa zinazopatikana mubashara kupitia mfumo huo ni kiasi cha madini yaliyofika sokoni, mauzo, bei na maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa kupitia mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Mfumo huo unasaidia katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati za mauzo. Mfumo huo umebuniwa na kutengenezwa na wataalam wetu wa ndani hivyo kuepuka gharama zisizo za lazima kwa kutumia wataalam kutoka nje. Mfumo huo unapatikana kupitia kikoa kidogo cha <https://masoko.madini.go.tz>.

(k) Kuimarisha Ulinzi Eneo Tengefu la Mirerani

75. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Pamoja (One Stop Centre) ndani ya ukuta wa Mirerani. Aidha, ufungaji wa miundombinu ya umeme na taa umekamilika na ufungaji wa kamera za ulinzi (CCTV) kuzunguka eneo la ukuta wa migodi ya madini ya tanzanite upo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa, shughuli zote zinazohusu biashara ya madini ya tanzanite zinafanyika ndani ya ukuta. Hatua hii itaimarisha upatikanaji wa takwimu, kudhibiti utoroshaji wa madini ya tanzanite na kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.



Picha Na. 13: Muonekano wa Mfumo wa Ulinzi wa CCTV kamera, Jengo la Kituo cha Pamoja na Ukuta Kuzunguka machimbo ya Tanzanite Mirerani – Manyara

76. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa ukuta umesababisha kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali kwa takribani mara 13 ya kiwango kilichokuwa kikikusanywa awali. Kwa mfano, katika mwaka 2019 makusanyo yaliongezeka na kufikia shilingi 2,150,000,000 ikilinganishwa na shilingi 166,094,043 zilizokusanywa mwaka 2017 kabla ya ujenzi wa ukuta.

(I) Shughuli za Kiutawala na Kiutumishi

77. Mheshimiwa Spika, Wizara na Taasisi zake imepokea jumla ya watumishi 220 kwa utaratibu wa ajira mpya, ajira mbadala na uhamisho kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali. Kati ya hao, watumishi 16 walijajiriwa Wizarani, 188 Tume ya Madini, wanne (4) STAMICO, wanane (8) GST, wawili (2) Chuo cha Madini (MRI) na wawili (2) Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC). Kupatikana kwa watumishi hao kumepunguza changamoto ya upungufu wa watumishi hivyo, kusaidia Wizara na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu yake.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA MADINI

78. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini inasimamia taasisi sita (6) ambazo ni: Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI); Chuo cha Madini (MRI); na Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC).

i. Tume ya Madini

79. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123, ikiwa na majukumu mbalimbali ikiwemo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini; kuimarisha ukaguzi wa masuala ya usalama, afya, mazingira, uzalishaji na biashara ya madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa; kudhibiti utoroshaji wa madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini.

(a) Uzalishaji na Ukusanyaji wa Maduhuli

80. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi kinachoanzia mwezi Julai, 2019 hadi Februari, 2020 jumla ya kilo 25,435.12 za dhahabu zenye thamani ya shilingi 2,772,331,030,317.99 zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika Migodi Mikubwa na ya Kati. Migodi hiyo ni pamoja na Geita Gold Mine, North Mara Gold Mine, Pangea Minerals (Buzwagi Mine), Bulyanhulu Gold Mine, Shanta Mine (New Luika), STAMIGOLD Company (Biharamulo Mine) na Busolwa Gold Mine (Tanzania). Aidha, katika kipindi hicho kilo 10,102.43 za dhahabu zenye thamani ya Shilingi 975,430,320,903.97 zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa madini.

81. Mheshimiwa Spika, katika kipindi tajwa kiasi cha karati 201,547.71 za madini ya almasi yenye thamani ya shilingi 84,377,839,160.40 yalizalishwa katika Migodi wa almasi wa Mwadui (Williamson Diamond Limited),

na karati 8,680.05 zenye thamani ya shilingi 5,472,619,953.21 zilizalishwa na wachimbaji wadogo wa almasi. Aidha, wachimbaji wadogo wa madini ya tanzanite wamezalisha tanzanite ghafi kiasi cha kilogramu 3,798.70; tanzanite zilizokatwa na kusanifiwa ni kiasi cha karati 95,104.50; kiasi cha kilogramu 26,343.86 ni cha madini ya tanzanite yenye ubora wa chini (Beads); na madini mengine ya vito kiasi cha tani 1,120 kilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

82. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makaa ya mawe, jumla ya tani 430,761.32 zilizalishwa kwenye Mgodu wa Ngaka na Kambas Mining Investment Mkoa wa Ruvuma; tani 9,908.43 katika Mgodu wa Kabulo – Songwe; na tani 2,733.19 katika Mgodu wa Edenville – Sumbawanga-Rukwa.

Aidha, tani 22,036,068.64 za madini ya ujenzi na tani 951,906.57 za madini mengine ya viwandani zilizalishwa katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, tani 7,046 za madini ya kinywe (Graphite) zilizalishwa kutoka katika Mgodu wa GodMwanga Mirerani.

83. Mheshimiwa Spika, kutokana na uzalishaji wa madini mbalimbali nchini, hadi kufikia Machi, 2020 Tume ya Madini ilikusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 358,643,870,797 sawa na asilimia 102 ya lengo la shilingi 352,765,797,750 kwa kipindi hicho. Makusanyo hayo yalitokana na malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi, ada ya pango ya mwaka, ada za kijiolojia, faini mbalimbali na mapato mengineyo.

(b) Utoaji wa Leseni

84. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Tume ya Madini ilitoa jumla ya Leseni 5,935 za madini kwa mchanganuo ufuatao: Leseni 13 za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs); Leseni 102 za Utafutaji wa Madini (PLs); Leseni 2,801 za Uchimbaji Mdogo (PMLs); Leseni kubwa 601 za biashara (DL); Leseni ndogo 2,376 za biashara (BL);

Leseni 38 za Uchenjuaji wa Madini (PCLs); Leseni 2 za Usafishaji wa Madini (RFL); na Leseni 2 za uyeuyushaji Madini (SL).

85. Mheshimiwa Spika, kati ya leseni zilizotolewa, asilimia 47.20 ni za wachimbaji wadogo. Hii inadhihirisha kuwa Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa kipaumbele kwa Watanzania kushiriki ipasavyo katika Sekta ya Madini ili wanufaike na rasilimali hizi ambazo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu.

(c) Ukusanyaji wa Maduhuli kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Serikali (GePG)

86. Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelekezwa na Serikali, Tume ya Madini iliendelea kutumia mfumo wa GePG katika Ukusanyaji wa Maduhuli. Kupitia mfumo huo, Tume ina uwezo wa kupata taarifa za makusanyo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mrabaha na tozo mbalimbali za madini kwa wakati. Mfumo huo pia umeondoa changamoto zilizokuwa zikiambatana na matumizi ya risiti za ERVs zikiwamo upatikanaji kwa wakati kwa vitabu hivyo na muda unaotumiwa na wateja kulipa na kufuatilia risiti hizo.

(d) Ukaguzi wa Migodi

87. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Madini iliendelea na utekelezaji wa jukumu la ukaguzi wa migodi ambalo ni muhimu katika Sekta ya Madini. Lengo la kaguzi hizo ni kuangalia jinsi migodi inavyotekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali za Madini na Mazingira. Kaguzi zilifanyika katika Migodi ya wachimbaji wakubwa, wa kati na wadogo. Kaguzi hizo zilihusisha migodi ya wachimbaji wakubwa ikiwemo Mgodu wa Dhahabu wa Buzwagi; Mgodu wa Dhahabu wa Bulyanhulu; Mgodu wa Dhahabu wa North Mara; Mgodu wa Dhahabu wa Geita na Mgodu wa almasi wa Mwadui (WDL).



Picha Na. 14: Timu ya Wakaguzi ikiwa katika Ukaguzi wa Mgodi

88. Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo pia ulifanyika katika migodi ya wachimbaji wa kati ikiwemo ya Nsoromero Minerals Co-operative Society Ltd; Mara Mine Development Ltd; Nyamongo (T) Ltd; Nyamongo Gold Mine Ltd; P.Z. Gold Mining Co. Ltd; MMG Gold Ltd; CATA Mining Co. Ltd; Perfalbion Minerals Ltd; ZEM (T) Co. Ltd; Sunshine Ltd; na Zem Development Co. LTD.

89. Mheshimiwa Spika, kaguzi hizi zilifanyika pia kwenye migodi zaidi ya 100 ya wachimbaji wadogokatika maeneo yenye shughuli za uchimbaji madini nchini. Ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Manyara, Geita, Kagera, Shinyanga, Singida na Tabora.


90. Mheshimiwa Spika, matokeo ya kaguzi hizi yalibaini kufanyiwa kazi kwa mapungufu yaliyoonekana katika kaguzi zilizotangulia. Hata hivyo, kaguzi zilibaini kuendelea kuwepo kwa mapungufu kadhaa ikiwemo uendeshaji wa shughuli za madini usiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu hususan zinazohusiana na utunzaji wa mazingira. Migodi ilielekezwa kufanya marekebisha katika mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kaguzi hizo.

ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

91. Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ni kufanya tafiti za jiosayansi na ugani wa jiolojia kwa lengo la kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia tafiti hizi taarifa mbalimbali za jiosayansi za uwepo wa madini nchini zinaandaliwa ili kuhamasisha uwekezaji katika utafiti wa kina (detailed exploration) kwa lengo la kuanzisha migodi mipya. Aidha, taarifa hizi za jiosayansi zinatumiwa katika sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, maji, ujenzi, na mipango miji. Vilevile, GST ina jukumu la kuratibu majanga ya asili ya jiolojia kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkano, kemikali hatarishi pamoja na maporomoko ya udongo.

(a) Ugani/Utafiti wa Jiosayansi na Uboreshaji Ramani za Jiolojia na Upatikanaji wa Madini

92. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, GST iliendelea kufanya ugani/utafiti wa jiosayansi na kuboresha ramani za jiolojia na taarifa za upatikanaji wa madini. Katika utafiti huo, GST ilikamilisha ugani wa jiolojia na jiokemia katika QDS 293 iliyohusisha Kata za Kibutuka, Chiola, Kipara Mnero, Lionja, Marambo, Mkoka, Mkotokuyana, Mnero, Mnero-ngongo, Mpiruka, Mtua, Naipingo, Namapwia, Namatula, Nambambo, Namikango, Nangowe, Nditi, Ruponda, Chienjere, Likunja, Luchelegwa, Makanjiro, Mandarawe, Mbekenyerera, Mnacho, Narungombe, Nkowe, katika wilaya ya Nachingwea na Ruangwa mkoa wa Lindi. Ramani pamoja na maelezo yake zipo katika hatua ya kuhaririwa kwa ajili ya uchapishwaji. Matokeo ya awali ya utafiti huo yalionesha kuwa katika QDS 293 kuna madini ya kinywe (graphite) yenye ubora mkubwa (flake graphite) na viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu.



Picha Na. 15: *Wajiolojia wakichunguza na kukusanya takwimu kuhusu miamba katika eneo la QDS 293 lililopo Nachingwea mkoani Lindi*

93. Mheshimiwa Spika, GST ilikamilisha uhakiki (field checks) wa ramani za jiolojia katika QDS tano (5) ambazo ni 267 na 268 zilizopo Mkoa wa Lindi, 160, 121, na 122 zilizopo Mkoa wa Singida. Ramani pamoja na maelezo yake (explanatory notes) kwa QDS 267, 268 na 160 zimekamiliwa na kuchapishwa. Ramani za QDS 121 na 122 zipo katika hatua za kuhaririwa (editing) ili ziweze kuchapishwa. QDS 121 na 122 zina viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu na shaba. Uchunguzi wa sampuli katika maeneo mengine bado unaendelea.

94. Mheshimiwa Spika, GST kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilikamilisha utafiti wa jiolojia na uchoraji wa ramani katika QDS nne (4) ambazo ni QDS 38, 39, 52 na 53 zenye jumla ya kilomita za mraba 11,664. Ramani maalum inayoonesha maeneo mapya ya utalii wa jiolojia (geosites) ilichorwa na taarifa ya maelezo ya kina ya *geosite* hizo imeandaliwa. Vivutio hivyo ni *Embulbul depression* lililosababishwa na bonde kuu la ufala Afrika Mashariki; *Moving Sand* - mchanga ambao unasadikiwa kwamba huwa unatembea; *Engaresero gorge* – eneo lenye maporomoko ya maji ambalo limekuwa kivutio kikubwa cha

watalii; *Nasera rock* - jiwe kubwa la kuvutia lililotokana na kupanda kwa magma iliyobeba mchanganyiko wa chembechembe za madini na kisha ukapoa na kutengeneza jabali kubwa la mwamba juu ya uso wa ardhi.

(b) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za Jiosayansi

95. Mheshimiwa Spika, GST imefanya tafiti za jiolojia na kutoa mrejesho wa tafiti hizo kwa wachimbaji wadogo. Baada ya kukamilika kwa tafiti hizo mafunzo juu ya namna bora ya kutambua miamba yenye mashapo na kuchenjua madini yalitolewa kwa wachimbaji wadogo 180. Mafunzo hayo yalitolewa katika maeneo ya Muhintiri na Mang'onyi mkoa wa Singida pamoja na Musasa na Matabe Wilaya ya Chato. Maeneo mengine ni Foresti Wilaya ya Bukombe na Mgusu Wilaya ya Geita. Lengo la tafiti hizo ilikuwa kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi kuhusu mashapo. Taarifa hizo zitasaidia kuongeza uzalishaji na hatimaye kuongeza kipato na kuboresha maisha ya wachimbaji wadogo.

96. Mheshimiwa Spika, utafiti mwingine ulifanyika katika eneo la wachimbaji wadogo Nholi Mkoa wa Dodoma ili kubaini namna bora ya kuchenjua madini ya dhahabu kutoka kwenye mbale. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa: mbale iliyopo maeneo ya Nholi ina dhahabu kiasi cha wastani wa gramu 1.98 kwa kila tani moja ya mbale; wachimbaji wadogo wanapata dhahabu kutoka kwenye mbale kwa kiwango cha asilimia 70 tu baada ya kuchenjua kwa kutumia zebaki. Utafiti ulifanywa kwa njia ya kuoza sampuli kwa kutumia sayanai na matokeo yake yalionesha kuwa, upatikanaji wa dhahabu kutoka katika mbale uliongezeka kutoka asilimia 70 hadi 87. Hata hivyo, utafiti unaendelea ili kubaini njia bora zaidi ya kuchenjua dhahabu ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wachimbaji wadogo. Nitoe rai kwa wachimbaji wadogo kuitumia Taasisi ya GST katika kutambua tabia za mbale za eneo husika ili kuweza kutumia njia sahihi ya uchenjuaji kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji.

(c) Tafiti Maalum za Jiosayansi

97. Mheshimiwa Spika, tafiti maalum za jiosayansi ni tafiti ambazo zinafanywa kutatua changamoto zilizojitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mfano kwenye maeneo mapya yaliyogundulika/kusadikika kuwa na madini na kuvamiwa na Wachimbaji (mineral rush); kuhitaji taarifa zaidi za jiosayansi kwenye eneo maalum; na maagizo au maombi kutoka kwa viongozi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla.

98. Mheshimiwa Spika, GST ilifanya tafiti katika eneo la Mradi wa Ufuaji Umeme wa Bonde la Rufiji (Julius Nyerere Hydropower Project) kwa lengo la kubaini uwezekano wa uwepo wa Makaa ya Mawe. Uchunguzi ulifanyika katika maeneo ya uchorongaji na uandaaji wa mifereji ya uchepushaji wa maji ikiwa ni pamoja na sehemu ya *inlet tunnel, outlet tunnel, adit* pamoja na kukusanya taarifa za jiolojia za sampuli za miamba choronge (rock cores). Uchunguzi huo ulithibitisha kutokuwepo kwa makaa ya mawe katika eneo lililofanyiwa utafiti. Wizara itaendelea kupeleka wataalam katika maeneo ya miradi mbalimbali inayohusisha uchorongaji wa miamba ili kuweza kubaini uwepo wa madini katika maeneo hayo.

99. Mheshimiwa Spika, Utafiti wa pili ulifanyika na kukamilika katika eneo la Lukwika wilaya ya Nanyumbu na kubaini uwepo wa madini ya dhahabu. Aidha, utafiti mwingine ulifanyika katika eneo la Kisisi Godegode na maeneo mengine katika Wilaya za Mpwapwa na Kilosa ambako ujenzi wa SGR unafanyika ili kubaini uwepo wa madini. Uchunguzi ulikamilika na kubaini kuwepo kwa miamba iliyobeba madini ya *ruby-corundum* na *red garnet* ambapo madini hayo hayakuwa na ubora wa kukidhi kuwa vito vya thamani. Pia, ili kuhakikisha Serikali inapata taarifa sahihi kuhusu uwepo ama kutokuwepo kwa rasilimali madini katika maeneo mbalimbali ya mradi wa SGR. Wizara imepeleka mtaalamu wa jiosayansi ambaye atakuwa anakusanya taarifa za jiolojia ili kubaini kama kuna madini ya thamani kubwa katika eneo la mradi husika.



Picha Na. 16. *Katibu Mkuu Wizara ya Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilano (Uchukuzi) wakiwa katika ziara ya kukagua uwepo wa madini katika eneo la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).*

(d) Kuboresha huduma za Maabara kwa wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi

100. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa GST inaendelea kutoa huduma za maabara zinazokidhi viwango vya kimataifa, maboresho ya mifumo ya uendeshaji yalifanyika. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kupitia ukaguzi uliofanywa na taasisi ya SADCAS inayosimamia ubora wa huduma za maabara katika Ukanda wa SADC, maabara ya GST ilikidhi vigezo vya kimataifa katika uchunguzi wa madini ya dhahabu. Hatua hii iliwezesha GST kupata ITHIBATI ya kimataifa ya uchunguzi wa sampuli za dhahabu kwa njia ya tanuru (fire assay) na kupewa ISO: 17025 tarehe 15 Oktoba, 2019.



Picha Na. 17: Wataalam wa Maabara ya GST Wakifanya Uchunguzi wa Sampuli

101. Mheshimiwa Spika, jukumu lingine la GST ni kufanya uchunguzi wa sampuli za wateja na ambazo zinahitaji vibali kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya sampuli 6,167 zilifanyiwa uchunguzi. Kati ya hizo, sampuli 5,596 zilikuwa za wateja na sampuli 572 kwa ajili ya kupata vibali vya kusafirisha kwenda nje ya nchi. Aidha, jumla ya vyungu vikubwa vya kuyeyushia sampuli za dhahabu (crucibles) 2,869 na vyungu vidogo (Cupels) 2,011 vilizalishwa.



Picha Na. 18: Vyungu vya kuyeyushia dhahabu (crucibles) na Cupels mara baada ya kutengenezwa katika maabara ya GST

(e) Kuboreshwa kwa Kanzi data ya Jiosayansi

102. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili, kampuni nane (8) zinazojihusisha nashughuli za madini kutoka Mikoa ya Mtwara na Lindi zilitembelewa kwa ajili ya kukusanya taarifa, kukagua mawe choronge (cores) zilizopo pamoja na kuzikumbusha wajibu na utaratibu wa kisheria wa uwasilishwaji wa taarifa/takwimu GST. Aidha, GST ilishiriki mashindano ya uchakataji wa picha za satelaiti (remote sensing data processing) yaliyofanyika nchini Botswana. Mashindano hayo yalilenga kuainisha maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuwa na madini kwa ufuatiliaji zaidi. Mashindano hayo yaliyohusisha nchi 12 za SADC. Katika mashindano hayo, GST ilishika nafasi ya nne na mwakilishi wake aliweza kutunukiwa cheti cha kuwa mkufunzi kwa nchi za Kusini mwa Afrika na kufanya idadi ya wakufunzi kutoka Tanzania kufikia wanne (4). Hii imeendelea kudhihirisha umahiri wa wataalam wetu wa ndani katika masuala ya uchakataji wa takwimu na taarifa za jiosayansi.

(f) Kukabiliana na Majanga ya Asili ya Jiolojia

103. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na majanga ya asili ya jiolojia na kutoa ushauri wa namna bora ya kupunguza madhara yanayoweza kutokana na majanga hayo, GST ilikusanya takwimu za matetemeko ya ardhi kutoka katika vituo vya kuratibu matetemeko ya ardhi vya Mtwara, Arusha, Mbeya, Geita na Dodoma. Takwimu zilichakatwa na kubaini kuwepo kwa matetemeko ya ardhi yaliyotokea kwa nyakati tofauti katika maeneo ya Kijiji cha Ngulu Mkoa wa Tabora, Nala na Haneti Mkoa wa Dodoma, Naberera Mkoa wa Manyara na Kijiji cha Sibwesa Mkoa wa Katavi. Matetemeko hayo yalikuwa na ukubwa wa kati ya 2.7 na 5.5 katika kipimo cha *Richter*. Taarifa za matetemeko hayo ya ardhi ziliandaliwa na kusambazwa kwa mamlaka husika na vyombo vya habari kwa lengo la kutoa tahadhari na kuelimisha jamii.

104. Mheshimiwa Spika, GST ilikamilisha uchunguzi kuhusu tukio lililosadikiwa kuwa ni volkano katika Kata ya Ndembezi

Manispaa ya Mji wa Shinyanga. Uchunguzi ulibaini kwamba kulikuwa na tabaka la tope lililochanganyika na maji ambalo lilibubujika na kusukumwa kuja juu ya uso wa ardhi. Tukio hilo kitaalam huitwa *Liquefaction* na siyo volkano. Baada ya uchunguzi huo GST ilitoa taarifa kwa uongozi wa eneo husika ikiwa ni pamoja na uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Shinyanga na kwa wananchi kwa ujumla kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kuwatoa wasiwasi juu ya tukio hilo.

105. Mheshimiwa Spika, GST ilikamilisha uchunguzi kuhusu tukio lililotokea tarehe 11 Desemba, 2019 la kusadikiwa kuwepo kwa tukio la volkano katika kitongoji cha Sang'ombe Kijiji cha Tatwe, Kata ya Gulibe Wilayani Rorya katika Mkoa wa Mara. Matokeo ya uchunguzi yalibaini kuwa tukio hilo lilikuwa ni maporomoko ya ardhi (landslide) yaliyosababishwa na kuwepo kwa mvua nyingi. GST ilitoa taarifa ya tukio hilo kwa wananchi wa kijiji cha Tatwe na kwa uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Mara na kwa Taifa kwa ujumla kupitia vyombo vya habari.

iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

106. Mheshimiwa Spika, majukumu makuu ya STAMICO baada ya maboresho ya hati ya uanzishwaji wake kupitia Gazeti la Serikali (GN)171 ya mwaka 2015 ni pamoja na: kuwekeza kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji, na uchenjuaji wa madini; kutoa huduma za kibiashara za uchorongaji miamba; utafutaji wa madini; kutoa ushauri elekezi wa masuala ya mazingira pamoja na kuratibu uendelezaji wa wachimbaji wadogo nchini kwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa wachimbaji hao.

107. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Shirika lilikukusanya kiasi cha shilingi 4,125,871,300.34 sawa na asilimia 113 ya lengo la makusanyo ya shilingi 3,663,954,619.00 katika kipindi husika. Makusanyo hayo yalitokana na vyanzo vya ndani vya Shirika.

(a) Uwekezaji katika Shughuli za Utafutaji, Uchimbaji, Uchenjuaji wa Madini

108. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa shughuli za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini nchini, miongoni mwa miradi iliyotekelezwa na Shirika ni kama ifuatavyo:

Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kabulo/Kiwira

109. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea na uchimbaji wa makaa ya mawe katika kilima cha Kabulo kilichopo eneo la Kiwira, Mkoani Songwe. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Shirika lilizalisha jumla ya tani 9,908.43 za makaa ya mawe ambapo kati ya hizo tani 4,419.10 ziliuzwa. Kutokana na mauzo hayo Shirika lilipata kiasi cha shilingi 271,642,828.65 na kulipa serikalini kiasi cha shilingi 30,825,217.98 kama mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Aidha, ili kuongeza mapato, STAMICO imeingia Mkataba na Mbeya Cement Company Ltd ili kuwauzia makaa ya mawe. Kadhalika, Shirika lipo kwenye hatua za mwisho za makubaliano na kiwanda cha Sunflag Tanzania Ltd kilichopo Arusha ili kuweza kuwauzia makaa ya mawe.

Mgodi wa Dhahabu wa STAMIGOLD

110. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya STAMIGOLD ambayo ni kampuni Tanzu ya STAMICO kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 imeweza kuzalisha na kuuza wakia 9107.45 za madini ya dhahabu na wakia 1,170.21 za madini ya fedha, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 31,539,991,237.11. Mgodi umelipa jumla ya shilingi 2,303,564,360.31 kwa ajili ya malipo ya mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Aidha, mgodi umeanza kuuza dhahabu inayozalisha kwenye masoko ya ndani ya madini. Hatua hii imekoa gharama ya usafirishaji kiasi cha shilingi milioni 131.8 kama dhahabu ingeuzwa nje ya nchi.



Picha Na. 19: Mtambo wa kuchenjua dhahabu katika Mgoji wa STAMIGOLD

Mradi wa kusafisha dhahabu wa Mwanza

111. Mheshimiwa spika, Shirika limeanza ujenzi wa mradi wa kusafisha dhahabu (gold refinery) jijini Mwanza. Mradi huo wa ubia unatarajiwa kukamilika Desemba, 2020 na kwa kuanzia utakuwa na uwezo wa kusafisha dhahabu wastani wa kilo 480 kwa siku. Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Marekani milioni 58.204. Kwa sasa kampuni ya ubia imeashanzishwa kwa jina la *Mwanza Precious Metals Refinery*. Ujenzi wa mtambo huu wa kusafisha dhahabu wenye teknolojia ya kisasa utasafisha dhahabu mpaka kufikia kiwango cha 999.9 *purity* unatarajiwa utaongeza mapato ya nchi kupitia mrabaha na tozo mbalimbali pamoja na kuongeza ubora wa dhahabu ya Tanzania kimataifa.



Picha Na. 20: Mchoro Wa Kitakachokuwa Kiwanda Cha Kusafisha Dhahabu Jijini Mwanza

Mradi wa Dhahabu wa Buhemba

112. Mheshimiwa spika, Shirika pia limeanza utekelezaji wa mradi wa kuchimba dhahabu wa Buhemba ambao makadirio ya gharama za awali za mradi huo ni Dola za Marekani milioni 24. Kwa sasa taratibu za kuagiza mtambo wa kuchenjua dhahabu zinaendelea baada ya majibu ya sampuli kupatikana kutoka katika maabara za nje na ndani ya nchi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Desemba, 2020.

(b) Uendelezaji wa Leseni za Shirika

113. Mheshimiwa Spika Shirika limeendelea kufanya utafiti wa leseni zake ili liweze kuziendeleza. Aidha, katika kipindi rejewa, Shirika pia limeweza kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Kampuni ya Madini ya kutoka nchi ya Indonesia PT TIMAH ili kuendeleza leseni za Shirika. Katika kuanza kutekeleza makubaliano hayo timu ya wataalamu wa Kampuni ya PT TIMAH pamoja na wataalamu wa Shirika wameshapitia maeneo ya leseni za Shirika ili kuainisha leseni za kuanza kuziendeleza.

(c) Huduma za Uchorongaji

114. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Shirika limeendelea kutoa huduma za kibiashara za uchorongaji miamba katika Sekta ya Madini na Mafuta. Shirika limefanikiwa kupata kandarasi nne za uchorongaji. Kati ya hizo, kandarasi 3 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.99 zimekamilika. Aidha, katika jitihada za kuimarisha shughuli za uchorongaji Shirika limeweza kutangaza shughuli zake za uchorongaji katika makampuni mbalimbali ya madini nchini. Kwa sasa Shirika lipo katika mazungumzo na Migodi mikubwa na ya kati kwa lengo la kupata kandarasi za uchorongaji. Napenda kutoa rai hususan kwa wachimbaji wadogo kutosita kuwasiliana na STAMICO pale wanapohitaji huduma hiyo.



Picha Na. 21: Wataalam wa STAMICO wakiwa katika Shughuli za Uchorongaji

115. Mheshimiwa spika, kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho, Shirika linatarajia kuchangia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kiasi cha shilingi bilioni 1.1 katika mfuko wa Serikali. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa huu ni mwanzo tu, kutokana na maboresho yanayoendelea ya kimuundo pamoja na usimamizi wa karibu wa Shirika, tija zaidi itaendelea kuonekana.

(d) Huduma kwa Wachimbaji wadogo

116. Mheshimiwa Spika, Shirika linaendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Katika kipindi cha Mwaka wa

Fedha 2019/2020 Shirika limekamilisha usimamizi wa ujenzi wa Vituo vya Mfano kwa wachimbaji wadogo katika maeneo ya Katente na Lwamgasa ambavyo kwa sasa vipo katika uzalishaji wa majaribio. Aidha, Kituo cha Itumbi kipo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Vituo hivyo vitatoa mafunzo ya vitendo katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa wachimbaji wadogo.

117. Mheshimiwa Spika, Shirika limewezesha vikundi vitano (5) vya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Singida, Kilindi na Morogoro kuelewa jiolojia ya maeneo yao ili kuweza kuainisha maeneo ya kuchimba na kupanga namna bora ya uchimbaji katika maeneo hayo. Vilevile, Shirika lilishirikiana na Chama cha Wachimba Madini Mkoa wa Geita, na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo zaidi ya 950 kuhusu upatikanaji wa leseni za uchimbaji mdogo, uchimbaji salama na uchenjuaji yaliyofanyika katika wilaya zote za Mkoa wa Geita.

iv. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

118. Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya TEITI ni kuimarisha na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, Desemba, 2019 TEITI iliweka wazi kwa umma Ripoti ya Ulinganishi wa Malipo ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Mapato ya Serikali kwa Mwaka 2016/2017. Ripoti hiyo imeonesha kuwa Serikali ilipokea shilingi 441,831,277,513.46 kutoka katika Kampuni 22 za Madini, Mafuta na Gesi Asilia zilizoingia katika zoezi la ulinganishi. Aidha, TEITI inatarajia kukamilisha ripoti ya ulinganishi wa malipo ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Mapato ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 kabla ya Julai, 2020.

119. Mheshimiwa Spika, ripoti ya nane (8) ya TEITI ya mwaka 2015/2016 ilionesha tofauti ya shilingi bilioni 30 kati ya mapato na malipo yaliyopokelewa kutoka Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia zilizofanyiwa ulinganishi. Kwa

mujibu wa Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015 ripoti hiyo inatakiwa kuwasilishwa Ofisi ya CAG kwa ukaguzi maalum. Baada ya Ukaguzi huo, Ofisi ya CAG iliwasilisha ripoti ya ukaguzi wa tofauti hiyo Wizarani na kwa Kamati ya TEITI, Novemba, 2019. Ripoti hiyo ilionesha kuwa, asilimia 90 ya tofauti imehakikiwa na kusuluhishwa.

120. Mheshimiwa Spika, Matokeo ya ukaguzi wa tofauti iliyojitokeza katika ripoti ya nane (8) ya TEITI ilisababishwa na makosa katika kutoa takwimu, kushindwa kuainisha malipo na mapatokwa usahihi na utofauti katika viwango vya kubadilisha fedha. Wakati Wizara inaendelea kufanyia kazi tofauti iliyobaki, nitoe rai kwa Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, na Taasisi za Serikali zinazohusika, kutunza nyaraka na takwimu zao kwa umakini na weledi mkubwa ili kuepusha kutokea kwa tofauti siku zijazo.

121. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Kifungu cha 16(1) (b) cha Sheria ya TEITA 2015, tarehe 31 Desemba, 2019 TEITI iliweka wazi taarifa za wamiliki wa hisa za kampuni 37 za Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika Tovuti ya TEITI. Lengo la kuweka wazi taarifa hizo ni: Kuimarisha uwazi katika umiliki wa Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; na kupunguza mianya ya rushwa pamoja na ukwepaji wa kodi. Kazi hii ni utekelezaji wa ahadi ya Serikali iliyotolewa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa mapambano dhidi ya rushwa uliofanyika London Mei, 2016 (London Anti-Corruption Summit). Aidha, hatua inayofuata kwa sasa ni uanzishaji wa rejesta itakayoweka wazi taarifa za wamiliki wa hisa katika kampuni hapa nchini.

122. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi ya takwimu zinazopatikana katika ripoti za TEITI pamoja na kuitangaza TEITI na majukumu yake, TEITI iliendesha vipindi kupitia vituo vya runinga vya TBC, Channel ten na Azam. Vipindi hivyo vililenga kuhamasisha matumizi ya takwimu zinazotolewa na kuibua mijadala kwa ajili ya kuboresha na kuhamasisha uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

v. Chuo cha Madini

123. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini ni Taasisi chini ya Wizara ya Madini yenye jukumu la kutoa mafunzo ya Ufundi Mchundo (Technicians) kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (Diploma). Chuo kina kampasi mbili za Dodoma na Nzega. Mafunzo yanayotolewa ni ya muda mrefu, mfupi na mafunzo maalum yanayoandaliwa kulingana na mahitaji ya wadau (tailor made courses).

124. Mheshimiwa Spika, kozi zinazofundishwa katika Chuo cha Madini ni pamoja na: Jiolojia na Utafutaji wa Madini; Sayansi za mafuta na Gesi; Uhandisi Uchimbaji Madini; Uhandisi Uchenjuaji Madini; Uhandisi na Usimamizi wa mazingira Migodini; na Upimaji Ardhi na Migodi. Mafunzo hayo yanatolewa kwa njia ya umahiri (Competency Based Education Training). Katika kipindi rejewa Chuo kimetekeleza majukumu yafuatayo: -

(a) Kutoa Mafunzo ya Kada ya Ufundi Mchundo Katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

125. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa masomo wa 2019/2020, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 548 waliodahiliwa katika fani za Madini, Mafuta na Gesi asilia. Wanafunzi 85 wamedahiliwa katika fani ya Jiolojia na Utafutaji madini; 98 katika Uhandisi Uchimbaji Madini; 115 katika Uhandisi Uchenjuaji Madini; 42 katika Uhandisi na Usimamizi wa mazingira Migodini; 72 katika Sayansi za Mafuta na Gesi; na 136 katika Upimaji wa Ardhi na Migodi. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 70 kutoka katika migodi mikubwa, midogo na Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi katika fani za uchorongaji na ulipuaji wa miamba, uchenjuaji na utafutaji wa madini.

126. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Masomo 2019/2020, jumla ya wanafunzi 100 wamehitimu mafunzo katika fani mbalimbali kwa ngazi ya Stashahada (Diploma).



Picha Na. 22: Wanafunzi wa Chuo cha Madini wakifanya mafunzo kwa vitendo mgodini.

(b) Kufanya Tafiti na Kutoa Ushauri Elekezi

127. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kuboresha namna ya kufanya tafiti na utoaji wa ushauri elekezi. Katika maboresho hayo, Chuo kimekamilisha Sera ya Chuo ya Utafiti na Ushauri Elekezi; na Mwongozo wa Mafunzo ya Uchorongaji na Ulipuaji wa Miamba pamoja na k u w a w e z e s h a Wakufunzi Wahandisi kufanya usajili katika Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB).

(c) Kuboresha Miundombinu ya Chuo cha Madini Kampasi ya Dodoma na Nzega

128. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi, 2020 Chuo kimeboresha miundombinu na mazingira ya kujifunzia kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la taaluma katika Kampasi ya Dodoma na kufanya ukarabati wa majengo, mifumo ya umeme, maji safi na maji taka katika Kampasi zote mbili. Maeneo yaliyokarabatiwa ni pamoja na madarasa, mabweni, nyumba za watumishi na ofisi. Aidha, Chuo kimeendelea kuimarisha utoaji wa huduma zake kwa kuongeza vifaa vya kufundishia na vya ofisi.

(d) Kuwajengea Uwezo Watumishi

129. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Chuo kwa kushirikiana na Wizara kimewezesha watumishi ishirini (20) wa kada mbalimbali kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi. Watumishi kumi na sita

(16) wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, Chuo kimefanikiwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mfupi ya kujiandaa kustaafu watumishi wake 4.

(e) Ukusanyaji wa Maduhuli

130. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2019/2020, Chuo kilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 532,610,000.00. Hadi kufikia Machi, 2020, Chuo kilikuwa kimekusanya jumla ya shilingi 225,380,000.00 sawa na asilimia 70.5 ya lengo kwa kipindi husika. Makusanyo haya yalitokana na ada ya mafunzo, usajili na malazi.

(f) Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

131. Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara kubaini uwepo wa changamoto za kitaaluma katika Chuo cha Madini, iliona kuna uhitaji wa Chuo hicho kulelewa na Chuo Kikuu chenye uzoefu wa kufanya ulezi wa vyuo vya namna hii hapa nchini. Lengo la Wizara kuomba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukilea Chuo cha Madini ni pamoja na: Kuongeza nafasi za udahili katika Chuo cha Madini; kukiwezesha Chuo cha Madini kuendesha programu zinazoendanana uhitaji wa soko la ajira; kuongeza ufanisi katika maeneo muhimu ya utafiti na uchapishaji; na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na Chuo cha Madini.



Picha Na.23: Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa pamoja wakitia saini hati ya makubaliano (MoU) kuhusu Chuo cha Madini kulelewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

132. Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, hati ya makubaliano kati ya Wizara na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya namna ya kukilea Chuo imekamilika na kusainiwa. Kwa sasa hatua inayofuata ni ukamilishwaji wa Sheria ya kuanzishwa kwa Chuo, Muundo pamoja na Miundo ya Kiutumishi.

vi. Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC)

133. Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC) ni pamoja na: kutoa mafunzo kwa ngazi ya Cheti na Stashahada (Diploma) katika fani ya teknolojia ya madini na usonara (gem and jewellery technology); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za *gemmology, gem identification, synthetic and treated gem identification, coloured gem grading and pricing, diamond grading and pricing, lapidary, gem and rock carving, jewellery design and manufacturing*; kutoa huduma za kusanifu madini ya vito na miamba; kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya

vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (Certificate of Authenticity); utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo, ushauri elekezi; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini. Katika kipindi rejewa Kituo kimefanya yafuatayo: -

(a) Kuendelea Kutoa Mafunzo kwa Ngazi ya Cheti k a t i k a Fani za Teknolojia ya Madini na Usonara

134. Mheshimiwa Spika, katika kipindi rejewa, Kituo kimedahili wanafunzi 36 kwa Mafunzo ya Muda Mrefu katika ngazi ya Cheti (NTA Level 4) katika fani ya Teknolojia ya Madini na Usonara. Udahili huo ni sawa na ongezekezo la asilimia 111.7 ikilinganishwa na wanafunzi 17 kwa Mwaka 2018/2019 na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi 53 wanaoendelea na mafunzo hayo. Aidha, wanafunzi 39 walidahiliwa kujiunga na mafunzo ya muda mfupi (miezi sita na mitatu) katika fani za utambuzi wa madini ya vito, ukataji na ung'arishaji madini ya vito ambao kati ya hao wanafunzi 11 walihitimu mafunzo na wengine wanaendelea na masomo hayo.



Picha Na. 24: Wanafunzi wa Kituo cha TGC wakiwa katika mafunzo ya uongezaji thamani madini

135. *Mheshimiwa Spika*, wanafunzi 17 katika teknolojia ya vito na usonara walihudhuria mafunzo ya ugani kwa muda wa wiki nane (8) katika ofisi za madini za mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Shinyanga, Mirerani-Manyara, mgodi wa Williamson Diamond Limited - Shinyanga na Arusha Gemological Laboratory. Aidha, wanafunzi wa fani ya ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito walihudhuria mafunzo ya ugani kwa muda wa wiki nne katika kampuni zinazojishughulisha na uongezaji thamani madini ya vito jijini Arusha, Dar es Salaam na Mirerani Mkoa wa Manyara.

(b) Kutoa Huduma kwa Wadau wa Madini

136. *Mheshimiwa Spika*, Kituo kiliendelea kutoa huduma mbalimbali za uongezaji thamani madini kwa wadau ikiwa ni pamoja na utambuzi wa madini ya vito, usanifu madini ya vito, uchongaji wa vinyago vya miamba pamoja na *gemstone tumbling* kwa wadau. Aidha, Taasisi za Serikali zimeanza kutumia bidhaa zinazozalishwa kituoni ikiwa ni kielelezo cha mwitikio wa kuthamini bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.



Picha 25: *Vinyago Vilivyotengenezwa kwa mawe na Kituo cha TGC Arusha kwa ajili ya Mapambo ya Nyumbani na Ofisini*

(c) Kuwajengea uwezo watumishi

137. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imepeleka nchini India wakufunzi wawili (2) ili kuwaongezea ujuzi katika masuala ya

jimolojia na usonara. Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Kituo hicho kulingana na mahitaji na upatikanaji wa fedha.

D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

138. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 - 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo ya Maendeleo E n d e l e v u (SDGs) 2015-2030; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2019/2020 – 2023/2024; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/2021; Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyoyatoa katika nyakati tofauti; na ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa nyakati tofauti.

139. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/21, Wizara imejiwekea maeneo yafuatayo ya kipaumbele:- kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na Rasilimali Madini; kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini; kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija; kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini.

140. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo; kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini; kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na madini mengine ya vito; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; k u i m a r i s h a Taasisi zilizo chini ya Wizara; kuimarisha shughuli za kitafiti

za kijiosayansi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

i. Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na Rasilimali Madini

141. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Wizara inapanga kukusanya jumla ya shilingi 547,735,863,597 ikilinganishwa na shilingi 476,380,613,492 kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 14.98. Kati ya fedha zitakazokusanywa, shilingi 526,722,547,000 sawa na asilimia 96.16 zitawasilishwa Hazina na shilingi 21,013,316,597 sawa na asilimia 3.84 zitatumika na Taasisi zilizochini za Wizara.

ii. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini

142. Mheshimiwa Spika, katika kipaumbele hiki Wizara itafanya yafuatayo: kukagua na kufuatilia utekelezaji wa kanuni za usalama, afya na mazingira na kurekebisha kasoro zitakazojitokeza ili kuwa na uchimbaji madini endelevu; kuhakikisha migodi inaweka Hati Fungani ya Uhifadhi wa Mazingira na Mpango wa Ufungaji Migodi; kukagua na kuhakiki kiasi na ubora wa madini yanayozalishwa; kuongeza ushiriki wa Serikali katika uwekezaji kwa kuhakikisha migodi ya kati na mikubwa itakayoanzishwa inatoa *free carried interest* isiyopungua asilimia 16 na kuzisimamia ili kuhakikisha matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo yanafikiwa; kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ya madini kwa kushirikiana na sekta binafsi; na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini katika shughuli za utafiti na uchimbaji madini.

iii. Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija

143. Mheshimiwa Spika, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini Wizara itafanya yafuatayo:- kuendelea kutenga maeneo yanayofaa kwa Wachimbaji Wadogo;

kuwapa elimu kuhusu uwepo na faida za kuuza madini yao katika masoko yaliyoanzishwa; kutoa huduma nafuu za kitaalam kwa Wachimbaji Wadogo ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha kuhusu uwepo wa mashapo katika maeneo yaliyobainishwa na kutengwa kwa ajili yao; na kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, biashara ya madini yenye tija na namna ya kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha.

iv. Kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini

144. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi na kukusanya takwimu za madini kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali, Wizara itafanya yafuatayo:- kuimarisha ukaguzi wa migodi mikubwa na ya kati ili kupata taarifa sahihi za uwekezaji, uzalishaji, na mauzo kwa lengo la kuhakikisha tozo na kodi mbalimbali za Serikali zinatozwa kwa usahihi; kuhakikisha kila mgodi mkubwa, wa kati na maeneo ya wachimbaji wadogo unakuwa na Afisa Mgodi Mkazi ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi za uzalishaji kwa lengo la kutoza tozo stahiki; kufuatilia taarifa za ununuzi na uuzaji (returns) kwa wafanyabiashara wa madini (Dealers & Brokers).

145. Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine ni pamoja na kusimamia Sheria katika kukuza ushiriki wa nchi na wananchi (local content) katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini; kufuatilia uwajibikaji wa Kampuni za uchimbaji madini kwa jamii (Corporate Social Responsibility); kuimarisha ukaguzi wa madini ya ujenzi na viwandani; kufuatilia wadaiwa wa tozo mbalimbali za madini kwa mujibu wa Sheria kwa wakati; kudhibiti uchimbaji na uchenjuaji haramu wa madini; na kuboresha na kuimarisha Mfumo wa kutoa leseni za madini na kutunza taarifa zake.

v. Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo

146. Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma ya kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo:- kuweka vifaa

muhimu vya upimaji wa madini katika masoko hayo; kuhakikisha kuwa huduma zote za msingi ikiwemo za kifedha na mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato mbalimbali zinakuwepo ili kuwaondolea usumbufu wauzaji na wanunuzi wa madini; kuimarisha usalama; kuhakikisha uwepo wa wataalamu wa kutosha katika masoko; na kuanzisha masoko mapya kulingana na mahitaji.

vi. Kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini

147. Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini, Wizara itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-kuendelea kuimarisha usimamizi katika maeneo yote ya uzalishaji kwenye migodi mikubwa na ya kati kwa kuwaweka Maafisa Migodi Wakazi (MROs) kusimamia na kuwasilisha taarifa za uzalishaji wa kila siku pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini; Wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika za Serikali itahakikisha kuwa katika maeneo ya viwanja vya ndege na mipakani wanakuwepo wasimamizi ili kuhakikisha kuwa madini yanapitishwa kwa vibali husika; na Kufanya kaguzi maalum za kimkakati mara kwa mara katika maeneo ya shughuli za madini.

ii. Kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na madini mengine ya vito

148. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha soko la madini ya tanzanite na madini mengine ya vito Wizara itafanya yafuatayo:- kuendelea kuimarisha ulinzi katika eneo tengefu la Mirerani; kuhakikisha kuwa shughuli zote za uchimbaji na biashara ya madini ya tanzanite zinafanyika ndani ya ukuta; kuhakikisha kuwa madini ya vito yanachimbwa na wazawa kwa mujibu wa Sheria; na kuhakikisha kuwa madini ya vito yanauzwa katika masoko ya madini nchini kwa kuzingatia bei elekezi ya soko la dunia.

viii. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

149. Mheshimiwa Spika, katika kukuza uwezo wa uongezaji thamani madini, Wizara itafanya yafuatayo:- kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vya kuchakata

madini hapa nchini kama vile *Smelters* na *Refineries*; kukiimarisha Kituo cha Jimolojia Tanzania ili kiweze kutoa wataalamu bora watakaokidhi mahitaji ya soko; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini na vito (usonara na uchongaji); na kubainisha na kuhamasisha matumizi ya madini ya viwandani katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

ix. Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara

150. Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya yafuatayo katika kuimarisha Taasisi zinazohusika na masuala ya madini:- kuzipatia rasilimaliwatu, fedha na vitendea kazi ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na kuzisaidia katika kuandaa Mipango Mikakati inayoendana na Sera na Mipango ya nchi.

x. Kuimarisha shughuli za utafiti za jiosayansi

151. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itahakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufanyia tafiti; kuimarisha maabara ya GST na kuhakikisha uwepo wa vifaa na wataalam; na kuwaendeleza wataalam ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia katika Sekta ya Madini.

xi. Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi

152. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo na kuongeza ujuzi kwa watumishi katika nyanja mbalimbali; kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY); na kutoa huduma ya lische kwa walioweka wazi kuwa na UKIMWI. Aidha, Wizara itaboresha mazingira ya kazi kwa kutoa vitendea kazi, kuboresha maslahi ya watumishi, kuhamasisha uadilifu na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

**KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA
KWA MWAKA 2020/2021**

i. Tume ya Madini

153. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2020/2021 Tume ya Madini inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a)Kusimamia biashara ya madini na masoko yaliyoanzishwa

154. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza jukumu hilo Tume ya Madini itafanya yafuatayo: kudhibiti utoroshaji wa madini; kusimamia shughuli zote za uthaminishaji madini nchini na kushiriki minada ya madini ndani na nje ya nchi; kuandaa bei elekezi; usimamizi wa shughuli za maabara; na kusimamia utekelezaji wa kanuni za uwezesaji wananchi kiuchumi (local content) katika Sekta ya Madini.

(b) Kuimarisha Shughuli za Ukaguzi wa Migodi na Mazingira nchini

155. *Mheshimiwa Spika*, katika eneo hili, Tume ya Madini itaendelea kufanya ukaguzi katika Migodi mikubwa na midogo nchini; kuendelea na vikao vya ufungaji wa migodi chini ya Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi (NMCC) kwa lengo la kuipitia Mipango ya Ufungaji migodi na kuithibitisha; pamoja na kuendelea na elimu ya ugani kuhusu usalama mahala pa kazi kwa lengo la kupunguza ajali migodini.

(c) Kuboresha shughuli za Usimamizi, utoaji wa Leseni na masuala ya TEHAMA

156. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Madini itaendelea kuimarisha shughuli za TEHAMA kwa kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo (*Local Area Network-LAN*) na (*Wide Area Network-WAN*) katika Ofisi mbalimbali za madini nchini ili kurahisisha upatikanaji wa Mfumo wa Usimamizi na Utoaji wa Leseni za Madini nchini kwa urahisi zaidi.

(d) Kuendeleza Rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi

157. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 Tume ya Madini itaendelea kuwajengea uwezo wa kiujuzi watumishi wake katika nyanja mbalimbali kulingana na uhitaji; kuboresha mazingira ya kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana; kuendelea kutoa elimu kwa watumishi juu ya kuzuia maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa huduma ya lishe bora kwa Watumishi waliokwisha athirika; na kuhamasisha uadilifu mahali pa kazi.

(e) Uelimishaji na Uhabarishaji Umma na Usimamizi wa Masuala ya Kisheria

158. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha migogoro inapungua au kuisha kabisa katika Sekta ya Madini, Tume ya madini itaendelea kutoa elimu na huduma ya ugani juu ya masuala ya kisheria pamoja na miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Madini nchini kupitia redio, runinga, *blogs* na tovuti juu ya maendeleo ya Sekta ya Madini nchini.

ii. Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

159. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

(a) Kuboresha kanzidata ya Miamba na Madini ya Taifa ili kuongeza uelewa wa jiolojia ya nchi na kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Madini nchini

160. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha kanzidata ya miamba na madini nchini GST inakusudia kufanya; Utafiti wa jiolojia katika QDS 124, 190 na 316 na jikemia QDS 124 na 125 zilizopo katika Mkoa wa Lindi na Dodoma kwa skeli ya 1:100,000; kufanya tafiti maalum mbili (2), kuendeleza tafiti na kuzalisha *crucible* na *cupels* 15,000; kuchora ramani 25

na ku-*scan* machapisho 1,000 kutoka katika mfumo wa karatasi na kwenda katika mfumo wa dijitali pamoja na sampuli za makumbusho (museum) 50 na kuweka kwenye *Geological Mineral Information System* (GMIS); kufanya utafiti wa jiosayansi kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia ya China (China Geological Survey).

(b) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kufanya tafiti za jiosayansi katika utafutaji, uchimbaji salama, uchenjuaji na uhifadhi wa mazingira

161. *Mheshimiwa Spika*, katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kutambua ulalo, muelekeo na tabia za mbale katika maeneo manne (4) ya wachimbaji wadogo yaliyopo Mkoa wa Katavi na Mara; Utafiti wa jiosayansi katika maeneo mawili (2) yatakayobainishwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

(c) Kuboresha Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi

162. *Mheshimiwa Spika*, katika kuboresha huduma za maabara, GST imepanga kufanya mambo yafuatayo: kufanya uchunguzi wa maabara kwa sampuli 15,000; kuendeleza programu mbalimbali za kusimamia ubora wa huduma za maabara; na kuboresha miundombinu, mitambo na vifaa vya maabara.

(d) Kuboresha kanzidata ya majanga ya asili ya jiolojia na kuelimisha wananchi namna bora ya kujikinga na majanga

163. *Mheshimiwa Spika*, katika kuboresha kanzidata ya majanga ya asili ya jiolojia, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kukusanya takwimu na kuzichakata kutoka katika vituo vyote tisa (9) na kuhuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kufanya utafiti wa kina wa hali ya matetemeko ya ardhi katika Mji wa Serikali; kusimika vituo viwili vipya vya kuratibu matetemeko ya ardhi katika Mkoa wa Kigoma na Kagera.

(e) Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato

164. Mheshimiwa Spika, Ili kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato, GST inakusudia kufanya mambo yafuatayo: kuboresha vitendea kazi na mazingira ya kazi; kuendeleza watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao; kuboresha muundo wa GST ili kuongeza ufanisi na kuboresha mtambo wa kutengeneza vyungu vya kuyeyushia sampuli za dhahabu na fedha ili uweze kuzalisha kibiashara.

iii. Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

(a) Kuimarisha shughuli za uchimbaji na uzalishaji madini

165. Mheshimiwa Spika, Mwaka wa Fedha 2020/21 Shirika linatarajia kutekeleza yafuatayo: kuongeza uzalishaji katika mradi wake wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira kwa kuongeza vifaa vya uchimbaji wa makaa ya mawe pamoja na masoko.

166. Mheshimiwa Spika, Shirika linatarajia pia kuongeza uzalishaji katika Kampuni ya STAMIGOLD kutoka wastani wa wakia 1,150 hadi kufikia wakia 1,500 kwa mwezi. Sambamba na hilo mgodi unatarajia kuanza utekelezaji wa mradi wa kuchenjua visusu vya dhahabu na kuimarisha shughuli za utafiti na uchorongaji ili kuongeza uhai wa mgodi.

(b) Kuanza utekelezaji wa Miradi mipya na kuimarisha shughuli za uchorongaji

167. Mheshimiwa Spika, Shirika pia linatarajia kuanza uzalishaji katika miradi mipya miwili ambayo ni mradi wa kusafisha dhahabu uliopo jijini Mwanza na mradi wa kuchimba dhahabu wa Buhemba. Miradi hii inatarajiwa kuanza uzalishaji Desemba, 2020. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za kibiashara za uchorongaji na kutoa ushauri wa mazingira kwa kuongeza vifaa na wataalamu. Vilevile, Shirika linatarajia

kununua mitambo mipya mitatu (3) ya uchorongaji (drilling rig).

(c)Kuendelea kuratibu na kuendeleza shughuli za wachimbaji wadogo

168. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa uratibu wa uendelezaji wa wachimbaji wadogo, Shirika litaendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo katika vituo vya Katente, Lwamgasa na Itumbi na kutoa elimu ya uchimbaji bora kwa wachimbaji wadogo nchini.

iv.Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

169. *Mheshimiwa Spika*, kazi zitakazotekelezwa na TEITI katika Mwaka 2020/2021 zitahusisha: kukamilisha na kutoa kwa Umma ripoti ya ulinganisho wa malipo ya kodi yanayofanywa na Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na mapato yaliyopokelewa na Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019; kuendelea kuelimisha Umma juu ya matumizi ya takwimu zinazotolewa katika ripoti za TEITI ili waweze kutumia takwimu hizo katika kuhoji uwajibikaji wa Serikali kwa njia ya warsha, matangazo, vipindi vya redio, runinga na makala; uwekaji wazi wa majina ya watu wanaomiliki hisa katika kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na kuweka wazi mikataba ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

v. Chuo cha Madini (MRI)

(a)Kuendelea Kutoa Mafunzo Katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

170. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini kinapanga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 548 kwa Mwaka wa Masomo 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 750 kwa Mwaka wa Masomo 2020/2021 sawa na ongezeko la **asilimia 36.9**. Ongezeko hili litapelekea kufikia lengo la Mpango Mkakati wa Chuo wa kuwa na wanafunzi 1,000 ifikapo mwaka 2022.

(b) Kuendelea Kuboresha Miundombinu ya Chuo

171. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini kitaendelea kukarabati miundombinu katika Kampasi za Dodoma na Nzega kama vile; mabweni ya wanafunzi, madarasa, maabara, nyumba za watumishi pamoja na miundombinu mingine ya maji na umeme. Aidha, Chuo kitaendeleza na kusimamia upatikanaji wa mawasiliano chuoni (ICT) ili kukidhi mahitaji yatokanayo na ongezeko la wanafunzi na watumishi; kuongeza vitendea kazi kama vile vifaa vya ofisi, maabara, vifaa vya kufundishia pamoja na vitabu.

(c) Kuwajengea Uwezo Watumishi

172. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo kitaendelea kuwajengea uwezo watumishi wa kada zote kupitia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwapa utalaam na ujuzi utakaowaongezea ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

(d) Kuendelea Kufanya Tafiti na Kutoa Ushauri Elekezi

173. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Chuo cha Madini chini ya ulezi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kitaendelea kufanya tafiti katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, kutoa ushauri elekezi (consultancy) katika Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia; pamoja na kuwasilisha maandiko juu ya kazi za kitafiti katika majarida mbalimbali ya kisayansi kwa ajili ya uchapishaji.

vi. Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC)

(a) Kutoa Mafunzo na Uzalishaji

174. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Jimolojia Tanzania pamoja na majukumu mengine kitatekeleza yafuatayo:- kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika fani ya Teknolojia ya Madini na Usonara (Gem and

Jewellery Technology); kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za *gemology, gem identification, synthetic and treated gem identification, coloured gem grading and pricing and diamond grading and pricing, lapidary, gem and rock carving, jewellery design and manufacturing*; kutoa huduma za kusanifu madini ya vito na miamba; kutoa huduma za kimaabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara kwa kutoa vyeti vya uthibitisho (Certificate of Authenticity); utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo (usonara); kutoa ushauri na ugani kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

(b)Kukijengea uwezo Kituo

175. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inatarajia kuwaendeleza kielimu watumishi wanne (4) katika vyuo vilivyobobea katika masuala ya uongezaji thamani madini. Aidha, Wizara imepanga kuajiri watumishi katika kada mbalimbali ambao watakuwa wakufunzi katika Kituo cha Jimolojia Tanzania.

E. SHUKRANI

176. *Mheshimiwa Spika*, nakiri kuwa azma ya Taifa letu ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025, inaendelea kutupa hamasa ya kufanya kazi kwa juhudi zaidi. Hamasa hii inatokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo Sekta ya Madini ninayoismamia. Kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuliongoza Taifa letu na kuwaletea watanzania maendeleo ya kweli yanayoonekana kwa vitendo.

177. *Mheshimiwa Spika*, ninamuomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amjalie Mheshimiwa Rais afya njema ili aendeleo kutekeleza majukumu yake na kutimiza ndoto na maono yake ya kulifikisha Taifa hili katika Uchumi wa kati

kupitia ujenzi wa viwanda na usimamizi thabiti wa utekelezaji wa ahadi za Ilani ya CCM.

178. Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii tena kuwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yao wanayotupatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, nimshukuru pia Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb.), Naibu Waziri wa Madini kwa namna anavyonipa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini.

179. Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Prof. Simon Samwel Msanjila, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini kwa namna anavyosimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru, Mhandisi David Mulabwa, Kamishna wa Madini, Prof. Idris Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO, Prof. Justinian Ikingura, Mwenyekiti wa Bodi ya GST, Bw. Ludovick Utouh Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI, Prof. Hudson Nkotagu, Mwenyekiti wa Bodi ya MRI, Makamishina wa Tume na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini uendeshaji wa Sekta ya Madini.

180. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha kuwa majukumu ya Wizara ya Madini yanatimizwa ipasavyo na hivyo kuifanya Sekta ya Madini kuzidi kuimarika na kwenda mbele.

181. Mheshimiwa Spika, niendeleo kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa ushirikiano wao ambao kwa namna moja au nyingine umeiwezesha Wizara kufikia malengo yake. Nipende kuwatambua kwa kuwataja baadhi yao kama ifuatavyo: Benki ya Dunia; Serikali za Jamhuri ya Watu wa

China, Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini, Misri, Australia na JOGMEC. Aidha, nazishukuru pia Taasisi, Mamlaka mbalimbali na Wadau wa Sekta ya Madini ambao wamesaidiana na Wizara katika masuala mbalimbali. Kipekee niwashukuru Uongozi Institute na REPOA kwa kutujengea uwezo katika masuala ya Uongozi na uandaaji wa Sera. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika ikuendeleza Sekta.

182. Mheshimiwa Spika, shukrani zangu za pekee na za dhati pia naomba nizitoe tena kwa wananchi wema, watu wa kusema na kutenda wa jimbo la Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniadini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu nilipokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Napenda kuwahidi na kuwahakikishia kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote kwa kipaji alichonipa mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Naomba ushirikiano huu udumu ili kwa pamoja tuendeleo kujenga Bukombe yetu.

183. Mheshimiwa Spika, napenda kipekee kabisa kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wetu Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

F. HITIMISHO

184. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara ya Madini katika Mwaka 2020/2021, naomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie na kupitisha makadirio ya Jumla ya **shilingi 62,781,586,000** kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni **shilingi 8,500,000,000**. ambazo zote ni fedha za ndani; na

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 54,281,586,000. ambapo **shilingi 21,045,927,000**. ni kwa ajili ya Mishahara na **shilingi 33,235,659,000** ni Matumizi Mengineyo (OC).

185. Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Kwa kuwa hili ni Bunge la mwisho kuelekea Uchaguzi Mkuu, naomba nichukue nafasi hii kuwatakia uchaguzi mwema. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.madini.go.tz. Vilevile, hotuba hii ina majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini.

186. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana kwa uwasilishaji mahiri wa hotuba yako na kwa kuzingatia muda. Ahsanteni sana.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, una dakika 20. Mheshimiwa Kitandula, Mwenyekiti karibu sana.

Labda Mheshimiwa Kitandula kabla hujaanza niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara hii tutaifanya kuwa ya leo tu kwa sababu ambazo jana mnafahamau nini kilitokea.

Kwa hiyo, leo tutamaliza. Kwa kuwa leo tutamaliza, maana yake ni kwamba inabidi kupiga kura leo. Kwa hiyo, kura yako ndiyo mahudhurio ya leo. Naomba walioko Msekwa na mahali pengine pia muweze kunielewa katika hili.

Pia tumegundua kwamba katika kupiga kura nakadhalika katika mahudhurio kwa ujumla wake kuna baadhi ya wenzetu sio waaminifu, wanabeba *tablets* za wengine. Kwa hiyo, tumeweka uangalizi na siyo vizuri kwa Mheshimiwa Mbunge kupatikana unafanya mambo ya ovyo ovyo, lakini tumeweka uangalizi. Camera zetu ukiacha hizi, ziko na za ziada katika majengo yetu yote ambayo tunayatumia kwa kazi hizi na kwa kweli ni *very childish* kama ikigundulika hivyo.

Vilevile watu wangu wanafanya *head count*, wanajua kabisa nani amehudhuria, wanajua nani hakuhudhuria. Kwa hiyo, wanajua kabisa ni nani ambaye amefanyiwa utaratibu ambao siyo. Ambacho bado hatujui, ni nani anayefanya hilo liwezekane? Hilo nalo halina muda, lakini na lenyewe tatalifahamu. Kwa hiyo, tusifanye hivyo, tutatangazana hapa itakuwa aibu.

Mheshimiwa Kitandula tafadhali, *20 minutes*.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia uhai na uzima kuweza kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote ya Kamati yetu iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge. Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) na 98(2) ya Kanuni ya Bunge toleo la Januari, 2016 Kamati ilifanya kazi zifuatazo:-

(i) Ilifanyakazi ya kutembelea na kukagua utekelezaji miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

(ii) Ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hiyo ilifanyika katika Mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Lengo la ziara ilikuwa ni kujionea utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka huo pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusiana na Matoeko ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo kwa Mwaka huo ni kama inavyoonekana katika taarifa yetu lakini pamoja na maelezo hayo, Kamati ina maoni ya jumla kuhusu ukaguzi huo:-

(i) Kamati inaona kwamba ipo haja kwa Wizara ya Madini ikwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo TASAC kuangalia upya namna ya kupunguza tozo zinazotumika katika kusafirisha nje madini. Aidha, kiwango cha tozo ambazo mfanyabiashara anatozwa kiwe rafiki na kilipwe kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini.

(ii) Ipo haja kwa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini kuendelea kutoa elimu kuhusu Sheria na Kanuni kwa Wachimbaji wa madini, wafanya biashara wa madini na wadau wote katika sekta ya madini ili kupunguza adha kwa wafanya biashara juu ya malipo ya tozo na kodi mbalimbali ambazo Kanuni inazitolea ufafanuzi.

(iii) Ipo haja kwa Serikali kuangalia namna bora ya upatikanaji wa vibali kwa wadau katika sekta ya Madini kwani upatikanaji wa vibali hivi wakati mwingine umekuwa na changamoto nyingi.

(iv) Kwa kuzingatia Sheria ya madini ya Mwaka 2010 na Kanuni za Madini za Mwaka 2019, Kifungu cha 6(3),

mchimbaji mdogo wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini hapaswi kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wala hapaswi kulipa kodi ya zuio yaani *withholding tax*. Hata hivyo, katika soko hilo hilo Sheria ipo kimya kwa wafanyabiashara wengine yaani *Dealers, Sonaras na Brokers* hivyo pindi wanapofanya biashara katika soko hilo hutakiwa kulipa VAT. Kamati inaona ipo haja kwa Wizara kupitia Tume ya Madini kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ili kuweka uwanja sawa wa ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020; jukumu la msingi la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya sekta ya madini nchini kwa kuweka mifumo thabiti ya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini ili kuhakikisha mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa unaongezeka. Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara Fungu Na.100 kwa kuzingatia mambo makuu matatu kama ifuatavyo:-

(i) Eneo la kwanza ilikuwa ni makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

(ii) Hali ya upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kutoka hazina.

(iii) Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa Bajeti ya Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 470,897,000,000 katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, shilingi 470,354,000,000 zilipangwa kukusanywa kupitia Tume ya Madini na shilingi 532,000,000.6 kupitia Chuo cha Madini na shilingi bilioni 10 kupitia Idara na Vitengo vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia februari, 20 jumla ya shilingi bilioni 319.0 ambazo ni sawa na asilimia 102 ya lengo

la makusanyo katika kipindi husika zilikuwa zimekusanywa.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Wizara iendelee kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini, usimamizi wa makusanyo na kuzuia utoroshaji wa madini ili kuhakikisha malengo yanafikiwa katika vipindi vyote.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa fedha; katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge liliidhinisha fedha za matumizi kwa Wizara hii jumla ya shilingi bilioni 49,466,898,200. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni saba sawa na asilimia 14.23 ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, shilingi bilioni 42 sawa na asilimia 85.7 ya bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa matumizi ya kawaida ambayo inajumuisha mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi februari jumla ya shilingi bilioni 27.79 zilitolewa kwa Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 98.26 ya lengo la mwaka kwa miezi nane. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 10.5 sawa na asilimia 64.2 ni fedha za matumizi mengineyo na OC na shilingi bilioni 17 sawa na asilimia 66.29 zilitolewa kwa ajili ya kulipa mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara bado haijatoa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge licha ya kwamba katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo Wizara ilitumia fedha zilizokuwa na mfuko wa mradi wa usimamizi endelevu takribani bilioni 6.1 hivyo kuweza kutekeleza miradi ya mendeleo. Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 maombi ya fedha ambayo yalipokelewa hazina ya fedha zake zitolewe kwa Wizara ili Wizara iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati; katika uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2019/2020, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuzingatia matakwa ya Kanuni ya saba ya nyongeza ya nane ya Toleo la mwaka 2016. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati ulizingatiwa na baadhi bado unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali kama inavyoonekana katika Taarifa hii. Hivyo ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutekeleza Maoni na Ushauri unaotolewa na Kamati yako.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya malengo ya Wizara kwa mwaka 2020/2021; Kamati inaridhishwa na malengo na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2020/2021. Hata hivyo, Kamati inatambua kuwa, kuwa na malengo ni jambo moja na kufanya juhudi au utekelezaji wa mikakati kufikia malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo Kamati inaamini kuwa Serikali itatekeleza mikakati hiyo kwa ufanisi ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato; Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 547.7 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 476.3 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hivyo kuwepo kwa ongezeko la asilimia 14.98 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kati ya fedha zitakazokusanywa, shilingi bilioni 526 sawa na asilimia 96 zitakusanywa na kuwasilishwa hazina na shilingi bilioni 21 sawa na asilimia 3.83 zitakusanywa na kutumika na Taasisi na Wakala chini ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio na Matumizi; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 62.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 49.4 zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka uliopita. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 26.92. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa nyongeza ya fedha hizo inatokana na kuongezeka kwa fedha za miradi ya maendeleo pamoja na fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeongeza fedha hizo

kwa Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Ofisi, hifadhi za sampuli za miamba ya madini, ununuzi wa vifaa na mitambo ya utafiti pamoja na uimarishaji wa mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kusisitiza kuwa Serikali ihakikishe fedha zinatoka kwa wakati ili Wizara na Taasisi zake ziweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kuhusiana na tozo ya asilimia moja inayotozwa na Wakala wa Meli-Tanzania yaani *TASAC*, Kamati inaona kuwa;

Kwa Kuwa, wafanya biashara wa madini wanaposafirisha madini nje ya Nchi wamekuwa wakitozwa kodi ya asilimia moja na Wakala wa meli Nchini yaani *TASAC* jambo ambalo siyo tu limekuwa likiongeza gharama kwa wafanya biashara bali pia limekuwa likiwatisha tamaa na hivyo kuikoshesha Serikali mapato. Kamati inaamini kwamba kupunguzwa ama kuondolewa kabisa kwa kodi hii kutachochea ukuaji wa biashara ya madini yanayosafirishwa kwenda nje ya Nchi.

Hivyo Basi, Kamati inahsuari Wizara ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo *TASAC* kuangalia namna ya kupunguza tozo hiyo ya kusafirisha madini nje ya nchi. Aidha, kiwango cha tozo ambacho mfanya biashara atatozwa kiwe rafiki na kilipwe kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwenye kodi ya ongezeko la thamani kwa wafanya biashara ya madini katika masoko ya madini; kwa kuzingatia Sheria ya madini ya Mwaka 2010 na Kanuni ya Madini ya Mwaka 2019, Kifungu cha 6(3) kinampa haki mchimbaji mdogo wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini asitozwe kodi ya ongezeko la thamani wala kodi ya zuiio.

Hata Hivyo, katika soko hilo hilo Kanuni ipo kimya kwa *Dealers, Brokers* ambao nao wanauza na kununua madini katika soko hilo hilo na hivyo wafanya biashara hawa pindi wanapouziana madini, mamlaka ya mapato imekuwa ikitaka walipe kodi ya ongezeko la thamani. Ni rai ya Kamati kuwa Wizara ya Madini na Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kuweka uwanja ulio sawa wa ulipaji kodi na hatimaye kuwaelimisha Wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa. (*Makofi*)

(iii) Mheshimiwa Soika, uendeshaji na uratibu wa masoko ya madini; kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokabili masoko ya madini kwa wafanyabiashara wa kadini katika maeneo mbalimbali hapa Nchini. Changamoto hizi zimejumuisha masoko kutokuwa kwenye maeneo stahiki ya kibiashara. Baadhi ya majengo ikiwemo ya Serikali kuwatoza kodi kubwa wafanya biashara, gharama kubwa za uendeshaji wa masoko hayo, mlolongo wa kodi n.k

Hivyo Basi, Kamati inaishauri Serikali kutokupitia Wizara ya Madini na Tume ya Madini kushirikiana na kwa karibu na mamlaka za Mikoa ili kuainisha maeneo stahiki yenye mvuto na hadhi ya kibiashara ili kutumika kama masoko.

Aidha, kushirikiana na mamlaka nyingine zinazomiliki majengo yanayotumika kama masoko ya madini kupunguza kodi ili kuwaondolea wafanyabiashara wa madini mzigo mkubwa wa gharama za uendeshaji. Sambamba na hilo ni kupunguza changamoto za mlolongo wa kodi kwa wafanya biashara kutachochea ufanisi wa dhana hii njema ya masoko

ya madini na kuondoa kabisa changamoto ya utoroshaji wa madini.

(iv) Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni masharti ya vyeti vya kitaaluma kwa waongeza thamani madini wanapoingia kutoka nje; Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuondoa sharti la vyeti vya taaluma kwa wachakata madini (*craftmen*) wanaoingizwa hapa nchini kutoka nje ya nchi zilizobobea kwenye sekta ya usonara kwani kwenye eneo hili mfumo unaotumika kuwapata watalaam wengi kwenye nchi hizo ni ule wa kurithishana ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine badala ya taaluma ya darasani hivyo kutarajia wataalam hawa kuwa na vyeti ni kuendelea kuwanyima fursa Watanzania kupata utaalam huu na hivyo kukosa wataalam wazalendo. Aidha, sambamba na hilo Serikali inapoteza makusanyo ya mapato kupitia shughuli hizi za uongezaji thamani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge na Spika wetu), Dkt.Tulia Ackson (Mbunge, Naibu Spika) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaomba afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati yao. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingine kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukurani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko (Mbunge, Waziri wa Madini), Mheshimiwa Stanslaus Haroun Nyongo (Mbunge, Naibu Waziri wa Madini) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nappenda kumshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Na.100-Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja ambayo ni shilingi bilioni 62.78.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA
MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSUMAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKAWA FEDHA
2020/2021 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yanayotekelezwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazosisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetekeleza ipasavyo majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kikanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatazo:

a) Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 [*Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*]; na

b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 [*Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*].

1.1. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma na Dar Es Salaam. Lengo la ziara likiwa ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake. Aidha, Ziara hizi zilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi tarehe 17 Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);

ii. Mradi wa Soko la Madini – Dodoma;

iii. Mradi wa Soko la Madini – Dar es Salaam;

iv. Kiwanda cha kutengeneza Mawe ya Nakshi (Dimension Stones) – Ntyuka, Dodoma;

1.2 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

1.2.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi endelevu wa Rasilmali za Madini (SMMRP) ulitekeleza kazi mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa vituo saba vya umahiri pamoja na ujenzi wa jengo la Taaluma katika Chuo cha Madini (MRI). Awali, Wizara kupitia Mradi ilibainisha Maeneo Saba kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Umahiri kwa ajili ya kutoa mafunzo mbalimbali ya nadharia na baadhi ya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya Wachimbaji Madini Wadogo. Maeneo hayo ni Bariadi, Musoma, Bukoba, Handeni, Chunya, Mpanda na Songea. Vilevile, Wizara kupitia Mradi imejenga jengo la Taaluma katika Chuo cha Madini (MRI) kwa ajili ya matumizi ya ofisi, madarasa, kumbi za mikutano na ofisi za Chama wa Wachimbaji Madini Wanawake Tanzania (TAWOMA) kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa jengo la Taaluma la Chuo cha Madini (Dodoma) unajengwa na mkandarasi SUMAJKT kwa usimamizi wa mshauri elekezi INTER CONSULT LTD. Mkandarasi SUMAJKT alikabidhiwa eneo la ujenzi lilipo ndani ya Plot 1-10, Block D (Mbwanga Area) lenye ukubwa wa mita za mraba 2,250 mnamo tarehe 14 Julai, 2018 na kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 30 Julai, 2018. Ujenzi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 2,863,161,369.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali pamoja na vifaa vya ofisi.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa jengo hili unajumuisha kazi za nje na ujenzi wa jengo kuu ambalo litajumuisha ofisi 35 zenye uwezo wa kuchukua watumishi wawili (2) kila moja, vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja, chumba kimoja cha kompyuta chenye uwezo wa kuchukua watu 30, chumba kimoja cha mikutano

(*Board Room*) chenye uwezo wa kuchukua watu 30 pamoja na ofisi moja ya pamoja (*Pool Office*) yenye uwezo wa kuchukua watu 10 kwa wakati mmoja. Vilevile, jengo hili litakuwa na ofisi ya mitihani 1 na chumba maalum cha kuhifadhia mitihani (Strong room) 1, stoo 1 pamoja na jiko.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua jengo la Utawala katika chuo cha Madini na kujionea hali ya utekelezaji wa mradi wa jengo hilo inavyoendelea. Hata hivyo, hadi Kamati ilipotembelea mradi huu ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 98**. Aidha, shughuli zilizokuwa zimemilika ni pamoja na ujenzi wa jengo lenyewe, uwekaji mfumo wa maji safi na maji taka, usimikaji wa mfumo wa umeme, usimikaji wa mfumo wa TEHAMA na usalama (security system), upakaji rangi, uwekaji wa bodi za juu ya dari (ceiling board), uwekaji wa nondo na madirisha ya vioo, uwekaji wa sakafu za kisasa (paving blocks), kusawazisha eneo na kupanda nyasi kuzunguka jengo, upandaji wa miti pamoja na usimikaji wa lifti.

Mheshimiwa Spika, Changamoto zilizobainika wakati wa ukaguzi wa mradi huu ni ucheleweshaji wa kumalizika jengo kwa **asilimia 100** kwa kuwa Jengo lilipaswa kumalizika mwaka jana Aprili 2019. Aidha, wakati wa ukaguzi wa mradi Jengo lilionekana kuwa na nyufa katika baadhi ya kuta zinazounda jengo sehemu ya mapokezi. Sambamba na hili, shughuli ambazo zilikuwa hazijakamilika ni pamoja na uwekaji wa vyoo vya walemavu pamoja na mabeseni ya vyooni (sink).

Mheshimiwa Spika, Kwa taarifa kutoka Wizara ya Madini wanategemea Jengo hili kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020 na mkandarasi SUMAJKT amelipwa jumla ya **Shilingi 2,721,110,846.74**.

1.2.2 Kiwanda cha kutengeneza Mawe ya Nakshi (Dimension Stones) – Ntyuka, Dodoma;

Mheshimiwa Spika, Mawe ya Nakshi (*dimension stones*) ni mawe ambayo huchaguliwa na kukatwa katika mwonekano

na ukubwa tofauti tofauti kisha hunakshiwa ili kupata vitu mbalimbali kutegemea na mahitaji yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji hufanyika kwa kutumia mitambo ambayo hutumia waya maalumu wenye ugumu wa hali ya juu kama vile *diamond wire saws* na *diamond belt saws*. Wakati mwingine pia kiasi kidogo cha baruti huweza kutumika ili kutoa mapande ya mawe (*blocks*).


Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilitembelea Mgodu wa mawe ya nakshi uliopo Ntyuka unaomilikiwa na Ndg. Israel Daud Chunga ambaye ni Mtanzania mwenye elimu ya juu aliyehitimu shahada ya kwanza ya Jiolojia katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kujionea shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazoendelea katika Kiwanda hiki. Mtanzania huyu ameingia ubia wa kuwezesha kimtaji na kiteknolojia na kampuni ya Udbhav International Ltd baada ya kupata leseni mwanzoni mwa mwaka 2016. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020, Ndg. Israel Daud Chunga alikuwa anamiliki leseni tano zenye jumla ya hekari 23.86 katika Kata ya Ntyuka kijumuisha na Mtaa wa Ngh ongh onha.

Mheshimiwa Spika, Katika kusimamia biashara ya mawe ya nakshi, Serikali kupitia Tume ya Madini hufuatilia kwa karibu biashara ya mawe ya nakshi (*dimension Stone*) na hatimaye hutoa bei elekezi kupitia kitengo cha biashara. *Dimension Stones* zikishapatikana, baadhi husafirishwa hadi jijini Dar es Salaam ambapo hufungwa na kupelekwa nje ya nchi na nyingine husafirishwa hadi Msata Mkoani Pwani ambako kuna mitambo mikubwa ya kukata mawe na hatimaye kutengeneza meza, tarazo, nk ambazo huuzwa hapa nchini. Aidha, masoko ya *dimension stones* yapo ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu kwa kiwango kikubwa hasa yakiwa na ubora unaotakiwa kimataifa. Hata hivyo, soko kubwa la *dimension Stone* lipo nje ya mipaka ya Tanzania.

Lifuatalo ni jedwali linalo oneshwa mauzo ya *dimension stone* kutoka mgodi wa Ntyuka kwa kipindi cha miaka minne iliyopita;

uzalishaji na mauzo ya mawe ya *dimension stones* kutoka katika machimbo ya Ntyuka.

Year	Weight (Mt)	Value(TZS)	Royalty (TZS)	CIF (TZS)	Total (TZS)
2016	490.00	117,357,313.00	3,506,050.00		3,506,050.00
2017	1,735.54	537,348,533.67	17,852,830.00	417,440.00	18,270,270.00
2018	642.00	165,015,136.03	4,800,493.25	1,202,857.75	6,003,351.00
2019	1,313.54	340,698,959.00	10,220,968.77	3,407,244.69	13,628,213.46
Jumla ya Makusanyo	4,181.08	1,160,419,941.70	36,380,342.02	5,027,542.44	41,407,884.46
Wastani	1,045.27	290,104,985.43	9,095,085.51	1,675,847.48	10,351,971.12



mwenendo wa makusanyo ya mawe ya dimension stones kutoka katika machimbo ya Ntyuka.

Mheshimiwa Spika, kutoka mwaka 2016 – 2019 Mgodi umelipa tozo mbalimbali kama vile;

a) Kodi mbalimbali za Halmashauri ya Jiji la Dodoma Shilingi 7,941,994

b) Kodi ya Ongezeko la Mapato (TRA) Shilingi 254,286,016

- c) Mfuko wa hifadhi ya Jamii (NSSF) Shilingi 43,968,300
- d) Workers Compensation Fund (WCF) Shilingi 2,298,385.20
- e) Kununua Ardhi (Eneo) kwa ajili ya machimbo Shilingi 32,410,000.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo katika ziara ya machimbo ya *dimension stone* ya Ntyuka;

a) Uelewa mdogo wa jamii iliyopo inayoenda sambamba na kuwepo kwa matishio kutoka kwa baadhi ya viongozi kutoka katika Serikali za mitaa kuwa watayafunga machimbo kutokana na hisia kuwa mwekezaji anapata mapato makubwa na mtaa kupata kipato kidogo;

b) Uwepo wa ushuru mwingi kwa madini hayo kwenye Halmashauri ya Jiji na Mtaa, Mfano tozo ya *Building Material Levy* (Shilingi 1,000 kwa tani);

c) Mchango wa “Coorporate Social Responsibility” (CSR) ipo mara mbili:-

i. Shilingi 500 kwa tani,

ii. Shilingi 1,000,000 kwa mwaka), na

d) Tozo ya bandarini inayotozwa na Tanzania Shipping Agency Cooperation (TASAC) inakuwa mara mbili kwani, tozo ya kwanza inalipwa kwa TASAC na nyingine unapaswa kutafuta agenti wa kutoa mizigo (clearing and forwarding) na kumlipa pesa nyingine ya kutoa mizigo.

1.2.3 Soko la Madini Dodoma na Dar es salaam

Mheshimiwa Spika, Masoko ya madini nchini yalianzishwa kufuatia changamoto kubwa iliyokuwa inaikabili Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu, hususan ya utorohaji na biashara haramu ya madini. Changamoto hiyo ilisababisha Serikali

kukosa malipo stahiki ya tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za madini. Athari nyingine iliyoambatana na kukosekana kwa masoko ni wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini kuuza madini yao kwa kificho na kupelekea kutonufaika na bei halisi ya madini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua ya kudhibiti hali hiyo ikiwemo kufanya Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 ambayo yalielekeza kuanzishwa kwa masoko ya madini. Msingi wa uanzishwaji wa Masoko ya Madini, kwa mujibu wa Sheria tajwani kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini; kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika na kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini. Masoko hayo pia yameongeza wigo wa ajira za moja kwa moja na zile zisizokuwa za moja kwa moja, kudhibiti uuzaji holela na kupunguza uwezekano wa utorohaji madini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara kupitia Tume ya Madini kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa imeanzisha masoko ya madini 28 na vituo vidogo vya ununuzi 28.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Masoko ya Madini kwa mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Soko la madini la Dodoma lilianzishwa tarehe 19 Mei, 2019. Biashara inayofanyika katika soko hili inahusisha madini ya metali hususan dhahabu. Kamati ilibaini kuwa Kabla ya Soko la Dodoma kuanzishwa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miezi sita ulikuwa jumla ya **Shilingi 118,401,227.63** (wastani wa **Shilingi 23,680,245.53** kwa mwezi) uliotokana na wastani wa uzito wa **kilogramu 4.22**. Kufuatia kuanzishwa kwa soko hilo, makusanyo yaliongezeka hadi kufikia jumla ya **Shilingi 486,817,451.87** kwa kipindi cha miezi tisa (wastani wa **Shilingi 54,090,827.99** kwa mwezi) uliotokana na uzito wa wastani wa **kilogramu 7.59**. Aidha, Ongezeko hilo limetokana na uwepo wa soko na uwazi katika biashara ya madini hususan dhahabu.

Mheshimiwa Spika, kwa soko la Dodoma changamoto zilizobainika ni pamoja na zifuatazo;

a) Kutokuwepo kwa baadhi ya miundombinu wezeshi kama vile majengo ya kudumu ya kufanyia biashara na majengo kuwa katika hali isiyo ridhisha;

b) Elimu na uelewa mdogo wa kufanya biashara katika masoko rasmi ya madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini;

c) Upungufu wa wajimolojia na baadhi ya vitendea kazi kwenye masoko ya madini.

Mheshimiwa Spika, Soko la madini Dar es Salaam lilianzishwa tarehe 17 Julai, 2019 na lipo kati kati ya Jiji la Dar es Salaam, kwenye Jengo la NHC, Mtaa wa Samora. Biashara inayofanyika katika soko hili inahusisha madini ya aina mbalimbali ikiwemo dhahabu na vito vya thamani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kabla ya Soko hili kuanzishwa ukusanyaji wa mapato ulikuwa wastani wa **Shilingi 25,764,040.81** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi nane kabla ya kuanzishwa kwa soko uliotokana na wastani wa uzito wa **kilogramu 6.36**. Kwa upande wa madini ya vito ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa wastani wa **shilingi 44,466,709.23** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi nane (8) kabla ya kuanzishwa kwa soko.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia kuanzishwa kwa soko hilo, makusanyo yaliongezeka hadi kufikia wastani wa **Shilingi 33,655,304.87** kwa mwezi katika kipindi cha miezi saba tangu soko hilo kuanzishwa ambayo yalitokana na uzito wa wastani wa **kilogramu 4.82**. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Ongezeko hilo limetokana na uwepo wa soko na uwazi katika biashara ya madini hususan dhahabu. Kwa upande wa madini ya Vito Ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa wastani wa **Shilingi 19,060,448.90** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi saba (7) baada ya kuanzishwa kwa soko.

Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini kwa kuhakikisha kuwa biashara ya Madini inafanyika kwa uwazi na soko lake kuwa la uhakika, aidha,

kwa kiasi kikubwa masoko haya yamepunguza na kudhibiti uuzaji holela wa madini na utoroshwaji wa madini, hivyo Serikali kujipatia mapato na wafanya biashara kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, Wakati wa ukaguzi wa soko la madini Dar es Salaam changamoto zifuatazo zilibainika;

- a) Kutokuwepo kwa baadhi ya miundombinu wezeshi kama vile majengo ya kudumu ya kufanyia biashara;
- b) Elimu na uelewa mdogo wa kufanya biashara katika masoko rasmi ya madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini;
- c) Tozo ya Tanzania Shipping Agency Corporation – Wakala wa Meli nchini (TASAC)

Madini yanapozalishwa yanalipiwa mrabaha wa asilimia sita ya thamani ya madini ghafi (raw minerals) yaliothaminishwa na tozo ya ukaguzi ya asilimia moja ya thamani ya madini yaliothaminishwa. Mfanyabiashara wa madini (dealer) anayefanya matayarisho ya kusafirisha madini nje ya nchi (export process) anawajibika tena kulipa asilimia sita ya mrabaha ya thamani ya madini ghafi (raw minerals) yanayosafirishwa nje ya nchi na asilimia moja ya tozo ya ukaguzi ya thamani ya madini yaliothaminishwa na kwa madini yaliyosanifiwa anatozwa asilimia moja ya mrabaha. Hapo hapo, msafirishaji anatakiwa tena alipe asilimia moja „plus (1+%) ya TASAC ya kiasi cha madini kilichothaminishwa ili kuweza kupata Kibali kinachotolewa na ofisi ya forodha (Release Order issued by customs office) cha kusafirisha madini hayo nje ya nchi (inspection and clearance fees). Aidha, ndani ya asilimia hiyo moja kuna **asimilia 18** ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo mfanyabiashara anatakiwa kuilipa kwa TASAC kama kodi. **Hivyobasi**, malipo haya ya asimilia moja zaidi (1+%) kwa TASAC yanaongeza gharama kubwa kwa mfanyabiashara wa madini ambae angetamani kuongeza thamani madini hayo hapa nchini na hatimaye kusafarisha nje ya nchi.

Gharama inazidi kuwa kubwa katika uendeshaji wa biashara ya madini kwa wafanyabiashara na wauzaji wa madini;

d) Kudaiwa risiti za ki elektroniki (EFD) kwa wafanyabishara pindi wanapo nunua mizigo bila kuangalia ununuzi umefanyika kwa wachimbaji wadogo, wa kati ama wakubwa;

e) Kukosekana kwa leseni za masonara kutoka Wizara ya Madini;

f) Usumbufu wa upatikanaji Vibali vya wafanyakazi wanao jihusisha na fani za kutengeneza vito pindi wanapo hitajika kuingia nchini.

1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

i. Wizara ya Madini kushirikiana na mamlaka nyingine kama TASAC (Tanzania Shipping Agency Cooperation) wanapaswa kushirikiana kwa pamoja ili kuangalia namna ya kupunguza Tozo katika kusafirisha madini nje ya nchi, aidha tozo ziwe na kiwango maalumu ambacho mfanyabiashara atatozwa na iwe inalipwa kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini;

ii. Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini wanapaswa kuendelea kutoa elimu kuhusu Sheria na Kanuni kwa wachimbaji wa madini, wafanyabiashara wa madini na wadau wote katika sekta ya madini ili kupunguza adha kwa wafanyabiashara juu ya malipo ya tozo na kodi mbalimbali ambazo kanuni inazitolea ufafanuzi;

iii. Serikali kuangalia namna bora ya upatikanaji wa vibali kwa wadau katika sekta ya madini, kwani upatikanaji wa vibali umeonekana kuwa na urasimu na changamoto za upatikanaji wake kwa wakati;

iv. Kwa kuzingatia Sheria ya madini ya mwaka 2010 na Kanuni za madini za mwaka 2019 kifungu cha 6 kifungu kidogo cha

tatu kinampa uhuru mfanyabiashara wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini asitozwe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wala kodi ya zuio (withholding Tax) lakini TRA bado wanataka pindi wafanyabiashara wanapo uza madini hawa “dealers”, sonara na “brokers” wengine kutozana VAT. Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara kupitia Tume ya Madini wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana na mamlaka nyingine ili kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

v. Wizara ya Madini inapaswa kushirikiana na Serikali za mikoa katika kuhakikisha kuwa masoko ya madini nchini yapo katika maeneo yenye hadhi stahiki na gharama za upangishaji wa masoko hayo ziwe na bei nafuu kwa kampuni zinazopanga katika masoko hayo. Aidha masoko yanapaswa kuakisi biashara ya madini;

vi. Serikali kuendelea kusimamia na kufatilia wawekezaji binafsi juu ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo ya makampuni mbalimbali ya uzalishaji hapa nchini aidha, wazingatie usalama wa watumishi pamoja upatikanaji wa maslahi ya watumishi kwa ujumla.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020;

Mheshimiwa Spika, Jukumu la msingi la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo thabiti ya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, Ili kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka kazi zilizo tekelezwa na Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Februari, 2020 ni pamoja na: -

- i) Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini,
- ii) Uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini,
- iii) Kudhibiti utoroshaji wa madini,
- iv) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini,
- v) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini,
- vi) Kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa,
- vii) Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini,
- viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini na kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

- a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;
- b) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina na;
- c) Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 470,897,011,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 470,354,398,000.00** zilipangwa kukusanywa kupitia Tume ya Madini, **Shilingi 532,610,000.00** kupitia Chuo cha Madini na **Shilingi 10,003,000.00** kupitia Idara na Vitengo vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 319,025,339,704.73** zimekusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 102** ya lengo la makusanyo katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara na kubaini kuwa ongezeko la makusanyo ya Wizara limetokana na Ongezeko la Ukusanyaji wa Mapato ya Mrabaha kwa Serikali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 malengo ya Wizara yalikuwa ni kukusanya kiasi cha **Shilingi 233,333,333,333.33** Aidha, hadi kufikia mwezi Februari 2020 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 252,419,691,968** sawa na Ongezeko la **asilimia 108.2** la Makusanyo.

Aidha, Kamati pia, ilibaini kuwa Ongezeko la Makusanyo ya Wizara pia limetokana na ulipaji faini na malimbikizo ya ada mbalimbali ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Februari 2020 Lengo la Wizara lilikuwa ni kukusanya kiasi cha **Shilingi 902,929,333.33** na hadi kufikia Mwezi Februari 2020 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,275,358,409.81** sawa na **asilimia 141.2** ya malengo kutokana ulipaji wa adhabu na faini za malimbikizo ya ada kutoka kwa wachimbaji na wafanya biashara ya madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati vilevile ilibaini kuwa ongezeko la makusanyo pia limetokana na ulipwaji wa ada za kijiolojia na utafiti ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 Lengo la Wizara lilikuwa ni kukusanya **shilingi 10,000,000,000**. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 Wizara imekusanya kiasi cha **Shilingi 10,510,454,265.34** Sawa na Asilimia **105.1** ya Lengo la Makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka 2019/2020 Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini, usimamizi wa makusanyo na utoroshwaji wa madini ili kuhakikisha malengo yanafikiwa kwa vipindi vyote.

2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilidhinisha Bajeti ya jumla ya **shilingi 49,466,898,200** kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, **shilingi 7,039,810,200** sawa na **asilimia 14.23** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 42,427,088,000** sawa na **asilimia 85.7** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo inajumuisha mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari 2020, Jumla ya **Shilingi 27,791,986,796** zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni sawa na **asilimia 98.26** ya lengo la Mwaka miezi nane kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,587,793,996** sawa na **asilimia 64.27** ni fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 17,204,192,800** sawa na **asilimia 66.29** zilipokelewa kwa ajili ya kulipa Mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **Shilingi 7,039,810,200**. Aidha, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020, Kamati ilibaini kuwa Wizara iliendelea kutekeleza majukumu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia Fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali (SMMRP) ambazo ni kiasi cha **shilingi 6,197,175,564.39** zilizotolewa na wadau wakati wa kufunga mradi Disemba 2018. Katika fedha zilizokuwa zimesalia Shilingi 2,839,151,286.14 zimetumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo zilitumika na mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Katente na Itumbi, na vya umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya. Aidha, Shilingi 3,358,024,278.25 zilitumika kwaajili ya ujenzi wa kituo cha pamoja cha Mirerani, uwekaji wa mfumo wa ulinzi

na kamera za usalama pamoja na miundombinu ya umeme kuzunguka ukuta wa Mirerani.

Aidha, kwakuwa Wizara bado haijapata Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge **Shilingi 7,039,810,200.00** kutoka hazina, kutokana na kuendelea na kukamilisha taratibu za kupata Fedha kwa kutumia mfumo wa sasa ambapo Taasisi husika inawajibika kuwasilisha maombi hazina yakiwa yameambatana na mikataba ya ukandarasi na ankara za madai kuthibistha maombi ya Fedha husika; **Kamati inasisitiza kuwa Serikali ihakikishe kabla ya kwisha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, maombi ya Fedha ambayo yamepokelewa Hazina yawasilishwe kwa Wizara ili Wizara sasa iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake.**

2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 inayoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni yafuatayo:-

i. Uanzishwaji na Uendelezaji wa Masoko ya Madini; Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kuhakikisha masoko ya madini yanaanzishwa bado kuna changamoto kubwa ya usimamizi masoko hayo, utoaji huduma, miundombinu na ulinzi katika maeneo ya masoko. Kwa muktadha huu, Serikali ihakikishe inaimarisha na kusimamia minada ya mauzo ya madini nchini; na kuhakikisha masoko hayo yanakuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye weledi wa masuala ya madini na masoko ili kuvutia wafanyabiashara wengi wa ndani na nje ya nchi.

ii. **Elimu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa Madini** - Kamati pia iliitaka Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa madini kuhusu Sheria ya Madini ili kupunguza migogoro mbalimbali kwa wafanyabiashara na wachimbaji wa madini nchini. Changamoto hii bado kwa kiasi kikubwa bado ipo, Elimu kuhusu Sheria na Kanuni za madini bado hazifahamiki kwa wadau husika kwani kumekua na mivutano mingi ya tozo na kodi mbalimbali kwa mamlaka za Serikali pamoja na wachimbaji na wafanya biashara wa Madini nchini.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kutekeleza maoni na ushauri unao tolewa na Kamati yako.

2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

2.4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilibaini kuwa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/2021 umezingatia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujielekeza katika uchumi wa viwanda ambapo **shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 85.23** ya Bajeti ya Maendeleo ya **shilingi 7,039,810,177** ya Wizara imeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati (*strategic projects*) ya kuongeza mapato ya Serikali.

Aidha, Maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2020/2021 katika Sekta ya Madini na kuzingatwa katika bajeti ni;

i. Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini;

ii. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika sekta ya madini;

- iii. Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija,
- iv. Kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini,
- v. Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo,
- vi. Kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini, Kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzania na madini mengine ya vito,
- vii. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini,
- viii. Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara;
- ix. Kuimarisha shughuli za kitafiti za kijiosayansi na;
- x. Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kamati inaridhishwa na malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2020/2021, hata hivyo kamati inatambua kwamba kuwa na malengo ni jambo moja na kufanya juhudi au kutekeleza mikakati kufikia malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo kamati inaamini kuwa Serikali itatekeleza mikakati iliyonayo kwa ufanisi ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa manufaa ya Taifa.

2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya Shilingi 547,745,866,597 kwa mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti hii ya makadirio ya mapato na kubaini kuwa mwaka 2019/2020 makadirio ya mapato yalikuwa kiasi cha Shilingi 476,380,613,492 hivyo sawasawa na ongezeko la asilimia 14.98 kwa Mwaka 2020/

2021. Kati ya Fedha zitakazokusanywa, **Shilingi 526,732,550,000** sawa na **asilimia 96.16** zitakusanywa na kuwasilishwa Hazina na **Shilingi 21,013,316,597** sawa na **asilimia 3.84** zitakusanywa na kutumika na Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara. Jedwali Lifuatalo linaonesha mchanganuo wa maduhili hayo.

Maduhuli yatakayokusanywa na Kuwasilishwa Hazina

Na.	Taasisi	Makadirio ya Maduhuli
1	Idara na Vitengo vya Wizara	10,003,000.00
3	Tume ya Madini	526,722,547,000.00
JUMLA		526,732,550,000.00
Maduhuli yatakayokusanywa na Kutumika na Taasisi		
1	Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania	508,386,000.00
2	Shirika la Madini la Taifa	19,431,609,797.00
3	Chuo cha Madini	913,320,800.00
4	Kituo cha Jemolojia Tanzania	160,000,000.00
JUMLA		21,013,316,597.00

Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021

2.4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Madini inakadiriya kutumia jumla ya **Shilingi 62,781,586,000** ikilinganishwa na **Shilingi 49,466,898,200** zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 hivyo makadirio haya ni sawa na ongezeko la **asilimia 26.92**. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Nyongeza ya Fedha hizo imetokana na kuongezeka kwa fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na Fedha za Matumizi ya Kawaida. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeongeza fedha hizo kwa Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya ujenzi wa miundominu ya ofisi, hifadhi za sampuli ya miamba ya madini, ununuzi wa vifaa na mitambo ya utafiti pamoja na uimarishaji wa mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetengewa kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000** ikiwa ni Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 fedha zilizotengwa kwaajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **Shilingi 7,039,810,200** hivyo ukilinganisha na bajeti ya mwaka **2020/2021** Fedha za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 20.74**.

Mchanganuo wa Fedha za Miradi ya Maendeleo


Kifungu	Maelezo ya Kifungu	Mchanganuo kwa kila Taasisi	Kiasi	Jumla ya Mradi
2001 - 1119	Mradi wa Usimamizi	Wizara	2,400,000,000	8,500,000,000
	Endelevu wa Rasilimali za Madini	Tume ya Madini	2,180,000,000	
		GST	2,400,000,000	
		STAMICO	1,520,000,000	

Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 54,281,587,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Bajeti hii inajumuisha **Shilingi 33,235,659,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake ambayo ni sawa na **asilimia 61.23** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, Wizara imetenga **Shilingi 21,045,927,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake ambayo ni **asilimia 38.77** ya bajeti ya Wizara ya Matumizi ya Kawaida.

MWENENDO WA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KUANZIA MWAKA 2017/2018 HADI 2019/2020

Mwaka	2017/2018	2018/2019	2019/2020
O.C	13,912,800,000	20,953,262,992	25,953,263,000
P.E	16,749,567,000	18,334,255,000	16,473,825,000
Matumizi ya Kawaida	30,662,367,000	39,287,517,992	42,427,088,000
Maendeleo	21,783,000,000	19,620,964,000	7,039,810,200
JUMLA YA BAJETI	52,445,367,000	58,908,481,992	49,466,898,200



Chanzo; Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Madini 2019/2020

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

3.1 Tozo ya 1% inayotozwa na Wakala wa Meli Nchini Tanzania (TASAC)

Kwa kuwa Wafanyabiashara wa madini wanapo safirisha madini nje ya nchi wamekuwa wakitozwa kodi ya 1% na Wakala wa Meli nchini Tanzania (TASAC), jambo ambalo sio tu limekuwa likiongeza gharama kwa wafanyabiashara bali pia limekuwa likiwakatisha tamaa na hivyo kuikoshesha Serikali mapato; Kamati inaamini kwamba kupunguzwa ama kuondolewa kabisa kwa kodi hii kutachochea ukuaji wa biashara ya madini yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo TASAC (Tanzania Shipping Agency Cooperation) kuangalia namna ya kupunguza Tozo hiyo ya kusafirisha madini nje ya nchi. Aidha, kiwango cha tozo ambacho mfanyabiashara atatozwa kiwe rafiki na kilipwe kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini;

3.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara wa Madini Katika Masoko ya Madini;

Kwa kuzingatia Sheria ya madini ya mwaka 2010 na Kanuni za madini za mwaka 2019 kifungu cha 6 kifungu kidogo cha tatu kinampa haki mchimbaji mdogo wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini asitozwe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wala kodi ya zuio (withholding Tax). Hata hivyo katika soko hilo hilo kanuni ipo kimya kwa *“dealers”* na *“brokers”* ambao nao wanauza na kununua madini katika soko hilihilo; na hivyo wafanyabiashara hawa pindi wanapo uziana madini Mamlaka ya Mapato (TRA) inawataka kutozana kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara na Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana kuweka uwanja sawa wa ulipaji kodi na hatimaye kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

3.3 Uendeshaji na Uratibu wa Masoko ya madini

Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazo kabili

masoko ya madini kwa wafanyabiashara wa Madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Changamoto hizi zimejumisha, masoko kutokuwa kwenye maeneo stahiki ya kibiashara, baadhi ya majengo ikiwemo ya Serikali kuwatoza kodi kubwa wafanyabiashara, gharama kubwa za uendeshaji masoko hayo, mlolongo wa kodi n.k. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Tume ya Madini kushirikiana kwa karibu na Mamlaka za mikoa ili kuainisha maeneo stahiki yenye mwamko na hadhi za kibiashara ili kutumika kama masoko. Aidha, kushirikiana na mamlaka nyingine zinazo miliki majengo yanayo tumika kama masoko ya madini kupunguza kodi ili kuwaondolea wafanyabiashara wa madini mzungu mkubwa wa gharama za uendeshaji. Sambamba na hili kupunguza changamoto za mlolongo wa kodi kwa wafanyabiashara kutachochea ufanisi wa dhana hii njema ya masoko ya madini na kuondoa kabisa changamoto ya utoroshwaji wa madini.

3.4 Miundombinu ya barabara Kiwira- Kabulo

Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI zinapaswa kuchukua hatua za haraka katika kuhakikisha zinamaliza changamoto za utengenezaji wa barabara katika mradi wa Kiwira-Kabulo kwakuwa kutotengenezwa kwa barabara hii kunaliingizia hasara Taifa kutokana na uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi huo kufanyika kwa gharama kubwa;

3.5 Masharti ya Vyeti Vya Kitaaluma kwa Waongeza Thamani Madini (Craftmen)

Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuondoa sharti la vyeti vya taaluma kwa wachakata madini (craftmen) wanaoingizwa nchini kutoka kwenye nchi zilizobobea kwenye sekta ya usonara kwani kwenye eneo hili mfumo unaotumika kuwapata wataalamu wengi kwenye nchi hizo ni ule wa kurithishana ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine badala ya taaluma ya darasani. Hivyo kutarajia wataalamu hawa kuwa na vyeti ni kuendelea kuwanyima fursa watanzania kupata utaalamu huu na hivyo kukosa wataalamu wazalendo.

Aidha, sambamba na hili, Serikali inapoteza makusanyo ya mapato kupitia shughuli hizi za uongezaji wa thamani madini;

3.6 Usimamizi wa Usalama wa Wafanyakazi kwa Makampuni ya Madini na Tume ya Madini

Kwa kuwa Kamati ilibaini kuwepo kwa malalamiko ya wafanyakazi katika makampuni ya uchimbaji madini ikiwemo suala la usalama katika maeneo ya kazi na kufanyishwa kazi kwa muda mrefu; na vilevile baadhi ya watumishi wa Tume ya Madini wanaosimamia maslahi ya Serikali katika madini wamekuwa wakihujumiwa, kutishiwa maisha na wakati mwingine kuhatarisha ajira zao. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia na kufatilia kwa karibu mienendo ya wawekezaji binafsi hususan kwenye eneo la usalama wa wafanyakazi ili kuhakikisha kuwa kanuni za usalama kwa watumishi pamoja upatikanaji wa maslahi ya watumishi kwa ujumla zinazingatiwa.

3.7 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Pamoja na ongezeko la mapato kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) bado Shirika limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali kupitia uwekezaji wake katika miradi mingi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa mtaji, miundombinu isiyofaa ya barabara kuelekea kwenye mgodi wa makaa ya mawe Kiwira- Kabulo, kutokamilika kwa umiliki wa hisa katika kampuni ya makaa ya mawe ya Kiwira pamoja na madeni makubwa sana ya wafanyakazi. Aidha, kwa upande wa kampuni ya STAMIGOLD ambayo ni kampuni tanzu ya shirika la STAMICO, kumekuwa na changamoto za gharama kubwa sana za uendeshaji na uzalishaji kutokana na matumizi ya mafuta mazito ya diesel, ufinyu wa mtaji katika shughuli za uchorongaji, upanuzi wa mgodi na uchenjuaji wa madini, uchakavu wa mitambo na miundombinu, mzigo mkubwa wa madeni kwa shirika unaofikia 39.37 bilioni; na ucheleweshwaji wa marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani. Kutokana na changamoto hizi, **Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine tena, Kuiangalia STAMICO kwa jicho la kipekee ili iweze kuwa chachu ya**

kuendeleza sekta ya Madini hapa nchini kwa kuipatia mtaji utakaowezesha Shirika kujikwamua katika uendelezaji wa migodi inayoisimamia.

3.8 Wajibu wa Makampuni ya Uchimbaji kwa Jamii zinazowazunguka

Kwakuwa Serikali imeendelea kusimamia kwa umakini mkubwa kuhakikisha makampuni mbalimbali ya madini nchini yanatoa sehemu ya mapato yake kisheria kuhudumia maeneo ya jamii zinazo yazunguka. Na kwakuwa, Kamati imebaini kuwa kwa sehemu kubwa kampuni za wazawa zimekuwa nyuma sana katika utekelezaji wa suala hili. Hivyo basi, kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa utekelezaji wa jukumu hili. Wigo huu sasa ushirikishe na kampuni nyingine zenye mikataba na kampuni za uchimbaji za kutoa huduma mbali mbali ili kuongeza ufanisi wa kimatokeo kwa jamii husika.

3.9 Uendelezaji wa wataalamu katika masuala ya Jiolojia

Kwa kuwa Wakala wa Jiolojia nchini (GST) imeendelea kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalamu wenye taaluma stahiki kama vile wakemia, wajiolojia, na wahandisi wa jiolojia; Kamati inaendelea kuishauri na kuisisitiza Serikali kuwekeza kwa kutoa fursa za masomo kwa wananchi na watumishi mbalimbali katika taaluma hizo ili kuweza kupata wataalamu. Aidha, Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wenye taaluma hizo kwani kazi wanazofanya ni kubwa na zina manufaa makubwa kwa Taifa.

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dr. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaomba afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb - Mjumbe
11. Mhe. John Wegesa Heche, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb - Mjumbe
18. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Doto Mashaka Biteko(Mb) – Waziri wa Madini, Mhe. Stanslaus Haroun Nyongo(Mb) - Naibu Waziri wa Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Herman Edgar Berege kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja ambayo ni **Shilingi 62,781,586,000**.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na Naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI

20 Aprili, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kitandula. Nakushukuru sana kwa kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati yako kwa Wizara hii. Sasa nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Madini. Una dakika 20 pia.

MHE. JOSEPH L. HAULE – K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kabla sijawasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunatoa pole kwako na kwa familia kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Ajali Akbar, Mbunge wa Newala Vijijini pamoja na Mheshimiwa Getrude Lwakatare, Mbunge wa Viti Maalum (CCM). Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, amen. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwasilishe hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Madini, Mheshimiwa John Heche ya Mapitio ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha katika Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Madini naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni hayo napenda kutumia fursa hii kuwapa pole wananchi wote walioathirika kwa namna moja au nyingine na janga la *corona* lililoikumba Nchi yetu. Aidha, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni napenda kuwapa neno la faraja Watanzania wote kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu na kwamba waendeleo kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya *corona* kama ilivyoelekezwa na wataalam wa afya na waendeleo kumtumainia Mungu ili aliepushe Taifa hili na janga hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutambua uwezo wangu na kuniamini kunitewa kuwa Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii. Aidha, namshukuru Waziri kivuli mwenye dhamana, Mheshimiwa John Heche, Mbunge wa Tarime Vijijini kwa kunipa heshima ya kusoma hotuba hii kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara mbalimbali pamoja na wasaidizi wao kwa kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi walizonazo. Ninawatakia kila la

heri katika majukumu haya ya kuwatumikia Watanzania na Taifa hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sitawatendea haki Wananchi wa Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla kama sitawashukuru kwa heshima kubwa waliyonipa kwa kunichangua kuwa Mbunge wao jambo ambalo limenipa heshima ya kitaifa ya kuwa Naibu Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Madini, kwa wote nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hati idhini namba 144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017 majukumu ya Wizara ya Madini ni kama ilivyoainishwa kwenye hotuba.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; fedha za Maendeleo zilizopokelewa; katika Mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 7.04 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia febuari, 2020 Wizara haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, Wizara ilipokea fedha 0%. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali haingii akilini kwamba inatengewa shilingi bilioni saba lakini haikupokea fedha yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maelezo kutoka Serikalini kwamba katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 licha ya kutopokea fedha za maendeleo, Wizara iliendelea na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kutumia fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) na kwamba fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 2.84 ziliwekwa katika akaunti ya amana wakati wa kufunga mradi mwezi Desemba, 2018 kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea. Ukweli ambao haubishaniwi hapa ni kwamba

Serikali imeshindwa kutoa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza inataka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwanini hadi Februari, 2020 Wizara ilikuwa haijapata fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu sasa mfululizo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara hii. Mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Madini kwa 3.83%, peke yake. Mwaka wa fedha 2018/2019 hali ikawa mbaya zaidi, Serikali sasa ilitoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa asilimia 0.5% ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo. Mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali haijatoa fedha yoyote (0%). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kutoka Serikalini sababu hasa za kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kwenye Wizara hii kwa miaka mitatu mfululizo ni zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, unaelekeza kwamba Serikali itatenga 40% ya bajeti yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni kwa nini dhana hii isitekelezwe kwenye sekta mbalimbali za Wizara. Haiwezekani kwa bajeti ya taifa kufikia lengo hilo wakati Wizara haitengi 40% ya bajeti yake kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Utaratibu wa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya matumizi mengineyo, ni utaratibu ambao haulisaidii taifa hili na unapaswa kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa ajili ya mwaka 2020/2021. Wizara ya Madini inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 62.8 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha shilingi bilioni 8.5 sawa na asilimia 13.54 ya bajeti yote ni fedha kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo; na shilingi bilioni 54.3 sawa na asilimia 86.46 ya bajeti yote ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya

fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi bilioni 21.05 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi 33.24 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maombi hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

(i) Kuhusu Miradi ya Maendeleo. Ikiwa Wizara ilishindwa kupata fedha hata shilingi moja kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imewezaje kuongeza bajeti ya fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka shilingi bilioni 7.04 kwa mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 8.5 kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la 20.74%?

Ikiwa Wizara imeomba kiasi hiki, tunasisitiza kwamba kiasi hiki cha fedha kitoke kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Serikali imeshindwa kutoa fedha za maendeleo. *(Makofi)*

(ii) Kuhusu fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ujumla wake. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoombwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni shilingi bilioni 42.43 na mwaka huu 2020/2021 fedha inayoombwa kwa ajili ya fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 54.3...

SPIKA: Mheshimiwa Joseph Haule, nilitaka tu *pull attention* ya *Chief Whip* wa Upinzani, unaona anavyoshuka na tarakimu na nini, kumbe mambo haya mnayaweza bwana, si unaona uchambuzi huo, endelea kuchambua bwana, siyo unapiga ngojera tu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. JOSEPH L. HAULE - K.n.y. MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba utunze muda wangu.

SPIKA: Mheshimiwa Joseph, hii safi kabisa bwana, muda wako nautunza usiwe na wasiwasi.

MHE. JOSEPH L. HAULE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Nakusifia tu kwamba mtu anaelewa unachokiongea ni kitu gani endelea.

MHE. JOSEPH L. HAULE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

(ii) Kuhusu fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ujumla wake. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyooombwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni shilingi bilioni 42.43 na mwaka huu 2020/2021 fedha inayoombwa kwa ajili ya fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 54.3. Kiasi hiki kinachoombwa kimeongezeka kwa shilingi bilioni 11.9. Hivi kuna matumizi gani yameongezeka kwa Wizara hii kwa kiasi cha shilingi bilioni 11.9?. *(Makofi)*

(iii) Kuhusu fedha za Mishahara ya Watumishi. Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini yake ilikuwa shilingi bilioni 16.5 na bajeti inayoombwa kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 ni shilingi bilioni 21.05 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Maombi haya yana ongezeko la shilingi bilioni 4.6. Katika mazingira ambayo Serikali haijatao ajira kwa Watanzania, watumishi mbalimbali hawajapandishwa mishahara na madaraja, tulitarajia gharama za mishahara itapungua lakini kinyume chake bajeti inapanda kwa takribani shilingi bilioni 4.6.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kiasi hiki cha shilingi bilioni 4.6 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi gani walioongezeka? *(Makofi)*

(iv) Kuhusu fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Mwaka wa fedha 2019/2020 fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ilikuwa ni shilingi bilioni 25.5 na kwa mwaka 2020/2021, Wizara inaomba jumla ya shilingi bilioni 33.24 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Maombi haya yameongezeka kwa shilingi bilioni 7.28 ambazo hazina maelezo ya nini kimeongeza matumizi kwa takribani shilingi bilioni 7.3. Kambi Rasmi inataka maelezo ya kina kuhusu ongezeko hili kubwa la fedha.

Mheshimwa Spika, makubaliano ya Tanzania na Kampuni za Uchimbaji Madini. Pamoja na Serikali kuingia makubaliano na kampuni ya *Barrick Gold Corporation* na hatimaye kuundwa kwa kampuni ititwayo *Twiga Mineral Corporation*, ikumbukwe historia ya jambo hili ilitokana na Serikali kuzuia usafirishwaji wa mchanga wa makinikia nje ya nchi na hivyo kupelekea kuundwa kwa Kamati mbili ambazo ni kamati ya Mruma na Osoro. Kamati hizi zilibainisha ukwepaji wa kodi na utoroshwaji wa madini yenye thamani ya bilioni 190 Dola za Kimarekani ambazo ni sawa na trilioni 426. Madai ya Kamati hizi yalithibitishwa pia na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleleza Bunge lako Tukufu ni lini kiasi hicho cha fedha kitalipwa kwa Serikali ili fedha hizo zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo. Je, wahusika wote waliohusika wamechukuliwa hatua gani? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kupitia aliyekuwa Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Prof. Kabudi, ilikuwa ni kwamba kabla ya kuanza majadiliano hayo, Kampuni ya BARRICK italipa fedha za utangulizi alizozita kishika uchumba, Dola za Kimarekani milioni mia tatu (300) sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 600. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu ni kwa nini Serikali ilianza mazungumzo hayo kabla ya kulipwa kiasi hicho cha fedha? Pili Serikali iliambie Bunge lako Tukufu ni lini kiasi hicho cha fedha kitalipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(1) cha Sheria ya *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty*

kimezuia makinikia kusafirishwa nje ya nchi na kuyataka makampuni yanayochimba madini kujenga mtambo wa kuchenjua makinikia. Taarifa za sasa zinaonesha kwamba Serikali imeruhusu makinikia yaliyokuwa yanashikiliwa bandari ya Dar es Salaam kusafirishwa nje ya nchi kinyume na matakwa ya kifungu cha 9(1). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili yafuatayo:-

(i) Ni kwa nini Serikali imeruhusu makinikia hayo kusafirishwa nje ya nchi kinyume na matakwa ya kifungu cha 9(1)? *(Makofi)*

(ii) Kwa nini miaka miwili na zaidi baada ya jambo hili kutokea *smelter* haijajengwa na wala hakuna taarifa wala dalili za kujengwa kwa mtambo huo kama makubaliano yalivyokuwa? *(Makofi)*

(iii) Nini mpango wa Serikali kuhusu wafanyakazi wa Tanzania zaidi ya 2,000 waliopoteza ajira kutokana na mgodi wa Bulyanhulu uliokuwa unazalisha makinikia kufungwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano baina ya Serikali na BARRICK, moja ya makubaliano ilikuwa Tanzania kufaidika kwenye faida za kiuchumi kwa uwiano wa 50 kwa 50. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuwa hizo faida za kiuchumi ni zipi? Pili, ni utaratibu gani unaotumika ili kufikia huo mgao wa 50 kwa 50? Tatu, Serikali iwaambie Watanzania hadi sasa tumeshapata asilimia ngapi ya hizo faida za kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu ni lini itaanzisha majadiliano na makampuni yote yanayofanya shughuli za uchimbaji wa madini ili kuendana na matakwa ya sheria mpya ambazo ni *“The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act ya mwaka 2017 na “The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act 2017 (“Contract Review Act”).* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa Madini Tanzaniaite. Biashara ya madini ya tanzanite inadorola na madini ya tanzanite yanaendelea kushuka bei na wachimbaji wengi wanakata tamaa. Zipo taarifa kwamba kabla ya janga la *Corona* madini ya tanzanite yalishashuka bei kwa zaidi ya asilimia 50 lakini sasa madini hayo yameshuka kwa zaidi ya asilimia 70. Kitendo hiki kimepelekea hofu iliyotanda kwenye madini ya tanzanite. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo ya kushuka kwa thamani ya madini ya tanzanite ni kuwa na mashaka ya uwekezaji (*uncertainty*) na kuondoka kwa wanunuzi wakubwa wa madini hayo *master dealer* kuweka vituo vyao vya biashara nchini Kenya na wengine wameacha kabisa biashara hii. Ni bahati mbaya kuwa Serikali haitambui kuwa kutotabirika kwa mazingira ya biashara kunaua biashara kuliko hata wingi wa kodi pamoja na ukosefu wa amani kwa wafanyabiashara. Mwenendo wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Maafisa Madini kuwanyanyasa na kuwatisha wafanyabiashara imeondoa kabisa morali ya biashara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatambua wafanyabiashara wote nchini, wakiwemo wafanyabiashara ya madini kama wadau wakubwa wa biashara nchini. Aidha, ujengwe utamaduni wa migogoro ya kodi iendeshwe na sheria za kodi tofauti na sasa ambako TAKUKURU na Ofisi ya *DPP* kuichukulia migogoro ya kikodi kama makosa ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi, jambo ambalo limefanya wafanyabiashara kuogopa kuja kuwekeza Tanzania kwa sababu jambo dogo la kutatuliwa na Baraza la Kodi la Usuluhishi wa Migogoro linaweza kumsababishia mfanyabiashara kuwekwa ndani na kukosa dhamana kwa makosa ya uhujumu uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *STAMICO*. *STAMICO* inamiliki makampuni kadhaa ya madini yakiwemo *STAMIGOLD*, Buhemba Gold, Makaa ya Mawe Kiwira kwa lengo la kuyaendesha kifaida. Miongoni mwa changamoto

zinazoikabili *STAMICO* ni uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika kuendesha shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba *STAMICO* imeshindwa kununua mtambo wa kusaga kokoto zilizotakiwa kwa ajili ya mradi wa *Standard Gauge Railway* kwa gharama ya Dola za Kimarekani 200,000 na hivyo kupoteza mteja muhimu na mapato ambayo shirika lingepata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata na taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa nyakati mbalimbali, *STAMIGOLD* kampuni tanzu ya *STAMICO*, imekuwa inajijendesha kwa hasara takribani miaka mitatu iliyopita kutokana na madeni, uwekezaji mdogo na kampuni kutofanya shughuli za uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kwamba Serikali haifanyi vizuri kuhusu *STAMICO*, pamoja na changamoto zinazozikabili Shirika la Madini la Taifa na ikizingatiwa kwamba shirika linajijendesha kwa hasara, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafuatayo:-

(a) Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwa *STAMICO* ikiwa ni pamoja na kuipa ruzuku na pia kuchukua dhamana ya madeni yanayoikabili ili iweze kuwa na uwezo wa kujiimarisha kifedha ili kumudu gharama za uzalishaji.

(b) *STAMICO* ifanyiwe mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo ili iwe kampuni hodhi (*holding company*) inayoweza kumiliki hisa au sehemu ya umiliki katika makampuni mengine ya migodi na pia iweze kukuza mtaji kwa kuingia makubaliano ya kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kumaliza hotuba yangu kwa kusisitiza mambo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa huu ni mwaka wa mwisho wa kipindi cha miaka mitano kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano, Kambi

Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaambie Watanzania hatma ya majadiliano na Kampuni ya ACACIA na fedha ambazo ilipaswa kulipwa kama zimeshalipwa kwa sababu ni jambo ambalo umma wa Watanzania ulishirikishwa tangu mwanzo. Ikiwa bado hazijalipwa ni kwa nini fedha hizo hazijalipwa? Ikiwa Makampuni haya yalikuwepa kodi kama ambavyo Watanzania tuliambiwa ni kwa nini hadi sasa bado hayalipa fedha hizo? Ikiwa Serikali iliudanganya umma, ni lini sasa Serikali itatoa taarifa sahihi kuhusu fedha hizo? *(Makofi)*

(ii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako Tukufu sababu za kutopeleka fedha yoyote kwenye Miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kwamba Bunge hili lilipitisha na kuidhinisha jumla ya shilingi bilioni 7.04 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

(iii) Serikali iliambie Bunge hili Tukufu sababu ya Wizara hii kuwa na ongezeko la shilingi bilioni 11.85 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida wakati Serikali hajatoa ajira kwa Watanzania, watumishi mbalimbali hawajapandishwa mishahara na madaraja, tulitarajia gharama za mishahara itapungua lakini kinyume chake bajeti inapanda takribani shilingi bilioni 4.6.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kiasi hiki cha shilingi bilioni 4.6 zimetegwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi gani walioongezeka? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua sababu inayopelekea ongezeko la bajeti ya Matumizi Mengineyo *(OC)* kwa kiasi cha shilingi bilioni 7.28. *(Makofi)*

(iv) Kambi Rasmi Bungeni inataka kujua ni lini wananchi walioathirika na maji ya sumu kutoka Mgodu wa North Mara watalipwa fedha kama sehemu ya fidia ya madhara walioyapata kwa kipindi kirefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni,

naomba kuwasilisha, lakini pia naomba hotuba yetu yote iweze kuingia kwenye Kumbukumbu za Bunge *Hansard*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**HOTUBA YA MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI, MHESHIMIWA JOHN
HECHE (MB), AKIWASILISHA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA
BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA,
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Madini, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni hayo napenda kutumia fursa hii kuwapa pole wananchi wote walioathirika kwa namna moja au nyingine na janga la Corona lililoikumba nchi yetu. Aidha kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni napenda neno la faraja kwa Watanzania wote kuwa na subra katika kipindi hiki kigumu na kwamba waendeele kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Corona kama inavyoelekezwa na wataalamu wa afya na wanaendeele kumtumaini Mungu ili aliepushe Taifa na janga hili.

3. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutambua uwezo wangu na kuniamini na kunitiua kuwa Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

katika Wizara hii. Aidha namshukuru Waziri Kivuli mwenye dhamana hii, Mheshimiwa John Heche (Mb) kwa kunipa heshima ya kusoma hotuba hii kwa niaba yake

4. Mheshimiwa Spika, Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wasemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara mbalimbali pamoja na wasaidizi wao kwa kuaminiwa na kuteuliwa katika nafasi walizo nazo. Ninawatakia kila la kheri katika majukumu haya ya kuwatumikia Watanzania na Taifa hili kwa ujumla.

5. Mheshimiwa Spika, sitawatendea haki wananchi wa Jimbo la Mikumi kama nisipowashukuru kwa heshima kubwa waliyonipa ya kunichagua kuwa Mbunge wao, jambo ambalo limenipa heshima ya kitaifa ya kuwa Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Nishati na Madini, kwao wote nasema asante sana.

6. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini Na.144 ya tarehe 22 Aprili, 2016 iliyofanyiwa marekebisho tarehe 15 Oktoba, 2017 majukumu ya Wizara ya Madini ni:

- i. Kubuni, kuandaa na kusimamia sera,
- ii. Kuandaa mikakati na mipango ya kuendeleza sekta ya madini,
- iii. Kusimamaia migodi na kuhamasisha shughuli za uchimbaji pamoja na utafutaji wa madini kwa kutumia tafiti za kijiofizikia na kijiolojia,
- iv. Kuratibu na kusimamia uongezaji thamani madini kwenye biashara ya madini,
- v. Kukuza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini nchini,
- vi. Kusimamia na kuratibu shughuli na maendeleo ya wachimbaji wadogo,

vii. Kusimamia taasisi na mamlaka zilizoko chini ya Wizara pamoja na kuratibu na kusimamia maendeleo na utekelezaji majukumu kwa watumishi wa Wizara. Aidha Wizara pia inasimamia taasisi sita ambazo ni Tume ya Madini Tanzania, Chuo cha Madini, Kituo cha Jemolojia Tanzania na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative-TEITI).

7. Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni moja ya Wizara muhimu miongoni mwa Wizara zinazosimamia rasilimali za Taifa, ambazo kama zingetumika ipasavyo taswira ya Taifa hili ingekuwa inafanana na utajiri mkubwa wa rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu amelijalia Taifa hili. Lakini katika hali ambayo inashangaza, ni jambo la kawaida kuona maisha ya wananchi wetu yakiwa duni, huduma za afya zisizoridhisha, miundombinu mibovu, huko vijijini upatikanaji wa maji ni shida, yote haya unaweza kujiuliza yanawezekanaje katika Taifa ambalo limejaliwa neema ya rasilimali ikiwemo madini.

8. Mheshimiwa Spika, Jawabu kwa matatizo hayo ni moja tu, nalo ni sera za CCM zisizowanufaisha Watanzania. Kwa kutambua hilo sisi CHADEMA kama chama kinachojiandaa kuchukua Serikali, tumeandaa sera mbadala, Toleo la Julai, 2018 kuhusu usimamizi madhubuti na endelevu wa sekta ya madini; kwamba Serikali chini ya CHADEMA itahakikisha inafanya mambo yafuatayo:

i. CHADEMA itahakikisha Sekta ya Madini inasimamiwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi.

ii. CHADEMA itahakikisha inarekebisha sheria zote zinazosimamia madini.

iii. CHADEMA itahakikisha tunaanzisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo kwa ajili ya kutunza kiwango cha faida inayotokana na madini, mafuta na gesi ili zitumike kwa maendeleo ya vizazi vijavyo hata baada ya rasilimari hizi kuisha. Jambo kama hili linafanyika Norway kwenye Mfuko wa Gesi na Botswana kwenye madini ya Vito.

iv. Itahakikisha kwamba uwepo wa madini unatumika kama dhamana kwa ajili ya Serikali kupata fedha za kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni endelevu.

v. CHADEMA itahakikisha inatoa mikopo kwa wachimbaji wadogo na wa kati, kwa ajili ya kufanya tafiti, kuendeleza na kuchimba madini.

vi. CHADEMA itahakikisha kunakuwepo na mkakati wa kurudisha mazingira katika hali yake ya kawaida baada ya shughuli za uchimbaji.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

9. Mheshimiwa Spika, Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **49,466,898,200.00** Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi **7,039,810,200.00** fedha za ndani sawa na 14% zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kiasi cha shilingi **42,427,088,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida shilingi **25,953,263,000.00** (OC) zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **16,473,825,000.00** zilitengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizochini ya Wizara.

10. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanywaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilipangiwa kukusanya **shilingi 470,897,011,000.00** kutokana na vyanzo mbalimbali katika jitihada za kuhakikisha sekta ya madini inaongeza mchango wake katika Pato la Taifa.

i. Fedha za Maendeleo Zilizopokelewa

11. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara iliomba na kuidhinishiwa jumla ya shilingi **7,039,810,200.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; hadi kufikia Februari, 2020 Wizara haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya

miradi ya maendeleo kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili. Kwa maneno mengine Wizara ilipokea fedha (0%). Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali, haiingii akilini kwamba inatengewa shilingi Bil 7 lakini haijapewa fedha yoyote.

12. Mheshimiwa Spika, Yapo maelezo kutoka kwa Serikali kwamba katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Februari, 2020 licha ya kutopokea fedha za maendeleo, Wizara iliendelea na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kutumia fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP). Na kwamba fedha hizo kiasi cha **Shilingi 2,839,151,286.14** ziliwekwa katika Akaunti ya Amana wakati wa kufunga mradi mwezi Desemba, 2018 kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea.

13. Mheshimiwa Spika, Shughuli hizo zimetajwa kuwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Katente na Itumbi, vituo vya umahiri vya Songea na Chunya. Lakini pia, ujenzi wa kituo cha pamoja cha Mirerani kwamba shughuli za uwekaji wa mfumo wa ulinzi na kamera za usalama pamoja na miundombinu ya umeme kuzunguka ukuta wa Mirerani zilifanyika kwa kutumia fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 3,358,024,278.25**.

14. Mheshimiwa Spika, Ukweli ambao haubishaniwi hapa ni kwamba Serikali imeshindwa kutoa fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Kwetu sisi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaona sasa uwezo wa Wizara umefikia kikomo, na ili tuweze kutekeleza majukumu yetu yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali kupitia Wizara ya Madini walieleze Bunge lako tukufu ni kwa nini hadi mwezi Februari, 2020 Wizara ilikuwa haijapata fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge hili.

15. Mheshimiwa Spika, hata hivyo kiasi cha fedha kilichotumika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa gharama za shilingi Shilingi **2,839,151,286.14** na kiasi kingine cha shilingi **3,358,024,278.25**. kilitolewa bila kuidhinishwa na Bunge hili.

Kwa utaratibu huu, kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ikisema Serikali inalizarau Bunge tutakuwa tumekosea?

16. Mheshimiwa Spika, takwimu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonesha kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kupeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo ya Wizara hii. Mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali ilitoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Madini kwa 3.83%, mwaka wa fedha 2018/2019 hali ikawa mbaya zaidi, Serikali sasa ilitoa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa asilimia 0.5%. ya bajeti yote ya Miradi ya Maendeleo iliyopangwa na kupitishwa na Bunge na kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali haijatoa fedha yoyote (0%). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu kutoka Serikalini sababu hasa za kushindwa kupeleka fedha za maendeleo kwenye Wizara hii kwa miaka mitatu mfululizo?

17. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utangulizi wa Randama ya Wizara ya Madini, Fungu 100 inaeleza kwamba katika kuandaa Mpango na Bajeti wa mwaka 2020/2021 na miaka mingine iliyopita Wizara imekuwa ikizingatia miongozo mbalimbali ya Kitaifa. Na kwa kuwa moja ya miongozo iliyotajwa kuzingatiwa ni pamoja Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020; Hivyo basi ni dhahiri kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kusema kwamba, sera zisizo na tija na ambazo zimeshindwa kutekelezeka ni pamoja na Ilani yenyewe na hivyo Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo imetekeleza Miradi ya Maendeleo chini ya 4% ya bajeti yote iliyotengwa kwa ajili ya miradi husika.

18. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, unaelekeza Bajeti ya Taifa kutenga 40% ya bajeti yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni kwa nini dhana hii isitekelezwe kwenye sekta mbalimbali za Wizara. Haiwezekani kwa bajeti ya Taifa kufikia lengo hilo wakati Wizara haitengi 40% ya bajeti yake kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Utaratibu wa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya matumizi

mengineyo, ni utaratibu ambao haulisaidii taifa hili na unapaswa kubadilishwa.

19. Mheshimiwa Spika, CHADEMA baada ya kugundua kwamba Serikali inapeleka na wakati mwingine haipeleki kabisa fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishiwa na Bunge lako tukufu, na kwamba kutokupeleka kwa fedha hizo ni matokeo ya sera mbaya za Serikali ya CCM ambazo zinasababisha Serikali hii kukosa fedha za kupeleka kwenye miradi ya maendeleo. Ndiyo sababu **CHADEMA katika Sera Mbadala** kama tulivyoainisha katika aya ya 8, tunatarajia kuanzisha Mfuko Maalumu wa Fedha zinazotokana na uwekezaji wa madini ili zitumike katika miradi mikubwa yenye manufaa kwa nchi na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi, sera hii itaondoa tatizo la Serikali kushindwa kupeleka Fedha za Miradi ya Maendeleo kama ilivyo sasa.

ii. Maombi ya fedha kwa ajili ya mwaka 2020/2021

20. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 62,781,586,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake. Kati ya fedha **Shilingi 8,500,000,000.00** sawa na **asilimia 13.54** ya Bajeti yote ni fedha kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo; na **Shilingi 54,281,587,000** sawa na **asilimia 86.46** ya bajeti yote ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 21,045,927,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 33,235,659,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

21. Mheshimiwa Spika, kutokana na maombi hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata ufafanuzi wa mambo yafuatayo:

i. Kuhusu miradi ya maendeleo: Ikiwa Wizara ilishindwa kupata fedha hata shilingi moja kwa ajili ya Miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imewezaje kuongeza bajeti ya fedha za Miradi ya Maendeleo kutoka **Shilingi 7,039,810,200.00** kwa mwaka 2019/2020 hadi **Shilingi 8,500,000,000.00** kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko

la 20.74%? Ikiwa Wizara imeomba kiasi hiki tunasisitiza kwamba kiasi hiki cha fedha kitoke kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo Serikali imeshindwa kutoa fedha za maendeleo.

ii. Kuhusu fedha za Matumizi ya Kawaida kwa ujumla wake:

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyooombwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikuwa ni **Shilingi 42,427,088,000.00** na mwaka huu 2020/2021 fedha inayoombwa kwa ajili ya fedha za matumizi ya kawaida ni **Shilingi 54,281,587,000.00**. Kiasi hiki kinachoombwa kimeongezeka kwa **Shilingi 11,854,499,000.00**, hivi Mheshimiwa Spika, kuna matumizi gani yameongezeka kwa Wizara kwa **bilioni 11.9?**

iii. Kuhusu fedha za Mishahara ya watumishi:

Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini yake ilikuwa **Shilingi 16,473,825,000.00** na Bajeti inayoombwa kwa mwaka huu wa fedha, 2020/2021 ni **Shilingi 21,045,927,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara. Maombi haya yanaongezeko la **Shilingi 4,572,102,000.00**. Katika mazingira ambayo Serikali hajatoa ajira kwa Watanzania, watumishi mbalimbali hawajapandishwa mishahara na madaraja, tulitarajia gharama za mishahara itapungua lakini kinyume chake bajeti inapanda kwa takribani bilion 4.6; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kiasi hiki cha Bilioni 4.6 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mishahara watumishi gani walioongezeka?

iv. Kuhusu fedha kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC);

Mwaka wa fedha 2019/2020 fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ilikuwa ni **Shilingi 25,953,263,000.00** na kwa mwaka 2020/2021 Wizara inaomba jumla ya **Shilingi 33,235,659,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Maombi haya yameongezeka kwa **Shilingi 7,282,396,000.00** ambazo hazina maelezo ya nini kimeongeza matumizi kwa takribani **bilioni 7.3** Kambi Rasmi inataka maelezo ya kina kuhusu ongezeko hili kubwa la fedha.

C. MABADILIKO KATIKA SHERIA ZA RASILIMALI MADINI NA HOFU YA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI

22. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ya Serikali kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya madini, mabadiliko hayo yamezua hofu kubwa kwa wawekezaji na wabia wa sekta hii. Hofu inatokana na maamuzi mengi kufanywa nje ya mfumo wa kisheria. Aidha ili kwa nchi kunufaika kwa muda mrefu, inatakiwa sera na sheria zinazolenga mafanikio ya muda mrefu ujao bila mabadiliko ya mara kwa mara. Mabadiliko ya mara kwa mara yanayotokana na malengo ya muda mfupi yanakwamisha uwekezaji wenye tija.

23. Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuandaa mjadala wa kitaifa utakaotufikisha kuwa na dira ya sekta ya madini (County Mining Vision), ili kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji na kuwaondolea mkanganyiko watendaji wanaosimamia sekta hii. Hii pia itaendana na Dira ya Kuendeleza Madini Afrika (Africa Mining Vision) iliyopitishwa na Viongozi wa Afrika 2009.

D. MAKUBALIANO YA TANZANIA NA KAMPUNI ZA UCHIMBAJI MADINI

24. Mheshimiwa Spika, Pamoja na Serikali kuingia makubaliano na Kampuni ya Barrick Gold Corporation na hatimaye kuundwa kwa Kampuni iitwayo Twiga Mineral Corporation; ikumbukwe historia ya jambo hili ilitokana na Serikali kuzuia usafirishwaji wa mchanga wa makinikia nje ya nchi na hivyo kupelekea kuundwa kwa Kamati mbili ambazo ni Kamati ya Mruma na Osolo.

25. Mheshimiwa spika, Kamati hizi zilibainisha ukwepaji wa kodi na utoroshwaji wa madini yenye thamani ya bilioni 190 dola za Kimarekani ambazo ni sawa na trilioni 426. Madai ya kamati hizi yalithibitishwa pia na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA). Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni lini kiasi hicho cha fedha kitalipwa kwa Serikali ili fedha hizo zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo;

na je, wahusika wote waliohusika wamechukuliwa hatua gani.

26. Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali kupitia aliyekuwa Waziri Katiba na Sheria Profesa Kabudi, ilikuwa ni kwamba kabla ya kuanza majadiliano hayo, Kampuni ya Barrick italipa fedha za utangulizi alizoziita kishika uchumba, dola za Kimarekani milioni mia tatu (300) sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 600. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako tukufu; ni kwa nini Serikali ilianza mazungumzo hayo kabla ya kulipwa kiasi hicho cha fedha. Pili Serikali iliambie Bunge lako tukufu ni lini kiasi hicho cha fedha kitalipwa.

27. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(1) cha Sheria ya The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act kimezuia makinikia kusafirishwa nje ya nchi na kuyataka makampuni yanayochimba madini kujenga mtambo wa kuchenjua makinikia. Taarifa za sasa zinaonesha kwamba Serikali imeruhusu makinikia yaliyokuwa yanashikiliwa bandari ya Dar Es Salaam kusafirishwa nje ya nchi kinyume na matakwa ya kifungu cha 9(1). Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili:-

i. Kwa nini Serikali imeruhusu makinikia hayo kusafirishwa nje ya nchi kinyume na matakwa ya kifungu cha 9(1).

ii. Kwa nini miaka miwili na zaidi baada ya jambo hili kutokea smelter haijajengwa na wala hakuna taarifa wala dalili za kujengwa kwa mtambo huo kama makubaliano yalivyokuwa.

iii. Nini mpango wa Serikali kuhusu wafanyakazi wa Tanzania zaidi ya 2000 waliopoteza ajira kutokana na mgodi wa Bulyankulu uliokuwa unazalisha makinikia kufungwa.

28. Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano baina ya Serikali na Barrick, moja ya makubaliano ilikuwa Tanzania kufaidika kwenye faida za kiuchumi kwa uwiano wa 50 kwa 50. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi kuwa hizo faida za kiuchumi ni zipi; **Pili** ni utaratibu

gani unaotumika ili kufikia huo mgao wa 50 kwa 50. **Tatu**, Serikali iwaambie Watanzania hadi sasa tumeshapata asilimia ngapi ya hizo faida za kiuchumi.

29. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuliambia Bunge lako tukufu ni lini itaanzisha majadiliano na makampuni yote yanayofanya shughuli za uchimbaji wa madini ili kuendana na matakwa ya sheria mpya ambazo ni "The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act ya mwaka 2017 ("Sovereignty Act") na "The Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act 2017 ("Contract Review Act").

30. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2017 Bunge lako tukufu lilitunga na kupitisha sheria mbili zilitwazo The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act 2017 ("Sovereignty Act") na "the Natural Wealth and Resources (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act 2017 ("Contract Review Act"). Mojawapo wa malengo ya sheria zile ni kuhakikisha kuwa Tanzania tunanufaika ipasavyo na rasilimali zetu, na kuzuia migogoro ya kibiashara kati yetu na wawekezaji kutopelekwa nje ya nchi.

31. Mheshimiwa Spika, tukitoa maoni yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tulishauri jambo hili kuangaliwa kwa upana wake bila mafanikio. Pamoja na kutochukuliwa kwa maoni yetu kama Kambi, mchakato wa upitishwaji wa sheria zile uliliaminisha Taifa kuwa kuanzia muda huo tutaweza kufanya maamuzi kuhusu madini yetu bila uoga wowote.

32. Mheshimiwa Spika, Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kwamba, utekelezwaji wa nia ya kutatua migogoro baina ya wawekezaji wa nje na Tanzania kwa kutumia mahakama zetu za ndani chini ya kifungu cha 11 cha sheria ya "The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty) Act" katika mazungumzo kati ya Serikali yetu na Barrick Gold Corporation, unaonekana kukwama.

33. Mheshimiwa Spika, Taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka vyanzo vyake zinadai kwamba mawasiliano kwa nyakati mbalimbali kati ya Barrick Gold na wadau wake yanaonyesha kuwa Tanzania imekubali kuwa migogoro itakayozuka kuhusu uendeshaji wa Twiga Mineral ipelekwe kwenye utaratibu wa utatuzi wa migogoro nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua sababu hasa za Tanzania kukubali kutumia mahakama za nje ya nchi kutatua mgogoro utakaozuka wakati awali ilikataa mapendekezo yaliyohusiana na kifungu cha 11 cha Sheria ya Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act.

34. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba ni bora Serikali ianze sasa kukubali ushauri unaotolewa na wadau mbalimbali yakiwemo maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni linapokuja suala linalohusu maslahi mapana ya Taifa hili. Hoja inatokana na ukweli kwamba Tanzania siyo kisiwa na hivyo haiwezi kuwa na utaratibu wa peke yake. Tusione aibu kufanya marekebisho ya Sheria zetu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

E. UCHIMBAJI WA MADINI YA TANZANITE

35. Mheshimiwa Spika, Biashara ya madini ya Tanzanite ina dorora na madini ya Tanzanite yanaendelea kushuka bei na wachimbaji wengi wana kata tamaa. Zipo taarifa kwamba kabla ya Corona virus pandemic madini ya Tanzanite yalishashuka bei kwa zaidi ya asilimia 50, lakini sasa madini hayo yameshuka kwa zaidi ya asilimia 70, kitendo hiki kimepelekea hofu iliyotanda kwenye madini ya Tanzanite kuwa kubwa sana.

36. Mheshimiwa Spika, Uchimbaji wa madini ya Tanzanite unawezekana tu pale ambapo madini haya yatakuwa na thamani kubwa kwani gharama za uchimbaji ni ghali sana kulinganisha na madini mengine ya vito.

37. Mheshimiwa Spika, Sababu mojawapo ya kushuka kwa thamani ya madini ya Tanzanite ni kuwa na mashaka ya uwekezaji (uncertainty) na kuondoka kwa wanunuzi

wakubwa wa madini hayo (master dealer) kuweka vituo vyao vya biashara nchini Kenya na wengine wameacha kabisa biashara hii. Ni bahati mbaya kuwa Serikali haitambui kuwa kutotabirika kwa mazingira ya biashara kunaua biashara kuliko hata wingi wa kodi pamoja na ukosefu wa amani kwa wafanyabiashara, mwenendo wa Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Maafisa Madini kuwanyanyasa na kuwatisha wafanyabiashara imeondoa kabisa morali ya biashara hii.

38. Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo huo, Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatambua wafanyabiashara wote nchini wakiwemo wafanyabiashara ya madini kama wadau wakubwa wa biashara nchini. Aidha, ujengwe utamaduni wa migogoro ya kodi iendeshwe na sheria za kodi tofauti na hali ya sasa ambako TAKUKURU na Ofisi ya DPP kuichukulia migogoro ya kikodi kama makosa ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi, jambo ambalo limefanya wafanyabiashara kuogopa kuja kuwekeza Tanzania kwa sababu jambo dogo la kutatuliwa na Baraza la Kodi la Usuluhishi wa Migogoro linaweza kumsababishia mfanyabiashara kuwekwa ndani na kukosa dhamana kwa makosa ya uhujumu uchumi.

39. Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wakiwemo wa madini wameamua kuacha kufanya biashara hii na kulazimika kuanzisha biashara ambazo hazina madhira kama yanayowakumba wafanyabiashara za madini hapa nchini.

40. Mheshimiwa Spika, Uchimbaji wa Tanzanite Mererani pamoja na hoja zilizoainishwa hapo juu, umegubikwa na sintofahamu baada ya Wizara ya Madini kusitisha majadiliano kati ya Serikali na Kampuni ya TanzaniteOne na badala yake Leseni ya Kitalu C iliyokuwa inamilikiwa na Sky Associate kwa ubia na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) mnamo Machi, 2020.

41. Mheshimiwa Spika, Taarifa za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba, yapo madai kutoka Wizara ya Madini kuwa ufutaji wa leseni hiyo ulikuja kufuatia maelekezo ya Kamati Maalum ya Bunge iliyoundwa kuchunguza biashara

ya madini ya Tanzanite kubaini kuwa leseni hiyo ilitolewa kinyume cha sheria. Ikiwa madai haya yana ukweli, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tulitarajia na bado tunategemea kupitia Bunge hili, Wizara italiambia Bunge hili tukufu ni akina nani walihusika na maamuzi hayo na hatua gani zilizochukuliwa dhidi yao.

42. Mheshimiwa Spika, Hata hivyo kumekuwa na kauli kinzani toka Tume ya Madini kuwa, Tume ya Madini ndiyo iliyofuta Leseni ya Tanzanite mnamo tarehe 23 Desemba, 2019 baada ya Kampuni ya TML kuandika barua Serikalini Desemba 10 kuomba kuachia eneo hilo na mbia mwenza STAMICO aliridhia ombi hilo Desemba 19, 2019. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni hasara kiasi gani nchi imepata kwa kusitisha uzalishaji wa mgodi wa TanzaniteOne na Serikali imechukua hatua gani kuwasaidia wafanyakazi 420 stahiki zao baada ya mgodi kufungwa. Serikali ina mpango gani wa kuanza uzalishaji kwenye mgodi huo baada ya kufungwa kwa takribani miaka minne iliyopita.

F. MAPITIO YA TAASISI ZILIZOCHINI YA WIZARA YA MADINI

i. Tume ya Madini

43. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini 2010 kama ilivyofanyiwa Marekebisho na Sheria Na. 7 ya mwaka, 2017. Mamlaka ya kuanzisha Tume na majukumu yake yameainishwa katika kifungu cha 21 na kifungu cha 22, ambapo miongoni mwa majukumu ya Tume hiyo ni kusimamia, kuratibu, kupanga, kudhibiti na kutekeleza masuala na shughuli zote zinazohusu madini na pia kuishauri Serikali kuhusiana na shughuli zote zinazohusu Sekta ya Madini nchini.

44. Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini ni chombo chenye mamlaka kamili ya kushitaki au kushitakiwa pale inapobidi. Changamoto kubwa ambayo inaikabili tume ni kutokueleweka kwa Sheria ya Madini kwa wadau na wafanyabiashara, ambao husababisha ugumu kwa Tume kukusanya baadhi ya tozo mbalimbali zinazotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini.

45. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Wizara kuhakikisha Tume ya Madini kuwa na mkakati kabambe wa kutoa elimu kwa umma mara kwa mara. Aidha itumie njia mbalimbali kama vile televisheni, redio za kitaifa na kijamii pamoja na mitandao ya kijamii ili umma Watanzania uelimike kuhusu Sheria ya Madini na kazi na mamlaka ya Tume ya Madini.

iii. Taasisi ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (TEITI).

46. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2015 Tanzania ilipitisha Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015 (The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act 2015. Pamoja na uharaka uliotumika kupitisha sheria ile, kanuni zake zilitungwa mwezi wa pili 2019, takribani miaka minne baada ya kupitishwa kwa sheria mama. Hii inafuatia kuteuliwa kwa Ndugu Ludovick Utouh kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI, na kumrithi Mwenyekiti aliyemtangulia Mhe Jaji Mstaafu Mark Bomani mnamo Juni, 2018.

47. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba sheria haiwezi kutekelezwa bila kanuni zake. Kucheleweshwa kwa kanuni za sheria hii kwa kipindi chote hicho ni dalili ya udhaifu katika utekelezaji wa maamuzi mbalimbali na mambo mazito ya kitaifa. Ni vyema sasa sheria inapotungwa ikawekewa muda maalumu (time frame) kwa Waziri husika na kutengeza kanuni za sheria husika.

48. Mheshimiwa Spika, Licha ya sheria ya Uwazi na Uwajibikaji Katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015 (The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act 2015 na kutambulika kwa nafasi ya Kamati Tekelezi (TEITI Commitee) ambayo inapaswa kutekeleza malengo ya taasisi husika, Ila ukweli ni kwamba Kamati hii chini ya Ndugu Ludovick Utouh haina rasilimali na miundombinu inayoweza kuwahakikishia Watanzania usimamizi bora wa rasilimali zake. Kwa sasa taasisi hii haina

Mtendaji Mkuu kwa miaka miwili sasa wala ofisi maalum pamoja na vifaa. Aidha, pamoja na bajeti yake kupitishwa na Bunge lako, Kamati hii imeendelea kufanya kazi kwa hali ngumu kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Changamoto zote hizo zinapelekea taasisi hii kuwa kama mtoto yatima.

49. Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ni kwamba usaili wa nafasi ya Mtendaji Mkuu ulifanyaka tangu Mei 2019, lakini hadi sasa kilichokuwa kinahitajika ni uthibitisho kutoka kwa Waziri. Aidha kucheleweshwa kwa uthibitisho huo na kutokana na ushindani wa soko la ajira, taarifa zinaonesha kuwa aliyepaswa kuthibitishwa kuwa Mtendaji Mkuu ameshapata ajira sehemu nyingine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni kwa nini hadi sasa Waziri ameshindwa kuthibitisha Mtendaji Mkuu kwa kipindi cha miaka miwili sasa.

50. Mheshimiwa Spika, Pamoja na kwamba, Serikali ilijitoa kwenye makubaliano ya kimataifa ya kuendesha Serikali kwa uwazi (**Open Government Partnership**) katika mpango wa uwazi lakini inapaswa kutekeleza baadhi ya majukumu ambayo tayari kabla ya kusitishwa kwa mpango huo yalikuwepo. Kwa mantiki hiyo, Serikali kupitia Wizara ya madini iharakishe mchakato wa upatikanaji wa **Taarifa na Uwazi wa Mikataba ya Madini** na **Rasilimali Zingine** kwa kuzingatia kwamba msingi mkuu wa kuanzishwa TEITI ni kwa ajili ya kukuza na kuboresha uwazi na uwajibikaji katika uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia.

iv. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA – STAMICO

51. Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa STAMICO ni moja kati ya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini. Hili ni Shirikia linalomilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja, ambalo lilianzishwa rasmi mwaka 1972 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (1969). Mwaka 2015 Shirika lilifanyiwa marekebisho makubwa ya kimuundo (restructuring) chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (mabadiliko ya uanzishwaji wa mashirika ya umma) 2015.

52. Mheshimiwa Spika, STAMICO inamiliki makampuni kadhaa ya madini yakiwemo STAMIGOLD, Buhemba Gold, Makaa ya Mawe Kiwira kwa lengo la kuyaendesha kifaida. Miongoni mwa changamoto zinazoikabili STAMICO ni uhaba wa rasilimali fedha zinazohitajika kuendesha shirika hilo.

53. Mheshimiwa Spika, Jambo la kusikitisha ni kwamba STAMICO imeshindwa kununua mtambo wa kusaga kokoto zilizotakiwa kwa ajili ya mradi wa Standard Gauge Railway kwa gharama ya Dola za kimarekani 200,000 na hivyo kupoteza mteja muhimu na mapato ambayo shirika lingepata.

54. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata na taarifa ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa nyakati mbalimbali, STAMIGOLD kampuni tanzu ya STAMICO, imekuwa inajijendesha kwa hasara takribani miaka mitatu iliyopita kutokana na madeni, uwekezaji mdogo na kampuni kutofanya shughuli za uzalishaji.

55. Mheshimiwa Spika, Kifungu namba 9 cha Marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, kupitia Sheria ya marekebisho Anuai Sheria Na. 7, 2017, Sheria inaelekeza umiliki wa Serikali usiopungua asilimia 16 katika makampuni ya madini, hata hivyo kutokana na mapungufu ya kisheria na kikanuni, sheria na kanuni zake hazitoi mwongozo kuhusu mamlaka ipi ya Serikali itahusika na jukumu la kusimamia umiliki huo. Kutokana na upungufu huu, CHADEMA inakusudia kupitia sheria zinazosimamia madini kwa mujibu wa sera zake ili ziwe na manufaa kwa wawekezaji na uchumi wa nchi yetu.

56. Mheshimiwa Spika, Kutokana na kwamba Serikali haifanyi vizuri kuhusu STAMICO, pamoja na changamoto zinazozikabili Shirika la Madini la Taifa, na ikizingatiwa mwamba shirika linajijendesha kwa hasara, Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafutayo:-

a) Kwanza tunapendekeza Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwa STAMICO ikiwa ni pamoja na kuipa ruzuku na pia

kuchukua dhamana ya madeni yanayoikabili ili iweze kuwa na uwezo wa kujiimarisha kifedha ili kumudu gharama za uzalishaji.

b) STAMICO ifanyiwe mabadiliko makubwa ya kimuundo na kimfumo ili iwe Kampuni Hodhi (Holding Company) inayoweza kumiliki hisa au sehemu ya umiliki katika makampuni mengine ya migodi na pia iweze kukuza mtaji kwa kuingia makubaliano ya kimkakati.

57. Mheshimiwa Spika, tulipendekeza katika hotuba zetu za miaka iliyopita na sasa tunarejea tena kupendekeza kwamba STAMICO ifanyiwe mabadiliko na ipewe jukumu la kusimamia na kuratibu umiliki wa asilimia 16 za Serikali katika makampuni ya madini kwa niaba ya Serikali. Aidha, STAMICO ijitanue na kufanya utafiti na uwekezaji katika aina tofauti za madini kama vile "graphite", coal". Kwa ushauri huo tunapenda kupata majibu ya hatua zilizochukuliwa na Serikali hadi sasa.

G. UKAGUZI WA FEDHA NA TAARIFA KWENYE SEKTA YA UZIDUAJI

58. Mheshimiwa Spika, Kwa nyakati tofauti, Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amekuwa hapewi taarifa za kifedha na za kimikataba kutoka mashirika na makampuni ya sekta ya madini, na sekta nyingine kama mafuta na gesi asilia.

59. Mheshimiwa Spika, Changamoto hii imesababisha ofisi yake kushindwa kufanya ukaguzi kwa mujibu wa sheria. Aidha ili kuweza kuchochea ongezeko la uwazi na uwajibikaji kwenye sekta ya madini pamoja na sekta nyingine zinazogusa rasilimali za Taifa hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inashauri kwamba sheria zinazohusu rasilimali za nchi hii kama Sekta ya Madini, mafuta na gesi asilia zipitiwe upya ili kumpa mamlaka ya moja kwa moja Mkaguzi na Mdhibili Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata taarifa zitakazosaidia ukaguzi wake kwa maslahi mapana ya nchi.

H. MADAI YA FIDIA KWA WANANCHI WALIOATHIRIWA NA MAJI YA SUMU KUTOKA KATIKA MGODI WA DHAHABU WA ACACIA NORTH MARA

60. Mheshimiwa Spika, Mgodhi wa Dhahabu wa Acacia North Mara ambao kwa sasa ni Barrick, uliopo Nyamongo Wilayani Tarime ulitoza faini ya bilioni 5.6 kwa kushindwa kudhibiti bwawa la maji yenye sumu na hivyo kuhatarisha afya za wakazi wanaozunguka mgodi huo.

61. Mheshimiwa Spika, Kitendo cha Serikali kutoza faini Kampuni hiyo kunathibitisha malalamiko ya muda mrefu ya wananchi wa Tarime wanaozunguka mgodi huo. Malalamiko ya wananchi hawa yamewahi kuchunguzwa na Kamati mbalimbali za Bunge hili kwa nyakati tofauti tofauti bila mafanikio. Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa James Lembeli iliwahi kufanya ziara Nyamongo. Madhumuni ya ziara hiyo ilikuwa ni kukagua utekelezaji wa maelekezo ya Kamati hiyo iliyoyatoa mwaka 2010. Pamoja na Serikali kuwatoza faini ya shilingi bilioni 5.6 tulitegemea Serikali ingeweza kuwalipa fidia wananchi ambao ndiyo waathirika wakubwa wa kemikali hizo, lakini hadi leo hawajalipwa fidia yoyote.

62. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ieleze ni lini itawalipa wananchi hawa ambao ni waathirika wakubwa wa kemikali ikizingatia kwamba Serikali tayari ilishapata shilingi bilioni 5.6 kutokana na mgodi kutiririsha maji yenye sumu yaliyoleta athari kwa wananchi na mazingira.

I. MUUNDO WA WIZARA YA MADINI

63. Mheshimiwa Spika, Kuna umuhimu wa kupitia upya muundo wa Wizara ya Madini na kufanya marekebisho katika idara au taasisi ambazo zinaonekana kuwa na majukumu yanayofanana. Mathalani, kuanzishwa kwa Tume ya Madini kwa mujibu wa Marekebisho ya Sheria ya Madini 2010, inapokonya mamlaka na kazi ambazo Idara ya Madini chini ya Kamishna wa Madini alikuwa nazo. Kwa mantiki hiyo, kuendelea kuwa na Idara na Taasisi ambazo zinafanya kazi

zinazofanana siyo tu kwamba zinatoa taarifa ya utendaji unaofanana ila pia ni kuingia gharama zisizo na tija kitu ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

J. HITIMISHO

64. Mheshimiwa Spika, Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusisitiza mambo yafuatayo:-

i. Kwa kuwa huu ni mwaka wa mwisho wa kipindi cha miaka mitano kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaambie Watanzania hatima ya majadiliano na Kampuni ya ACACIA na fedha ambazo ilipaswa kulipwa kama zimeshalipwa kwa sababu ni jambo ambalo umma wa Watanzania ulishirikishwa tangu mwanzo. Na ikiwa bado hazijalipwa ni kwa nini fedha hizo hazijalipwa. Ikiwa makampuni haya yalikwepa kodi kama ambavyo Watanzania tuliambiwa ni kwa nini hadi sasa bado hayajalipa fedha hizo. Na ikiwa Serikali iliudanganya umma, ni lini sasa Serikali itatoa taarifa sahihi kuhusu fedha hizo.

ii. Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge lako tukufu sababu za kutopeleka fedha yoyote kwenye miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kwamba Bunge hili lilipitisha na kuidhinisha jumla ya **Shilingi 7,039,810,200.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

iii. Serikali iliambie Bunge hili tukufu sababu ya Wizara hii kuwa na ongezeko la **Shilingi 11,854,499,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ni jambo linalostajabisha kwa sababu, Randama zinaonesha kwamba:-

a) Kuna ongezeko la shilingi 4,572,102,000.00 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi) Shilingi 4,572,102,000.00 zimeongezeka katika bajeti ya mwaka huu kutoka Shilingi **16,473,825,000.00** ambazo Wizara ilipitishiwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizoko chini yake. Ongezeko hilo linaifanya Wizara kuomba Shilingi **21,045,927,000.00**. kwa ajili ya kulipia mishahara tu; sasa katika

mazingira ambayo Serikali haijatoa ajira kwa Watanzania, watumishi mbalimbali hawajapandishwa mishahara na madaraja, tulitarajia gharama za mishahara itapungua lakini kinyume chake bajeti inapanda kwa takribani shilingi bilioni 4.6; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka maelezo ya kiasi hiki cha bilioni 4.6 zimetengwa kwa ajili ya kulipa mishahara watumishi gani walioongezeka?

b) Ongezeko la Shilingi 7,282,396,000.00 kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC); Ikiwa mwaka wa fedha 2019/2020 fedha zilizoombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ilikuwa ni **Shilingi 25,953,263,000.00** na kwa mwaka huu wa 2020/2021 Wizara inaomba jumla ya **Shilingi 33,235,659,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Maana yake ni kwamba, maombi haya yameongezeka kwa **Shilingi 7,282,396,000.00**. Kambi Rasmi hapa inataka kufahamu kilichotokea hadi Wizara kuwa na matumizi mengineyo ya nyongeza kwa gharama ya takribani **bilioni 7.3**.

iv. Wananchi walioathirika na maji ya sumu kutoka Mgodu wa NorthMara watalipwa kiasi gani cha fedha kama sehemu ya fidia ya Madhara waliyopata kwa kipindi kirefu?

65. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

.....
Joseph Leanard Haule (Mb)

**K.N.Y. MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA MADINI**

20 Aprili, 2020

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Haule, Mbunge wa Mikumi kwa usomaji wako mahiri wa taarifa yako kwa niaba ya Kambi yenu. Kama nilivyokukatiza wakati ule, kwa kweli nashukuru kwamba kabla hata hatujaonana tukazungumza wenyewe mmekaa mkaona matundu ambayo yalikuwemo katika hotuba zilizopita. Nafikiri sasa

hotuba zinazokuja nazo zitakuwa zinajielekeza kwenye mada iliyopo hapo mezani kama inavyotakiwa ingawaje mmpiga maswali mengi, maswali karibu 1,000. Sasa hayo Mheshimiwa Waziri kwa nusu saa kweli ataweza, basi ngoja tuone.

Wachangiaji wa leo, kama tunavyofahamu tunamaliza leo leo kwa hiyo iko kazi hapa. Wachangiaji nao, patachimbika hapa leo. Haya tuanze na Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Nchambi.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nilleta mabadiliko badala ya Mheshimiwa Jesca anachangia Mheshimiwa Salome Makamba.

SPIKA: Sijayaona mabadiliko hayo, kwa hiyo nafuta hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Suleiman Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, wabheja sana...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, samahani sijakuelewa, unafuta jina la Mheshimiwa Jesca au unafuta nafasi maana tayari tulishapeleka mabadiliko haya mapema katika Ofisi ya Katibu.

SPIKA: Tuliza *ball!* Kabla Mheshimiwa Jenista hajasimama tulia kabisa, Mheshimiwa Nchambi tafadhali. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, *wabheja sana*. Kwanza, naomba niishukuru sana Wizara kwa kazi wanazozifanya. Naomba nijikite kwenye eneo hili la madini na hasa hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Salome Makamba tarehe 14 Aprili, kuhusu makinikia katika Wilaya na Jimbo la Kishapu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda sana nitoe uthibitisho ambao unajadili hoja na kutoa majibu juu ya uongo mkubwa alioutoa Bungeni Mheshimiwa Salome Makamba. Nafanya haya kwa kutoa *evidence*, endapo

nitahitajika popote kupelekwa kwenye Kamati yoyote kutoa majibu juu ya uongo uliotolewa na Mheshimiwa Salome Makamba basi nitakuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salome Makamba aliongelea suala la makinikia. Kwanza, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa miaka mingi sana tangu tumepata Uhuru Watanzania walikuwa wakiomba makinikia tangu miaka ya 1970 yaliyokuwa yakisafirishwa na *WDL* lakini hawakuweza kufanikiwa. Awamu hii ya Tano Mheshimiwa Rais akatoa maelekezo baada ya maombi yangu tangu mwaka 2012 Desemba, 2018 akaruhusu kupitia Wizara.

Pia nimshukuru Mheshimiwa Doto Biteko kwa moyo wake wa kumkumbusha Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya jambo hili. Kwa hiyo, ukamilifu wa jambo hili umekamilika Awamu ya Tano na tulifanikiwa kupata ruhusu kutoa makinikia yaliyopo katika Mgodini wa *WDL* ili wananchi waweze kujifanyia shughuli zao za uchumi Desemba, 2018. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nimshukuru Waziri aliunda Tume ama timu ndogo ambayo ilishughulika na namna bora ya kuyatoa makinikia yale. Ilianza kazi tarehe 25 Desemba na imekamilisha utaratibu wote na tarehe 25 Machi tulianza kazi ya kutoa udongo na kusafisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salome Makamba alisema kuwa wananchi wanahangaika kusafisha makinikia kwa miezi sita sasa jambo ambalo ni la uongo na *Hansard* inaonesha. Sisi tumeanza kusafisha makinikia Machi na tunaendelea na Aprili hii.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Salome Makamba pia aliongea jambo la uongo kuwa tangu wameanza kusafisha makinikia ni vikundi takribani 50 peke yake ambavyo vimeweza kufanikiwa kusafisha makinikia hayo. Ninao ushahidia hapa nitautoa mbele yako wa vikundi 700 ambavyo vimekwishafanya kazi hii mpaka juzi katika

Mgodi wa *WDL*. Ninao ushahidi hapa wa kimaandishi nitaikabidhi kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Mheshimiwa Salome Makamba alisema kuwa Serikali ilitengeneza mpango wa kutoa makinikia ili kuongeza *own source* katika Halmashauri. Jambo hilo ni la uongo na alisema kabisa kuwa Manispaa ya Shinyanga imesajili vikundi 1,000 na ikiwa ni chanzo cha mapato kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Huo ni uongo mkubwa na Serikali hii haiwezi kufanya jambo hilo, mimi ni mbunge wa eneo husika. Vikundi vilivyosajiliwa katika suala zima la makinikia ni 768 na vikundi 514 vikitoka Jimbo la Kishapu, vikundi 200 vilivyosalia ndiyo vinatoka Shinyanga Manispaa na maeneo mengine. Kwa hiyo, yeye Mbunge aliyetoa takwimu hizo ni za uongo, hajawahi kufika *site*, hajawahi kutembelea vikundi, hajawahi kufika Wilaya ya Kishapu sehemu ambako tunafanya kazi hiyo, anatoa takwimu kutoka kichwani. Wabunge wa namna hii ni hatari na wanaweza kuwapotosha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbali tu ya kusema uongo ningeshauri Wabunge wa aina hii waitwe kwenye Kamati Maalum kwa sababu wanawapotosha wananchi na wanawavunja moyo kwa kile ambacho wanakifanya. Ninayo orodha ya vikundi pia nitaikabidhi kwako, lakini Mheshimiwa Salome Makamba alisema tangu ameanza mpaka leo hawajapata chochote wanahangaika na jua, ni jambo la uongo, takwimu hizi ninazo hapa. Hivi leo ninavyoongea almasi zilizokwishapatikana tangu tarehe 25 Machi ni *pieces* 1708 na jana peke yake ambapo walikuwa wakisafisha vikundi 33 walipata almasi 352 za *size* tofauti.

SPIKA: Mheshimiwa Nchambi kama nakumbuka Mheshimiwa Salome alisema hawajawahi kupata hata *size* ya sukari hata moja, leo Salome, hebu endelea Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, leo ninavyoongea mpaka saa sita mchana watu wanakwenda *break* almasi zilizokwishapatikana ni vipande 134 *na vipande*

hivi 134 kwa kiuno cha Mheshimiwa Salome Makamba zinaweza zikaenea na akamburudisha shemeji yangu, hivi tu vilivyopatikana kwa leo. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, sasa anavyosema havijapatikana vipande vyovyote, ni uongo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, alisema jambo lingine kwamba vikundi vinaghamika kati ya 50,000 na 150,000...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Mheshimiwa Nchambi namuona *Chief Whip* wa Upinzani amesimama, naona mishale imekuwa mikali sana, Mheshimiwa Ester Bulaya nimekuona.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza...

SPIKA: Nilisema mapema kwamba leo patachimbika.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikuhakikishie kwamba hakuna mishale yeyote ambayo itatusumbua sisi, tuko imara sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe umetuelekeza, umesema tumeanza vizuri. Kuna mifano ya kutoa, lakini kuna mifano mingine si ya kutoa. Anavyosema hizo almasi zinaweza zikazunguka kiuno cha Mheshimiwa Salome na kumridhisha shemeji yake, hiyo ni lugha ya kudhalilisha wanawake. Achangeie, akosoe vyovyote lakini kuna lugha hatutazikubali sisi wanawake na hatutakubali kudhalilishwa kwenye Bunge hili. Kwa hiyo naamini kiti chako kitakuwa *firm* tukifanya sisi makosa, tukitoe lugha za ajabu sema hili futa, Mheshimiwa Nchambi hiyo kauli aifute ni ya udhalilishaji.

SPIKA: Ahsante sana. Nafikiri hili tulimalize tu haraka haraka unajua sikushtuka sana kwa sababu unajua nilikuwa na-*imagine* shanga za almasi tupu kwenye kiuno, duh nikasema hii itakuwa ni shanga yenye thamani kubwa sana. Mheshimiwa Nchambi hilo nimelifuta kwenye *hansard* endelea na uchangiaji.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine alilolisema ni kuhusu wananchi wanagharamika kati ya 150,000 kwa kikundi ili kujisajili, Mheshimiwa Mbunge ni jambo la hatari kama Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga hajui mambo yanayoendelea katika mkoa, ni jambo la ajabu sana, haelewi anachokifanya. Usajili wa kikundi ni Sh.11,000 tena kwa kutumia *control number*. Mheshimiwa Makamba amesema vile vile Katiba wanauziwa wale wanakikundi. Katiba unafahamu Kamati zako zinavyokaa hapa, wanakaa kikundi wanachagua uongozi wa muda, wanatengeneza Katiba yao wanachagua uongozi wa kudumu, wanakwenda kusajili kwa shilingi 11,000 tu katika halmashauri yoyote ambayo kikundi kimeundwa. Yeye anasema 150,000, amewahi kukaa na kikundi gani ambacho yeye hata amekifadhili kimoja akakilipia 150,000 na risiti anayo, huo ni uongo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nilimsikiliza kwa makini Mheshimiwa Salome Makamba anasema anaomba majibu kwa Waziri, Mheshimiwa Waziri kama atampatia takwimu ama majibu ya aina yoyote ama hoja yoyote juu ya jambo hili atakuwa amekosea, yeye ni Mbunge anatakiwa azitoe changamoto kwa wananchi azilete kwa Waziri ama Bungeni, awatete, lakini Mbunge wa aina gani wa ajabu, huyu ni Mbunge juha, anakuja kuomba hoja za wananchi kwa Waziri awapelekee, badala ya kutoa matatizo kwa wananchi ayalete kwa Waziri au Wizarani ama Bungeni kuwatetea.

Mheshimiwa Spika, ninachowaasa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga Mheshimiwa Salome Makamba nitasimama leo, kesho na kesho kutwa, ni Mbunge muongo

na hajui ambacho alikuwa akikifanya. Serikali hii amesema kwamba Wizara ya Madini inakwenda kusimamia suala la uchenjuaji wa yale madini kwa wachimbaji wadogo, sio kazi ya Wizara. Wizara inakwenda pale mtu anapopata almasi, tena namshukuru sana Mheshimiwa Doto miongoni mwa Waziri vijana ambao wanafanya kazi nampongeza sana. Leo kuna mhandisi pale Joseph, RM wa Mkoa, mwananchi wa Jimbo langu la Kishapu akipata almasi, kijijini aliko anampigia simu, anakwenda anamfuata mpaka kule kwa sababu watu walikuwa wakiibiwa, Mheshimiwa Doto anajua, kuna watu waliibiwa almasi za thamani ya milioni 40 na *brokers* tukawasiliana na Mheshimiwa Doto na RM, walikwenda wakakamatwa walioiba zile almasi kwa bei chini, zikarudishwa kwenye mkutano wa hadhara na RM Joseph, anatangaza Nchambi kuna *pieces* mbili hizi hapa zikarejeshwa, badala ya almasi kuuzwa kwa milioni mbili zikauzwa kwa zaidi ya milioni 40. Sasa Serikali hiyo anayosema haisimamii, haisaidii wananchi ni Serikali gani?

Mheshimiwa Spika, nataka nijikite sana kwenye hoja ya Mheshimiwa Salome Makamba kwa sababu...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba aache uongo na naunga mkono hoja ya Wizara. Wabheja sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana.

Nilitegemea Mbunge mwingine yeyote wa CCM angesimama kuhusu utaratibu, nashangaa watu wote wamekaa, kwamba Mbunge ambaye ameongea uongo zaidi ya mambo 10, Mheshimiwa Spika utaratibu unasemaje, lakini naona wamekaa, wamenyamaza, kwa hiyo basi bwana. Ila sasa Mheshimiwa Salome aliomba kuchangia, mimi naona bora asichangie tu, kwa sababu umeelezwa

hapa uongo mfululizo, sasa nikikupa kuchangia itakuwaje, maana yake itabidi twende maadili mwisho wake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Bulembo. Hiyo *introduction* Mheshimiwa Salome, kujaribujaribu majimbo sio mchezo. Mheshimiwa Bukwimba.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Madini. Kipekee kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa wanayoendelea kufanya kwenye Wizara ya Madini. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wa dhiti kwa kuhakikisha kwamba madini ya Taifa yanasimamiwa kwa ukamilifu kuweza kuwachangia na kuwasaidia wananchi hasa wanyonge.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, kipekee kabisa napenda kuishukuru Wizara hasa kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kuleta mabadiliko ya sheria hapa ndani ya Bunge letu. Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, Sura 123 pia kwenye ile Sheria ya Kodi, Sura 332 na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148. Mabadiliko haya ya sheria ambayo yalipitishwa hapa Bungeni kwa kweli yamekuwa na mchango mkubwa sana hasa kwa wale wafanyabiashara wa madini hasa wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa hatua madhubuti ya kuweza kuleta mabadiliko ya sheria hii ambayo imekuwa na manufaa makubwa sana hasa kwa wananchi wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naishukuru Serikali kupitia ule mradi wa usimamizi wa rasilimali endelevu ambao unajenga vituo saba vya umahiri. Pia umeweza kujenga vituo vitatu vya mfano na Mkoa wa Geita pia kwenye Jimbo la Busanda wameweza kujenga kituo Rwamgasa. Nitumie nafasi hii kuishukuru sana Wizara kwa kutujengea hicho kituo, ninaachoomba tu kujua sasa ni lini kituo hiki cha Rwamgasa

kitaanza kazi rasmi, wananchi wanahitaji kujua hilo kwa sababu wanasubiria kutokana na manufaa ambayo tunatarajia wayapate kutokana na kituo hicho, kwani watu wengi watapata ajira kupitia kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti iliyopita ya Mheshimiwa Waziri ukurasa 18 alizungumzia habari ya kufanya marekebisho kwenye Sera ya Madini ya Mwaka 2009. Nataka kujua sasa kwamba mmefikia wapi je, mabadiliko yako tayari au bado ili iendane na wakati wa sasa? Naomba kujua jambo hilo na kama bado basi nitoe ushauri kwa Wizara waweze kufanya marekebisho ya hiyo sera ili iweze kuendana na wakati wa sasa ambapo tayari tumeshabadilisha sheria ambazo zilifanyiwa marekebisho mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, vilevile ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba wananchi hasa wachimbaji wadogo wa madini na wachimbaji wa kati na wachimbaji kwa ujumla, wanachohitaji ni uwezesho kutoka Serikalini hasa katika miundombinu muhimu itakayowezesha wao kuweza kufanya kazi zao vizuri. Kwa mfano tulishuhudia mgodi wa GGM ulipoanzishwa walihakikisha upatikanaji wa maji safi kutoka Ziwa Victoria pia walihakikisha kumekuwepo na umeme wa uhakika. Kwa hiyo naomba pia hata wachimbaji wa madini wadogo wadogo pamoja na wakati, tunaishauri Serikali kupitia Wizara ya Madini wahakikishe hii miundombinu muhimu inakuwepo kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo. Kwa mfano upatikanaji wa umeme; katika maeneo mengi ya wachimbaji wadogo hayana umeme.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuiomba Wizara ya Madini ikishirikiana na Wizara ya Nishati ikiwezekana hata bajeti hii iweze kutenga fedha maalum kuhakikisha kwamba wachimbaji hawa wanapatiwa umeme katika maeneo yao, kwa sababu bila ya umeme hawawezi wakaanzisha viwanda vya uchenjuaji wa dhahabu, bila kuwa na maji haiwezekani kuweza kufanya shughuli ya uchenjuaji wa dhahabu. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie masuala haya ili kuwawezesha wachimbaji hasa wadogowadogo wa madini waweze kufanya shughuli zao vizuri na kwa tija kwa sababu bila ya

kuwa na miundombinu hii muhimu haiwezekani wakaweza kufanya shughuli zao kwa tija.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara pia ijaribu kuangalia hawa wachimbaji wadogo na kuweza kuwapatia maeneo. Natambua kazi inayofanyika na Wizara, wanaenda hatua kwa hatua, lakini niombe kuna baadhi ya maeneo hawajayafikiria kabisa kutupatia maeneo. Nilikuwa najaribu kusoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha wameangalia baadhi ya maeneo Mkoa wa Mara, Mkoa wa Shinyanga lakini kwa upande wa Geita sijaona kabisa kwa sababu Geita pia ndio ina wachimbaji wa madini wengi. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri hebu atuangalie na sisi, kuna wananchi walio wengi wameanzisha vikundi mbalimbali, wanahitaji kupewa maeneo ya uchimbaji wa madini waweze kurasimishwa.

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora wameanzisha mradi wa urasimishaji kwa wachimbaji wadogo wa madini. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa hatua kubwa ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo hata na Watanzania kwa ujumla wanaweza kuwasaidia katika mahitaji yao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la mitaji ni jambo la msingi sana nilikuwa naiomba wizara iendelee kuangalia namna ya kuwasaidia wachimbaji hawa wa madini. Natambua kwamba Serikali katika Wizara nyingine kama Kilimo, Serikali inatenga fedha kwa ajili ya kununua pembejeo na vitu vinavyohusiana na kilimo. Kwa hiyo niombe hata Serikali kwa upande wa madini, wale wananchi ambao wanashughulika na masuala ya madini tuangalie namna ya kuwasaidia kwa kuwapa hata ruzuku, tuwawezeshe kuweza kuchimba kwa tija kwa sababu bila ya mitaji haiwezekani kufanya kazi hizi na kwa tija, kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali iangalie namna ya kuweza kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja nikiamini kwamba

Mheshimiwa Waziri amesikia na kwamba wataweza kuyatekeleza masuala ambayo nimeweza kuyazungumzia. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba. Nilishamtaja Mheshimiwa Bulembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Heche.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kujielekeza kwa kuwapongeza Wizara ya Madini, nianze na Mheshimiwa Waziri wa Madini hongera sana kwa kazi anazozifanya, ni kazi nzuri. Naibu Waziri wake, mapacha wako vizuri, Mungu awape nguvu zaidi waendeleo kutumikia watu wa madini hao. Katibu Mkuu Profesa lakini na zaidi nipongeze Tume ya Madini. Tume ya Madini nianze hapo kazi wanayofanya ni kubwa sana, nchi hii ni kubwa na maeneo yaliyopimwa ni mengi, lakini na leseni zinatoka kwa wakati. Kwa kweli tuna haki ya kuwapongeza, kweli tulikuwa tunapata tabu siku nyingi, siku hizi hakuna kupandishana leseni, ukitaka ukishafuata utaratibu, unapata tunaendelea kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nianzie kwenye eneo linaitwa *TRA*; kwenye ulipaji wa madini. Kwanza tumpongeze Mheshimiwa Rais alituitisha mkutano wachimbaji wadogo wote pale Dar es Salaam. Tukaenda tukasema hoja zetu zote tukamaliza, tukafanya kikao cha jumla Makamu wa Rais na Wadau wote, tukakubaliana kuwa kwamba zile kodi zilikuwa zinafika karibu asilimia 26 zinatoka zinaenda saba, kila mtu anajua hivyo na tukakubaliana wachimbaji hakuna sababu ya kutorosha maana yake kodi imepungua.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wanisikie vizuri hapa kwenye eneo hili hasa Wizara ya Fedha. Sisi Rais alishamaliza tukaambiwa tunalipa asilimia sita ukiongeza moja saba, lakini ukienda kwenye eneo linalouziwa madini, unakuta mtu wa *TRA* amekaa pale anakwambia umeshauza nataka *VAT*, jamani! Mtawarudisha hawa watu, badala ya kwenda kwenye maeneo ya kuuzia madini, waanze tena kwenda njia za panya, sio lengo la Rais kwa wachimbaji wadogo.

Tumekaa kikao cha pamoja tumekubaliana mambo ya kufuata, wachimbaji wanafuata bila matatizo, lakini hili suala la *TRA* kila mtu kwenye wilaya yake anataka kuonyesha amekusanya nini, linaanza kuleta mgogoro.

Mheshimiwa Spika, suala hili linaweza kupunguza mapato haya na tusikutane tena, tukaanza kukamatana mitaani huku. Kwa hiyo Mawaziri nawaomba sana waambieni *TRA* lakini sisi wachimbaji kule hakuna *order* hakuna nini, ukishapata leseni unaenda kuchimba. Ukishaenda kuchimba umepata mazao yako, unayapeleka sokoni kwa utaratibu wa leo, mnakubaliana maana yake hapa hatuwezi kulipana, hela tulipane benki, unaenda kulipa milioni 500 au bilioni moja, kuziweka ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Fedha naomba anisikilize; kuziweka zile fedha benki ni rahisi, kuanza kuzitumia sasa ni kero, ulizipataje? Leseni ya madini iko wapi? Utaratibu uko wapi, kama watu wa mabenki na *TRA* hawajui taratibu za madini, wachukue vijana waliosomea madini wawapeleke *TRA* wasaidie sekta hii, kwa sababu sasa mtu anapata kero, ameshapata hela yake, alishakopa watu wake wameandamana kule, lakini hawezi kutoa hela benki, anaambiwa hizi hela ni nyingi. Kwenye madini saa nyingine hela nyingi wakati mwingine hela kidogo, lakini watalazimisha wachimbaji hawa badala ya kupeleka tena hela benki wanaweka vibubu kule ndani, hatutaziona hazitazunguka. Mtu anaweza kupeleka hela yake benki leo, kesho anataka kuchukua milioni 100 maelezo ni marefu subiri kidogo, subiri kidogo tu-*confirm* benki kuu, sasa tatizo liko wapi? Mtu ameshalipa *TRA* kodi yake hela ni za kwake, kuzitumia ni dhambi. Kwa hiyo naomba Wizara ya Fedha waongee na *TRA* wawaambie watu wa mabenki sisi wachimbaji hela ikishaingia benki inatumika yote, siyo ya kwako utaonekana milioni 500 wamejipanga watu 20 kule wanazitaka pesa zao, lakini kutoka benki inakuwa mzozo.

Mheshimiwa Spika, ninachokisema kwa Serikali yangu, tukiendelea kufanya utaratibu wa kutopokea na kuwapa ushirikishwaji wachimbaji watarudi kwenye magunia

watakuwa wanagawana mtaani hatutajua tunachokipata Serikali itaanza kupoteza mapato yake.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye hiki kilio alichosema Mheshimiwa Kishimba siku moja hapa kwa Wizara ya Fedha. Kuna *corona*, *corona* hii kwenye mifuko na yenyewe imeingia, lakini kuna watu ambao tulisema kuna fursa kwenye *corona*, kuna wachimbaji wa dhahabu, *Tanzanite* na *Gemstorne*, wachimbaji hawa wakichimba leo wameweka mali ndani. Twende kwenye hesabu ndogo tu, mimi si Mchumi sipo kwenye kampuni zenu hizo, lakini Wachumi wengi wako humu hebu tujadiliane.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda kwenye *world market* kilo moja ya dhahabu inaenda kati ya dola 56,000 kwenda 60,000. Leo ukirudi mtaani kwetu kwa wachimbaji wadogo kwa sababu hawana mahali pa kuuza inakwenda dola 40,000 mpaka 45,000 hapa kuna tofauti karibu ya dola 10,000 mpaka 12,000. Sasa Serikali wanawekaje hela benki wakati sasa tunahangaika kukusanya mapato kwenye kipindi cha *corona*, Serikali ingetoa pesa ikazirudisha kwa hawa wachimbaji wadogo wadogo, wakapata hela mfukoni zingerudi huku kusaidia matatizo tuliyonayo, leo watu dhahabu wanayo.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania hesabu yangu ndogo, wachimbaji tuna uwezo wa kukusanya kwa mwezi kati ya kilo 1200 mpaka kilo 1300, tani moja mpaka tani 1.3, hizi ni hela nyingi kwa nini hawazitaki na siku hizi hakuna *kakumba* kwenye dhahabu, tunanunulia kwenye masoko, watafute benki wanazoziamini wawapeni pesa waende kuokoa hili tatizo lililoko huko chini, ni kubwa sana. Dhahabu imejaa hata hapa kwako Dodoma tukiita kesho kwamba kuna dhahabu kilo 100 na 150 anapata pale pale bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali kwani *formula* ni ipi ya kukusanya hela? Kwa nini hamuitaki? Ninyi kama Benki Kuu ya nchi, mkishapata hizi hela mkanunua dhahabu halali ikaingia benki, mnaongea kule Ulaya tu, mnaingiziwa mapesa

watakuja kuchukua mzigo wao. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Fedha, nawaomba sana; mimi sielewi kwa sababu sisi hatuwezi kukopesha mabilionea, hatuna uwezo huo, lakini ninyi mnazo. Kipi bora; kuziangalia Dola za Benki Kuu au kuweka na thamani ya dhahabu ikakaa Benki Kuu? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, *Corona* hii imekuja, watu wanajifungia majumbani, watu wana mali zao kwenye majumba, wengine mtaenda kuwakamata wana mali nyingi kwa sababu hawana mahali pa kwenda kuuza. Naiomba Serikali yangu, najua ni sikivu sana, nendeni mkae chini, mna uwezo wa kukusanya shilingi trilioni moja, mbili kwenye miezi miwili, mitatu bila kuwatoa watu jasho kwa sababu mali ipo wanunuzi hwapo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kuna yale maeneo ambayo Maaafisa Madini hawatoshi, kwa sababu unakuta Afisa Madini Mkazi mmoja kwenye mkoa na wasaidizi wake wawili au watatu, lakini kuna maeneo ya kuchimba zaidi ya 30, 40 au 50. Tunawaomba Wizara mwongeze nguvu, kama ni ajira, kama ni nini, mwongeze kule watu ili kazi hii iwe rahisi Serikali ikusanye kodi. Sisemi sana lakini kwa sababu ya mianya hiyo ambayo haijaka vizuri bado upotevu unaweza ukatokea tukaendelea kupoteza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara ni vizuri mkaajiri upya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bulembo, tunakushukuru kwa mchango wako. Kwa kweli hili la mtu anachukua hela yake benki, kama liko hivyo kweli tukuombe

Mheshimiwa Waziri wa Fedha mkaliangalie maana yake tusi-*criminalize* watu kufaidi hela zao. Kama mtu ana hela yake, amelipa kodi na ni yake, anataka kuchukua kwa ajili ya mambo yake, achukue hela yake, si yake! Kama hilo lipo kwa kweli lina haja ya kufanyiwa kazi, maana vinginevyo tutarudi kule kule.

Nilikutaja Mheshimiwa Heche, utafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma, baada ya hapo tutakwenda Msekwa kumsikiliza Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wangu wa tano hapa Bungeni, nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu walionileta hapa, wamenipa heshima kubwa, nimewawakilisha kadri ya uwezo wangu na ninataka niseme, kuna watu wanajipitisha, wanapiga kelele sana, wanataka *attention*. Nawaambia mimi ni kisiki cha mpingo na Tarime ina uzoefu wa kushughulikia watu kama wale. Sitaki kuwapa jina sana, tukutane ulingoni. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, jambo la pili...

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Nchambi.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Heche, hili aliloliongea linahusiana na Bajeti ya Wizara ama halina mahusiano? Kama halina mahusiano, basi aliondoe. (*Kicheko*)

SPIKA: Taarifa hiyo, Mheshimiwa Heche endelea.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, tafadhali sana, hii tabia inayojengwa na Wabunge ambao ni wa Chama Tawala; nitunzie muda, lakini ni vyema tukasema Watanzania wajue, siyo sawa.

SPIKA: Endela Mheshimiwa, muda wako unakwenda.

MHE. JOHN W. HECHE: Mtu anaanza kusema jambo moja tu mtu anainuka na taarifa! Nitaku... (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naanza na jambo ambalo nimelizungumza kwa miaka yote; malipo ya fidia ya watu wa Tarime maeneo ya Nyamongo. Mheshimiwa Doto umekuja pale mara kadhaa, alikuja Mheshimiwa Waziri Prof. Muhongo na kila Waziri amekwenda pale. Mara ya mwisho Mheshimiwa Rais alipita pale akiwa na Mawaziri karibia wote, akamwagiza Waziri wa Ardhi, Waziri wa Madini, Waziri wa Maji kwamba suala lile la Nyangoto, Kewanja, Nyakunguru na Matongo lishughulikiwe liishe.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Doto ile ni haki ya watu. Mtu anachukua eneo lako ambalo unaishi na watoto wako, siyo hisani. Watu wa Tarime hawaombi hisani popote, wanataka haki yao. Ninyi wenyewe Serikalini mmethibitisha kwamba watu wamepatwa na maji ya sumu, watu wamekufa, mifugo yao imeharibika, imekufa, ardhi zao maeneo ya Kwinyunyi, Kwimange uliona pale, hailimiki tena. Watu wamepata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali yenu inajali watu wanyonge, maliza lile suala liishe na lisikae kuwa suala la kisiasa la wanasiasa kuwa wanajitafutia chakula. Lile ni suala ambalo liko wazi, watu wamechukuliwa ardhi yao. Sheria ya Madini mwaka 2010 inasema, mtu ambaye yuko kwenye *mining active areas, 200 meters* ndani alipwe ahamishwe. Tafadhali hilo suala liishe na nilitaka hilo nianze nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ushauri. Sasa hivi kwenye janga hili la *Corona*, nimesoma kwenye taarifa yako

umesema wafanyakazi wa migodi ni zaidi ya 190,000 ambao wameajiriwa kwenye migodi. Unapokuja ku-*wind up* uwaambie Watanzania, hao wafanyakazi mmechukua hatua gani kama Serikali kuhakikisha wako salama na familia zao zinakuwa salama?

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi, kuna mpango gani; kama hali itakuwa mbaya na tukalazimika kwenda kwenye *lockdown* isije ikawa kama kwenye shule sasa hivi, nimepata *message* hapa, walimu wanaofanya kazi kwenye shule binafsi wameanza kuondolewa kazini na wanaambiwa hawatalipwa mishahara. Kwa hiyo, aseme na uelekeze kwamba kitokea migodi imesimama kuzalisha watu hawa wasisimamishwe mishahara yao, waendeleo kupata haki kwa sababu wanahitaji chakula, wanahitaji kutunza watoto wao na madawa. Hilo ni jambo la pili.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni suala linalohusu Mkataba wa Barrick na Serikali. Mwaka huu Januari mkataba ulisainiwa kati ya Serikali na Barrick na ikaundwa kampuni inayoitwa Twiga ambayo sisi kwenye taarifa ya Waziri hapa amesema tunamiliki asilimia 16 na watu wa Barrick wanamiliki asilimia 84.

Mheshimiwa Spika, ukichukua Sheria za Madini mbili tulizotunga za mwaka 2017, ukachukua na sheria ya mwaka 2010 ambazo zote zinafanya kazi kwa pamoja ndani ya nchi hii, zinaleta mkanganyiko mkubwa. Mgodi kwa mfano wa *GGM* wa Geita unafanya kazi kwa sheria ya mwaka 2010. Migodi yote ya Barick inafanya kazi kwa sheria ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka Mheshimiwa Doto anapokuja hapo awaambie Watanzania; na nilitamani sana Mheshimiwa Prof. Kabudi awepo; ni kwa nini hamjaanzisha majadiliano na kampuni nyingine zote zinazofanya kazi kwenye nchi hii kuchimba madini? Tunakuwa na nchi ambayo ndani ya nchi moja makampuni mbalimbali yanafanya kazi kwa sheria mbili tofauti. Kama kweli

makampuni haya yalikuwa yanatuibia ni pamoja na Kampuni ya GGM inayofanya kazi kule Geita. Ni kwa nini mnaacha waendeleo kuwaibia Watanzania kama mliyowaambia? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la nne; suala hili la mchanga wa makinikia ni suala ambalo lilitikisa nchi na kila mara nimekuwa nikiwakumbusha kwamba tusitake kusahaulisha Watanzania na tukawafanya kama hawaelewi na kwamba wanaweza kusahau jambo kubwa kama hili. Wakati mjadala huu unaanza, ulianza kwa sababu tuliambiwa kwamba makampuni yalikuwa yanatuibia na mchanga wa makinikia ukazuiliwa. Huo ndiyo mwanzo wa mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, mchanga wa makinikia ukazuiliwa na ikasemekana tumeibiwa Dola bilioni 190 ambazo ni sawasawa na shilingi trilioni 426. Sasa hizi pesa ni nyingi kweli kweli. TRA wakatumba kufanya *verification*, Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa. Kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Mamlaka ya Mapato Na. 14, ukishafanya uthamini hiyo kodi haiwezi kusamehewa. Hawa watu tuliambiwa ni wezi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka leo Mheshimiwa Doto atuambie, anapojibu hapa; Serikali mmesamehe mabeberu shilingi trilioni 426 zetu au deni liko pale pale au ni nini kinachoendelea? Kwa sababu hili siyo suala ambalo litapotezewa tu. Sisi tatalidai, tatalidai, tatalidai na tutaendelea kulidai kwa sababu Watanzania wanasubiri kwa makini sana kupata Noah moja moja kutoka kwenye shilingi trilioni 426. Hili suala haliwezi kusahaulika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwenye hilo, hapa tuliambiwa pesa za kishika uchumba; na hapa hayo mambo hayawezi kusahaulishwa kiurahisi. Tuliambiwa pesa za kishika uchumba shilingi bilioni 600...

SPIKA: Samahani kidogo. Hizo takwimu maana yake zinamchanganya Spika; yaliongelewa hapa Bungeni au?

MHE. JOHN W. HECHE: Humu humu!

SPIKA: Maana yake sikumbuki, kuna *Hansard* hiyo kweli!

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, wakati ule mlikuwa mnatuzomea sana, huwezi kukumbuka. Yaani zomeazomea ilikuwa nyingi, usione watu wame-*freeze* hapa, ndiyo maana sisi tunawakumbusha ili waendeleo kuzomea pia. Tunataka hizo pesa, tunataka pesa zetu za kishika uchumba tujibiwe, ziko wapi?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Mlinga tafadhali.

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Heche kuwa fedha zilizokuwa zinaibiwa kweli zilikuwa zinaibiwa na sasa hivi tunazipata na ndiyo maana umeona miradi ambayo tulikuwa tunaamini haiwezi kufanyika inafanyika. *Stiegler's* ile inaendelea, *SGR* inaendelea na ndege tumenunua na posho yake kalipwa ya wiki tatu mbele. Kwa hiyo, hela zipo na tunazipata.

SPIKA: Pokea taarifa Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, nilitamani sana Bunge liwe *live* ili wananchi wake waone uwakilishi wa aina hii. Tunahoji hapa vitu vikubwa ambavyo dunia tulikuwa *laughing stock* kwenye dunia, tukasema tumechaji watu bilioni 190 ikawa ni kichekesho duniani. Sasa tunahoji haya mambo kwa sababu sisi kuna watu waliumizwa hapa. Leo hatuko na mwenzetu hapa, aliumia kutokana na kuhoji haya mambo. Sasa hamwezi kuja hapa mkafikiri hili jambo litaisha hivi hivi. Tutaendelea kuhiji tena na tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Twiga na kwa mujibu wa sheria, vifungu ambavyo vilipitishwa kwenye sheria mbili za mwaka 2017 zinataka mikataba yote inayoingiwa na Serikali ya rasilimali zetu iletwe Bungeni hapa, Wabunge waipitie. Tunataka anapokuja Mheshimiwa Waziri kujibu hapa atuambie ni lini Bungeni italetwa mikataba ya madini ili Watanzania; mimi natoka kwenye eneo ambalo lina madini, nione kwa niaba ya wananchi wangu kwamba kweli tulichoambiwa ndicho ambacho tunapata. Kwa sababu Mheshimiwa Prof. Kabudi amedanganya vitu vingi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Kuna taarifa Mheshimiwa Heche.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Heche anatoka kwenye eneo ambalo lina mgodi, nami Nchambi ninatoka kwenye eneo ambalo lina mgodi wa almasi. Taarifa ninayotaka kumpatia ni kwamba mikataba iliyokuwa ikifanyika Twiga, sasa hivi kuna mkataba unaoendelea wa Mgodi wa *WDL* na Serikali wa maridhiano kwenda huko alikosema kwenye asilimia ambayo Serikali inataka. Nami kama Mbunge wa wananchi, ninashiriki kimalikifu kuona namna bora ya ule mkataba kuwa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa yeye kama hakushiriki huko Dar es Salaam huo ni upungufu wake, atafute utaratibu wa kumwandikia aidha Spika kwa ajili ya kuweza ku-*penetrate* kujua hayo mambo. Awe makini tu ashinde jimboni na atapata hizo taarifa tangu hatua za awali mpaka mikataba inapokamilika.

Mheshimiwa Spika, ni taarifa hiyo tu.

SPIKA: Ahsante sana. Bahati mbaya muda wenyewe nao umeisha kabisa. Kwa hiyo tunaendelea...

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, taarifa lazima nijibu.

SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Musukuma.

MHE. JOHN W. HECHE: Huyu alikuwa amekamatwa kwa wizi...

SPIKA: Muda umeisha kabisa Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Hakuwepo, alikamatwa kwa wizi na TAKUKURU kule *STAMIGOLD*.

SPIKA: Bahati mbaya muda umeisha. Nakuomba muda umeisha. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa kama Mbunge ninayetoka kwenye eneo la uchimbaji, naomba niipongeze sana Wizara ya Madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini nampongeza sana Katibu Mkuu, Mwenyekiti wa Tume. Kwa mtu yeyote mwenye akili timamu na aliyetoka kwenye neema ya dhahabu asipokupongeza Waziri na timu yako kiukweli huyo jina lake ni jepesi tu; ni mnafiki. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, la pili, mimi najua vizuri dhahabu, alizungumza Mheshimiwa Nchambi hapa; mfano mmoja, niliona *Chief Whip* wa Upinzani amesimama kulalamika, labda nitoe shule kidogo.

Mheshimiwa Spika, kazi ya vito; dhahabu, almasi na madini mengine, labda *Chief Whip* pia akatueleza kazi kubwa ya hivyo vitu ni nini? Kwa mimi ninayefahamu kazi ya hivi vitu ni urembo ikiwemo hereni na shanga. Kwa hiyo, Mbunge alipotoa mfano kwamba almasi ile inaweza kuenea kwenye kiuno cha Mbunge wala hakukuwa na tatizo. Kwa hiyo, alikuwa sahihi na ndiyo kazi halisi ya madini tunayoyachimba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naungana na Mheshimiwa Bulembo; ni kweli ukienda sokoni kwa sasa dhahabu imeshuka sana thamani. Kwenye Kamati tulitoa ushauri kwamba tunayo kampuni yetu ya *STAMICO*. Kampuni hii ina wataalam waliobobea na tunajikita kuchimba kila mwaka tunakula hasara, tunajaa madeni kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kweli alivyosema Mheshimiwa Bulembo na pesa tunazo; kwa nini *STAMICO* isiingie madukani ikaokoa hii dhahabu ya Tanzania kwa kipindi hiki cha *Corona*? Maana hatuhitaji kutafuta wataalam, wataalam tunao *STAMICO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutafute chumba kimoja na hao ma-*broker*, wakae; unahangaikaje na kuchimba kubahatisha wakati faida iko dirishani? Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuja kujibu hapa ni vizuri zaidi akatueleza kama wameweza kukubaliana na ushauri wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyechangia hapa amezungimza kuhusiana na suala la fidia. Saa nyingine sisi Wabunge tunawasababisha hata wananchi wetu wapate matatizo ya kutokulipwa fidia. Mimi Mbunge ninayetoka Geita tumelipwa fidia, kauli pia za ku-*approach* kuwazungumzia watu wako ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa Rais alikuja Tarime na timu yake ya Mawaziri, unakumbuka kilichotokea? Ulipopewa nafasi ya kuwazungumzia wananchi wako ukatia mikono mifukoni ukaanza kuongea mambo ya u-CHADEMA. Sasa ni vizuri zaidi pia tunapopata viongozi tutumie hizo fursa kuwazungumzia watu wetu ambao wametuchagua.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Nchambi, taarifa.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Musukuma, kama kwake ambavyo mgogoro uliisha baada ya kuwa na mwakilishi makini, ndivyo mgogoro ulivyoisha pale Mwaui kuzunguka Maganzo na Songwa baada ya kuwa na Mbunge makini. Tulikaa tukakubaliana na Serikali tukawaongoza wananchi sheria inavyotaka wakalipwa na hakuna mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nimpe Mheshimiwa Musukuma taarifa, nimpongeze pia kama kwangu ambako mgogoro uliisha. Kwa hiyo, vyanzo pia ni Wabunge ambao ni wakorofi wanasababisha mambo yanakuwa hayaendi.

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma, pokea taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, naipokea, ni kweli. Aliyeelezwa nadhani anajielewa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumza suala la watumishi ambao ni Watanzania wenzetu kuingwa kule mgodini. Najuliza mara mbili, labda Mheshimiwa Heche siku hizi amehama Tarime. Hata kabla ya *Corona* hakuna sehemu ambayo inajali suala la usalama kama migodini. Nasi tunaotoka kule kabla hata ya sisi kuanza kuingwa Bunge, ukienda kwenye maeneo ya migodi yanakingwa na dawa mpaka kupulizwa. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Heche akarudi jimboni kwake akachukua takwimu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kupiga watu biti kwenye Bunge, naona kama siyo sahihi. Mwenzi yuko *front* na wewe nadhani ungeenda kule kule mkapambana. Wewe kaa humu mwenzi anakula vichwa kule Mheshimiwa Heche. Kwa hiyo, unapotupiga biti kwamba kuna watu wanazunguka, hakuna anyetaka jimbo lako, anayetaka jimbo lako yuko kazini. Kwa hiyo, kaa kusubiri posho, watu wananawa na Ubunge kule, utakuja kuambilia manyoya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, tusitishane hapa; pamoja na majadiliano yaliyoendesha na timu ya Mheshimiwa Prof. Kabudi, tulichokipata tumekipata na ndiyo maana yakaitwa majadiliano. Kama walijadiliana wakaamua vinginevyo, basi Mheshimiwa Waziri ataeleza, lakini tusianze kutishana eti mliumizwa. Tukumbuke hapa sera yenu ninyi ilikuwa kututisha kwamba tutashtakiwa. Tulichokipata leo tumeshtakiwa wapi na Wazungu wamenyoosha maelezo hapa? Kwa hiyo, ni vizuri tukapeana muda; ukiwa unasema maneno, ukumbuke na wewe mwanzoni ulizungumza vitu gani? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine limezungumzwa hapa suala la kushuka thamani kwenye *Tanzanite*. Hili suala tulizungumza hata kwenye Kamati, tusitake mambo ya sifa. Kwanza kushuka thamani kuna vitu vingi; ni kweli sisi kama Kamati tumeliona, kuna watu waliofanya kazi ya kuhujumu ili kushusha thamani ya dhahabu, wanaeleweka. Tulitoa maoni yetu tukaelekeza Wizara ichukue hatua kwa wale watu wanaokwamisha na kuwapiga biti watu na kuleta mambo ya ovyo ovyo kuwahamisha wale wanunuzi wakubwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine na mvua; hata ukimwuliza Mheshimiwa Waziri leo dhahabu haipatikani kama *Tanzanite* kwa sababu kumejaa maji. Mvua hii ni neema kubwa imetokea lakini utendaji kazi umekuwa ni mgumu. Kwa hiyo, huwezi kulinganisha soko la kipindi cha kiangazi na leo katika upatikanaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Henche, ni vizuri pia, Mheshimiwa Heche tunapokuwanaye kwenye kamati, ni mjumbe mwenzangu, tatizo tukikaribishwa kwenye chai anakuwa wa kwanza, hamalizi hoja. Ni vizuri ukawa unatoa haya mawazo tunakusaidia kuliko kuja kuonekana hufai na wewe ni mwalimu; sasa najjuliza Mheshimiwa Heche ukimaliza ubunge unategemea kuwa mwalimu au mfanyabiashara?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Jamani, nilisema leo patachimbika hapa, lakini jambo muhimu ni kwamba, Mheshimiwa Heche anaambiwa watu wako *site*, hilo ndio jambo muhimu, watu wako *site*. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ambaye yuko kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Maftah Nachuma ambaye wote wako Msekwa.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia, lakini pia niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa leo na kuweza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze kabisa kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kuweza kufanya yale ambayo Watanzania walikuwa wakiyahitaji kutuondoa sehemu moja na kutupeleka sehemu nyingine. Na hususan sisi wachimbaji wadogo alipokubali kukaa na sisi na kuweza kusikiliza changamoto zetu kwenye Wizara hii ama sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, nipende kumpongeza Makamu wa Rais Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri Mkuu kwa kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais kuweza kulisukuma gurudumu la maendeleo la nchi yetu ya Tanzania, lakini pia niwashukuru Mawaziri, Manaibu wa Mawaziri, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu, pamoja na watumishi wengine wa Wizara zote kwa kumuunga Mheshimiwa Rais kwa kauli yake aliposema hapa kazi tu. Na kweli, kazi imefanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia, nipende kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, na Naibu Spika kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya ndani ya miaka hii mkitano kuweza kuborsha Bunge letu na kutusimamia na kutupa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi za hili gonjwa lililoko mbele yetu, janga la kimataifa, janga la corona. Kwa kweli, Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi imechukua hatua mbalimbali kuweza kuwaelimisha wananchi kuweza kujikinga na hili tatizo la corona, lakini nataka nitoe ushauri kidogo; sisi

tunaishi huko mtaani kwa kweli, Wananchi wetu bado wanahitaji elimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vijana wetu wa bodaboda hawajaelewa kabisa bado wanapakia mishkaki, lakini pia bado kuna mikusanyiko mingi, kwenye mabaa, bado baa ziko wazi, mikusanyiko mbalimbali ipo. Naiomba Serikali yangu kwa kweli, ijaribu sana kutoa elimu maeneo hayo mbalimbali, hususan suala la bar, kuna mchangiaji mmoja alichangia hapo nyuma akasema kwa nini bar hizo zisifungwe baada ya janga hili zifunguliwe. Na mtu kama ni mlevi ama mnywaji apitie pombe yake anywee nyumbani, lakini hali hi kwa kweli bado inatisha, wananchi wetu wengi bado hawajafahamu ukubwa wa hili janga.

Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza Waziri wa Madini na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kweli, kwa kazi nzuri ambazo mnazifanya. Mheshimiwa Waziri wa Madini nataka nichangie kidogo tu leo. Kwanza nikushukuru wewe kwa kuweza kutupa leseni 22 za wachimbaji wadogo katika eneo la Burulu, Wilaya ya Nyanghwale. Kwa mara ya kwanza Wilaya ya Nyanghwale imeweza kupata leseni kwa wachimbaji, vikundi 22, lakini bado kuna maeneo mengine kuna mapungufu naomba nitoe maombi:-

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ombi la kwanza kwamba, kuna maeneo ambayo wachimbaji wetu wanaendelea kuyachimba, nilikuwa ninaomba, kama kuna uwezekano wakarasimishwa maeneo hayo, ili waweze kupata leseni za uchimbaji. Maeneo hayo yako mengi ikiwemo kama Isonda, Nyamalapa, Kasubuya na maeneo mengine, lakini pia napenda nilete ombi kwako Mheshimiwa Waziri kwamba, sasa hivi Watanzania walio wengi ambao ni wachimbaji kwa kweli, hili suala la soko limeleta shida kutokana na hili gonjwa la corona.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa ananisikia pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri wa Madini kwamba, kama kuna uwezekano hawa ma-*super dealer* ama *master dealer* wakopeshwe fedha.

Mheshimiwa Spika, mfano ana mtaji wake wa kilo 200, kilo 200 aweze kuja kuziweka benki, apewe pesa tena za kutosha kwenda kununua kilo 100. Kama zitamalizika hizo kilo 100 alete kilo 100 apewe tena mkopo wa kilo 50, iende hivyo, yawezekana Mwenyezi Mungu akafungua hali ikarudi ile ya kawaida, ataanza kurejesha malipo kutokana na mfumo uleule wa mwanzo. Kama alianza mara ya mwisho alikopa kilo 50 arudishe fedha ya kilo 50 anapewa zile kilo 100 zake anaenda anauza tena anaenda anagomboa mpaka zile kilo 200 kwa sababu, wenzangu wameshasema, kama Mheshimiwa Bulembo kwamba, soko kule ama Mheshimiwa Musukuma kwamba, sasahivi dhahabu kule inazagaa haina wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, na iwapo Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kwenda kununua dhahabu hiyo, itaweza kukusanya mapato yake kwa sababu, mrahapa utalipwa na fedha itakuwa iko katika usalama zaidi. Lakini Mheshimiwa Waziri wa Madini sisi Wilaya ya Nyanghwale tayari tumeshajenga soko letu la dhahabu pale. Ninashindwa kuelewa ni tatizo gani ambalo limechelewesha kufunguliwa kwa hilo soko kwasababu, soko hilo litakapofunguliwa litamfanya yule mwenye dhahabu yake asi-*risk*. Sasa hivi Wilaya ya Nyanghwale ukipata dhahabu unaipeleka kilometa 100 kwenda Geita kuuza na kurudi kilometa 100 ni sawa na kilometa 200 ni *risk* kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu jingine ni kwamba, tufunguliwe Ofisi ya Afisa Madini pale kuepusha usumbufu wa kufuata vibali Geita kilometa 100 kwenda kufuata na kurudi kilometa 100. Kwenda kuuza kilometa 100 na kurudi kilometa 200, unatumia kilometa 400 kwa kweli, inatugharimu sana na inawagharimu sana wachimbaji wadogo. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kwamba, soko hilo lifunguliwe, ili kuweza kupunguza safari za kwenda mbali kwenda kuuza madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa kumalizia maeneo ambayo nimeyataja kumekuwa na uchimbaji ambao unaendelea na Wananchi walio wengi dhahabu ile

pale inakuwa haiieleweki inaenda wapi kwa hiyo, Serikali inapoteza mapato yaliyo mengi sana. Nakuomba Mheshimiwa Waziri fuatilia maeneo hayo, ili sasa kama yako wazi ama kulikuwa na wale watafiti wenye leseni zao za utafiti na hawafanyi utafiti, basi maeneo yale yaweze kupewa wale wachimbaji wadogo. Mheshimiwa Waziri nitakuwa sina mengi sana, yangu yalikuwa ni hayo machache.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Nassor, Mbunge wa Nyanghwale. Nimeshakutaja Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma kutoka kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba; Mheshimiwa Nachuma.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii ya Madini. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah ambaye ameendelea kutupa afya njema na pamoja na ugonjwa huu kwamba, umeingia hapa Bungeni, bado Wabunge wengi tuko salama kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa kifupi sana kama ifuatavyo; mwaka jana wakati nimechangia Wizara hii Mheshimiwa Waziri Dotto Biteko aliniahidi kwamba, atanipeleka kwenda kuona ile inaitwa *One Stop Centre* kule Arusha, lakini ahadi yake hajaitekeleza. Kwa hiyo, kwa kuwa alizungumza ndani ya *Hansard*, ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimuombe Mheshimiwa Dotto Biteko kwamba, mwaka huu aweze kunipeleka ili tuweze kuona hiyo inayoitwa *One Stop Centre* ambayo wakati ule tunafanya uchunguzi wa Madini ya *Tanzanite* tuliweza kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka jana nilieleza hapa kwamba, madini yote ya *blue sapphire* duniani kwa kiasi

kikubwa yanaonekana yanatoka Sri Lanka kule kwenye Mji wa Colombo, pale Sri Lanka. Na mwaka jana nilihoji nikamhoji Mheshimiwa Waziri kwamba, madini haya yanachimbwa kule Kusini kwa kiasi kikubwa sana hasa kwenye maeneo yale ya pale Tunduru na pale Tunduru kuna wageni wengi kutoka Sri Lanka.

Mheshimiwa Spika, nilieleza mwaka jana kwamba, yale madini yakichukuliwa pale Tunduru, Kusini mwa Tanzania, yanapelekwa kwenye ji wa Colombo kule Sri Lanka. Wale wenzetu wa Sri Lanka wameweka *Certificate of Origin* kwamba, yale madini yanatoka Sri Lanka wakati kwa kiasi kikubwa yale madini yanatoka kwetu Tanzania hapa. Mwaka jana nilihoji ndani ya Bunge hili nikamuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Spika, na ilikuwa ni mapendekezo ya Kamati yako uliyounda kwamba, madini haya yawanufaishe Watanzania. Na kamati pia ilipendekeza kwamba, madini yote yanayotoka Tanzania, ikiwemo hii *Blue Saphire*, ambayo haijulikani kabisa wala haitajwi kabisa, hata kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hataji kabisa hii *Blue Saphire* ambayo ina thamani kubwa sana kuliko pengine hata Madini ya *Tanzanite*, lakini haijulikani kama sisi Watanzania tunayo hii *Blue Saphire* kwamba, ili tuweze kuifahamu Watanzania na walimwengu waweze kujua kwamba, madini haya yako Tanzania ni lazima tuwe na cheti kile cha asili kwamba, haya madini tunayo sisi Tanzania maeneo ya Kusini, *Blue Saphire*.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa.

SPIKA: Tunakusikia vizuri Mheshimiwa Nachuma, endelea tu na mchango wako.

SPIKA: Kuna Taarifa huko Msekwa?

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, eeh! kuna Taarifa huko Msekwa.

SPIKA: Haya, ahsante, anayetaka kutoa Taarifa aendelee.

T A A R I F A

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana; napenda nimpe Taarifa Mheshimiwa Maftah kuwa, hata Alexander, Madini aina ya Alexander, yanapatikana Tunduru, lakini katika Taarifa ya Madini hawaitaji Tunduru, matokeo yake tunakosa uchumi mkubwa kutoka Tunduru wakati wangeweza kutengenezea mazingira mazuri. Na hiyo napenda nikupe kama Taarifa, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lulida, Mheshimiwa Nachuma endelea, pokea Taarifa hiyo.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naipokea kwa mikono miwili hiyo Taarifa ya Mheshimiwa Lulida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa nasema ni kwamba, Serikali iweke mkakati wa dharti, lakini pia ifuatilie kwa hali ya umakini wa hali ya juu sana. Madini haya ya *Blue Saphire* ni madini ambayo yana thamani kuliko hata Madini ya *Tanzanite*. Tunaomba Tanzania tuwe na cheti cha asili kutokana na haya Madini ya *Blue Saphire* pale Tunduru.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda kuchangia; tulielezwa hapa kwamba, pale Mererani, Arusha, ambapo kunachimbwa madini haya ya *tanzanite* Serikali ilitoa leseni nyingi sana. Na kamati yako ilitoa mapendekezo kwamba, zile leseni ambazo zimetolewa kwa wachimbaji wadogowadogo ambazo zinasababisha kutobozana kule chini na mwisho wa siku wanakutana na wanauwana na wengine wanauwawa na ule mgodi wa *Tanzanite One Limited*, wale wachimbaji wa kule ndani wakikutwa wanapigwa risasi, wengine wanapigwa mapanga, wanapigwa masururu, majembe, wanakufa kule chini kwa chini na makaburi yao yanakuwa kule chini kwa chini.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza kwamba, ili kuondoa vifo na mauaji ya hawa wachimbaji wadogowadogo, leseni zimetolewa nyingi zaidi ya 900, eneo lenyewe ni dogo la Mererani pale, basi hizi leseni ziunganishwe. Mwaka jana tulizungumza ndani ya Bunge tukapendekeza kwamba, yale mapendekezo ya kamati yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze kwamba, wamefukia wapi? Yale mapendekezo ya kamati ya kuziunganisha leseni zaidi ya 900 zilizotolewa pale Mererani, Arusha, wale wachimbaji wadogo wawe kwenye vikundi ili kuondoa kuuawa kwa Watanzania kwenye mitobozano kule chini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Kamati yako ilichunguza sana ikabaini ya kuwa wale waliopewa mgodi wa *TML* pale Mererani, Arusha, wakishirikiana na *STAMICO* ambayo ni Kampuni ya Serikali wamekuwa wakiiba madini yale kwa wakati ule kabla tume zile za Mheshimiwa Ossoro na Prof. Huruma ambazo Mheshimiwa Rais aliziunda. Wale watu waliweza kugundulika wameiba zaidi ya ndoo sita za madini ya *tanzanite* na kamati ilipendekeza wale watu wachukuliwe hatua. Lakini baada ya huku na huku tukaambiwa wale watu walioiba zile ndoo na ushahidi upo, wameiba mandoo ya *tanzanite* bilioni kwa mabilioni yenye thamani ya bilioni nyingi sana, wale watu hawajachukuliwa hatua mpaka leo wanaendelea kutembea pale Mererani, Arusha, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, na tulimkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa wale ni wezi na ushahidi umebainika. Wale akina Ridhiwani Ulaah, wanaonekana kwenye *clip* ya *video* ile wakiiba madini ya *tanzanite* na kuikoshesha Serikali mapato, zaidi ya fedha ambazo hazijulikani, ndoo zaidi ya sita. Wale watu bado wanatembea pale na wameendelea kupewa ule mgodi wanaendelea kutuibia tena. Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri atekeleze maagizo ya kamati yako ambayo wewe uliunda

ya kuchukunguza kwa nini madini ya *tanzanite* hayawanufaishi Watanzania na wale watu waliohusika na wizi wachukuliwe hatua, bado wanaendelea kutuibia pale Mererani, Arusha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri alizingatie sana. Mwaka jana wakati tuko kwenye kipindi hiki cha bajeti kulikuwa na taasisi hapa zimekuja kufanya maonesho ya madini, mwaka huu sijaona sijui kwa sababu tuna corona, hatuwezi kulizungumzia sana hilo, lakini mwaka jana walikuja wakatusieleza kwamba, kuna maeneo ambayo tayari wamefanya utafiti wa kuweza kuchimba madini ya *graphite*. Na madini haya yamegundulika kule Ruangwa, kule jimboni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, walitueleza hapa ndani ya Bunge lako na akatuambia kwamba, tayari vibali vyote vimepatikana kwa hiyo, ni kila kitu kimepatikana bado kupewa ruhusa tu na Wizara waende kuanzisha ule mradi, waweze kuweka ile *branch* pale Ruangwa kule kwa Waziri Mkuu waweze kuchimba madini ya *graphite*. Madini ambayo walitueleza ya kwamba, yakichimbwa yanatengeneza mashine za ndege na mambo mengine, Wananchi wa Mikoa ya Lindi, Wananchi wa Mtwara na Lindi tungeweza kupata ajira sana kama huu mgodi ungeruhusiwa wale wazungu wakaja kuchimba. Na Serikali...

SPIKA: Kengele ya pili eeh?

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:...haijaambiwa itoe hata senti tano...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nachuma...

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:...wale wazungu wanakuja kuwekeza wana fedha zao wao wenyewe. Kinachotakiwa kifanywe Serikali ni kuwasainia tu.

Mheshimiwa Spika, ni kengele yangu ya kwanza hiyo?

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abdallah Nachuma, tunakushukuru sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Salome Makamba na atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige na atakayefuata Mheshimiwa Nape Nnauye

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi nichangie Wizara hii nyeti ya Madini ambapo pia na mimi nimetoka Shinyanga, sehemu ambapo kuna madini mengi ya almasi na dhahabu.

Kabla sijaanza mchango wangu rasmi, kuna Mbunge mmoja humu ndani ametumia zaidi ya 95% ya muda wake wa kuchangia kutaja jina langu kwa hiyo, nikaona ni busara sababu, kwa kweli, nilikuwa simfahamu, yaani ndio nimemuona leo nikawa nashanga huyu ni Mbunge kweli! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nikatupia jicho pembeni kidogo niangalie kwenye mtandao na tafiti, nikagundua huyu Mbunge anaitwa Mheshimiwa Nchambi, kumbe ni Mbunge wa Kishapu, lakini nikagundua, nikaona kwenye taarifa kwamba, huyu Mbunge ni miongoni kati ya Wabunge watoro kwenye Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na nikajjuliza kwa nini amekuwa mtoro kwa sababu, aliomba mwenyewe nafasi hii ya kuja kuwakilisha wananchi wa Kishapu, hata wananchi hao wameamua kuniita nije niwawakilishe badala yake? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nikagundua kumbe huyu jamaa alikuwa ni mmoja kati ya *suppliers* kwenye Mgodu wa *Stamigold*. Na katika Mgodu ule wa *Stamigold* huyu jamaa yetu Mheshimiwa Nchambi, kuna tume maalum iliundwa kwenda kuchunguza ubadhirifu mkubwa wa pesa uliofanyika kule, sasa huyu alikuwa ni mmoja kati ya *suppliers* na alikamatwa kwa kosa la kujaribu ku-over charge billions of money Serikali kule Mgodu wa *Stamigold*, alikamatwa akawekwa ndani zaidi ya wiki nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata sifa tu ya kuwa Mbunge, hivi sasa hivi alitakiwa awe ndani kama watuhumiwa wengine wowote wale.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Hata sifa ya kuwa Mbunge kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mashaka kidogo kwa hiyo, alikuwa anatafuta namna ya kuonekana kwamba...

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: ...yuko Bungeni kupitia nafasi ya Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Salome kuna Taarifa, sijajua iko Msekwa au ipo wapi Taarifa? Mheshimiwa Salome naomba upokee Taarifa tafadhali, Taarifa iko wapi?

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, Taarifa iko hapa.

SPIKA: Ndio!

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Salome. Na ninaomba Taarifa ninayompa, nakuomba Mzee wangu unisikilize kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, anachokiongea ni uwongo mtupu, sijawahi kuwekwa ndani wiki moja, lakini pia Taarifa ninayompa kama anao ushahidi au-*table* mbele yako na kamati yako ifanye uchunguzi kama nimewahi kuwekwa ndani wiki moja. Na kama itakuwa vinginevyo, nimekuambia kwenye hotuba yangu huyu Mbunge ni mwongo ni jiongo

kubwa hili limama kwa hiyo, naomba Taarifa ninayompa atoe ushahidi juu ya kile alichokieleza.

SPIKA: Ahsante sana, sasa ningeliomba hebu mjepushe kwanza na *personal attacks* turudi kwenye hoja za msingi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe unafahamu kabisa *attacks* alizokuwa ananifanyia Mheshimiwa Nchambi ni kinyume na taratibu, ni kinyume na kanuni. Na nilikaa kimya kwa sababu, nilijua nitapata nafasi ya kueleza kuhusu Mheshimiwa Nchambi, nilikaa kimya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, usi...

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Salome unanilazimisha kusimama unaposema ni kinyume na Kanuni na msimamizi wa Kanuni nipo, maana yake hapo sasa na unaniweka kwenye chungu ambacho nadhani sipo. Amesema ni nini ambacho ulisema siku za nyuma na kwa kweli vitu vingi alivyovisema ni kweli ulivisema. Siwezi kusema vyote lakini ni vingi na akaeleza ni kwa nini yeye anatofautiana na ulichokisema. Sasa ukisema kikanuni imekuwakuwaje hapo kidogo utanipa taabu, labda unionesha ni Kanuni ipi iliyovunjwa. Sasa na yeye kama ni suala la Kanuni ametaka tu kujua uliposema aliwekwa ndani wiki moja, endapo jambo hilo ni kweli au sio kweli.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Ni kweli.

SPIKA: Ili ulifute ili tuendelee na mambo mengine, basi. Kama una ya kujibu katika yale, wewe endelea tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Lakini ukija kwenye Kanuni unatugusa sasa inakuwa taabu, labda uanze kutuonesha ni Kanuni ipi iliyovunjwa na kadhalika. Hilo la wiki moja, jaribu kuliweka sawa tu kama bado una- *insist* au hilo unaliondoa ili uendele.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, wewe ni mwalimu wangu wa Kanuni, Mheshimiwa Nchambi alikamatwa na TAKUKURU, Mheshimiwa Nchambi ana kesi Mahakamani ambayo inamkabili kwa kosa la ku-*collude* na wafanyakazi wa *STAMIGOLD* kutaka kuiibia Serikali kwa ku-*overcharge*. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Nchambi anaomba huruma ya Bunge lako na Serikali kwa kujaribu kuni-*attack* na hilo amekwama. Wananchi wa Kishapu hawataki Mbunge mtoro ambaye hahudhurii Bunge. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa hilo, naomba hebu vuka maana hawa Wasukuma wanataka kuniharibia utaratibu, endelea na lingine. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Nchambi hayupo kwenye kiti chake.

SPIKA: Halafu Nchambi naomba urudi kwako. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Analeta *Corona*.

SPIKA: Nawaomba Wabunge wengine wote ambao mnazunguka kwenye viti, tafadhali msifanye hivyo, mnajua mazingira tuliyonayo. (*Makofi*)

La pili, nawaomba wale ambao mnamuandikia sana Waziri Mkuu vikaratasi, hebu punguzeni *unless ni absolutely necessary* na uwe na *sanitizer*, basi uki-*sanitize* lakini simu yake iko *on*. Hata mimi kama unataka kuniambia jambo niandikie kwenye simu, simu yangu iko *on*, *message* yako naipata tu bila tatizo lolote. Pia tunashauri wale ambao mnakuja na mabegi makubwa makubwa kutoka nyumbani au wapi huko na hasa Wabunge akina mama, hapa napunguza sauti kidogo, hebu tupunguze tuje na vibegi vidogo vidogo hivi na kadhalika kwa sababu huu ni wakati wa *risk*, kubeba mavitu makubwa makubwa kwenye maeneo yale ambayo *tray* tunaweka wote vitu mbalimbali na kadhalika, tuchukue hizo *measures*.

Nilikuwa nam-*cool down* Salome ili arudi kwenye mstari sasa. Mheshimiwa Salome endelea. (*Kicheko*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nilikuelewa.

Mheshimiwa Spika, wakati Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anawasilisha hotuba yake, alinipa majibu ya maswali mengi niliyokuwa najiuliza hasa kwenye namna ambavyo bajeti ya Wizara hii imekuwa haipelekwi. Alisema mwaka 2017/18, Wizara ya Madini ilipelekewa asilimia 3.8; mwaka 2018/2019 walipelekewa asilimia 0.5; na mwaka 2019/20 ambayo ndiyo tunaimaliza wamepelekewa *zero budget*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikajiuliza maswali, hivi ni kwa nini Wizara ya Madini imekuwa ikitumia mlango wa wanaouita kurasimisha wachimbaji wadogo wadogo kama ndiyo njia ya kujipatia mapato ili iweze kujiendesha? Majibu yako kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilianza kwa kusema kipindi kile kwenye Wizara ya TAMISEMI nikasema kwamba Serikali kwa sababu ya kutokupeleka pesa zile ambazo Bunge hili limepitisha inalazimisha watendaji wa Serikali na Wizara

kutafuta namna mbadala ya kujipatia mapato ili iendeshe Wizara hizo. Hapa nitajikita kwenye wachimbaji wadogo wadogo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye sekta ya wachimbaji wadogo wadogo, Wizara ya Madini inajipambanua kwamba imeleta mkakati wa kurasimisha sekta hii. Wanarasimisha vipi? Wanatengeneza vikundi ambavyo vinawasimamia wachimbaji wadogo wadogo, vikundi vile ni vya watu wa kawaida, hawana utaalum wa aina yoyote, wenyewe wanadai kwamba wale watu wana uzoefu wa madini ...

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Salome, kupitia Wizara hiihii ya Madini tumetengeneza Kikosi Kazi cha kila Mkoa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Kwa Mkoa wa Shinyanga ambako yeye anatoka tuna kitu kinaitwa SHIREMA ambao ni Umoja wa Wachimbaji Wadogo wa Mkoa mzima wa Shinyanga ambao yeye mpaka leo hii hajawahi kukutana na uongozi wala wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, tumenufaika nini na SHIREMA kupitia Wizara ya Madini? Kwa kupitia SHIREMA leo Shinyanga ni Mkoa wa pili ambao unakusanya mapato mazuri na makubwa kwa Wizara ya Madini. Kwa nini makusanyo hayo yanapatikana? Ni kwa sababu baada ya kurasimishwa yaani baada ya Wizara kusimamia wachimbaji wadogo wapewe maeneo, wafanye shughuli zao, tumewapa elimu kupitia SHIREMA na Wizara ya Madini lakini pia wamepata usimamizi wa hali ya juu, wanazalisha na ndiyo sababu tunakusanya. Mkoa huo huo wa Shinyanga ni mkoa ambao una soko kubwa la madini linaloongoza nchi hii, linanunua madini ya

almasi na dhahabu kwa wakati mmoja lakini hata *BoT* pia tumewapa nafasi ya kukaa pale ili kuwasaidia wachimbaji wadogo wanapofanya shughuli zao.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimpe tu taarifa wachimbaji wadogo wamenufaika na yeye kwa sababu hayuko Mkoa wa Shinyanga kwa wachimbaji wadogo hawezi kujua hiyo taarifa nayompatia. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome, pokea taarifa hiyo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, amesahau sehemu moja tu, angesema ana hisa ngapi kwenye SHIREMA halafu *a-declare interest* ili twende vizuri, angesema hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi niendeleo. Sasa wanatengeneza hivi vikundi maalum ambavyo vinakwenda kusimamia wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo hayo ya wachimbaji kama hapo Mwadui au kwenye *rush* mbalimbali. Wakifika pale, wale watu wanasimamia nini? Kwanza wanasema wanasimamia usalama. Pili, wanasema wanakusanya mrahaba wa Serikali, kazi ambayo mimi naamini mfumo wa Serikali ambao unaweza kufanya kazi ya kukusanya mrahaba *at zero cost* upo lakini watu wanalipwa.

Mheshimiwa Spika, mrahaba wa Serikali ni asilimia 7, hawa watu kwa sababu wanaenda kusimamia usalama na usalama huo wanaousimamia labda wanasubiri mtu akifukiwa kwenye mashimo wasaidie kuratibu shughuli za mazishi na mambo kama hayo, ndiyo huo usalama wanaouongelea, kwa kufanya hivyo, wanatoza asilimia 30 ya *gross production*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naposema *gross production* namaanisha. Mimi leo Salome niende kwenye eneo la

wachimbaji wadogo nikaombe shimo nianze kuchimba nafunga matimba, nalipa vibarua, navuta maji, zote hizo ni gharama, nikifika kwenye mwamba nitatoa mifuko 10, nikileta huku juu bila kujali gharama za uzalishaji, mifuko mitatu lazima niwape kile kikundi ambacho Serikali inakisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni wizi kama wizi mwingine wowote unaofanywa kwenye Taifa hili.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, tena ni wizi wa hali ya juu. *(Makofi)*

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, hawa watu siyo wataalam, hawachangii chochote kwenye gharama za uzalishaji, hawajali umeingia hasara kiasi gani kikubwa wanachokijua ...

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa hajakaa siku nyingi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kikubwa wanachokijua ni kwamba wenyewe wanasimamia mrahaba wa Serikali ambao ni asilimia 7 na ukishamaliza kupandisha hii mifuko kutoka kwenye shimo kuja juu, watakukata asilimia 30. Hutaki, wanakupa kesi, unakwamisha kukusanya mapato ya Serikali, kama hutaki utafukuzwa kwenye mgodi au utaingia kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote siwalaumu Wizara ya Madini, yanasababishwa na kutokupeleka pesa ambazo tumepanga kwenye Bunge lako Tukufu.

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimia Salome, kuna taarifa. Imesemekana unaongelea eneo ambalo wewe ni mgeni sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Musukuma, Taarifa tafadhali.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa taarifa mchangiaji mjomba wangu Salome na siyo mgeni kama alivyosemwa. Salome amekulia kwenye madini na hata kabla ya *degree* na yeye alikuwa kwenye huo mfumo. Kwa hiyo, napenda azungumze tu ukweli maana anachokizungumza ni upotoshaji. Kama kweli ni sahihi mimi nataka amshari Waziri kwamba tufanyaje kwa sababu sisi tumekulia kwenye hiyo *industry* na wewe ukiwemo ila kwa sababu uko upande wa pili, wale wanaotoka kwenye machimbo wanafahamu, usipoweka huo udhibiti watu watauana leo leo hakuna machimbo yataendelea. Sasa leo Salome kaamua kabisa kupotosha, naomba atoe mbadala wake yeye Salome tuusikilize.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa *rush* aliouongea, samahani.

WABUNGE FULANI: Aaaa.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *rush* ni asilimia 70 kwa asilimia 30 anayoisema Mheshimiwa Salome, asilimia 15 ni ya mtu mwenye shamba, asilimia 15 ni ya mtoa huduma na 70 huyu mchimbaji mdogo ambaye alikuwa hana eneo lolote ndiyo anakwenda pale. Anapotosha umma, wachimbaji wadogo wanamshangaa yaani kuna asilimia 70 kwa asilimia 30. Kuna asilimia 15 ya mwenye shamba na kuna asilimia 15 nyingine, hafahamu hizi takwimu, aje kwetu sisi Wabunge tunaoshughulika na wachimbaji wadogo tumpe elimu asimsumbue Waziri.

SPIKA: Ahsante sana. Niliongeza tu kwa sababu ni jambo la elimu, siyo Wabunge wote hapa wanashughulika na mambo ya madini lakini ukweli unaozungumzwa ndiyo huo Salome, ndiyo ukweli wenyewe kwamba yule mchimbaji mdogo anachukua asilimia 70. Hii asilimia 30 inayoongelewa ndiyo wanagawana hao watu wa usalama na mwenye eneo lile. Ukiwaondoa hawa watu wanaoweka usalama maeneo yale basi watu watapigana mapanga kugawana ule udongo pale itakuwa ni *disaster* kubwa. Hata hivyo, tunatunza muda wako na kama unataka kulfafanua hilo endelea Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza ningekuomba, hii Wizara leo si tunajadili siku nzima na wewe una mamlaka ya kuongeza muda, kwa hiyo, kama watu wanataka kuchangia watachangia, wacha mimi nimalize, tafadhali. (*Makofi*)

SPIKA: Wanachosema ni kwamba unapotosha, hilo tu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, ngoja niweke sawa. *Speaking about* mwenye mashamba, nikutolee mfano mdogo tu. Pale nyuma ya mgodi wa Bulyanhulu kuna eneo linaitwa namba tisa...

SPIKA: Hapo unaongelea dhahabu sasa?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, *of course*, naongelea dhahabu.

SPIKA: Maana kuna almasi na dhahabu ili tuwe pamoja.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kujibu kabla ya kusikiliza ni kukosa busara tu. Wenyewe wanajibu hawajanisikiliza, wangenisikiliza nimalize halafu walete *arguments* zao. Mimi nimesema nimetoka Shinyanga, Shinyanga kuna madini mengi, ukilazimisha niongelee *perspective* ya almasi wakati mimi nataka niongelee ya

dhahabu ndiyo matokeo haya unapiga nje ya mstari.
(Kicheko/Makofi)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Tunaongelea dhahabu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Kuhusu hilo suala la mwenye mashamba, tena umenikumbusha jambo la muhimu sana. Nyuma ya mgodi wa Bulyanhulu eneo la *buffer zone* kuna mgodi wa wachimbaji wadogo ulikuwa pale kinyume na taratibu lakini Serikali ilikuwa inakusanya mapato. Sasa kuja kwenye hii dhana ya vikundi niliyokuwa naielezea, hiki kikundi kiko pale eneo hilo ninalolisema mimi watu wote walishalipwa fidia wakaondolewa, wote! Hakuna mtu anamiliki pale, ilikuwa inamiliki Mgodi wa Bulyanhulu ambao sasa hivi unaitwa Twiga. Sasa hicho kikundi ambacho Mheshimiwa Waziri anakijua, kimefika pale kinakusanya hiyo asilimia 30 na wanasema kwenye asilimia 30 kuna mgawanyo kwa ajili ya watu wanaitwa wenye mashamba, hao wenyewe mashamba wametoka wapi?

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa nazikataa kwa sababu...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, ya mwisho.

SPIKA: Tulieni kidogo. Kengele ya pili imeshalia Mheshimiwa Salome kaa na taarifa sipokei.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Mheshimiwa Salome sasa muda wako umeisha. Bahati nzuri Waheshimiwa anayefuatia kuchangia hapa ni Mbunge wa eneo ambalo Salome analiongelea, Bulyanhulu. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Maige kule Ukumbi wa Msekwa na wewe utatupatia maelezo ya hili jambo kama yapo.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nilikuwa natamani sana na mimi nitoe taarifa lakini huku ulikuwa hauruhusu. Naomba tu niongezee dakika moja au mbili katika mchango wangu ili niweze kulifafanua jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme anachokisema Mheshimiwa Salome Makamba ni kweli. (*Makofi*)

SPIKA: Naomba mtulie.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, Eneo la Namba 9 na Namba 2 ni maeneo ambayo yalivamiwa na wachimbaji wadogo wadogo. Wale wachimbaji wali-*organize* vikundi vyao; kuna vikundi vya wenyeji ambavyo vilikuwa vikifanya kazi pale vikazuiwa, wakaletwa wasimamizi bwana mmoja anaitwa Mwananyanzala ambaye amekuwa na mzozo mkubwa sana ukiongea na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga amewahi mpaka kumweka ndani kwa sababu ya usimamizi wa eneo hilo. Tukasema kwamba hizo asilimia 30 anazopewa siyo sawa, mimi nimemwandikia barua Mheshimiwa Waziri yenye kurasa tisa (9) nikieleza suala hili na nikamueleza nini kifanyike. (*Makofi*)

SPIKA: Naomba tumpe nafasi tumsikilize Mheshimiwa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nikasema asilimia 15 inayolipwa kwa msimamizi inalipwa kwa kutumia uwiano wa nchi nzima wakati *mineral rich* inatofautiana. Kwa mfano, pale kwenye *pit* au eneo la namba 2 au namba 9 kuna wakati mfuko mmoja wa kilo 20 unazalisha hadi gramu 30 za dhahabu. Kuna eneo lingine kwa mfano Wisolele ambako ni kijijini kwangu, mfuko mmoja wa kilo 20 unazalisha hadi gramu 0.2. Ukiangalia huku anazalisha 0.2 anapewa mifuko 15 katika 100 huku anazalisha gramu 30 kwa mfuko anapewa mifuko hiyo hiyo 15 kama msimamizi. Nikasema suala hilo siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu niseme kwamba kimsingi anachokisema Mheshimiwa Salome

Makamba kwenye eneo hilo yuko sahihi. Mheshimiwa Waziri nilishamuandikia barua kuhusu suala hilo naomba aifanyie kazi barua yangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba tu niende kwenye mchango wangu. Kwanza naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo anachukua katika kupambana na janga la Corona.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

T A A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, tunaomba uturuhusu.

SPIKA: Mheshimiwa Maige unapea taarifa. Mheshimiwa Musukuma, tafadhali kifupi.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nimpe taarifa Mheshimiwa Maige.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maige ni mchimbaji mwenzetu na ameishi kwenye maisha ya uchimbaji tunafahamiana. Kitendo cha kusema kwamba kuna wachimbaji walivamia maeneo ya mgodi, sio kweli! Sehemu ya Namba 9 ni sehemu ambayo ilikuwa haijalipwa fidia na mmiliki wa lile shamba alikuwa anaitwa Mayunga.

WABUNGE FULANI: Aaaa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Tuelewane, ninyi hamuelewi takwimu za mgodi, tuongee watu wenye dhahabu humu ndani.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, baada ya kurudi kwenye mashamba yao, Wizara imefanya kazi kubwa ya kuushawishi mgodi umemlipa Mayunga na tunavyozungumza hakuna mtu.

Mheshimiwa Spika, wasikuchanganye, sehemu yoyote panapopatikana neema nchi hii hakuna maana ya kufunga kwamba hapa ni Kahama, huku ni Geita, hata leo Geita tuna watu wa Kahama. Kama tunalianzisha hili, tunajuana humu ndani tukawaondoe wa kwenu kule Geita wabaki watu wa Kahama tuone kama tutakuwa *fair*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, anachokisema Mheshimiwa Maige, tungeacha kuweka *personal interest*, kama mtu ulikosa, mwingine alipata, hayo mambo yalishapita. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Maige, taarifa hiyo ipokee.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, kiukweli kabisa ndani ya dhamiri yangu nimekuwa Bungeni miaka 15 unanifahamu, huwa sipendi kubishana hivi. Niseme nilichoandika kwa Waziri, nilimshauri kwamba kiasi ambacho analipwa yule anayeitwa msimamizi ambaye *in most cases* anakuwa *superimposed* na Kamisheni ya Madini, wananchi wa pale wameunda vikundi vyao, wanakuja kuambiwa ili mfanye kazi hapa lazima muwe na huyu. Kwa mfano, kuna eneo pale Wisolele kijijini kabisa kwa baba yangu, kuna eneo linaitwa Namba 5, walianza kuchimba Kikundi cha Chapakazi kinachoishi Segese, kikaja Kikundi kingine kinaitwa Mchakamchaka kikaambiwa ili muweze kusimamia eneo hili

lazima muungane na Kikundi cha Mchakamchaka na leo walikuwa wanasaini makubaliano ya namna ya kugawana kati ya Kikundi cha Mchakamchaka na Kikundi cha Chapakazi kwa ile asilimia 15 wanayoipata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, mimi ambacho nimekuwa nikilalamikia na ndiyo maana suala hili linaleta vurugu kubwa kwamba...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, mbona huko unawaruhusu.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, hawa wanaoitwa wasimamizi wanapewa kiwango kikubwa mno cha *share* ambacho hakiendani na kazi wanazozifanya kwa sababu miongoni mwa kazi ambazo zina-*justify* kupewa asilimia 15 ni kwamba watoe huduma za kijamii...

SPIKA: Mheshimiwa Maige, kuna taarifa unapewa na itakuwa ya mwisho. Mheshimiwa Salome.

T A A R I F A

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Maige kwamba baada ya mimi kufanya ziara kwenye eneo hilo Namba 9 na kusema nitawasemea jambo lao Bungeni, wale watu wameenda kufukuzwa, sasa hivi hawapo pale wana hali ngumu *as* kwa nini wametoa taarifa kwa Wabunge.

Moja kati ya mapendekezo ambayo atayasema Mheshimiwa Maige, niongezee, nataka Tume Maalum iundwe ili kwenda kuchunguza maeneo yote ya *rush* Tanzania hii namna ambavyo yanawaibia wananchi kupitia hiki kinachoitwa urasimishaji wa vikundi kwa asilimia 30. (*Makofi*)

SPIKA: Taarifa hiyo Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru nimeisikia, naomba tu niendelee na mchango wangu lakini kiukweli hilo eneo lina shida kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba katika mchango wangu nilikuwa nimedhamiria kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo anachukua katika kupambana na janga la *Corona*. Namwombe sana kwa Mwenyezi Mungu yeye na Serikali yote waweze kutuvusha kwenye janga hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa ambazo zinafanyika, napenda kwenye hili nishauri angalau mambo mawili yafuatayo. Kwanza, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri, kila mmoja afikirie kwenye Wizara yake, anaweza akatoa mchango gani katika kupambana na janga hili. Kwa sasa hivi ninavyoona Mawaziri karibu wote wameungana na hoja ya Mheshimiwa Ummu Mwalimu ya *sanitizer* na kunawa mikono wakati shughuli nyingine zinapaswa zifanyike.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sasa hivi kwenye Soko la Dunia bei ya mafuta imeanguka hadi chini ya dola 20. Mwezi Februari pipa moja la mafuta lilikuwa linauzwa zaidi ya dola 60. Hiyo kupungua kwa bei hivi kwa nini *EWURA* hawaja-*reflect* kwenye bei ya hapa Tanzania? *EWURA* ni taasisi ambayo inapaswa iingilie kati kuwanufaisha wananchi kutokana na janga la *Corona* kwa kutoa bei elekezi ambayo inaendana na mazingira ya sasa lakini hilo halifanyiki.

Mheshimiwa Spika, leo hii bei ya dhahabu kwenye migodi kama ambavyo umetusikia tunagombana imeshuka sana. Pale kwangu Segese sasa hivi dhahabu inauzwa kwa zile gramu 12 Sh.1,300,000 lakini kwenye soko la dunia inauzwa kati ya dola 1,710 ambazo ndio inaitwa *ounce*. Mwezi Februari kabla ya janga la corona pale Segese dhahabu ilikuwa inauzwa Sh.1,500,000 ina maana imepungua. Kule kwenye Soko la Dunia ilikuwa inauzwa kwa dola za Kimarekani 1,430

imeongezeka, sasa katika mazingira haya nini kinachoweza kufanyika?

Mheshimiwa Spika, kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais siku za nyuma, Benki Kuu haraka iwezekanavyo waingie katika kununua dhahabu kwanza ili kuongeza bei ya dhahabu katika soko la ndani lakini pia inajulikana kabisa kwamba dhahabu ndio inaitwa *safe harvest/ safe storage of value*. Inaweza ikafanya hivyo badala ya kutunza fedha za kigeni hizi tunazosema zinaweza zikaagiza kwa miezi sita bidhaa nje, inaweza ika-*convert* zile fedha kwa kununua dhahabu na ika-*store* dhahabu na kwa maana hiyo kwa sababu bei inazidi kupanda, ikaja kuuza kwa bei kubwa. Hili linawezekana Waziri wa Fedha akilifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu napenda sana nziombe hizi Wizara ziweze kufanya kazi kila moja, wa *EWURA* angalie kwenye mafuta tunafanyaje, wa Maji aangalie kwenye maji sasa hivi akinamama lishe wanachota maji kwenye madimbwi wanawanawisha watu, wasaidie namna gani hizi Mamlaka za Maji zinasaidia upatikanaji wa maji na kupunguza gharama za maji ili watu wapate maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa madini, ukiacha hayo tuliyoanza nayo kule mwanzo, kikubwa naomba niipongeze sana Wizara imefanya kazi kubwa, upo upungufu wa kiutendaji kwenye ngazi za chini hasa Ofisi ya Madini pale Kahama. Haya yote tuliyoyasema yanatokana na menejimenti ambayo haijawa nzuri pale Kahama na viongozi nafahamu tumekuwa tukiwasiliana nao kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, hivi juzi kwenye suala la kuwapatia wachimbaji wadogowadogo maeneo ya kufanyia kazi kwenye eneo la Wisolele, Tambalale, Bushimangira na Mwazimba tulisema kwamba maeneo haya baada ya Kampuni ya Mikumi *Exploration* muda wake kuisha, eneo hilo litolewe kwa wachimbaji wadogowadogo. Hata hivyo, juzi

wakati unafanyika ugawaji imetolewa leseni kwa kampuni moja, *actually* kwa *individuals* leseni 17 na vikundi vikapewa leseni mbili na vikundi vingine bado havijapewa leseni.

Mheshimiwa Spika, nNiombe leseni zitolewe kwa vikundi na wizara iwe karibu na Ofisi ya Madini Kahama, kuna upungufu ambao unajitokeza kutokana na usimamizi wao, unaleta migogoro, unachafua kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Waziri wetu, lakini unachafua kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais kwa sababu unatengeneza manung' uniko kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwenye majadiliano ya makinikia nilimuandikia barua Mheshimiwa Waziri Mkuu nikiomba hoja za wenyeji ziwekwe katika majadiliano, mojawapo ni fidia ya wananchi wa Bulyanhulu ambao hawakulipwa fidia mwaka 1996 walivyoondolewa. Suala hili nilijibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nitulie, litajadiliwa na baada ya majadiliano Kampuni ya Twiga italifanya kazi.

Nimuombe Mheshimiwa Waziri msimamizi wa sekta hii asimamie suala la fidia na wagonjwa wanaotokea kule mgodini, lakini kubwa zaidi asimamie madai ya *service levy* ambayo Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambayo imekuwa ikidai Mgodi wa Bulyanhulu kutoka mwaka 2000 zaidi ya shilingi bilioni 16 ambazo zimejadiliwa na TAMISEMI na Wizara ya Madini zile ambazo zimekuwa *reported* katika takwimu za *Barrick* wenyewe wala sio hizo za Osolo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba yale ambayo niliyapendekeza kwenye barua yangu ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa...

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini nimuombe Mheshimiwa Waziri

azingatie maombi yetu hayo kwamba hoja za wenyeji zizingatiwe katika utendaji kazi wa *Twiga Minerals Corporation*. Nashukuru na naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige. Sasa ni Mheshimiwa Nape Nnauye kama nilivyosema na baada ya hapo kwa sababu ya muda sasa tutakwenda upande wa Serikali na ataanza Mheshimiwa Ashatu, Mheshimiwa AG na Mheshimiwa Nyongo atafuatia. Mheshimiwa Nape Nnauye.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Madini. Nianze kwa kutoa pole kwa wale wote walioguswa na msiba wa shangazi yangu Mheshimiwa Mama Mchungaji Rwakatare, lakini pia nitoe pole kwa Watanzania ambao wamepoteza maisha yao kutokana na janga la *corona* na wale ambao ni wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, nipongeze juhudi za Serikali katika kulishughulikia suala zima la *corona*; Serikali pamoja na Watanzania kwa ujumla wake. Zipo jitihada kubwa zinafanyika na yapo maelekezo yanatolewa.

Mheshimiwa Spika, kipekee nizungumzie jambo moja hapa, kumekuwepo na jitihada pia za viongozi wa Serikali na dini kuturejesha kwenye nafasi ya Mungu katika Taifa letu. Bahati mbaya kumeanza kujitokeza *trend* ya kubeza na kukejeli nafasi ya Mungu kwenye maisha ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nadhani pamoja na tofauti zetu za imani na tunachokiona, tusibeze nafasi ya Mwenyezi Mungu kwenye jambo hili. Tuwaunge mkono viongozi wetu na wote niliowasiliza viongozi hawajasema tupuuze ushauri wa wataalam na maelekezo ya kisayansi, lakini nadhani kwa tofauti za chuki tu hizi tunabeza mno kiasi kwamba nafasi ya Mwenyezi Mungu kwa Taifa letu inataka kuwekwa mahali ambapo sio sahihi; tunajenga Taifa la ajabu sana. Tunaanza

asubuhi hapa kwa kumwomba Mungu atubariki, atusaidie tufanye maamuzi yetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa unyenyekevu sana, wale wanaokosoa tuchague maneno ya kutumia ili tusipoteze nafasi ya Mwenyezi Mungu kwa Taifa letu. Niwashukuru viongozi wetu kwa kuliona hili na isiishie kwenye *corona*, twende mbali na kwenye mambo mengine namna tunavyopendana, namna tunavyojali haki katika Taifa letu, tukimtanguliza Mwenyezi Mungu haki na ubinadamu utastawi katika nchi yetu na hilo litakuwa jambo jema. Hapa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuliona hili na kutupeleka huku, tuisahau nafasi ya Mwenyezi Mungu kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano na hasa Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa kuanzisha Wizara maalum inayoshughulikia madini, nadhani huu ulikua ni uamuzi wa busara sana. Tumeona hapa tunajadili madini peke yake lakini muda haututoshi, sasa ingekuwa nishati na madini ingekuwa kazi kubwa, hivyo nadhani uamuzi uliofanyika ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kumteua Mheshimiwa Doto Biteko kuwa Waziri wa Wizara hii ulikuwa ni uamuzi wa busara sana. Mheshimiwa Rais amefanya jambo kubwa, Mheshimiwa Biteko ameituliza Wizara hii na ametutendea haki vijana, ameonesha vijana tukipewa dhamana tunaweza.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Doto na wenzake na Mheshimiwa Doto amethibitisha wale waliohusika kumfanya awepo hapo wakiwemo wapiga kura wake kwamba walifanya jambo kubwa, la busara na ni matumaini yangu kwamba watamrudisha tena Bungeni hapa aje aendelee kulumikia Taifa letu. Najua sio yeye peke yake pamoja na Naibu wake na watendaji wote katika Serikali wamefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015 - 2020 upande wa wachimbaji wadogo inasema hivi, naomba niinukuu: *“Serikali itaelekezwa na Chama cha Mapinduzi kuwawezesha wachimbaji wadogo kujajiri kupitia sekta hii kwa kufanya yafuatayo:- Moja, kuwatambua, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji wa madini.”*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili sio suala la kwao, wameelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Serikali haijakurupuka kuwatambua, kuwarasimisha na kuwapatia maeneo ya uchimbaji na yapo maeneo mengine ya mafunzo, ruzuku na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne na kitu hii, Serikali imefuta leseni kubwa 554 za utafiti, leseni kubwa watu walikuwa wamemiliki maeneo, hawayaandelezi, Serikali imezifuta leseni hizo na hayo maeneo wamepewa wachimbaji wadogo, ni kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ni maelekezo. Ukitaka kupima utendaji, una-*benchmark*, *benchmark* yetu ni Ilani ya Uchaguzi. Tuliwaelekeza wawatambue, wawarasimisha na wawape maeneo; Serikali imefuta maeneo makubwa na imeyachukua na kuyapeleka kwa wachimbaji wadogo. Nadhani eneo hili ni eneo la kupongezwa sana, ni kazi nzuri imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Shinyanga yapo maeneo Segese, Mwabomba, Mwakitolyo na Mwazimba; Manyara, Geita, Simiyu, Singida, Mwanza, Kagera, Katavi, Pwani na maeneo mengine. Kazi hii imeajiri wafanyakazi zaidi ya 320,000, haya ni maelekezo ya Ilani. Ndio maana nasema Mheshimiwa Doto na wenzake wameitendea haki Wizara hii, wamefanya kazi nzuri na kazi hii hawakujituma wenyewe, wametumwa na Chama cha Mapinduzi na sisi tuliingia mkataba na wananchi tukawaambia wakituchagua hichi ndicho tutakachofanya. Eneo la wachimbaji wadogo, mimi nimezunguka katika maeneo haya, kama kuna maeneo wametuliza kelele ni eneo hili. Sasa kama yapo maeneo

ambayo bado yanahitaji marekebisho tuendeleo nayo.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, liko moja limezungumzwa na Mheshimiwa Mzee Bulembo na baadhi ya Wabunge hapa kwamba baada ya kazi hii nzuri, madini haya hasa dhahabu imepatikana kwa wingi, kwa sababu ya *corona* inawezekana wanunuzi sasa wanayumba hapa na pale, ni wakati muafaka Benki Kuu iingilie kati, ichukue hizi dhahabu, fedha hizi ziende kwa wananchi, dhahabu waitunze baadaye wataiua kwa bei nzuri. Kama sio Benki Kuu basi wawadhamini hata wafanyabiashara, waweke *guarantee* waende wakachukue madini haya.

Mheshimiwa Spika, naamini ushauri huu ukichukuliwa kwanza tutapeleka fedha itakwenda kusaidia, lakini tutawaokoa hawa wachimbaji wadogo na tutabaki na dhamana kubwa kwenye Benki Kuu kwa sababu hii dhahabu ipo na tutakwenda tukaiuze.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Unapewa taarifa Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Musukuma tafadhali.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa tu mzungumzaji kwa maneno mazuri anayozungumza kwamba Serikali yetu sikivu kama ilivyofanya kwenye kuokoa zao la korosho kule Lindi na Mtwara, iokoe pia dhahabu ambayo tulipigana kwa muda mrefu kuiokoa isikwepeshwe. Leo tunakusanya karibu tani moja na nusu kwa mwezi. Serikali ichukue pesa ikaokoe pia dhahabu kama ilivyookoa korosho. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa taarifa ya ndugu ya Mheshimiwa Musukuma. Bahati mbaya wakati tunatetea korosho alipata shida, ila kwenye

dhahabu mimi namtetea kwa sababu ni wachimbaji wadogo na ni Watanzania ambao mimi nilishiriki kusikiliza maoni yao na kutengeneza Ilani ya Uchaguzi. Kwa hiyo inapotekelezwa nina wajibu wa kuipongeza Serikali yangu kwamba imefanya kazi nzuri. Kwa hiyo, namshukuru kwa taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huu ni ushauri Benki Kuu iingilie kati, lakini kama Benki Kuu inaona tabu basi wazungume na mabengi au wafanyabiashara, tuwaokoe wasibaki na hizi dhahabu majumbani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho; pale Mkoa wa Lindi, Jimboni Mtama Kampuni ya *Volt* walipewa leseni ya utafiti wa madini ya buni au *graphite*, wamefanya utafiti wao, wamepata yale madini; haya maeneo yamechukuliwa ni maeneo ya wananchi. Mchakato huu umechukua muda mrefu kukamilika. Wananchi wamechukuliwa maeneo yao na fidia hawajapata, ni eneo moja tu la Kata ya Namanga ila lina wananchi wengi na maeneo yao yaliyochukuliwa ni makubwa. Nilitamani Waziri atoe neno hapa, aseme mchakato huu umefikia wapi ili wananchi wajue wanafanya nini tuendelee na utaratibu wa maendeleo kwenye eneo letu.

SPIKA: Ahsante malizia

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nampongeza Waziri, naipongeza Serikali, waendelee kuchapa kazi. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana kwa mchango wako.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Madini, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, usimamizi mzuri wa mikakati na sheria za ulinzi wa rasilimali na maliasili zetu umekuwa chachu ya kukua na kuimarika kwa sekta ya madini nchini. Usimamizi huo umeifanya sekta hiyo kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la Taifa. Mathalani, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019/2020 mchango wa sekta ya madini ulikuwa asilimia 13.7. Katika kipindi hicho, sekta ya madini ilishika nafasi ya pili katika kuchangia pato la Taifa baada ya sekta ya ujenzi iliyochangia asilimia 16.5.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi saba kufikia Januari 2020, maduhuli ya Serikali yaliyokusanywa kupitia sekta ya madini ni shilingi bilioni 284.4. Kiwango hicho ni sawa na asilimia 60.4 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 470.89. Mafanikio hayo ni ishara tosha ya kuendelea kuimarika kwa sekta hii kufuatia usimamizi thabiti unaowekwa na Serikali. Pia kutokana na uanzishwaji wa masoko ya madini yapatayo 28 na vituo vidogo vya ununuzi wa madini 28, katika kipindi cha mwezi Machi, 2019 hadi Januari 2020, jumla ya kilogramu 9,237.34 za dhahabu; karati 12,973.14 za madini ya almasi; kilogramu 20,099.17 za madini ya bati na kilogramu 514,683.28 za madini ya vito mbalimbali ziliuzwa na kuipatia Serikali mapato ya shilingi bilioni 66.57 ambazo zimetokana na mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafaninikio ya sekta ya madini, Serikali inashauriwa kuchukua hatua za kuimarisha zaidi sekta hii muhimu ili kukabiliana na athari za za kiafya na kiuchumi kutokana na janga la mlipuko wa homa kali ya mapafu ijulikanayo kama Covid-19. Bei za madini yetu

zitayumba kwenye soko la ndani, lakini inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuwekeza kwenye madini hasa dhahabu ambayo ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza. Katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi, bei ya madini ya chuma na hata makaa ya mawe haiyumbi na Serikali inaweza kupata mapato mengi katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali kuchukua hatua za makusudi na kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa chuma (*Liganga Iron Ore*) ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe (*The Mchuchuma Coal Mining and Power Projects*). Mradi wa Liganga na Mchuchuma unatarajia uwekezaji wa US\$ bilioni tatu na kuzalisha ajira zaidi ya 30,000 na hii inaweza kuwa fursa nzuri katika hiki kipindi cha balaa la *corona virus* (*Covid-19 Pandemic*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium (*FeNb*) ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR*, kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapo kwetu. Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo inapatikana *Panda Hill*, Songwe Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium (*FeNb end product*) ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka (*quick wins*) ili kuhakikisha inakabiliiana na athari za kiuchumi kutokana na *corona virus crisis*. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa

wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000*. Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 (*US\$ 220 million*) ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 (*US\$ 22 million*) uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika (*Modern Manufacturing Plant and Smelter*). Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi (*skills transfer*) pia itakuwa itachangia huduma za kijamii (*corporate social investment in community*) na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Madini kama ifuatavyo; kwanza madini ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe Mchuchuma imekuwa ikizungumzwa katika bajeti zote za awamu zote za Serikali zilizopita na hii ya sasa. Eneo la makaa ya mawe la Mchuchuma ambalo linamilikiwa *NDC* ligawanywe na kupewa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini ili kutoa fursa kwa wananchi kujipatia kipato na kulipa kodi badala ya sasa linavyokaa bila kutumika.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Mchuchuma na Liganga bado haijawanufaisha Watanzania kwa sababu bado haijaanza na kumekuwa na majadiliano yasiyoisha kati ya Serikali na mwekezaji, Serikali ifikie tamati ya mazungumzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliotoa maeneo yao kupisha miradi hiyo kwani ni muda mrefu toka waachie maeneo yao. Wakati Serikali inaendelea na mazungumzo na mwekezaji iweke vivutio katika maeneo ya miradi hiyo ili uwekezaji ufanyike kwa urahisi. Mfano barabara, umeme, maji na kadhalika.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha bajeti hii na hatimaye kuiwasilisha kwa umakini na ubora wa hali ya juu. Mungu awape ushirikiano ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kutoka maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la mafunzo kwa wafanyakazi wa Wizara; kama tunavyojua kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu katika nchi yetu na ni Wizara mpya hivyo inahitaji watumishi wake kuwa na utaalum wa kuendesha Wizara hii. Aidha, Wizara hii ni moja kati ya Wizara inayoweza kuongeza pato la Taifa. Ushauri wangu katika Wizara hii kwa Serikali kuwekwa fungu maalum la kuweza kuwapatia elimu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha za miradi kwa wakati. Kumekuwa na ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na wakati mwingine kukosekana kabisa jambo ambalo linaleta uzoroteshaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika suala hili ni kuhimiza Serikali kuwapatia Wizara fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Spika, awali nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zipelekwe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa iweze kutekelezwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe elimu kwa wananchi ili waweze kutunza mazingira baada ya uchimbaji

madini, sababu mara nyingi baada ya uchimbaji wachimbaji huacha mashimo ambayo huathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itafute njia mbadala ili kuondokana na uchenjuaaji wa kutumia zebaki ambayo ina athari kwa binadamu na mazingira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali idahili wanafunzi wa kutosha katika vyuo vyetu kwenye taaluma hii ya madini ili tuweze kupata wahitimu wa kutosha wenye taaluma ya madini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa wale wachimbaji wadogo, Serikali itoe vifaa vya kutosha vya uokoaji pindi maafa ya kufukiwa na vifusi yakitokea ili iwe rahisi kufanya uokoaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naishauri Serikali itoe mikopo kwa wachimbaji wadogo yenye riba nafuu.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kuhusiana na hoja iliyoko mezani ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza kwanza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa *reforms* kubwa alizofanya katika Wizara ya Madini. Nimpongeze pia Waziri Mheshimiwa Biteko na Naibu wake Mheshimiwa Nyongo pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Madini kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuendelea kuboresha sekta ya madini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja iliyoko mezani kwa kumwuuliza Waziri swali moja ambalo nahitaji ufafanuzi na jambo la pili ni ushauri mdogo kuhusu haja ya kuweka alama (*beacons*) zinazoonekana juu ya ardhi ili kubainisha mipaka halisi ya vitalu vya wamiliki maeneo ya machimbo ya *ruby* ya Mundarara, Wilayani Longido.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia na swali; naomba kufahamu Serikali imefikia wapi katika suala la kumbainisha mmiliki halali wa sasa wa *Mundarara Ruby Mine* ulioko Wilayani Longido. Nauliza swali hili kwa sababu kuna utata kuhusu umiliki wa mgodi huo kwa muda mrefu sasa. Waziri aniambie mmiliki wake halali na mwenye leseni halali ni nani kwani manung'uniko yaliyoko ni kwamba leseni ya aliyewahi kukodishiwa mgodi huo na Serikali uliisha muda wake miaka mingi na mtu anayeendelea kuchimba kwenye mgodi huo hana leseni na amekuwa akiwaingilia wachimbaji wadogo walioko jirani na eneo hilo kwa kuwatoboza na kudai kuwa eneo lote ni lake.

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili ni ombi na ushauri kwamba Serikali iweke *beacons* za kubainisha mipaka halisi juu ya ardhi ili kutenganisha maeneo ama vitalu wanavyomiliki kihalali wachimbaji wadogo wanaopakana na *Mundarara Ruby Mine*. Hili litamaliza migogoro inayojitokeza mara kwa mara kutokana na kutobozana ambako wachimbaji wa *Mundarara Ruby Mine* huingilia vitalu vya wachimbaji wadogo na kuvuna madini katika maeneo ambayo si yao. Kwa mfano, *Sendeu Agrovet* ambayo ni kampuni changa ya wachimbaji wadogo ambao ni wazawa wa Mundarara wamekuwa wakiingiliwa na *Mundarara Ruby Mine* mara kwa mara kwa kuwatoboza na kung'ang'ania maeneo yasiyo yao.

Mheshimiwa Spika, suala hili la kuweka *beacons* ni kilio cha wachimbaji wadogo katika Migodi ya *Ruby* kule Mundarara na mimi ninaona moja ya sababu za kutobozana ni kwa vile hakuna *beacons* zinazoonesha mipaka bayana ya mwanzo na mwisho wa kila kitalu juu ya ardhi. Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee suala hili jibu atakapohitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi

Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John J. P. Magufuli kwa namna anavyosimamia kikamilifu kuhakikisha rasilimali madini nchini inalindwa na kusimamiwa ipasavyo. Wizi wa rasilimali madini umepungua kwa kiasi kikubwa kama sio kwisha kabisa, kwani uwepo wa rasilimali madini nchini sasa manufaa yake yanaonekana kwa uwazi na kwa faida kwa wote bila kujali mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuisimamia Wizara hii na kuhakikisha rasilimali hii inasimamiwa vyema kwa manufaa na ustawi wa nchi yetu. Pongezi pia ziwafikie watumishi wote katika Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa wanaouonesha katika kusimamia rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa hapo juu, naomba kuishauri Serikali kwa mambo yafuatayo ili kuboresha mambo mbalimbali yanayosimamiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, madini ya ujenzi; kumekuweko na mvutano usio wa lazima kati ya makandarasi wengi katika miradi mbalimbali katika Halmashauri zetu nchini juu ya malipo ya madini kwenye miradi ya Serikali. Jambo hili sio tu limekuwa likileta usumbufu bali pia limekuwa likichelewesha miradi na hatimaye mingine kufutwa na hazina kwa kuchelewa kuanza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine katika hili la madini ya ujenzi ni bei ya hayo madini, maafisa wengi hukadiria bei wao wenyewe, jambo linaloleta migogoro mingine kuchelewesha baadhi ya miradi. Je, Serikali haioni haja ya kusamehe kodi ya madini ya ujenzi hasa kwa miradi ya

barabara za vijijini na miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali ambayo hutumia nguvu za wananchi?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalopenda kushauri ni juu ya wachimbaji wadogo nchini, kwa kuwa walio wengi uwezo wao bado ni mdogo naishauri Serikali kuendelea kuwawezesha wachimbaji hawa wadogo ili kuwa na zana za kisasa ili waweze kuchimba kwa tija na kuongeza usalama wao wawapo migodini. Lakini pia elimu ya kutosha itolewe juu ya uwepo wa masoko ya madini katika maeneo mbalimbali katika Halmashauri zetu. Mfano Halmashauri ya Liwale bado hakuna soko la uhakika pamoja na kuwa na machimbo ya dhahabu na safaya katika vijiji vya Lilombe (Kitowelo), Naujombo, Ngumbu na Kipelele, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ziko kampuni zinazojishughulisha na utafiti na utafutaji wa madini nchini. Kampuni hizi zimekuwa zikifanya uharibifu mkubwa wa mazingira katika ardhi za vijiji vyetu bila ya kufanya urejeshaji wowote wa uharibifu huo. Moja ya makampuni hayo ni Kampuni ya Ngwena inayofanya kazi katika Vijiji vya Kipelele, Naujombo, Ngumbu na kadhalika, sio vijiji tu hata Halmashauri ya Liwale haijawahi kupata chochote kutokana na utafutaji huo. Pamoja na kwamba vibali hutolewa na Wizara, je, nini wajibu wa Serikali za vijiji katika kulinda ardhi ya vijiji na rasilimali hii ya madini. Kwani hali ilivyo sasa hakuna mwongozo ulio wazi kwa Serikali zetu za Vijiji juu kampuni za utafiti na utafutaji wa madini. Hii ni bora likaenda sambamba na mwongozo wa ulipaji wa fidia wa maeneo ya utafiti na utafutaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia kuipongeza Serikali kwa kuisimamia sekta ya madini na kuiwezesha sekta hii kuweza kuchangia pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa naomba Maafisa Madini wawepo kila kwenye Halmashauri zetu na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuunga hoja mkono na kuwapongeza

Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote kwa kazi nzuri waifanyayo.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza hususani Mheshimiwa Rais kwa kufanya mabadiliko muhimu katika sekta hii ya madini ambapo kwa sasa inaweza kuchangia ongezeko kubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la uanzwishaji wa masoko kwa kiwango kikubwa na vituo vya ununuzi wa madini ni suala la kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ambae amefika Jimboni kwangu Muheza sehemu ya Sakale, Amani ambapo aliongea na wananchi wa Amani na kuwahakikishia dhahabu ambayo imegundulika maeneo hayo utafanyika utaratibu ili kuona wanaweza kuchimba kwa namna gani ili isiingiliane na chanzo cha maji cha Mto Zigi, wataalam wa kutoka sekta zote muhimu walifika na wametoa taarifa yao.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ambalo limeamuliwa ni kupata mwekezaji mkubwa ambaye anaweza kuchimba kwenda chini. Nafurahi kusema kwamba tumeanza mchakato wa kumpata mwekezaji mwenye uwezo ambapo kwa sasa tunataka kujua kuna dhahabu kiasi gani. Tunachoomba ni ushirikiano wa Wizara hii na Wizara ya Mazingira ili tuweze kufanya kazi hiyo kwa ushirikiano mkubwa ili wananchi wa Muheza waweze kufaidika na madini yao.

Mheshimiwa Spika, tungependa kupongeza hatua za kujenga ukuta wa Mererani kwenye madini ya *Tanzanite* na hatua za ufungaji wa *CCTV camera*, cha msingi katika mapendekezo ya Tume uliyowahi kuiunda moja ya mapendekezo ilikuwa kufanya pia biashara hiyo kwa njia ya mnada. Ningependa kufahamu kama uuzwaji wa *Tanzanite* kwa njia ya mnada ulianza na kama umeliingizia faida Serikali kwa kiwango gani hata kama bei ya *Tanzanite* kwenye soko la dunia imeporomoka. Aidha, tungependa kufahamu ujenzi wa viwanda vya *smelting* umefikia kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Spika, mimi nianze na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa mnazozifanya kwa kuwaletea maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi ni Mjumbe wa Kamati, napongeza pia mashirikiano ya Kamati na Wizara, mchango wangu nianze na *GST*; bajeti wanayopata ni ndogo sana, tukumbuke kituo hiki ni cha utafiti na kwa kweli wakikifanya vizuri kitawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwaongezee bajeti ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi, pengine masoko ya madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa kazi nzuri ya uanzishwaji wa masoko ya madini. Niombe Serikali kwa yale masoko kama ya Dodoma basi tuyaboreshe ili yaendane na biashara yenyewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia.

SPIKA: Sasa tunaelekea upande wa Serikali lakini muda wenyewe haupo upande wetu, kwa hiyo tujitahidi kwa muda huo ambao tutakuwa nao. Mheshimiwa Dkt. Ashatu dakika tano na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika tano.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii muhimu ya kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Madini. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Doto pamoja na Mheshimiwa Nyongo kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na kaka yangu Profesa Msanjila kwa kazi njema wanayoitendea Taifa hili na wale wote wanaowasaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache ndani ya dakika hizi tano na niseme naunga mkono hoja hii. Tayari nimeshapiga kura yangu ya ndiyo tayari kwa utekelezaji wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kulisemea kidogo ni utozaji wa asilimia 18 ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ambayo imesemwa vizuri na Mheshimiwa Bulembo, lakini pia Kamati yetu ya Nishati na Madini wamesema vizuri. Uzuri Kamati ya Nishati imerudi kwenye sheria na ikaitaja Sheria ya Madini nini inasema. Naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba dhamira njema ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake mema kwa wachimbaji wetu wadogo, tulifanya marekebisho ya sheria hii Bunge la mwezi wa 11 mwaka jana kama sikosei ili kuhakikisha matatizo yaliyokuwepo kwa wachimbaji wetu wadogo yasiwepo tena na sheria ile ikarekebishwa. Tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, wakati sheria ile inarekebishwa haikuwagusa *dealers* na *brokers*, kwa hiyo kulaumu moja kwa moja Mamlaka ya Mapato kwamba inakiuka sheria, inakwenda *against* maelekezo ya Serikali, siyo sahihi hata kidogo. Mamlaka ya Mapato inatekeleza sheria na sisi kama Wizara kwa wale ndugu zangu kutoka Shinyanga waliokuwepo kwenye kikao cha wadau kilichoitishwa na Serikali, tulilisema mbele ya wadau wetu wa madini kwamba jambo hili tunalitambua kama Serikali. Kodi inakusanywa kufuata sheria na sasa tupo kwenye mchakato wa kurekebisha sheria mbalimbali ambazo zinahusu masuala ya kodi na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo yamewasilishwa na Wizara ya Madini ni jambo hili la asilimia 18. Kwa dhamira ileile njema naamini Bunge lako Tukufu litaturuhusu kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka huu tutakapoleta mbele ya Bunge lako Tukufu kufanya marekebisho haya ili kuondoa changamoto hii ambayo imeonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulisemea kidogo nalo ni jambo ambalo limesemwa na Mheshimiwa Bulembo pia kwamba kuna mlolongo mrefu na wewe kaka yangu ukaliwekea nguvu, mlolongo mrefu wa utoaji fedha.

Naomba pia nirejee kwenye sheria; Bunge letu Tukufu kwa kujua hatari ya fedha haramu ndani ya uchumi wetu, tatizo la utakatishaji wa fedha jambo hili pia linatekelezwa kisheria na anaulizwa tu maswali ya kawaida, akiweza kuyathibitisha maswali hayo anayoulizwa, pesa hizo kazitoa wapi, anakwenda kufanya nini, wala hazuiwi mteja wetu kutoa fedha zake kwenye taasisi zetu za kifedha. Kwa hiyo, pia ni sheria yetu inatuelekeza hivyo na inatekelezwa na taasisi zetu za kifedha kwa malengo mapana kabisa ambayo Bunge letu Tukufu iliona na tukatunga sheria hiyo ili kuhakikisha uchumi wetu unaendelea kuwa imara.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulisemea kidogo nalo ni hili la kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa madini yetu na hasa dhahabu imesemewa kwa nguvu kubwa lakini pia kuruhusu mabenki yetu waweze kununua madini yetu kwa ujumla. Jambo hili Serikali yetu pia inatambua nini maana ya jambo hili kwenye uchumi wa nchi...

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa malizia.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kusema tunakamilisha kuandaa kanuni kwa ajili ya kusimamia jambo hili, zitakapokamilika na tunazikimbiza kwa sababu tunajua changamoto tuliyonayo pamoja na janga la *corona*, lakini umuhimu pia wa madini yetu na usalama wa fedha za wananchi wetu zinapoingia katika biashara hii ya madini. Kanuni zipo katika hatua za mwisho na tukizikamilisha hatuna muda mrefu basi tutaweza kufanya yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wanaishauri Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana Naibu Waziri wa Fedha, nakushukuru kwa maelezo. Kwa jinsia alivyo-*present* Mheshimiwa Bulembo ni kwamba wanapochukua fedha benki kunakuwa na ukiritimba, mimi nilifikiri benki wangejuliza habari ya utakatishaji wanapopokea zile fedha umezitoa wapi, imekuwakuwaje na kadhalika lakini fedha umeipokea, akija mwenye hela ndo inaaza kuwa, hapo ndo kidogo inakuwa ina mashaka. Benki wajiridhishe na fedha wanazozipokea, wakisha-*clear*kila kitu anapokuja kuchukua hela zake ni hela zake, kuliko inapokuwa mtu anapotaka kuchukua chake ndo inakuwa tabu, inamfanya yule mtu ajifunze tu kwamba, kumbe hawa jamaa siku nyingine nisiwalettee hela zangu, dawa hela zangu nikalale nazo mchagoni na kila mahali ninapojua basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa AG nilishakutamka, una dakika tano pia, halafu atafuata Mheshimiwa Nyongo, Naibu Waziri; sijui wamegawanaje na Mheshimiwa Waziri lakini basi nitakupa dakika 15 Mheshimiwa Nyongo. Mheshimiwa AG.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa sababu ya ufinyu wa muda, nijielekeze moja kwa moja katika baadhi ya hoja za kisheria zilizotoka katika michango ya Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na mchango wa Mheshimiwa Heche aliyeeleza kwamba makampuni tofauti yanatumia sheria tofauti. Yako makampuni yanayotumia *Mining Act*, 2010 na yapo yanayotumia *Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty* 2017.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumfahamisha Mheshimiwa Heche kwamba nadhani hapo ni mkanganyiko tu, sheria hizi mbili zinatakiwa kutumika kwa makampuni yote; kama ni makampuni yanayoshughulika na madini, basi Sheria ya Madini ya 2010 itatumika. Pia sheria ya *Natural Wealth and Resources Permanent sovereignty* pamoja na ile nyingine nayo itatumika kwa sababu hii inahusu maliasili zote ikiwemo madini. Kwa hiyo, najua ni mkanganyiko na kwa sababu ya muda, lakini akihitaji ufafanuzi zaidi naweza kumpatia.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kumetokea maoni au pengine kushangaa kidogo na hii inahusu suala la kupeleka mashauri nje ya nchi na kwamba msimamo wa sheria ni mashauri hayo yasiende nje ya nchi lakini makubaliano ya Serikali na Barrick yanaonekana yamekiuka msimamo huo wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda nifafanue kwamba hilo siyo sahihi. Changamoto inatokana na kutafsiri hilo neno "nje". Kwa Kiswahili tunatumia neno "kupeleka mashauri nje ya nchi." Sheria inasemaje? Ukiisoma inasema: "*pursuant to article 27 (1) of the Constitution Permanent Sovereignty of Wealth and Resources shall be a subject of proceedings any foreign court or tribunal.*"

Mheshimiwa Spika, niliwahi kueleza hapa kwamba neno *foreign courts or tribunal* haijumuishi *international courts and tribunals* na hii ndiyo tafsiri sahihi kwa sababu hata tunapotumia neno *foreign law* hatumaanishi sheria ya Kimataifa. *Foreign laws* zote ni sheria za nchi fulani husika. Kwa hiyo, kilichokusudiwa hapa kwa maana inayosomeka hapa moja kwa moja ni kutopeleka masharti haya katika Mahakama au *tribunals* za nje ya nchi, lakini haikuzungumzia juu ya *international courts and tribunals*.

Mheshimiwa Spika, tulipofanya marekebisho kwenye sheria ya *arbitration* tuliiweka hiyo vizuri, kwa hiyo, inawezekana kwamba kwenye *arbitration* mashauri yanaweza kwenda katika *international courts and tribunals* lakini kuna mfumo wake ambao umetengenezwa na sheria yetu ya *arbitration*. Muda hautoshi, ningeweza kueleza zaidi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na pendekezo katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ni vema sasa nchi yetu ikawa na kitu kinaitwa *Country Mining Vision* na hiyo ijengwe juu ya misingi ya *African Mining Vision*. Kungekuwa na muda wa kutosha ningeweza kueleza juu ya hilo, lakini hapa itoshe tu kusema sisi Tanzania tume-*implement* vizuri zaidi na kwa vitendo ile *African Mining Vision*

kupitia zile sheria mbili za *Permanent Sovereignty of Natural Wealth Resources*.

Mheshimiwa Spika, hilo nalizungumza kwa hakika na kwa unyenyekevu mkubwa; nimekuwa *Senior Mineral Law Advisor* wa *UN Economic Commission of Africa* kupitia ile *African Mineral Development Centre*. Kazi yetu ilikuwa ni kujaribu ku-*implement African Mining Vision* katika *individual countries* za Afrika. Ni Tanzania peke yake ndiyo iliyochukua hatua zinazopongezwa na bara zima la Afrika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa ridhaa yako, kumekuwa na mjadala mkubwa sana kuhusu hili suala la wachimbaji wadogo, lakini tatizo lake hasa ni kwamba (na hiyo ilianza wakati wa mkoloni) tumewatengenezea mfumo wa uchimbaji, tunaoweka katika sheria rasmi za nchi, lakini wao nao wana mfumo wao *parallel* wa uchimbaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nchi nyingi Afrika imekuwa ni *debate*, tuwatengenezee mfumo wao, sheria yao au tuwa-*accommodate* kwenye hii sheria nyingine? Hili tumeshaliona hata kwetu na kazi imeshaanza ya kuona kama tunaweza kuwatengenezea mfumo wao tofauti na huu mfumo mwingine ambao ni rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi huo mzuri. Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 15 halafu Waziri mwenyewe dakika 25.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na kutulinda sisi sote na kuwa na afya njema mpaka tupo hapa leo tunafanya shughuli ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile nachukua fursa hii kukupa pole wewe kwa msiba huu uliojitokeza, wa mama yetu Mbunge wa Viti Maalum Mheshimiwa Getrude Lwakatare.

Vile vile natoa pole kwa ndugu na familia ya Mheshimiwa Akbar ambaye alikuwa ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Nishati na Madini, kwa msiba uliowakuta.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niendeleo kukushukuru tena wewe kwa ushirikiano uliotupatia katika Wizara yetu kwa namna ya ushauri na mapendekezo mbalimbali katika kuhakikisha kwamba tunasimamia Sekta yetu hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kutoa pongezi kwa Waziri wangu, Mheshimiwa Dotto Biteko kwa kazi tunavyoifanya kwa ushirikiano wa pamoja; kwa kweli niseme kabisa kwa moyo mweupe, Waziri wangu amekuwa ni mtu mwenye kutoa ushirikiano wa hali ya juu kuhakikisha kwamba tunaendelea kusimamia Sekta yetu ya Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Sekta hii ya Madini ni ngumu, ni sekta ambayo kwa kweli inagusa maslahi ya watu wengi hasa maslahi ya kifedha na ndiyo maana hata leo hapa katika Bunge hili kidogo tu umeweza kuona *temper* ya Wabunge ambao wanahusika katika masuala ya uchimbaji. Kwa hiyo, hili ni jambo la kawaida kabisa, sisi huko tumeshazoea sasa kuona jinsi gani watu jasho na mate yanavyotoka wakati wa mabishano ya masuala ya madini. Kwa kweli kuna matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, amekuwa akituongoza vizuri. Kwa kweli tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwanza kwa kuhakikisha kwamba anabadilisha Sheria ya Madini na kwa kweli imetuongoza vizuri sana katika kuhakikisha kwamba tunasimamia Sekta hii ya Madini na kuweza kutoa tija kwa wananchi na kuisaidia Serikali kwa maana ya kukusanya mapato na maduhuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, katika mabadiliko haya ya sheria kuna kipengele cha kuanzisha masoko, kwa kweli tumeona kwamba masoko tuliyoyaanzisha yalikuwa ni masoko maalum

kwa ajili ya wachimbaji wadogo; na kwa kweli yameonekana kuwa na tija kubwa. Kuna dhahabu, kuna almasi na Tanzanite nyingi ambayo hatukuwahi kuiona. Kwa kuanzisha masoko haya tumeweza kuona dhahabu nyingi na madini haya yakipita katika masoko haya.

Mheshimiwa Spika, tumekusanya fedha nyingi sana kupitia masoko haya ya madini. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, wasimamizi wote wa sekta hii, watumishi wote wa Wizara ya Madini, Tume ya Madini kwa ushirikiano waliouonyesha kuhakikisha kwamba tunasimamia maduhuli na kuweka mazingira mazuri katika masoko haya na kuhakikisha kwamba Serikali inaendelea kupata kile ambacho imekitarajia kukipata.

Mheshimiwa Spika, tumeona kabisa katika masoko haya vile vile kwa kushirikiana na leseni nyingine za wachimbaji wakubwa; kwa maana ya wachimbaji wakubwa na miradi mikubwa mikubwa, hata maduhuli ya Serikali yameongezeka.

Mheshimiwa Spika, wakati tumeingia katika Wizara hii mwaka 2017 nikiwa na Mheshimiwa Angellah Kairuki, tukaungana na Mheshimiwa Dotto Biteko, tulikuwa tunakusanya maduhuli ya shilingi bilioni 194 tu kwa mwaka, lakini mwaka uliofuata 2017/2018 tuliweza kuongeza mapato tukaenda hadi tukakusanya shilingi bilioni 250. Mwaka uliofuata tukawekewa *target* ya shilingi bilioni 310, tulikusanya zaidi ya shilingi bilioni 320. Mwaka uliofuata 2019/2020 tukawekewa *target* ya kukusanya shilingi bilioni zaidi ya 475, lakini tumekwenda mpaka sasa hivi tuko zaidi ya 105% ya mapato ambayo tulikuwa tunayasubiria tuyakusanye mpaka sasa hivi. Kwa maana hiyo, mpaka kufikia mwezi wa Sita *target* yetu ya shilingi bilioni 475 tutakuwa tumeitimiza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hiyo ni hatua kubwa sana. Sasa hivi katika mwaka huu wa fedha mwaka 2020/2021 ni kwamba tumepangiwa zaidi ya shilingi bilioni 530 na kitu tuendelee kukusanya. Nina hakika, tuendelee kuomba Mungu, kama tutaendelea kuwa katika Wizara hii kama

Mungu atatujaalia na tukarudi; na unajua tunakwenda kwenye uchaguzi; kama tutaendelea kusimamia sekta hii na ushirikiano tulionao pamoja na Tume ya Madini, tuna hakika kwamba tutaendelea kukusanya.

Mheshimiwa Spika, *target* yetu ikiwezekana ni kukusanya zaidi ya kiwango hicho. Siku tukifika kukusanya shilingi triloni moja kwa mwaka tutakuwa katika hali nzuri na pengine ule mpango wetu wa kutaka asilimia 10 ya pato la Taifa kutokana na Sekta hii ya Madini, kutoka sasa hivi ambapo ilikuwa chini ya 5% basi tutaweza kufika hizo 10%.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge na hata kwa wachimbaji wadogo. Ni kwamba kama inavyosema Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tuwarasimisha na tuwatambue. Tumefanya kazi hiyo na kwa kweli tumewarasimisha, tumewatambua na wachimbaji wadogo sasa hivi kulinganisha na miaka ya nyuma wanaonekana kabisa wanafanya kazi yao kwa raha mustarehe, wanachimba na maeneo tumewapa. Mbunge anayelalamika kwamba hatujawahi kuwapa maeneo wachimbaji wadogo, nadhani labda hajui nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nikueleze kabisa kwamba maeneo yote ambayo tumefuta leseni kubwa; leseni za utafiti na zile leseni ambazo zilikuwa hazifanyiwi kazi, zaidi ya leseni 5,000 na kitu tumezifuta na tumewapa wachimbaji wadogo. Waheshimiwa Wabunge wengi wanaotoka maeneo ya wachimbaji wadogo hili wameliona na wanashukuru kwa hilo. Taharuki iliyotokea hapa leo, ni taharuki ya kugombania mali, siyo kutafuta maeneo ya kuchimba.

Mheshimiwa Spika, vile vile niendeleo kuzungumzia kuhusiana na hili ambalo limejitokeza hapa kabla sijaongea na mengine. Labda nichukue nafasi hii nitoe ufafanuzi. Maeneo mengi tuliweza kuwapa wachimbaji wadogo lakini katika maeneo haya kuna sehemu ambazo tumewarasimisha kwa kuwapa leseni ambayo ni *primary mining licence*. Pia wapo wachimbaji wengine walikuwa wanakwenda maeneo

ya *rush*, yaani maeneo ambayo sisi kule Kisukuma tunaita maeneo ya *kuhila*, maeneo ambayo hayana leseni, ama maeneo ya mlipuko wa uchimbaji. Watu wanapokwenda kuchimba maeneo hayo kuna utaratibu wake. Utaratibu huo, Mheshimiwa AG amezungumza hapa kwamba wao wenyewe wanaelewana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019 mwezi wa Kumi tuliweza kutoa waraka kwenda kwa Maafisa Madini wote wa Mikoa na tulitoa waraka huo kwa madhumuni maalum. Dhumuni kuu ilikuwa ni kutoa mwongozo kwa Maafisa Madini wa Kazi (*RMOs*) na watumishi wengine kuhusu kusimamia au kudhibiti shughuli za uchimbaji madini hasa mapato ya Serikali kwenye maeneo yenye mlipuko wa madini (*rush*). Aidha, malengo mengine ni pamoja na kuboresha usimamizi wa mazingira, afya na usalama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyokuwa, kwanza kulikuwa kuna mwingiliano wa majukumu kati ya taasisi mbalimbali za Serikali katika kusimamia maeneo hayo; pili, mahusiano ya siri kati ya baadhi ya viongozi wa Serikali na wachimbaji wa madini wakiwemo wanasiasa wa maeneo hayo; vile vile baadhi ya Maafisa wa Serikali walikuwa wanawatetea wachimbaji wa madini wanaohusika na ukwepaji wa kodi hasa wanapokuwa na maslahi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya viongozi wengine wasiokuwa waaminifu walikuwa wanashiriki na wachimbaji ambao wanawajua wao kwa maana ya kupata migao. Vile vile Maafisa Madini walikuwa wanachelewa kufika katika maeneo yenye mlipuko wa *rush* wa madini kwa wakati. Kwa hiyo, unatokea mlipuko wa uchimbaji, Maafisa wa Madini wanachelewa kufika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwepo na baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wasio waaminifu ambao hushiriki kwenye utoroshwaji wa madini kwa lengo la kukwepa kodi. Vile vile wanyabiashara wenye uwezo wa kifedha wamekuwa wanafadhili wachimbaji wadogo kwa makubaliano ya kuuziwa dhahabu itakayozalishwa na

mwisho baadhi ya wachimbaji kudharau kwa makusudi mamlaka ya Serikali zinazosimamia Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona hilo, sisi tulitoa waraka mwezi wa Kumi mwaka 2019 na waraka huo unasema:-

Kwanza katika eneo lolote utakapotokea mlipuko wa madini (*rush*) utaundwa uongozi wa kufuatilia na kusimamia usimamizi wa eneo hilo. Uongozi huo utajumuisha wafuatao: Afisa kutoka Ofisi ya Madini ambaye atakuwa ni Mwenyekiti; Afisa kutoka Ofisi ya Usalama ya Wilaya (*GSO*) ambaye yeye atakuwa Katibu na Wajumbe ni kutoka TAKUKURU, *OCD*, Chama cha Wachimbaji Wadogo na Halmashauri husika ya eneo lile.

pili, uongozi utakaoundwa hapo juu, utateua Kamati ya Usimamizi wa *Rush* hiyo ili kusimamia masuala ya usalama, mazingira uhibititi wa mapato ya Serikali na Kamati hiyo itajumuisha Mwenyekiti wa Wachimbaji mzoefu hasa katika usimamizi wa maeneo ya aina hiyo ambaye hana historia ya wizi wa fedha wa Serikali na uaminifu na Mweka Hazina na Wawakilishi ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji, Mjumbe wa REMA, Mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wachimbaji Wanawake na mwakilishi wa eneo (mwenye shamba).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa dada yangu Salome alikuwa akizungumza hapa kuhusiana na *rush* ya Na. 9 ambayo iko Bulyanhulu; na yenyewe tunaiweka katika kundi hili kwa sababu *rush* hiyo ni eneo la leseni kubwa ya Bulyanhulu na wachimbaji wadogo walivamia lile eneo. Wakati wamevamia lile eneo, sisi kwa shingo upande kama Wizara tuli-*hold* tukaona kwamba hawa watu wamevamia na ni wengi, kuwaondoa kwa haraka usalama utakuwa ni mdogo. Tukatumia utaratibu huu tuliouweka kuhakikisha kwamba tunasimamia yale yote ambayo yako katika waraka huu kwa maana ya mazingira, mapato ya Serikali na kuhakikisha usalama katika uchimbaji huu.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Wabunge wote, naomba nitoe *breakdown* ya mgawanyo kwa asilimia kwa kila namna wanavyochimba. Wanapochimba tunatambua madini ni mali ya Serikali, hata kama wewe una ardhi hapa, madini ni mali ya wananchi wa Tanzania. Ili uchimbe lazima tukupe leseni; na leseni inatolewa na Wizara ya Madini. Kama hakuna leseni hapo, usimamizi huu na waraka tuliutoa ndiyo utakaochukua nafasi kwa maana ya kusimamia namna ya uchimbaji ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia ziko kama ifuatavyo: ukishavuna madini hayo, kabla hujatoa gharama yoyote, unachotakiwa kwanza kukitoa ni mrabaha wa 6%. Cha pili unachotakiwa kukitoa ni 1%, yaani *clearance fee* na cha tatu, unatakiwa utoe *Service Levy* ambayo ni 0.3%. Ukishatoa hayo, sasa wewe kile kinachobaki unaunda kuwa ni asilimia 100. Asilimia 15 kinapewa kikundi cha usimamizi, asilimia 15 anapewa mwenye shamba na asilimia 70 inayobaki anapewa aliyewekeza, aliyechimba aliyeingia gharama ya kuchimba, yaani mmiliki wa duara. Kwa hiyo, kama haya yanatokea kinyume na haya ninayoyazungumza. *that is a special case*, naomba iletwe na tuisimamie. Kwa hiyo, haya ninayozungumza ndiyo ya kweli na mtu asipotoshe ukweli huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuzungumza kwamba kuna katika Sekta hii ya madini niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais, haya yote ameturuhusu na tunayafanya na kwa kweli ametusaidia sana. Katika mabadiliko haya ya Sheria ya Madini kuna kipengele ambacho kinazungumzia masuala ya *local content*. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeeleza kabisa kwamba Sekta ya Madini ni lazima tuifunganishe na sekta nyingine. Kwa kipengele cha *local content* Watanzania wengi sasa hivi wanafanya biashara na migodi mbalimbali.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Malizia Mheshimiwa dakika mbili.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, migodi hiyo inawapa fursa Watanzania kufanya biashara katika migodi hiyo na kuhakikisha kwamba Watanzania wananeemeka katika uwekezaji wa Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na Kamati ya Nishati na Madini kwa jinsi wanavyotushauri na kutupa maoni mbalimbali na jinsi tunavyoweza kusimamia Sekta hii ya Madini.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niwapongeze zaidi wapiga kura wangu wa Maswa Mashariki kwa imani waliyonipa ya miaka hii mitano na kazi kubwa niliyoifanya na nikuhakikishie wanasema na wazee wa Maswa wanasema kwamba hata mwaka 2020 wataendelea kuniadini na nitarudi katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada yakusema hayo ninakushukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Nyongo Naibu Waziri Madini sasa nimuuite mtoa hoja Mheshimiwa Doto Biteko najua hoja ni nyingi mno lakini jitahidi hizo dakika 25 utakazoweza ndio hizo hizo zingine tutapata kwa maandishi. Mheshimiwa tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza naomba kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama tena mbele yako, ili kuweza kuitimisha hoja hii. Lakini vilevile naomba kukushukuru sana wewe kwa namna ambavyo unatuongoza kwenye Bunge hili, na kwa kweli unarahisisha sana kazi ya mtoa hoja kuchukua maoni ya Wabunge kwa sababu unatutengenezea utulivu mkubwa hapa Bungeni. Naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyonipatia ya kuhudumu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tulivyorekebisha Sheria ya Madini mwaka 2017 sheria ile ilisema kwamba madini yote ya Tanzania ni mali ya watazani na yataweka chini ya uangalizi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli msimamizi mkuu wa sekta ya madini ungeniuliza ningesema ni Mheshimiwa Rais mwenyewe, kwa sababu amekuwa akitoa miongozo mingi sana ya namna ya uboresha sekta hii. Na kwa kweli mafanikio yote ambayo yataajwa na mtu yoyote hapa na nje ya Bunge mtu anayestahili kuchukua *credit* katika ni Mheshimiwa Rais. Tunamshukuru sana na tunampongeza sana kwa uthubutu wake wa kuweza kusimamia madini ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nimpongeze Makamu wa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa miongozo yake anayotupatia kila wakati sisi Wizara ya Madini, na kwa kweli hatujawahi kutindikiwa kila wakati kukiwa na jambo tunapata maelekezo kutoka kwake. Kwa namna ya pekee nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa Kasim Majaliwa. Yeye amekuwa kiongozi wetu wa kila siku tunapokuwa tunatekeleza majukumu yetu pale wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wengi sana wanakwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakiwa na shida na matatizo mbalimbali, wanapokelewa kwa mikono miwili wanasilikizwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu anatupa maelekezo yakufanyia kazi kila wakati. Niseme tu kama walivyosema wengine Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi wa mfano kwa namna ambavyo angependa kuona matokeo na siyo *story*. Nasema kuona matokeo na siyo *story* Mheshimiwa Waziri Mkuu akikuletea hoja, anataka kujua kuna fanyika nini na lini na siyo mchakato ukoje. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye amekuwa *champion* wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata uanzishwaji wa masoko, soko la kwanza yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu alinyanyuka hapa alienda kulifungua soko la kwanza Geita Machi, 17. Na akiwa pale alitoa maelekezo ya ufunguaji wa

masoko nchi nzima, na Mheshimiwa Rais baadaye akiwa Chunya akatoa *deadline*. Nataka nimdhibitishie Mheshimiwa Waziri Mkuu sisi wasaidizi wake tutaendelea kufanyia kazi maelekezo yake, na bila shaka tunataka kuitoa sekta hii kwenda mahali ilipo kwenda mahali fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa kamati niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote. Kwenye Bunge hili sisi Wabunge wapya tulioingia kwa mara ya kwanza tutakuwa mashahidi, tumewakuta Wabunge wa muda mrefu mmetupokea vizuri sana mmetulea sana na wakati mwingine huweze kuchora mstari kati ya Mbunge aliyeingia kwa Awamu ya Kwanza na Mbunge aliyemo miaka mingi. Mmetufanya kuwa ndugu, mmetufundisha na tabia na nidhamu ya Kibunge wengi tumejifunza kutoka hapa chini ya uongozi wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni bajeti ya mwisho nawiwa kuwa na deni kubwa na deni kubwa la kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao tunakutana Bungeni, ambao tunakutana kwenye *corridor*. Kama kuna jambo tunauliza tunaelimishana, naomba kwa moyo wa dhati mpokee shukrani zangu na wenzangu wizarani kwamba tumekuwa na oksijeni ya kutosha pale wizarani pale mnapokuja kutupa miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo Naibu Waziri Madini. Mheshimiwa Nyongo ananipa ushirikiano mkubwa sana, kama unavyofahamu yeye alitangulia wizarani alikuwa na uzoefu wa kutosha na tajiriba, amekuwa pamoja na kwamba Naibu wangu amekuwa mwalimu wangu wa kunifundisha na nimejifunza kwa haraka kutoka kwake yeye amesema hapa anajifunza kwangu. Lakini naomba nikiri kwamba kwa uzoefu wake aliyokuwa ameupata nimejifunza mengi kutoka kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Madini chini ya Prof. Simon Msanjila Katibu Mkuu,

watendaji wote walioko kwenye taasisi mbalimbali. Naomba nikiri kama kuna mtu amezungukwa na watu wenye weredi na uzoefu mkubwa ni mmojawapo. Nina wazee ambao wametumikia nchi hii kwa miaka 40 wana uzoefu mkubwa nami nimechukua muda mwingi ku-*take potential* kutoka kwao kujifunza ili tuweze kuendesha wizara hii nakupata matokeo makubwa.

Kwa niaba yangu mwenyewe na kwa naiba ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nimshukuru sana watendaji wetu wote wa Wizara ya Madini, Maafisa madini wa mikoa pamoja na watendaji wa taasisi zote na wenyeviti wa bodi kwa ushirikiano wanaotupatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa zimezungumzwa hoja mbalimbali na naomba nieleze mwanzo kabisa, nikiri kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge yote ukiingalia kwa ujumla wake ina nia ya kujenga sekta ya madini iweze kukua. Siamini kama kuna Mbunge anasimama hapa ku-*challenge* kwa ku-*challenge* tu, ana *challenge* kusudi ili tubadilishe mahali fulani ambapo hatuendi vizuri ili tuboreshe vizuri zaidi. Na hiyo ndiyo sprit ninayoina kwa wabunge wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii Waheshimiwa Wabunge kuwahakikishieni michango yenu mliyoitoa hapa hakuna mchango hata mmoja tutakaoupuuza. Hata kama upo mchango kwa kweli ukweli wake upo *diluted* kwa kiwango fulani tunaichukua kama changamoto. Na mimi ni mtu muumini ninayeamini hata saa mbovu kuna wakati inasema ukweli kwa siku. Inawezekana katika hayo yanasemwa na mengine yanayozuliwa inawezekana kuna kitu cha kuchifunza kwanini mtu aweze kuzua jambo inawezekana kuna mahali fulani tutajifunza.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie sisi tutayafanyia kazi yote kama yalivyo lakini tuombe watukubalie Waheshimiwa Wabunge kwamba yapo mambo mengine ambayo tukiyazungumza huku ndani yakienda nje yataonekana ni hali halisi kumbe siyo hali halisi na haya

tutayafafanua kwa ufupi ili tuweze kuzungumza hali halisi ilivyo na Waheshimiwa Wabunge waweze kuelewa kwa kupitia wao wananchi wajue hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na hoja ya kwanza iliyoelezwa hapa na Mheshimiwa Bukwimba. Hoja ya kituo cha mfano kule Rwamgasa kitaanza kufanya kazi lini?

Kwanza naomba nieleze kwamba Mheshimiwa Bukwimba katika Wabunge wanaofuatilia masuala ya madini hapa Bungeni pamoja na Ofisi Wizarani yeye amekuwa mstari wa mbele sana. Maafisa wangu pale Wizarani kuna eneo fulani *Bacliff*, kuna eneo fulani linatwa Buziba. Mheshimiwa Bukwimba akija wataanza kutaniana maafisa kwamba yule Mama wa *Bacliff* amekuja. Na kwa kufanya hivyo lile eneo la *Bacliff* tayari kuna wachimbaji wadogo kwa mkono wa Mheshimiwa Bukwimba yeye mwenyewe amekua akisukuma kwa nguvu zote. Naomba nikupongeza sana Mheshimiwa Bukwimba na nadhani kwa sauti hii wananchi wa Busanda wananisikia, mama huyu amefanya kazi kubwa na kwa kweli kama kuna zawadi wanaweza kumpatia wampatie kwa kazi aliyofanya nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari ya umeme Wizara ya Nishati tunaishukuru sana sisi tunapokea maombi ya wachimbaji ambao wanahitaji maeneo wenye maeneo wanahitaji umeme. Nikiri Wizara ya Nishati imekuwa nyepesi sana kuwahudumia wachimbaji wadogo tulipeleka maeneo 27 ambayo yaliletwa kupitia Wabunge, tukayapeleka kwa Mheshimiwa Kalemani na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu. Naomba kuripoti kwenye Bunge lako kwamba maeneo yote ambayo tuliyaombea yapatiwe umeme Mheshimiwa Kalemani kazi hiyo alishaifanya yameshapewa umeme yote. Kama yapo maeneo mengine ambayo yanahitaji kupatiwa umeme tunaomba wayalete kama wanaweza kuyapeleka wao moja kwa moja sisi hatuna tatizo. Lakini nataka niwahakikishie kwamba serikali kupitia Wizara ya Nishati imekuwa ikafanya hiyo kazi kwa *speed* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine alilozungumza hapa Mheshimiwa Musukuma ni *STAMICO* ianze kununua dhahabu. Naomba nitoe taarifa kwamba *STAMICO* imeomba leseni mbili za kununua dhahabu hapa nchini na tunataka *STAMICO* waingie sasa kwenye biashara. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge Shirika letu la *STAMICO* lilikuwa na matatizo makubwa. Matatizo hayo yalikuwa matatizo ya kimuundo na matatizo ya kiusimamazi. Wizara tumerekebisha hizo kasoro kama mmeangalia kwenye taarifa yetu tulikuwa na shirika ambalo muda wote limekuwa linatengeza hasara. Tumechora huo mstari sasa hivi hatutengenezi hasara, mmeona wenyewe tumzalisha fedha zaidi ya shilingi bilioni 30 tumelipa mraba zaidi ya shilingi bilioni mbili hatujachukua hata shilingi moja toka hazina kwa sababu tunajua fedha ni kidogo zinahitajika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali tunalojuliza kama mchimbaji mdogo ambaye hajasoma hata *degree* hana, akipewa leseni moja anazalisha dhahabu na analipa kodi hivi iweje *STAMICO* shirika lenye *degree* nyingi, ambalo lina maeneo mengi yenye dhahabu nyingi lenyewe eti lipewe fedha na Serikali kwa ajili ya kujiendesha. Tukasema hapana ninyi mngeuza hizo *asset* mlizonazo ziwe mataji, huo mtaji muabadilishe muwekeze, mkisha kuwekeza mlipe kodi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, leo ninavyozungu hakuna hasara inayotengezwa na shirika la *STAMICO* ni bahati mbaya kuna maelekezomengine ambayo tunazunguza kwenye kamati tunayasahau. Imezungumza hoja ya kurekebisha muundo, muundo wa shirika tulishabadilisha saa nyingi na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili ni mjumbe wa kamati, anajua muundo tulishaurekebisha na tuliuleta kwenye kamati na yeye akiwemo aliona mabadiliko tuliyoyafanya tumepunguza idadi ya Kurugenzi tulizokuwanazo zimekuwa chache kwa nia ya kupunguza gharama za uendeshaji, tumepunguza gharama za undeshaji leo tunaona faida. *STAMIGOLD* ilikuwa inatengeneza madeni kila mwezi leo *STAMIGOLD* haitengenezi deni hata moja inalipa madeni tuliyoyarithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie shirika la *STAMICO* lina hali nzuri sana, mwaka jana tulitoa mchango kwa Serikali kwa mara ya kwanza, toka limeanzishwa mwaka 75 na mwaka huu kama nilivyoeleza kwenye taarifa yangu tunapeleka tena machango wa bilioni moja na milioni mia moja kuonyesha tu kwamba hili shirika sasa limepiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msukuma namshukuru sana kwa mchango wake, ameeleza vizuri kwamba sasa hivi dhahabu kule wanunuzi hakuna, na hii *scenario* ipo hivi. Baada ya corona kutokea bei ya dhahabu duniani imepanda, lakini wanunuzi wa ndani fedha waliyokuwa nayo imekwisha. Kwa sababu wanunuzi tulionao wananunua wanakwenda kuuza nje wanapata fedha wanakuja kununa tena. Sasa katika wizara hamuwezi kukaa hapo mkulalamika mkasema corona, corona lazima muangalie mu-*unlock* wapi ili mzunguko uweze kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza tuliyoifanya masharti ya leseni ya *dealer ship* yamewekwa kwa kanda tumeondoa sharti hilo mfanyabiashara yoyote mwenye fedha, aje aende akanunue mahali popote na kutumia kwa kutumia nafasi hii liyopewa hapa naomba nitoe tangazo kwa wanunuzi wote wa madini nchini, ule utaratibu wa kununua kwa kanda tunauvuka, mfanyabiashara yoyote aende kwenye soko lolote mahali popote na fedha yake anunue dhahabu ataruhusiwa na kupewa *permit* zote zinazohitajika bila kujali mpaka wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili hapa tumeshazungumza na benki, na benki wamekubali kuweza kuungana na wanunuzi wa madini, mnunuzi atapewa fedha na benki, atachukua dhahabu zake atapeleka mahali ambapo benki watakubaliana, benki itabaki na *certificate* yakuonyesha hii ni dhahabu kiasi gani yenye *purity* kiasi yenye thamani kiasi gani imelipiwa mraba na baadaye siku tukipata fursa balaa hili likapitwa watu waka *export* mtu yule anapewa dhahabu

yake ana-*export* fedha ya benki anarudisha na yeye anakwenda.

Mheshimiwa Spika, majadiliano haya wananunuzi wenyewe tumeshazumza nao tumeshachukua hatua hizo. Tunaomba tupewe nafasi, hili jambo twende nalo taratibu. Kwa sababu hili jambo pia lina-*involves risk* mbalimbali. Benki zimekuja na maandiko waneleza *risk* ambazo zipo na sisi tunaelewa. Kwa sababu huku nyuma historia iliwahi kutokea, watu walinunua dhahabu baada ya muda unakwenda kuangalia dhahabu unakuta ni kakumba hakuna dhababu. Benki hizi lazima zijiridhishe na zenyewe fedha hizi ni za *shareholders* zisipotee, kwa hiyo tunalifanyika kazi hilo jambo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la tatu utaratibu wa mtu kupewa leseni ya dira ungeweza kuchukua muda mrefu kwa sababu moja awe na *bank statement* ya kiasi gani cha fedha, mbili lazima awe na ofisi iliyokaguliwa tumeiona ofisi yake hii hapa, tatu awe na mashine za kukata madini kama ni *dealership license* lazima awe na mashine 30. Masharti hayo tunayalegeza kwa sababu ya hali halisi tuliyonayo. Mtu yoyote mwenye mtaji anayetaka kununua madini aende akanunue ili mradi atalipa mraba na pale atakapotunza Serikali itakuwa inachua ametunza wapi.

Mheshimiwa Spika, siku tuki-*unlock* mpika hii baada ya janga hili kuisha basi kuakuwa na *smooth transition* ya watu kusafirisha madini.

Naomba nikuhakikishie tunalichukua kwa uzito wake tunaelewa wachimbaji wetu wanakutana na hali ngumu. Wametokea watu madalali huku, wanapunguza bei dhahabu kwa nguvu wanawalazimisha wachimbaji wetu maskini wanahitaji fedha wengine ni *substance* anahitaji achimbe leo apate shilingi laki moja akale yeye na mtoto wake, ukimwambia subiri tunasubiri michakato uvumilivu huo hawana, fedha yoyote itakayokuja mbele yake anachukua. Mtu wa kumbana hapa ni huyu anayenunua asiwaibie wengine kwa kigezo cha corona.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa kweli hata ile *margin* ya kushindana tulikuwa tunapunguza asilimia kumi tumeshusha hadi asilimia kumi na mbili. *Margin* ya kushinda kwa wafanyabiasha iwe kubwa ziadi ili watu weweze kuvutia kuanza kununua.

Mheshimiwa Spika, nina watu wamenipigia simu wanalamimika hatuna fedha, nimezungumza na wafanyabiashara wengine ambao hawamo kwenye sekta ya madini wana viwanda wana biashara nyingine kuwashawishi waweze kupeleka fedha wakanunue na wengine wamepeleka Chunya, mfanyabishara mmoja alipeleka na ninamshukuru sana siwezi kumtaja hapa. Dola mia mbili zimezunguka chunya zime-*offset* ile *frustration* iliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakishie tunalichukua kwa uzito wake nia yetu nguvu wanayoitumia wachimbaji wadogo hapa nchi isipotee bure. Kwa sababu ikipotea bure kwa kipindi hiki wao watakuwa wamepata hasara zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala jingine limezungumzwa na Mheshimiwa Heche, suala la fidia, naomba nieleze tu suala hili la fidia lina historia ndefu. Ukilizungumza suala la fidia, ukaishia kusema fidia bila kuzungumza historia yake mtu yoyote anayesikiliza anaweza kuamini Serikali haichukui hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili lina historia, historia yenyewe ni kwamba huko nyuma tulipotoka watu walikwenda kufanya biashara kwenye fidia, unakuta eneo la *square* mita 100, lina miche ya migomba 1000 haiwezekani hesabu ya kawaida haikubali. Baadaye Accacia ameondoka, alivyoondoka tulikuwa tumefika mhali fulani amekuja Barrick, Barrick kwa sababu serikali tumo ndani tumelisukuma kwa *speed* kubwa. Na *signature* ya kwanza ya Barick na serikali imefanyika mwezi wa kwanza. Nina barua hapa, barua ambayo Barick wameniletea wakionyesha *commitment* ya kulipa.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie *Chief Valuer*, na nichukue nafasi hii nimshukuru Waziri wa Ardhi pamoja na *Chief Valuer* tumepelekwa timu wakati wote kwenda kule kuhakikishi kwamba wananchi wa Tarime wanalipwa fidia yao na hili hatufanyi siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Heche nataka nikuhakikishie kwamba wananchi watalipwa, wananchi watalipwa wanaostahili sio waliotegesha. Waliotegesha tulikuwa mimi na wewe tukawaambia hakuna mtu atalipwa shilingi moja chini ya uongozi wetu na wewe tunakubaliana. Lakini haya mambo mkianza kuingiza kuna siasa mna-*frustrate* wananchi *unnecessary* taratibu zipo lazima tuzifuate na tukishakuzifuata wananchi watapata haki yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie mgodi ule serikali ina hisa, hakuna mtanzania hata mmoja atadhurumiwa shilingi moja, awe hai awe amekufa madhari familia yake ipo haki yake ataipata. Sitaki nikueleza lini nataka nikwambie kabla Bunge hili halijaisha fidia hizi zitakuwa zimeanza zimelipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tuliweke sawa, mdogo wangu Mheshimiwa Heche amezungumza hapa na nimefurahi Mheshimiwa Heche amezungumza hapa hotuba aliyoisoma Msomaji wa Kambi ya Upinzania alijua ina ulakini hakuisoma yeye, akampa mtu mwingine na alijua kwa sababu mambo mengi anayajua amezungumza hapa kwamba Wizara ya Madini inaongozwa kwa sheria mbili si kweli. *Literally* sio mwanasheria tuna sheria moja ya madini ya mwaka 2010, yenye marekebisho ya mwaka 2017 tuliyofanya hapa tulirekebisha baadhi ya vipengere hiyo hai-*qualify* kuifanya marekebisho hayo kuwa sheria kamili na ndiyo maana tunalifaa kama sheria madini ya mwaka 2010. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa marekebisho tulikouja kuyafanya kwenye sheria ile, unapokuwa unatekeleza utakuana na ugumu mahali fulani sisi ni binadamu tunatengeneza sheria kwa ajili yetu sio sisi kwa ajili ya sheria.

Tukiona kuna shida tunarekebisha kwa hiyo, hizi sheria sio msaafu, wakati wa kutekeleza ukigundua hapa kuna shida unarudi kuwaomba waliotunga sheria turekebishe hapa biashara iende. Ndio maana unaona kuna sheria mbalimbali zinapitishwa hapa kurekebihshwa. Siyo dhambi ni *actually* ndiyo uungwana wenyewe, usikomae na jambo ambalo *practically* haliwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uungwana nikugundua kwamba hili jambo hatuliwezi, turudi kwa waliotengeneza sheria tuwaombe na hiyo ndiyo *spirit* ya Mheshimiwa Rais wetu. Anakwambia kabisa, kama mmeaona haliwezekani pelekeni kwa Wabunge lirekebishwe na tumefanya marekebisho. Leo umesikia hapa, VAT tumelifanyia marekebisho tukaondoa VAT, tukaondoa *withholding tax* kwenye chumvi tuliondoa kodi zaidi ya 13 tuliziondoa kwa sheria hapa hapa zilikuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo Waziri wa Fedha ametuambia hapa kwenye *Finance Bill* inayokuja na hayo tutaya-*take on board*. Sasa tusichukue muda mrefu kulaumiana tunawachanganya wachimbaji, uchimbaji ni *capital intensive, labour intensive and time intensive*. Ukivizungumza hapa tu kwa sababu umeamua kuzungumza kwa kweli unawavunja moyo wachimbaji. Mdogo wangu Mheshimiwa Heche hebu twende tuwahudumie wachimbaji wadogo. Mimi namshukuru sana Mheshimiwa Mbowe kukuteua kuwa Msemaji wa Upinzani kwenye Wizara hii. Imani yangu ni kwamba utawatendea haki Watanzania kwa kuwaeleza ukweli kwenye sekta ya madini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi tunahitaji kuyafanya, namba zitungumze, mimi nataka nisimame hapa tuzungumze namba, tulikuwa wapi, tuko wapi, tumefika wapi. Tulikuwa kwenye eneo ambapo wachimbaji walikuwa wanafukuzwa kama manamba kwenye nchi yao, wanapigwa mabomu wanaondolewa ili mgeni aje achimbe. Tumehama kwenye *line* hiyo leo wachimbaji wanapewa maeneo, zaidi ya leseni mia tano na kitu tumewapatia wachimbaji wadogo. Tumetoka kwenye ukusanyaji wa

mapato kwa mwaka mzima Mererani shilingi milioni 166 leo tunakusanya shilingi bilioni 2.9. Mkoa wa Geita mmoja tuliokuwa tunafanya biashara ya dhahabu ya shilingi milioni 20 kwa mwaka mzima leo tunafanya biashara ya shilingi bilioni 239. Tumetoka kwenye kukusanya kwa mwaka mzima kilo za dhahabu zisizofika 500 leo tunakusanya tani tatu kwa mwaka mzima. Sasa namba hizi zikizungumza dhambi iko wapi, kwa nini tuanze kulaumiana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie, maelezo mazuri ameyaeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa habari ya *rush*. Mtu yeyote ambaye amekulia kwenye uchimbaji mdogo, wachimbaji wadogo toka miaka ya nyuma wakati wa Chonjo, AG anajua vizuri, wachimbaji walikuwa na mfumo wa kusimamiana na sisi tumekwenda na *spirit* ileile ya kuwaambia wachimbaji wadogo *regulate yourself or perish*. Ukitaka ku-*impose laws* kwa wachimbaji wadogo utachukua muda mwingi wa kukamatana na watu, jambo hilo hatulitaki Wizara ya Madini. Wana vyamba vyao vya uchimbaji mdogo, tumevitambua na wao wenyewe wanapokwenda kuunda uongozi kwenye *rush* sisi kazi yetu ni kuwasaidia kuunda huo umoja, Wizara haiundi msimamizi wa *rush*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maige ni shahidi amezungumza hapa, leo tunagombana kwa sababu ya mgawanyo wa asilimia hatugombani kwa sababu ya watu kuibiwa. Hiyo hatua zamani ilikuwepo watu wanachimba wanaibiwa, leo tunagombana msimamizi anapata asilimia nyingi lakini twende kwa msimamizi hiyo asilimia 15 ya mawe anayoyapata anafanyia nini? Msimamizi huyo wakati akipata hizo fedha ndiyo anawajibika kuweka miundombinu ya vyoo kwenye machimbo pale, msimamizi huyo akitokea mtu amefariki yeye ndiyo anawajibika kumtibia mtu huyo.

Mheshimiwa Spika, leo kwenye *Corona*, nenda ukaangalie tumetengeneza kila *rush* kwenye *entry* moja, anayesimamia utaratibu wa ku-*sanitize* wachimbaji na ku-*regulate* ni huyo mwenye asilimia 15 na huyo hateuliwi na Wizara ya Madini anateuliwa na wachimbaji wenyewe kwa usimamizi wa Kamati iliyoundwa na ameileza Mheshimiwa

Naibu Waziri. Watu waliomo mle ni Afisa Madini, *DSO, OCD*, Mkurugenzi na mwakilishi wa *REMA*. Hawa wanateua watu wa kusimamia *rush*. Kama kuna matatizo tujadiliane tusianze kurushiana lawama, *at least* tunazungumza kwa sababu jambo jema limetokea.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, imezungumzwa kwamba pale Bulyanhulu hapakuwa na watu waliokuwa wamelipwa fidia. *With due respect*, mimi nilikuwa Naibu, Waziri wangu Mheshimiwa Angella Kairuki yuko mbele yangu hapa, alitisha kikao Mheshimiwa Maige akaja na Madiwani wake na uongozi wote, tulikuwa na watu wanaodai fidia wakaambiwa wa-*produce evidence* nini wanachodai, watu wawili ndiyo waliotokea akina Mzee Mayunga wakasema hawa ndiyo wanadai. Tukamwambia *ACCACIA* lipa hawa watu fidia, *ACCACIA* akaleta kiburi kwa historia yake, eneo lake lilipovamiwa tukamwambia wewe si una nguvu kawaondoe mwenyewe akashindwa ndiyo maana ile *rush* kutokea. Sasa *rush* ikishakutokea watu wanapata mkate wao unapeleka utaratibu watu wasiuane.

Mheshimiwa Spika, baada ya Barrick kuja...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, dakika moja malizia.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, baada ya Barrick kuja tumeweka utaratibu mzuri na hilo eneo lote limerudi kwa mwenyewe kwa sababu ile ni mali ya Serikali pamoja na Barrick. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naweza nikachukua muda mrefu kuzungumza mambo ya madini lakini naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana wewe, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa michango yao, niwashukuru na watani zetu wa Upinzani kwa michango yao. Naamini nia yetu ni moja, ni kujenga sekta ya madini ili iweze kukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono kabisa kabisa. Tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa kuhitimisha hoja yako kwa kufafanua mambo muhimu. Najua muda hautoshi mambo ni mengi, ungekuwa na muda wa kutosha ungeweza kupitia mambo mengi zaidi. *(Makofi)*

HOJA ZA KISERA

SPIKA: Sasa kwa muda huu mdogo uliobaki baadhi tutapata nafasi ya kuuliza maswali ya kisera lakini kwa sababu muda ni mdogo hatutarudia. Mheshimiwa Kafumu kifupi *straight* tumpe nafasi mtu mwingine.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kuuliza suala la kisera kwamba sekta ya madini ili ichangie vizuri zaidi katika uchumi wa nchi ni lazima iwe mchimbaji mdogo, mchimbaji mkubwa na uongezaji thamani katika nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana mafanikio tuliyoyapata kwenye uchimbaji mdogo kwenye *speech* yake kipengele namba 5.2 na kweli mmefanikiwa nawapongeza sana wadogo zangu lakini uchimbaji mkubwa nao ni sekta ambayo inaweza ikainua sana uchumi, tukiwa na migodi mikubwa kama hiyo ya Bulyanhulu na mingine kuna ajira nyingi na mambo mengi yatatokea.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri, analeta mikakati gani sasa katika siku za usoni kufufua utafutaji wa madini katika nchi yetu ili tuweze kupata migodi mkubwa itakayochangia zaidi katika uchumi wa taifa letu. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, migodi mikubwa, Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Kafumu, mimi huwa namwita mbobezi wa jiojio nchini na dunia kwa hoja yake hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mikakati tuliyokuwa tumejiwekea, ndiyo maana tulitengeneza *The International Forum of Mining* tuliyofanyia Dar es Salaam Februari. Pale tuliita makampuni mbalimbali ambayo yana *interest* ya kuwekeza kwenye madini. Nataka tu nimpe *comfort* kwamba tumezungumza uchimbaji mkubwa kwa sauti ndogo, tukazungumza kwa sauti kubwa uchimbaji mdogo kwa sababu kwa kweli kwa kiwango kikubwa uchimbaji mdogo ni kama tulikuwa tumeusahau kwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, *comfort* ninayotaka kumpa ni kwamba hivi tunavyozungumza tunazo leseni mbili kubwa za uchimbaji madini ambayo ziko kwenye hatua ya *development*, ya kutoa leseni *SML*. Mgodi wa kwanza ni wa Nyanzaga ambao ukubwa wake ni sawasawa tu na migodi mingine hii mikubwa tuliyonayo, lakini tuna Kampuni *Pick Resources* ambayo na wao wameomba kuchimba uchimbaji mkubwa wa kuchimba *rare earth elements*. Kwa hiyo, Serikali inapitia maandiko yao na baada ya kukamilisha basi leseni hizo zitatolewa na uchimbaji utaanza.

SPIKA: Mheshimiwa Adadi Rajab.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi kuhusiana na Madini ya Tanzanite. Nilikuwa mmoja wa wajumbe wa Tume yako ambayo uliunda na Mheshimiwa Waziri alikuwa ni Mwenyekiti wetu. Pamoja na mapendekezo mengine ya ujengaji wa ukuta na mambo ya *cameras* kuna pendekezo moja ambalo lilipendekezwa la kuanzisha uuzaji wa Tanzanite kwa njia ya mnada. Nataka kujua kama pendekezo lile limeshaanza kufanyiwa kazi na kama limeanza kufanyiwa kazi ni faida gani ambayo imekwishapatikana?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. La kwanza ni kweli kwamba tulikuwa na minada ya tanzanite siku za nyuma na minada hii baadaye Serikali ilisitisha baada ya kubaini kuna udanganyifu kwa kiwango kikubwa. Kwa sababu namna minada ile ilivyokuwa inaendeshwa ni watu wawili wanajifungia ndani wanatengeneza *lot*, wanajiba bei baadaye wanatoka nje kuwatangazia watu, Serikali ikasitisha utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukaamua sasa kujenga *One Stop Center* ambayo tutafanya *trading* zote za madini ndani ya ukuta. Nafurahi kusema kwamba *One Stop Center* imekamilika na sasa tunakuja kuanzisha utaratibu, ilikuwa tuanze kabla ya Bunge hili la bajeti lakini bahati mbaya kulikuwa na miundombinu mbalimbali ambayo ilikuwa hajakamilika ambayo tayari imeshakamilika baada ya muda minada hiyo itanza upya.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Mbarouk simuoni, Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na kuipongeza wizara kwa kazi kubwa na iliyotukuka wanayoifanya, naomba ufafanuzi kwenye jambo moja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 tumepitisha Sheria ya Umiliki wa Serikali wa Hisa asilimia 16 na mpaka sasa kwa taarifa niliyonayo ni kampuni moja tu ya Barrick ambayo ndiyo wameingia makubaliano na Serikali.

Hata hivyo, tuna orodha ya makampuni mengi ikiwemo Jimboni kwangu zipo kampuni zaidi ya tatu zimekwama yaani Serikali hajatoa utaratibu wa makampuni kufikia makubaliano ya mgawanyo wa 16% matokeo yake yale makampuni yamekosa ufadhili wa fedha kutoka kwenye benki za nje kwa sababu bado hakuna *clear Memorandum of Understanding*. Mnajua kukopa fedha benki inatakiwa

makaratasi na haya makaratasi Wizara imeachia Wizara ya Fedha, yaani imekuwa kama imewatelekeza kwa hiyo wako katikati.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha wanayachukulia haya makampuni kama vitu vya ziada, hawayachukulii kwa uzito. Wizara ya Madini inasema hili jukumu ni la Wizara ya Fedha, kwa hiyo, watu wako katikati. Nataka kujua msukumo wa Wizara ya Madini ili kufika hitimisho la haya makampuni yaweze kuingia hii mikataba na Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Madini, ufafanuzi tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Mheshimiwa Mlinga huwa tunazungumza sana na anazungumzia kampuni yake inayochimba *graphite* kule Mahenge.

Mheshimiwa Spika, nieleze tu kwamba kuna jukumu moja ambapo makampuni haya yanatakiwa ku-*list* hapa nchini na hilo jukumu linasimamiwa na *Capital Market Security Authority* ambao kwa kweli ndiyo wanasukuma hayo mambo. Mgawanyo wa asilimia 16 kila mwenye mgodi baada ya sheria ile kupita anafahamu kwamba ndani ya mgodi wake kuna asilimia 16 ya Serikali wala hauhitaji majadiliano, wala hauhitaji kuwaita kwa sababu wanajua. Isipokuwa tunatakiwa kuwaeleza wafanyabiashara hawa kwamba tunaanza lini ku-*charge* hiyo asilimia 16 kitu ambacho sisi ndani tunawasiliana nao na kwa kweli hatujawa na matatizo makubwa kwenye eneo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, nilikuona.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nina hoja moja tu kwamba Wilaya ya Mpwapwa kuna madini aina ya ruby, *copper* na *tourmaline*. Tulikwishaomba Wizara ya Madini hawa wachimbaji wadogo wadogo wasaidiwe kupata vifaa vya kisasa ili waweze kuboresha uchimbaji wao lakini

hatujaona wataalam kufika pale kutoa elimu kwa sababu wanaharibu sana mazingira hasa maeneo ya Mlembule, Tambi na Winza.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wataalamu wake wafike pale angalau waweze kuwaelemisha wale wananchi kuhusiana na uchimbaji mdogo mdogo ili waboreshe uchimbaji wao na madini yaweze kuwanufaisha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante Senator umeshasikika. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni la kuchukua tu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa tukutane tuzungumze tupange ratiba, tutatuma watu waende kufanya kazi hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru na nataka nimshukuru Kaka yangu Mheshimiwa Doto kwa kukubali na kutaja kwamba kipindi hiki watu wa Nyamongo watalipwa stahiki zao ambazo wamedai kwa muda mrefu, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nilitaka anipe ufafanuzi kwa sheria tuliotunga Sheria Na. 6 ya *Unquestionable Terms* ya mwaka 2017, kifungu cha 5 kinasema baada ya mkataba kusainiwa ndani ya siku sita za kikao kinachofuata cha Bunge mikataba italetwa Bungeni kwa ajili ya Wabunge kujadili. Ni lini Serikali italetu huo mkataba na ni kwa nini Serikali kwa muda wote huu Mabunge yamepita mawili haijaleta mkataba humu ili kwa niaba ya wananchi tuujadili na tutoe mapendekezo tuone mapungufu kama yale niliyoyaona kwamba kwenye Randama unasema tutagawana faida za mauzo 50 kwa 50, ukurasa wa 13 lakini kwenye hotuba unasema ni faida za kiuchumi. Sasa faida ya gawio na faida za kiuchumi ni nini na nini? Sasa hivyo vitu vinachanganya ndiyo maana sheria ili-*provide* katika kifungu

cha 5 kwamba utaleta mkataba. Sasa ni kwa nini haijaletwa na inaletwa lini hapa?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi. (*Makofi*)

SPIKA: Sijui anajibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali au nani? Haya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, hoja hii uzuri iliibuliwa pia kwenye Kamati na Mheshimiwa Heche alilibua vizuri tu na tulitoa majibu tukamwambia kwa sheria ile akiisoma vizuri Bunge likihitaji mikataba hiyo wakati wowote litaletewa.

SPIKA: Nafikiri imeeleweka...

WABUNGE FULANI: Hapana.

SPIKA: Haya Mheshimiwa Heche maana ni jambo muhimu hili na ndiyo maana nilisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Kicheko*)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimetaja na kifungu...

SPIKA: Hebu kisome.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, ngoja nikisome, mtanivumilia kidogo kwa sababu nilikuwa nimefunika na imepotea kidogo, tafadhali.

SPIKA: Wakati unatafuta namuita Mheshimiwa Mbogo, wewe tafuta tu kwa amani.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Ili kuweza kudhibiti madini nchini Serikali iliweka msisitizo kuwa na *smelter* Tanzania lakini kuna changamoto ya uwekezaji wa hizi *smelter* na hususani maeneo ambayo yanapatikana madini zaidi ya aina moja karibuni saba mpaka tisa, kwa mfano ukanda wa Mkoa wa

Katavi. Changamoto hiyo ya uwekezaji wa *smelter* imeleta tatizo kwa wawekezaji ambao wameshafanya uwekezaji wa awali wa kuwa na uchimbaji. Serikali inaenda kuwasaidia vipi *either* kwa kuwekeza kujenga hizo *smelter* au kuwaruhusu kwa utaratibu ambao mtaona unafaa ili waweze kuuza makinikia na Serikali iweze kupata mapato? Nini wazo la Serikali?

SPIKA: Ufafanuzi wa jambo hilo, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yetu ni kwamba tumetoa leseni za watu kujenga *smelter* na maeneo ambayo yanajengwa *smelter* ni ya Mwanza, Geita pamoja na Kyerwa kwa ajili ya madini ya bati. Nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli changamoto hiyo ipo ya watu kusafirisha madini ambayo ni ghafi.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyokumbuka mwaka wa juzi tulitengeneza mwongozo wa kusafirisha madini ghafi ambayo ni kipindi cha mpito na wako watu kweli ambao wanahitaji kusafirisha makinikia. Kuna taratibu ambazo tulikuwa tunazikamilisha kwa ajili ya kuwapa utaratibu maalumu baada ya mwongozo ule kutoka ili tuweze kuwapa vibali vya kusafirisha. Imani yangu ni kwamba wawe na subira tukishakamilisha jambo hilo basi tutatoa vibali hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Heche tunarudi kwako tusomee.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kifungu cha 5 kinasema: "*All arrangements or agreements on natural wealth and resources made by the Government shall, within six sitting days of the National Assembly next following the making of such arrangement or agreements be reported to the National Assembly*". (Makofi)

SPIKA: Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, ahsante kama alivyosoma mwenyewe Mheshimiwa Heche hapa inazungumza juu ya *reporting to the National Assembly* haizungumzii *submitting the agreement to the National Assembly*. Ahsante. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana. Niwathibitishie ilikuwa *reported* kwa Spika na nilipata barua ya Serikali. Halima ni wapi inaposema kwamba Spika akishapata sasa na yeye a-*submit*? Hicho Kingereza tunajua wote jamani, msifikirie mnakijua peke yenu, kwa hiyo, twende taratibu na Mheshimiwa Heche kwa sababu ni mjumbe mnapaswa kuli-*sort-out* kule vizuri zaidi kama kuna *omission* basi inaweza ikarekebishwa na kadhalika.

Tayari Mheshimiwa Waziri alishatoa hoja na ilikwisha unywa mkono. Tulipofika ni wakati wa kupiga kura na kuweza kutekeleza jukumu la kuipima ile hoja kwamba mkubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kura zimekwisha kupigwa na walio wengi wameafiki na wameshinda. Kwa hiyo, hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Madini imepita rasmi. (Makofi)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 100 – Wizara ya Madini.....Sh.54,281,586,000

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 100 – Wizara ya Madini.....Sh. 8,500,000,000

SPIKA: Kwa niaba yenu basi nawatakia kila kheri, Mheshimiwa Waziri Doto Biteko; Mheshimiwa Naibu Waziri Stanslaus Nyongo; Katibu Mkuu Prof. Msanjila; Mwenyekiti wa Tume, Prof. Kikula; wataalamu wote na Wakurugenzi ambao

mnafanya kazi chini ya Wizara hii ya Madini muendeleo kufanya kazi nzuri mnayoendelea kuifanya. Tunawatakiya kila kheri kwa kweli mmeituliya Wizara hii ilikuwa ni Wizara yenye makelele mengi ajabu lakini imetulia tuli. Hata mambo mengi ambayo yalikuwa yanazungumzwa hapa utaona ni kwamba yanaweza tu kufanyiwa kazi yakawekwa vizuri katika michakato ya kuendelea kuboresha utendaji kazi. Kwa hiyo, tunawapongeza sana, muendeleo kufanya kazi mkijua kabisa kwamba wenzenu tunawaunga mkono, tunawatakiya kila kheri. (Makofi)

Kwenye mgawanyo ule wa asilimia 15 au sijui ngapi hasa kwa wachimbaji wadogo mimi sizungumzii wachimbaji wakubwa (*certificate* kubwa), mtaona mgawanyo ule halmashauri inapata asilimia 0.3. Hili nalo siku za mbele nafikiri lije litazamwe kidogo. Kwa sababu huyu asilimia 15, huyu ngapi, huyu ngapi, halafu halmashauri kiduchu. Kwa leseni kubwa asilimia 0.3 bado ni *substantial* lakini huku kwa wachimbaji wadogo nao wangepata angalau mfuko mmoja siyo mbaya sana au kitu fulani hivi ambacho kidogo kinasogeza kidogo hiyo asilimia 0.3, nayo ije iangaliwe. Kwa wachimbaji wakubwa, hapana, ni hela nyingi akina Mheshimiwa Musukuma watachanganyikiwa ikiongezwa hiyo lakini kwa wadogo wadogo huko iko haja ya kuongezeka. (Makofi)

Pia elimu itolewe, sijui ni Wizara ya Madini au Wizara ya Fedha au Wizara gani, iko haja ya kutoa elimu ya *handling* ya fedha. Wachimbaji walio wengi ni wenzake Mheshimiwa Musukuma. Namtaja yeye kwa sababu ni mtani wangu yaani *somebody* ana *land* katika fedha nyingi ambazo mwingine hajawahi kuwa nazo. Kwa hiyo, anatamani tu aende benki achukue yaani wamuone kwamba anazo na kadhalika na kadhalika na matumizi ya hovy hovy. Kwa hiyo, iko haja ya kupata mafunzo ili kutopenda sana kusomba mamilioni ya shilingi wakati mwingine bila sababu ya msingi ya kwa nini anachukua lakini ni zake. Kwa hiyo, iko haya ya kupata mafunzo, akina Mheshimiwa Kalemani hawa bwana fedha hata kama zako taratibu taratibu kidogo. (Kicheko)

Nakumbuka safari moja nilikuwa naangalia *Youtube* mahali, nikawa namsikiliza tajiri namba moja wa Afrika nzima ambaye ni Alhaji Aliko Dangote akawa anasema alikwenda alipofikia mahali pa kuanza na kuwa na *millions of dollars actually* alikuwa bilionea wa dola, safari moja alienda benki akachukuwa *cash* kitu kama dola milioni moja hivi, sikumbuki *figure*. Akachukua *cash* (dola) akaweka kwenye buti ya gari akaenda nayo nyumbani akalala nayo halafu kesho yake asubuhi akairudisha benki ili kujiridhisha hizi fedha ni zangu kweli yaani hizi zangu hizi nyingi namna hii. (*Kicheko*)

Sasa hawa Wasukuma wakati mwingine namuambia Dada yangu Mheshimiwa Ashatu yaani akipata haya mamilioni anataka achukue hata milioni mia aende nazo nyumbani akaonyeshe mkewe na yeye azipapasepapase, aamke usiku aangalie hivi hizi zote zangu mimi. Sasa tuwape raha hiyo, akitaka kuchukua fedha yake maswali mengi yaani yeye shida yake ni hiyo tu, halafu kesho yake anawarudhishia tena ameshaamini kwamba hii fedha kweli ni ya Ndugai hii. Maana mtu kama hujawahi kugusa fedha kama hizo ina raha yake ya kuziona kwa macho. Hivi kweli hizi au ni *figure* kwenye karatasi tu wananidanganya hawa au zangu kweli? Wengine kinachowasumbua ni hicho tu wala siyo kitu kingine. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna jukumu la Kikatiba lile la kujaza zile Fomu za Maadili za Mali na Madeni, wengi wenu mmekwishajaza. Karibu Wabunge 356 wamejaza lakini kuna Wabunge 29 ambao fomu zao ofisi yangu haijawai kuzipata, *I hope* zilienda kule Maadili moja kwa moja, kwa hiyo, tutawasiliana nao. Muda wa kufanya hivyo ume-*expire*, kwa hiyo, nina Wabunge 29 ambao sina fomu zao na wengine nawaona hapa hapa, wengine ni Mawaziri na wengine, orodha ni ndefu ya Wabunge 29. Kwa hiyo, kama ukipuuzia jambo hili ni kwako na kwangu sasa nafunga kila kitu ili kuhakikisha kwamba kila kitu kiko sawasawa kule, kwa hiyo, yakikupata kazi kwako. Ndiyo mtabakia kulalamika kama wengine oooh fulani alionewa, fulani alionewa, hakuna anayeonewa tufuate utaratibu tu. Ni vizuri kujiridhisha kama huna uhakika sana unapita pale ofisini kwangu pale kwa

msaidizi wangu anakueleza kama fomu yako ilipokelewa au haijapokelewa, au kwa nini na kadhalika ili kujiweka sawa, ni wachache tu 29 tu basi.

Kesho tutaendelea na Wizara ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, ya Habari. Kwa hiyo, naomba tutoe ushirikiano kama kawaida Waheshimiwa Wabunge, ni Wizara ya siku moja tuitendee haki.

Nimalizie kwa suala la Marehemu Mchungaji Dkt. Rwakatare, ofisi yangu imekuwa ikiendelea kuwasiliana na familia na familia ilikuwa imetoa ushauri wa mambo mawili Serikalini, siyo kwa Bunge. Wameomba kwamba Mchungaji na Mama yao ikiwezekana azikwe kwenye eneo la Kanisa la Mlima wa Moto. Hilo ni ombi la kwanza, *strongly* wameomba sana hilo. Pili, wameomba sana tarehe ya mazishi iwe kesho kutwa tarehe 23 Aprili, 2020, siku ya Alhamisi. Sina hakika sana na upande wa Serikali lakini majibu niliyonayo ni kwamba Serikali haina shida na yote mawili haya.

Waheshimiwa Wabunge, ila niwajulisheni tu kwa hatua hii ni kwamba Serikali ndiyo itakayosimamia mazishi hayo ambayo washiriki wa mazishi hayo hawatazidi kumi na kwamba huo ndiyo utaratibu utakavyokuwa. Sisi Bunge basi tunaomba ushirikiano kwa wahusika wote mahali pote kuelewa Serikali, kuelewa Bunge na ushiriki wetu uwe ni kwa kadri ya ushauri ambao tunapewa na Serikali.

Baada ya maelezo hayo, naona kazi za leo zimekamilika na kwa jinsi hiyo basi, naomba tuahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

(Saa 12.34 Jioni Bunge Liliarishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)